**20 MEI, 2026**

# BUNGE LA TANZANIA

---

## MAJADILIANO YA BUNGE

---

## MKUTANO WA TATU

**Kikao cha Thelathini na Tatu — Tarehe 20 Mei, 2026**

*(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Mwenyekiti (Mhe. Deodatus P. Mwanyika) Alisoma Dua*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa, tukae.

Katibu.

**NDG. ASIA MINJA – KATIBU MEZANI:**

**HATI ZA KUWASILISHA MEZANI**

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na:-

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:**

Hotuba ya Bajeti ya Wizara ya Ujenzi kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027.

**MHE. MARIAM SAID KHAMIS K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA MIUNDOMBINU:**

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu kuhusu Utekelezaji wa Majukumu ya Wizara ya Ujenzi kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026 pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027.

**MWENYEKITI:** Ahsante.

Katibu.

**NDG. ASIA MINJA – KATIBU MEZANI:**

**MASWALI NA MAJIBU**

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, nitoe angalizo kabla hatujaanza maswali. Leo ni Wizara ya Ujenzi, tuna wachangiaji wengi sana, ndiyo Wizara ambayo imevunja rekodi kwa kuwa na wachangiaji wengi. Kwa hiyo basi, kwa kuwa ninataka watu wengi zaidi mchangie, tutapunguza au kuondoa kabisa maswali ya nyongeza. Tutakwenda kwenye maswali ya msingi, na labda tunaweza kuruhusu swali moja tu la nyongeza ili wote tupate nafasi ya kuchangia, na sijui kama tutawamaliza. *(Makofi)*

Basi, tunaanza na Ofisi ya Waziri Mkuu - TAMISEMI, ninamwita sasa Mheshimiwa Abdallah Jafari Chaurembo, Mbunge wa Chamazi, aulize swali lake.

Na. 386

**Ujenzi wa Barabara ya Mzambarauni – Daraja la Kilungule**

**MHE. ABDALLAH J. CHAUREMBO** aliuliza:-

Je, lini Serikali itajenga Barabara ya Mzambarauni - Mikoroshini – *Saku Store* – Saku Mwisho hadi Daraja la Kilungule iliyopo kwenye Mradi wa *DMDP?*

**MWENYEKITI:** Majibu Mheshimiwa Dkt. Festo Dugange, Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE)** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI, ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa

Abdallah Jafari Chaurembo, Mbunge wa Jimbo la Chamazi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inatambua umuhimu wa barabara ya Mzambarauni – Mikoroshini – *Saku Store* – Saku Mwisho hadi Daraja la Kirungule kwa wakazi wa Chamazi, hasa katika kurahisisha usafiri na kuchochea shughuli za kijamii na kiuchumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inaendelea na usanifu wa barabara hii kupitia Mradi wa *DMDP* Awamu ya Pili. Utekelezaji wa ujenzi wa barabara hii kwa kiwango cha lami umejumuishwa katika mpango wa maendeleo wa Halmashauri ya Manispaa ya Temeke, unaolenga kukabiliana na changamoto mbalimbali za miundombinu, ikiwemo ujenzi na uboreshaji wa barabara. Mpango huu ni sehemu ya mkakati mahususi wa Serikali wa kuboresha miundombinu katika maeneo ya mijini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati mpango huo ukiendelea kukamilishwa, sehemu ya Barabara hii inayotumiwa na wananchi kwa sasa hususan kipande cha Mzambarauni – Mikoroshini – *Saku Store* – Saku Mwisho, itaendelea kufanyiwa matengenezo ya mara kwa mara ili kuhakikisha inapitika wakati wote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mwaka wa fedha 2025/2026 barabara hii imetengewa shilingi milioni 69.30 kwa ajili ya kuweka changarawe kwa urefu kilometa 0.3, kujenga mtaro upande mmoja urefu wa mita 300 na kuchonga barabara urefu kilometa mbili.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Abdallah Chaurembo, swali la nyongeza.

**MHE. ABDALLAH J. CHAUREMBO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa Serikali imekiri inafahamu umuhimu wa barabara hii, je, Serikali haioni ipo haja ya kujenga daraja la muda ambalo litaunganisha kati ya barabara hii na Jimbo la Chamazi na lile Jimbo la Temeke?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili. Je, Serikali ni lini itajenga sasa Barabara ya Kwa Mkongo - Kwa Karata mpaka Saku Ilulu ambayo inaenda kuungana na barabara hii?

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimpongeze sana Mheshimiwa Abdallah Jafari Chaurembo, Mbunge wa Jimbo la Chamazi, amefuatilia mara nyingi kuhusiana na ujenzi wa barabara hii na Serikali hii sikivu sana ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan imeendelea kupeleka fedha kuhakikisha kwamba barabara hii inajengwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara hii ya Mzambarauni - Mikoroshini - *Saku Store* - Saku Mwisho inaunganisha Kilungule na katika maeneo maarufu kama daraja la maji, tayari tuko kwenye hatua za kumpata mzabuni kwa ajili ya kujenga daraja mning'inio kwa maana ya *suspension bridge* ili wananchi waendelee kupita kwenye daraja hilo la muda wakati tunajiandaa na ujenzi wa daraja la kudumu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vivyo hivyo, barabara hii tayari tumeshapata mkandarasi, na tayari yuko *site* anaendelea kumwaga kifusi na kuziba mashimo katika barabara hii ili wananchi wapite vizuri. Kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba, Serikali inaona umuhimu huo na ndiyo maana mkandarasi tayari yuko *site* na kazi zinaendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitumie nafasi hii nimpongeze sana Mkurugenzi wa Halmashauri ya Manispaa ya Temeke, Ndugu Jomaary Mrisho Satura amekuwa mfano wa Wakurugenzi kutenga fedha za mapato ya ndani kwa ajili ya kuboresha barabara. Serikali ilitoa maelekezo kwamba Manispaa na Majiji yatenge asilimia ya fedha kwa ajili ya kuboresha barabara katika maeneo yao, na Temeke ni moja ya mfano bora sana wa Wakurugenzi ambao wanatekeleza maelekezo ya Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, kuhusiana na barabara ya Kwa Mkongo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba, nayo tuko kwenye hatua za kumpata mzabuni kwa *DMDP II,* lakini pia kwa mapato ya ndani na tutahakikisha kwamba inajengwa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Musukuma.

**MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru. Ujenzi wa madaraja unaoendelea kwenye Jiji la Mwanza umesababisha foleni kubwa sana kwa takribani siku tatu zilizopita mpaka sasa. Barabara inayotoka Mji wa Mwanza - Igoma – Nyegezi - kwenda *Airport* ni barabara moja tu ambayo *bypass* yake huwa ni Rufiji, lakini kumechimbwa daraja, Rufiji kumechimbwa mlango mmoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sasa kitendo cha kutoka *Nyerere Road* kwenda Mabatini inatuchukua mpaka masaa matatu. Je, Waziri yuko tayari kuambatana na Mbunge wa Nyamagana kwenda kumhimiza yule mkandarasi afanye ujenzi usiku na mchana, kwa sababu anajenga bila kutengeneza *bypass*. Kwa hiyo, tunapita kwenye njia moja, foleni ni kubwa.

**MWENYEKITI:** Majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, niko tayari kuambatana na Mheshimiwa Mbunge wa Jimbo la Nyamagana, na pia nimpongeze sana Mheshimiwa Musukuma kwa kuleta hoja hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitumie nafasi hii kumwelekeza Meneja wa *TARURA* Mkoa wa Mwanza kwamba, pamoja na umuhimu wa kujenga madaraja na barabara zetu, lakini ni lazima tuzingatie pia kupunguza usumbufu wa foleni ambao unaweza kuleta changamoto kwa wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, barabara ya Mwanza – Igoma - Nyegezi kuelekea *Airport* waone utaratibu mzuri; kwanza, mkandarasi aongeze *speed* kuhakikisha huo ujenzi unakamilika

mapema na kuondoa adha hiyo ya foleni, lakini ikiwa kuna namna ya kuwa na barabara ya mchepuko, ni vizuri wafanye hivyo ili kurahisisha usafiri kwa wananchi wanaoenda katika maeneo haya.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa tunaendelea, nimwite sasa Mheshimiwa Amina Mussa Mkumba, Mbunge wa Kibiti, aulize swali lake.

Na. 387

**Ujenzi wa Barabara ya Kipoka – Mahimbwa (Kibiti)**

**MHE. AMINA M. MKUMBA** aliuliza:-

Je, lini Serikali itaikarabati Barabara ya Kipoka - Mahimbwa kwa kiwango cha changarawe ili kufungua Kata za Delta?

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE)** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI, ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Amina Mussa Mkumba, Mbunge wa Jimbo la Kibiti kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kupitia Wakala wa Barabara za Vijijini na Mijini *(TARURA)* inatambua umuhimu wa Barabara ya Kipoka – Mahimbwa katika kuwezesha mawasiliano na shughuli za kiuchumi katika Kata za Delta ambazo ni (Kiongoroni, Mbuchi, Msara na Salale) Wilayani Kibiti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imeendelea kutenga bajeti za ujenzi na ukarabati wa barabara katika Wilaya ya Kibiti ambapo katika kipindi cha mwaka wa fedha 2021/2022 hadi 2025/2026 jumla ya shilingi bilioni 12.18 zimepelekwa Wilaya ya Kibiti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2026/2027, Serikali imetenga kiasi cha shilingi milioni 700 kwa ajili ya ukarabati wa barabara za Kipoka - Usimbe na Kipoka - Mahimbwa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Amina Mkumba, swali la nyongeza.

**MHE. AMINA M. MKUMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa swali la nyongeza. Pamoja na majibu mazuri kutoka kwa Serikali nina maswali mawili ya nyongeza. Kwa kuwa barabara ya Kingwira - Mchukwi hospitali yenye kilometa nane imekuwa kero kubwa sana kwa wananchi wa Mchukwi, je, ni lini Serikali itapeleka fedha ili barabara hiyo iweze kujengwa katika kiwango cha changarawe? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali lingine, kwa kuwa Daraja la Luhoyi ambalo linaunganisha vijiji vya Mtunda, Kikale na Muyuyu limeharibika kabisa kipindi cha mafuriko, na sasa watu wanavushwa na mtumbwi, nini kauli ya Serikali juu ya Daraja hilo la Luhoyi ambalo liko Kata ya Mtunda? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimpongeze sana Mheshimiwa Amina Mussa Mkumba, Mbunge wa Jimbo la Kibiti kwa ufuatiliaji wake kwa maslahi ya wananchi wa Jimbo la Kibiti. Nimhakikishie kwamba tulishamweleza Mameneja wa *TARURA* ngazi ya wilaya na mkoa; Mkoa wa Pwani na pia Wilaya ya Kibiti, wamewasilisha changamoto ya barabara hizi kama ambayo Mheshimiwa Mbunge umewasilisha hususan barabara hii inayoelekea Hospitali ya Mchukwi *Mission* pale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge, kwamba Serikali iko kwenye hatua za mwisho za kuandaa taratibu za kibajeti kwa ajili ya kwenda kufanya ukarabati wa barabara hizi zilizoharibiwa na mvua ikiwemo ujenzi wa daraja hili ambalo limeharibika.

**MWENYEKITI:** Tunaendelea, bado tupo Wizara hiyo hiyo, nimwite sasa Mheshimiwa Innocent Lugha Bashungwa, Mbunge wa Karagwe, aulize swali lake.

Na. 388

**Ujenzi wa Soko la Kisasa Kayanga**

**MHE. INNOCENT L. BASHUNGWA** aliuliza:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuanza ujenzi wa Soko la kisasa Kayanga ambapo ni Makao Makuu ya Wilaya ya Karagwe?

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE**) alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI, ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Innocent Lugha Bashungwa, Mbunge wa Jimbo la Karagwe, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inatambua umuhimu wa eneo la Kayanga Jimbo la Karagwe kuwa na soko la kisasa kwani eneo hilo ni makao makuu ya wilaya. Serikali imefanya usanifu wa mradi huu ambapo shilingi bilioni 5.17 zinahitajika kwa ajili ya ujenzi wa mradi huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imepanga kutekeleza mradi huu kwa awamu. Katika mwaka wa fedha 2026/2027 Serikali imetenga shilingi 1,000,000,000 kwa ajili ya kuanza ujenzi.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Innocent Bashungwa, maswali ya nyongeza.

**MHE. INNOCENT L. BASHUNGWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri ya Serikali, ninaomba kwanza

nimshukuru sana Rais wetu, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kutekeleza jambo ambalo tulimwomba wakati wa kampeni kuhusu ujenzi wa soko la kisasa pale Makao Makuu ya Wilaya ya Karagwe. Ninamshukuru sana Rais wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na shukurani, gharama ya kujenga soko hili la kisasa kama alivyosema Mheshimiwa Naibu Waziri ni shilingi bilioni 5.17 na kwenye mwaka wa fedha wa 2026/2027 zimetengwa shilingi bilioni moja, kwa maana tukienda kwa awamu itachukua miaka mingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimwombe Mheshimiwa Naibu Waziri atusaidie fedha ipatikane angalau soko hili liweze kukamilika ndani ya miaka miwili ili wananchi wa Wilaya ya Karagwe waweze kufurahia soko la kisasa chini ya jemedari wetu Mheshimiwa Rais wetu, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, nimpongeze sana kaka yangu Mheshimiwa Innocent Lugha Bashungwa, Mbunge wa Karagwe kwa uchapakazi wake na uwakilishi mahiri sana wa wananchi wa Jimbo la Karagwe. Kwa hakika wananchi wa Karagwe wamepata Mbunge mchapakazi kweli kweli.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali ina dhamira ya dhati kuhakikisha kwamba tunajenga soko hili, na ndiyo maana tayari tumeshatenga shilingi bilioni moja mwaka wa fedha 2026/2027 huu unaoanza Julai, 2026. Nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba tutajenga kwa awamu lakini haina maana kila awamu itapelekwa shilingi bilioni moja. Inaweza ikawa awamu moja hii ya kwanza, ya pili tukapeleka fedha zote na jengo likakamilika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ninaomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali itahakikisha tunakamilisha

ujenzi wa soko hilo mapema ili kuleta huduma bora kwa wananchi wa Jimbo la Karagwe.

**MWENYEKITI:** Nimekuona Mheshimiwa *Engineer* Johnston Mutasingwa.

**MHE. ENG. JOHNSTON J. MUTASINGWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Jimbo letu la Bukoba Mjini imeelezwa kwenye Ilani kwamba tunapaswa kujenga masoko manne: Soko la Samaki na Dagaa *(custom),* Soko la Kashai, Soko la Hamugembe na Soko la Ndizi Kagondo. Je, Serikali ina mpango gani wa kushirikiana na Halmashauri ya Manispaa ya Bukoba kuhakikisha haya masoko yanajengwa kwa wakati? Ahsante.

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, masoko ni sehemu muhimu ya huduma katika jamii zetu, lakini pia ni chanzo cha mapato kwa halmashauri zetu ikiwemo katika Manispaa ya Bukoba. Pia, ni kweli kwamba uko mpango wa kujenga masoko katika Manispaa ya Bukoba, uko mpango pia wa *TACTIC* kuhakikisha kwamba tunaboresha miundombinu hiyo, na pia iko mipango mingine ya maboresho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba maeneo hayo ambayo ameyaainisha tutahakikisha kwa awamu tunaendelea kutenga fedha za bajeti ya mapato ya ndani ya halmashauri, na fedha za Serikali Kuu kwa kadiri itakavyowezekana ili kuhakikisha tunatimiza dhamira ya Serikali ya kujenga masoko katika maeneo hayo.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, tunakushukuru kwa majibu yako kwa Waheshimiwa Wabunge.

Tunaendelea na Ofisi ya Rais, Utumishi na Utawala Bora, sasa nimwite Mheshimiwa Dkt. Catherine Canute Joachim, Mbunge wa Viti Maalum, aulize swali lake.

Na. 389

**Utekelezaji wa Mfumo wa Serikali Mtandao**

**MHE. DKT. CATHERINE C. JOACHIM** aliuliza:-

Je, utekelezaji wa Mfumo wa Serikali Mtandao umefanikiwa kwa kiwango gani katika kurahisisha upatikanaji wa huduma za Serikali kwa Wananchi?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kutekeleza Mfumo wa Serikali Mtandao na kurahisisha upatikanaji wa huduma za Serikali kwa wananchi, Serikali ilitunga Sheria ya Serikali Mtandao, Sura 287 pamoja na Kanuni zake za mwaka, 2020. Sheria hiyo ilianzisha Mamlaka ya Serikali Mtandao *(e-GA)* ili kuratibu, kusimamia na kuendeleza utekelezaji wa jitihada za Serikali Mtandao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mamlaka ya Serikali Mtandao kwa kushirikiana na taasisi nyingine, imejenga na kuboresha mifumo mbalimbali ya kielektroniki ikiwemo, e-Watumishi, e-Utendaji, e-Mrejesho, e-Ardhi, *e-Office*, Bunge Mtandao, *TAUSI*, *LUKU*, *MUVU*, *MAJIIS* na *GePG*. Mifumo hiyo na mingine imerahisisha upatikanaji na utoaji wa huduma kwa wananchi, kuongeza uwazi, ufanisi na uwajibikaji katika utendaji kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuboresha Utekelezaji wa Mfumo wa Serikali Mtandao, Serikali itaendelea kuwekeza zaidi katika usalama wa mifumo, elimu kwa wananchi, na upanuzi wa miundombinu ya *TEHAMA* ili kuimarisha utoaji wa huduma kwa wananchi.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Dkt. Catherine Canute Joachim.

**MHE. DKT. CATHERINE C. JOACHIM:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri ya Serikali kuhusiana na suala la Serikali Mtandao, nina maswali mawili ya nyongeza. Kwa kuwa upatikanaji wa huduma ya Serikali Mtandao hususan kwa wananchi wa vijijini bado una changamoto kubwa, nini mpango wa Serikali kuhakikisha huduma hizi zinawafikia wananchi hususan waishio vijijini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili. Wananchi wamekuwa wanalazimika kurudia kujaza taarifa mbalimbali pindi wanapotumia mifumo ya Serikali kama vile *NIDA*, *TRA* na mifumo mingine iliyoko katika halmashauri zetu. Nini mpango wa Serikali wa kuhakikisha mifumo hii inaunganishwa ili iweze kuwasaidia wananchi kuweza kujaza taarifa zao kwa haraka? Ahsante,

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nimpongeze Mheshimiwa Mbunge kwa maswali yake mazuri, lakini nimpongeze kwa namna ambavyo anaendelea kuwasemea wananchi wake katika eneo lake la uwakilishi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, azma ya Serikali ni kuhakikisha kwamba huduma zinarahisishwa kwa wananchi. Ndiyo maana Serikali kupitia Mamlaka ya Serikali Mtandao imekuja na mfumo na mifumo mbalimbali ambayo inamrahisishia mwananchi kupata huduma. Hata hivyo, ili wananchi wa vijijini wapate huduma hizi, Serikali imeona ni muhimu kuunganisha mifumo kutoka kwenye kutumia vifaa kama simu janja, lakini kwa sasa Serikali imeelekeza na kurahisisha namna ya kutumia simu za kawaida, kwa maana kwamba anaweza akatuma meseji badala ya kutumia tu simu janja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, wananchi wa vijijini wanapokuwa katika maeneo yao, wanaweza wakapata huduma kule waliko badala ya kufuata huduma kwenye ofisi za Serikali kwa kutumia simu janja; hata kama hana ile simu kubwa,

basi anaruhusiwa kutumia ile simu janja kwa kutuma meseji na anapata huduma akiwa huko huko maeneo ya vijijini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuzingatia hilo, Serikali imeendelea kutoa elimu ya kutosha sana kuhakikisha wananchi wanaelewa mifumo ambayo imeshajengwa na Serikali, lakini kuwajengea uwezo watendaji wa Serikali namna ya kutumia mifumo hii ya kutoa huduma Serikalini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukienda kwenye swali lake la pili, kwa kuzingatia maelekezo ya Mheshimiwa Rais ya kuhakikisha kwamba taasisi za Serikali zinazungumza kwa pamoja, Serikali kupitia Serikali Mtandao imeanzisha mfumo ambao unarahisisha Serikali kubadilishana taarifa; Mfumo wa *Government ESB (Government Enterprise Service Bus)*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, mifumo hii inakwenda kusomana kwa maana ya mfumo mmoja kwenda mwingine. Badala ya wananchi kubeba makabrasha au kubeba viambata kwenda kila ofisi, basi mfumo huu umerahisisha kwamba mwananchi anapokwenda kupata huduma katika ofisi hiyo, anaweza kupata taarifa kutoka ofisi hiyo na ofisi nyingine akaweza kubadilishiwa taarifa hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, na kwa kuzingatia hilo, taarifa nyingi zimeunganishwa katika mfumo wa *NIDA*. Kwa hiyo, mtu anapokwenda kupata huduma, taarifa zake nyingi zitakuwa katika mfumo wa *NIDA*. Kwa kuzingatia hilo, tayari taasisi nyingi, taasisi 202 tayari zimeshaanza kubadilishana taarifa na ikiwemo mifumo 260 tayari inafanya kazi hiyo ya kubadilishana taarifa, ili kurahisisha wananchi wasipate shida au wananchi wasipate ile kuzunguka na *dokument* katika kupata huduma hizo za Serikali.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, tunakushukuru kwa majibu yako kwa Waheshimiwa Wabunge.

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Wizara ya Madini. Nimwite Mheshimiwa Joseph Zacharius Kamonga, Mbunge wa

Ludewa, aulize swali lake. Kwa niaba yake litaulizwa na Mheshimiwa...

**MHE. REBECA S. NSEMWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba.

**MWENYEKITI:** Sawa endelea.

Na. 390

**Fidia kwa Wananchi wa Mgodi wa Makaa ya Mawe – Ketewaka**

**MHE. REBECA S. NSEMWA K.n.y. MHE. JOSEPH Z. KAMONGA** aliuliza:-

Je, lini wananchi wa eneo la Mgodi wa Makaa ya Mawe Ketewaka watalipwa fidia ili waachie eneo hilo na kufanya shughuli zao maeneo mengine?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, kwa niaba yake linajibiwa na Mheshimiwa Waziri wa Madini.

**WAZIRI WA MADINI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, uthamini wa mali za wananchi wanaotakiwa kupisha utekelezaji wa Mradi wa Makaa ya Mawe wa Ketewaka ulikamilika mwezi Disemba, 2022. Katika zoezi hilo, wananchi 693 walihakikiwa na jumla ya kiasi cha shilingi bilioni 2.89 kiliidhinishwa na Mthamini Mkuu wa Serikali kwa ajili ya malipo ya fidia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mradi huu unamilikiwa na Shirika la Taifa la Maendeleo *(NDC)* kupitia leseni tatu za uchimbaji wa kati ambazo ni *ML 694/2023*, *ML 695/2023* na *ML 696/2023*. Kwa sasa, Shirika limepanga kutekeleza mradi huo kwa mfumo wa ubia na kampuni ya *MM Steel Resources PLC (MMSR)* ili kuharakisha maendeleo ya mradi na upatikanaji wa mtaji. Majadiliano baina ya pande hizo mbili yamekamilika, na hatua inayofuata ni utiaji

saini wa mikataba ya ubia pamoja na kukamilisha uhamishaji wa leseni husika kutoka *NDC* kwenda kampuni ya ubia. Maombi ya uhamishaji wa leseni tayari yamepokelewa na Tume ya Madini na yanafanyiwa kazi kwa mujibu wa sheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tayari mwekezaji huyo amejiandaa kifedha kwa ajili ya malipo ya fidia. Hivyo, mara baada ya hatua za kisheria na kimkataba kukamilika, wananchi wanaostahili wataanza kulipwa fidia, na utekelezaji wa mradi utaendelea rasmi.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Nsemwa, swali la nyongeza.

**MHE. REBECA S. NSEMWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Wananchi wa Mchuchuma waliolipwa fidia wanaishukuru sana Serikali na wamehamia eneo la Idusi, lakini eneo hilo halina barabara, zahanati wala shule ya msingi. Je, Serikali haioni umuhimu wa kupeleka huduma hizo ili wananchi hao wasipate usumbufu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, zipo leseni zilizotolewa kwa wawekezaji mbalimbali katika eneo la Mchuchuma, na muda ambao walipewa kwa ajili ya kufanya shughuli hiyo umeisha. Je, Serikali kwa nini isiwanyang'anye leseni hizo na kuwapatia wawekezaji wengine ambao wana nia thabiti na kuanza kufanya uwekezaji huo ili wananchi wa Ludewa waweze kunufaika? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, swali la kwanza kama unaweza kulijibu. La pili, nadhani ndiyo swali lako hasa.

**WAZIRI WA MADINI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue fursa hii kwanza kabisa kuwapongeza sana Waheshimiwa Wabunge wa Mkoa wa Njombe, wakiongozwa na Mheshimiwa Kamonga pamoja na Mheshimiwa Rebeca Nsemwa kwa kufuatilia kwa dhati kabisa juu ya maendeleo ya mradi huu wa Mchuchuma na Liganga pamoja na mradi wa Ketewaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la kwanza, kwa mujibu wa taratibu za ulipaji wa fidia; fidia pia inahusisha miundombinu ambayo ilikuwepo pale awali ikiwemo shule, zahanati na mahitaji mengine muhimu kwa ajili ya jamii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika utaratibu wa ulipaji wa fidia, mojawapo ya mambo ambayo yalizingatiwa pia ni pamoja na hayo. Ni imani yangu kwamba Waheshimiwa Wabunge wakishirikiana pamoja na halmashauri husika, pamoja na mwekezaji watahakikisha mambo hayo yote yanatekelezwa kama ambavyo yaliandaliwa pale awali ili wananchi wa maeneo husika waweze kupata huduma hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili la kuhusu leseni. Nilishatoa maelekezo kwa *RMO* wote nchi nzima kuleta leseni zote ambazo hazifanyiwi kazi na wameshaziwasilisha. Hivi sasa tupo kwenye uchambuzi. Tutafuta leseni zote ambazo hazifanyiwi kazi na wananchi watapangwa vizuri kwa ajili ya kuweza kumilikishwa. Ninakushukuru.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Tinnar Chenge, swali la nyongeza.

**MHE. TINNAR A. CHENGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru. Kwa kuwa eneo la Dutwa Wilaya ya Bariadi linafahamika kuwa na madini mengi ya aina ya *nickel*, je, lini uchimbaji wa madini haya utaanza katika eneo hili ili kuinua uchumi wa wananchi wa Dutwa?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**WAZIRI WA MADINI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli eneo la Dutwa Mkoa wa Simiyu ni eneo ambalo limebarikiwa kuwa na madini ya *nickel*. Pia pale palikuwa na leseni hodhi *(Retention License)* ambayo hivi sasa tupo katika majadiliano ya mwisho na mwekezaji kwa ajili ya kumrejeshea leseni, ili kazi ya uendelezaji wa mradi huo uanze rasmi.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, tunakushukuru kwa majibu yako kwa Waheshimiwa Wabunge.

Tunaendelea na Wizara ya Uchukuzi. Nimwite Mheshimiwa Yustina Arcadius Rahhi, Mbunge wa Viti Maalum, aulize swali lake.

Na. 391

**Ujenzi wa Uwanja wa Ndege Mwada – Manyara**

**MHE. YUSTINA A. RAHHI** aliuliza:-

Je, lini Serikali itajenga Uwanja wa Ndege Mwada Mkoani Manyara?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa David Kihenzile.

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Uchukuzi, ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Yustina Arcadius Rahhi, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imeanza zoezi la utwaaji wa ardhi katika Vijiji vya Mwada na Ngoley, vilivyopo Wilaya ya Babati, Mkoa wa Manyara kwa ajili ya kuwezesha utekelezaji wa mradi husika. Zoezi hili linafanyika kwa kuzingatia taratibu, sheria na miongozo ya nchi ili kuhakikisha haki na stahiki za wananchi zinazingatiwa ipasavyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kukamilika kwa zoezi hilo, Serikali itaanza taratibu za upatikanaji wa rasilimali fedha kwa ajili ya kuanza utekelezaji wa ujenzi wa mradi huo, kwa lengo la kuboresha huduma, kuchochea maendeleo ya kiuchumi katika eneo husika, na kuongeza mchango wa sekta husika katika uchumi wa Taifa kwa ujumla.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Yustina Rahhi.

**MHE. YUSTINA A. RAHHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru sana kwa majibu mazuri ya Serikali. Kwa umuhimu wa uwanja wa ndege Manyara, ukizingatia jiografia ya Manyara,

wafanyabiashara wa Mererani au Ngorika wakitaka huduma inabidi wapitie Kilimanjaro, Arusha na kwenda Babati, lakini kwa ajili ya uchumi wa kitalii kwa sababu tuna Tarangire pale ya madini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika bajeti iliyopita, sijaona fedha iliyoitengwa kwa ajili ya kujenga uwanja wa Manyara kwa ajili ya umuhimu huo. Sasa ni nini kauli ya Serikali kujenga Uwanja wa Ndege Manyara?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, Chama cha Ushirika cha *RIVACU* kiliwahi kutenga eneo kwa ajili ya ujenzi wa kiwanja cha ndege Mwada, lakini kwa sababu eneo lile lilibaki kwa muda mrefu, wananchi wamevamia na kuendeleza shughuli za kibinadamu. Ni upi mpango wa Serikali kuendelea kutambua maeneo haya aidha kuweka *beacon* au kuweka uzio, ili shughuli hizo za uvamizi na kuendeleza shughuli za kibinadamu zisiendelee kuwa ni adha kubwa na gharama kubwa ya kufidia?

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, na nimeona Mheshimiwa Naibu Spika tena anapiga makofi, nina hakika pia ni hoja yake hii. Nianze kujibu swali la pili kwamba ninatambua, na Serikali inatambua umuhimu wa viwanja vya ndege nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikijibu swali lake la pili, ushauri huo tunaupokea. Tutaielekeza mamlaka yetu ya viwanja vya ndege kwenda kwenye eneo husika kulitazama kwa kina na kuweka mkakati ili kuzuia uvamizi usiendelee, kwa sababu tayari Serikali ilishalitambua eneo na ilikuwa imeshaanza taratibu za awali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikirudi kwenye swali la kwanza ambalo ameuliza, ni ipi kauli ya Serikali juu ya ujenzi wa uwanja wa ndege wa Mwada Mkoani Manyara? Ninapenda kumjibu swali hili Mheshimiwa Rahhi pamoja na Wabunge wa Mkoa wa Manyara na Mbunge wa Jimbo mwenyewe ambaye ni Naibu Spika wetu na watumiaji wa uwanja kwa ujumla, kwamba Serikali

hii inayoongozwa na Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, inayo dhamira ya dhati kujenga viwanja vya ndege katika mikoa takribani yote nchini na imeshaanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa Manyara, taratibu za awali zimeshaanza ikiwa ni pamoja na kushirikiana na uongozi wa mkoa kutambua eneo. Kwa sasa, kinachofanyika na kinachoendelea kufanyika ni kutazama idadi, pengine gharama itakayoweza kutumika kulipa fidia wananchi watakaoweza kufikiwa, na namna bora ya kuweza kuliendea, hii ikiwa ni mwendelezo wa makakati wa Serikali wa kujenga viwanja mbalimbali katika nchi yetu ambao unaendelea.

**MWENYEKITI:** Ninakuona Mheshimiwa Ado.

**MHE. ADO S. ADO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza. Kwa kuwa Tunduru haina uwanja wa ndege wa Serikali kutokana na uwanja uliopo kuonekana kuwa haufai, na kwa sababu uwanja huo ambao umeonekana kuwa haufai upo katikati ya mji wa Tunduru na kuachwa kwake kumesababisha taswira mbaya sana ya mji, na kwa kuwa Halmashauri ya Wilaya ya Tunduru imeshatenga eneo katika Kijiji cha Chimbulungulu litakalotumika kwa ajili ya uwanja mpya wa ndege:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni ipi sasa kauli ya Serikali ya kukikabidhi kiwanja ambacho kiko katikati ya mji kisichotumika ili taasisi za Serikali ikiwemo Jeshi la Polisi, Jeshi la Magereza, hospitali na wananchi kwa ujumla waweze kujenga katika eneo hilo na kustawisha na kuboresha Mji wa Tunduru?

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Ado Shaibu kama ambavyo amezungumza. Ni kweli kabisa eneo analolisema ambalo kilikuwepo kiwanja cha ndege cha zamani cha Tunduru ni eneo ambalo limevamiwa, limekuwa mjini sana kwa namna

ambayo sasa matumizi yake yale ya msingi ya kuweka kiwanja cha ndege inakuwa ni changamaoto.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeshaanza mazungumzo na Halmashauri ya Wilaya ya Tunduru, na Mheshimiwa Ado ni Diwani. Tulichokubaliana sisi kama mamlaka, watutafutie eneo ambalo liko huru, limeshafanyiwa kazi tayari, na bahati nzuri eneo hilo tumeshaoneshwa na tumeridhikanalo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ombi langu na maelekezo ya Wizara kwa halmashauri husika, kupitia TAMISEMI, wakamilishe taratibu zilizobakia ikiwa ni pamoja na; kama kulikuwa na masuala ya fidia, wakishamaliza, sisi kama sekta tutakuwa tayari kuwakabidhi eneo lile la pale mjini, na tuchukue eneo lile tuanze maandalizi ya ujenzi, ili kuendeleza kasi ya Mheshimiwa Dkt. Samia ya kuwapelekea tabasamu Wanatunduru.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri tunakushukuru kwa majibu yako.

Tunaendelea na Wizara ya Maji, nimwite Mheshimiwa Asia Abdulkarim Halamga, Mbunge wa Hanang, aulize swali lake.

Na. 392

**Mradi wa Maji Bassotu**

**MHE. ASIA A. HALAMGA** aliuliza:-

Je, lini Serikali itajenga Mradi wa Maji Bassotu?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka wa fedha 2026/2027, Serikali itaanza utekelezaji wa mradi wa maji kwa kutumia chanzo cha maji cha Ziwa Bassotu kwa lengo la kunufaisha zaidi ya

wananchi 5,985 waishio kwenye vijiji viwili vya Diling'ang na Endamudayga vilivyopo Wilaya ya Hanang' mkoani Manyara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kazi zinazotarajiwa kutekelezwa kupitia mradi huo ni pamoja na ulazaji wa mabomba umbali wa kilometa 88.9, ununuzi na ufungaji wa pampu za kusukuma maji pamoja na ujenzi wa vituo 45 vya kuchotea maji ambapo utekelezaji wake unatarajiwa kuchukuwa muda wa miezi 12.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Halamga, swali la nyongeza.

**MHE. ASIA A. HALAMGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuweza kuuliza maswali madogo mawili ya nyongeza. Mradi huu wa maji wa Bassotu ni mkubwa na wa muda mrefu, na kwa sasa tunaishukuru Serikali kwa kujenga tenki la maji ambalo litakwenda kuhudumia vijiji vya Diling'ang, Dang'aida pamoja na Endamudayga na Kata ya Laghanga Kijiji cha Muungano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaiomba Serikali iharakishe ulazaji wa mabomba kwa sababu kazi kubwa imeshafanywa chini ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan ya kutujengea tenki. Tunachokihitaji sasa ni maji yatoke kwa wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali langu la pili, tunaishukuru Serikali kwa kutujengea miradi miwili mikubwa ya maji. Mradi ya maji Mogitu – Gehandu, mradi wa maji Bassotu Hang. Mradi wa maji Mogitu – Gehandu unaenda sasa *phase* ya tatu. Je, ni lini Serikali italeta fedha kukamilisha miradi hii mikubwa miwili ili tuondokane na adha ya maji kwa wananchi wa Hanang? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninampongeza sana dada yangu, Mheshimiwa Asia kwa kazi nzuri anayoifanya, na sisi Wizara ya Maji tunamshukuru sana, alienda kupokea mabomba ya mradi huu wa Mogitu – Gehandu ambao ni wa gharama ya shilingi bilioni 1.67 ambao mpaka sasa umefikia

70% ya utekelezaji wake. Tumtoe hofu, huu mradi tunaupa kipaumbele na tutaenda kuukamilisha bila ya kuwa na changamoto.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, huu mradi wa Bassotu – Hanang, una gharama ya shilingi bilioni 1.687 ambao mpaka sasa umefikia 60% ya utekelezaji wake. Katika vipaumbele vya Wizara, hii miradi tumeweka katika kipaumbele kuhakikisha kwamba tunapeleka fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, katika huu mradi, kama nilivyojibu katika jibu langu la msingi, mradi ukishakamilika, Serikali imeshajenga tanki. Baada ya kujenga tanki, kazi iliyobaki ni kusambaza mabomba. Tumtoe hofu Mheshimiwa Mbunge kwa sababu tanki limeshajengwa, halafu tusisambaze maji maana yake ni kwamba tumepoteza fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, kwa vile tumeshakamilisha tanki, kazi inayofuatia ni kuhakikisha kwamba tunaenda kusambaza mabomba ili yawafikie wananchi. Nimtoe hofu Mheshimiwa Mbunge kwamba tunaenda kumpatia fedha ili mradi huu uweze kukamilika na wananchi wapate huduma ya majisafi na salama, ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Getere, nilikuona.

**MHE. BONIPHACE M. GETERE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Naibu Waziri alikuja Jimbo la Bunda, akatazama mradi wa maji wa kutoka Butiama - Nyamuswa. Mheshimiwa Naibu Waziri alitoa sauti pale, na juzi Mwenezi wa CCM Taifa alienda pale, akasikia wananchi wanalia na mwenezi anasikitika. Nini kifanyike sasa sauti za Mawaziri zisikike wanapokuwa wanatoa amri jambo lifanyike? Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli nilifika katika mradi wa Nyamuswa na bahati nzuri kulikuwa na kazi ambayo ilikuwa imeanza kufanywa, na tulikuwa kwenye

*foundation* ya tanki, na sasa tanki limenyanyuka. Ninachofahamu ni kwamba, tulikuwa na mkandarasi ambaye alikuwa anadai malipo yake, na sasa Katibu Mkuu yupo katika hatua za mwishoni kabisa kumlipa mkandarasi ili aweze kuendelea na hatua nyingine. Ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Shabiby, nimekuona.

**MHE. AHMED M. SHABIBY:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa wakandarasi; wa Gairo wa *Kings* anadai shilingi bilioni tisa na wa Mradi wa Chagongwe anadai shilingi bilioni 21, na ameshafikia wakati wa *certificate,* je, ni lini atapewa fedha ili kuendelea na Miradi ya Maji Gairo? Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kama ambavyo tunatambua, tunayo miradi mingi ambayo inaendelea zaidi ya 1,206, lakini tunachokifanya ni kuangalia miradi ambayo inaweza kutoa matokeo kwa haraka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimtoe hofu Mheshimiwa Mbunge kwamba, tunaichukua miradi yake kwenda kufanya tathmini na tuone namna gani tunaweza tukapeleka fedha ili wakandarasi hawa waendelee kutekeleza miradi hii, na ili ikamilike kwa wakati na kutoa matokeo yanayotarajiwa, ahsante.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa tunaendelea, bado tupo Wizara ya Maji. Nimwite Mheshimiwa Mashimba Mashauri Ndaki, Mbunge wa Maswa Magharibi, aulize swali lake.

Na. 393

**Kulipwa Fedha Mkandarasi wa Maji Malampaka na Malya**

**MHE. MASHIMBA M. NDAKI** aliuliza: -

Je, lini Mkandarasi wa Mradi wa kupeleka maji Malampaka na Malya atalipwa fedha zake ili kukamilisha Mradi huu?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Maji, ninapenda kujibu swali la Mheshimiwa Mashimba Mashauri Ndaki, Mbunge wa Jimbo la Maswa Magharibi, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ina dhamira ya kuhakikisha inakamilisha utekelezaji wa miradi ya maji inayoendelea kote nchini, mijini na vijijini. Mradi wa upanuzi wa maji ya Ziwa Victoria kutoka Hungumalwa kwenda katika maeneo ya Malya Wilayani Kwimba, Mkoani Mwanza na Malampaka Wilayani Maswa, Mkoani Simiyu ni miongoni mwa miradi inayoendelea nchini na inagharimu shilingi bilioni 20.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hadi kufikia mwezi Aprili, 2026, mradi huo umefikia wastani wa 20% za utekelezaji, ambapo Serikali imefanikiwa kumlipa mkandarasi anayetekeleza mradi huo kiasi cha shilingi bilioni 3.1, kama malipo ya fedha za awali *(advance payment)*, huku akiwa anadai shilingi bilioni 2.002 kama malipo ya hati namba moja na namba mbili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali itatoa kipaumbele cha kulipa madai hayo kadiri fedha zinavyopatikana ili kuhakikisha mradi huo unakamilika ndani ya mwaka wa fedha 2026/2027 na kuanza kutoa huduma iliyokusudiwa kwa wananchi wapatao 131,000 wa maeneo ya Malampaka na Malya.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mashimba Ndaki, swali la nyongeza.

**MHE. MASHIMBA M. NDAKI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa sasa mkandarasi wa mradi huu hayupo *site* kama mwaka mzima sasa hivi, na shida yake kubwa ni kwamba amefanya kazi lakini hajalipwa fedha zake, Serikali inaonaje kumlipa fedha angalau hati moja ili aweze kurejea kwenye *site* na aweze

kuendelea na kazi kwa kuwa hata kazi aliyoanza kuifanya sasa itaharibika ikiwa atakuwa hayupo *site* kwa muda mrefu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, kuna mkandarasi pia Kata ya Zanzui na Kata ya Mwamashimba, naye anadai shilingi kama bilioni nne hivi, naye hajalipwa karibu mwaka mzima. Serikali inasemaje kuhusu kumlipa mkandarasi huyo?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa ridhaa yako nimpongeze sana Mheshimiwa Mashimba Mashauri Ndaki kwa kazi kubwa ya kuwatetea wananchi wa Maswa Magharibi hasa katika kuzingatia utekelezaji wa Ilani ya Chama cha Mapinduzi. Tunatambua kwamba huduma ya majisafi na salama ni kichocheo cha uchumi wa nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninatambua tunayo madai, na Serikali inatambua tunayo madai hayo ya mkandarasi anayetekeleza mradi huu ambao unaanzia kwenye Jimbo la Mheshimiwa Mashimba Ndaki unaenda mpaka kwa Mheshimiwa Moses Bujaga upande wa Sumve. Ni mradi mmoja wenye gharama ya shilingi bilioni 20.8, lakini pia, mradi huu mpaka sasa umeshafikia 20% za utekelezaji wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hilo, ninataka kumjulisha tu Mheshimiwa Mbunge kwamba mkandarasi huyu nilimwita hapa Dodoma, nikakaa naye kikao pamoja na wasimamizi wa mradi, *KASHWASA*. *Eng.* Zamba alikuwepo hapa, kwa pamoja tukamhusisha na Mheshimiwa Mbunge wa Sumve. Tukakaa tukakubaliana kuweka *milestone* za namna gani tutamlipa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa tuko katika hatua za mwishoni kabisa za kuhakikisha yale ambayo tulikubaliana, basi aweze kulipwa na aweze kurejea nchini, kwa sababu tunafahamu hii ni kampuni ya kigeni ambayo ni *Shanxi Construction Company*, ambaye mmiliki wake tayari alisharudi China. Sasa tumejulishwa

kwamba tayari ameshsarudi, kwa hiyo, tunaamini kwamba baada ya kumlipa ataendelea na kazi kama kawaida.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa Zanzui – Mwamashimba, huu mradi tunafahamu kwamba ni wa kimkakati katika kata za Mheshimiwa Mbunge. Sisi tunalipokea kwenda kuangalia namna bora zaidi ya kulitekeleza kwa sababu tunafahamu kwamba *ACTC*, kampuni ambayo inatekeleza mradi huo ilikuwa ina changamoto kidogo, lakini tunaendelea vizuri na mazungumzo ambayo tumefikia hatua nzuri. Tunaamini kwamba baada ya kuwa tumefikia mwafaka wa nini kifanyike, tutaenda vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna hili kidogo niliseme. Ni kweli kabisa kuna wakandarasi ambao wanadai, lakini sasa wamefikia hatua nyingine za kuwa *confiscated* na benki kiasi kwamba tunapochukua fedha tuwalipe ili waendelee na mradi, zile fedha zinaenda kupitiwa moja kwa moja na benki. Sasa zikishaondoka, maana yake anashindwa tena kurudi kwenye utekelezaji wa mradi. Ndiyo maana tunakaa chini sasa kuanza kuzungumza namna gani tufanye, kusudi tutakapomlipa, fedha hizi ziende ku-*reflect* katika mradi ambao tunatarajia akaufanye. Ninakushukuru sana.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Waheshimiwa Wabunge, wengine hamkuwepo wakati ninatoa tangazo. Tumesema kwamba tuna wachangiaji wengi sana kwenye Wizara ya Ujenzi, na wote tunataka ikiwezekana mchangie. Kwa hiyo, leo maswali ya nyongeza tumepunguza, tumerudi kwenye kanuni.

Kimsingi, kanuni inatutaka tutumie saa moja wakati wa bajeti kwa ajili ya maswali ya nyongeza. Kwa hiyo, ukiona tunaongeza kidogo muda, ni kwamba tunanajaribu kuwa-*accommodate*. Kwa hiyo, tukisema hatuwa-*accommodate* mtuelewe.

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea. Mheshimiwa Naibu Waziri tunakushukuru, bado unaendelea? Nimwite sasa Mheshimiwa Salma Rashid Kikwete, Mbunge wa Mchinga, aulize swali lake.

Na. 394

**Kukamilika kwa Mradi wa Maji – Mchinga**

**MHE. SALMA R. KIKWETE** aliuliza: -

Je, lini Serikali italeta fedha za kumaliza Mradi wa Maji Awamu ya Pili katika Jimbo la Mchinga?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Maji ninapenda kujibu swali la Mheshimiwa Salma Rashid Kikwete, Mbunge wa Jimbo la Mchinga, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imekamilisha utekelezaji wa Mradi wa Maji Mchinga awamu ya kwanza kwa gharama ya shilingi bilioni 10.52 ambapo umeanza kunufaisha zaidi ya wananchi 12,000 waishio kwenye maeneo ya *Mchinga I, Mchinga II,* Ruvu pamoja na Sinde. Miongoni mwa kazi zilizotekelezwa katika awamu hiyo ni pamoja na ujenzi wa tanki lenye ujazo wa lita 680,000, ulazaji wa mabomba umbali wa kilometa 180, sanjari na ujenzi wa vioski 20 vya kuchotea maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, awamu ya pili ya utekelezaji wa mradi huo itaanza katika mwaka wa fedha 2026/2027 ambapo itahusisha uchimbaji wa visima 10, sanjari na ulazaji wa mabomba ya usambazaji maji umbali wa kilometa 280. Kukamilika kwa awamu hiyo kunatarajia kufikisha huduma ya majisafi na salama kwa zaidi ya wananchi 55,000 wa maeneo 11 ya Majimbo ya Lindi Mjini na Mchinga.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Salma Rashid Kikwete, swali la nyongeza.

**MHE. SALMA R. KIKWETE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Mheshimiwa Naibu Waziri pamoja na Waziri, ahsante kwa

majibu mazuri sana ya Serikali. Hata kwenye dini wanasema: "*La yashkur Allah man la yashkur Nasa.*" Ninaomba shukrani zangu dhati kabisa zimfikie Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kuwatua wanawake wa Mchinga ndoo kichwani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninasema hivi, nina sababu ya msingi. Kuanzia tupate Uhuru, Jimbo la Mchinga lilikuwa halijapata majisafi na salama. Tulikuwa tunategemea maji kutoka kwenye visima. Kwa hiyo, nina sababu ya kumshukuru Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kazi kubwa na nzuri ambayo ameifanya katika Jimbo la Mchinga. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, maswali yangu mawili ya nyongeza: swali la kwanza, ninataka kujua, lini Serikali itatuongezea fedha au itatupatia fedha kwa ajili ya ukarabati wa mradi wa maji katika Tarafa ya Milola? Kwa sababu mradi huu ni wa tangu mwaka 1980 na tatizo kubwa, mabomba yameharibika na maji mengi yanapotea. Hilo ni swali langu la kwanza la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, ninataka kufahamu, katika Kijiji chetu cha Likonde, ni kijiji ambacho kina uzalishaji mkubwa wa mazao ya chakula na mazao ya biashara. Sasa, kutokana na hayo, wananchi wale hawana maji hata kidogo. Lini Serikali itatupatia kiasi cha fedha cha shilingi milioni 91 kwa ajili ya kuchimba kisima ili wananchi wale waweze kunufaika na kuondoa tatizo kwa wanawake na watoto?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Salma Rashid Kikwete, Mbunge wa Jimbo la Mchinga. Nianze kwa kumpongeza mama yangu, ninatambua nilikuja kwenye Jimbo na alinipitisha katika maeneo mbalimbali na kulikuwa na mkwamo wa baadhi ya miradi, na sasa miradi hiyo inafanya kazi vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia ninatambua pongezi zake kwa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, na kwa niaba yake,

ninazipokea, kwa niaba ya Serikali ya Awamu ya Sita kwa kazi kubwa ambayo inaendelea kufanywa kwa Falsafa ya mama ya "Kumtua Mama Ndoo Kichwani."

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika bajeti yetu ya juzi tuliyoipitisha, mkakati wa kwanza wa Serikali ni kumalizia miradi ambayo inaendelea. Mkakati wa pili, ni kuhakikisha tunaendelea kudhibiti upotevu wa maji. Upotevu wa maji ni hasara kubwa. Sasa ukiangalia katika upotevu wa maji, moja ya sababu inayosababisha upotevu wa maji ni uchakavu wa miundombinu. Kwa hiyo, kwa sababu liko ndani ya mkakati wa bajeti yetu ya fedha ya mwaka huu, nimtoe hofu Mheshimiwa Mbunge, kwenye tarafa hii ya Milola, katika miradi ambayo ilitekelezwa miaka ya 1980, ni ndani ya kipaumbele cha kuhakikisha kwamba tunadhibiti upotevu wa maji kwa kuboresha zaidi miundombinu ambayo ni chakavu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ninapenda kumwambia Mheshimiwa Salma Rashid Kikwete, tunalipokea na tutalipa uzito stahiki ili wananchi wa tarafa hii wapate huduma ya majisafi na salama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, nchi nzima tuna vijiji zaidi ya 12,318. Kijiji cha Likonde, ambacho kina eneo ambalo wakulima wanafanya shughuli zao ni sehemu ya vijiji 1,575 ambavyo vimebaki kuwa katika kipaumbele cha Serikali ambapo tutaanza na baadhi ya vijiji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda kumwambia Mheshimiwa Salma Kikwete, siyo kijiji hiki tu, tunavyo vijiji 10, na sasa tumepanga mpango wa kuanza na vijiji viwili, baada ya viwili mpaka kwa miaka mitano vijiji vyake 10 tutakuwa tumevimaliza kikiwemo Kijiji cha Likonde.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunalipokea kwa ajili ya utekelezaji kwa niaba ya Serikali, ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, tunakushukuru kwa majibu yako.

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Wizara ya Kilimo. Nimwite sasa Mheshimiwa Anton Albert Mwantona, Mbunge wa Rungwe, aulize swali lake. Kwa niaba yake swali hilo litaulizwa na Mheshimiwa Baraka Mwamengo.

Na. 395

**Kugawa Mashamba ya Chai ya Mohamed *Enterprises* kwa Wananchi-Rungwe**

**MHE. BARAKA A. U. MWAMENGO K.n.y. MHE. ANTON A. MWANTONA** aliuliza:-

Je, lini Serikali itachukua Mashamba ya Chai ya Mohamed *Enterprises* zaidi ya hekta 2,000 ambayo yamekuwa mapori na kuwagawia wananchi?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Silinde.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sasa Serikali inaendelea kufanya jitihada mbalimbali za kuhakikisha mashamba ya Mohamed *Enterprises* yaliyopo Mkoani Mbeya yaliyofungwa kutokana na sababu mbalimbali ikiwemo mashauri yaliyopo Mahakamani yanayoendelezwa ili kumhakikishia mkulima soko la majani mabichi ya chai. Jitihada hizo ni pamoja na kuiomba Kampuni hiyo kusitisha mpango wa kusimamisha uzalishaji wa chai na kuhuisha mkataba wa ununuzi wa majani mabichi ya chai kwa wakulima wadogo wa chai anaowahudumia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile, Serikali inaendelea na majadiliano na Uongozi wa Kampuni ya Mohamed *Enterprises* ili iweze kununua mashamba hayo kwa lengo la kuwagawia wakulima wadogo na viwanda kukabidhiwa kwa Vyama vya Ushirika vya zao la chai vya Wilaya za Rungwe na Mbeya. Hatua hiyo itawezesha kutatua changamoto ya upatikanaji wa soko la majani mabichi ya chai na kuongeza kipato cha wakulima.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Baraka Mwamengo, kwa niaba.

**MHE. BARAKA A. U. MWAMENGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru kwa majibu mazuri ya Serikali, lakini nina maswali mawili madogo ya nyongeza. Maeneo hayo kwa sasa ni mapori makubwa sana, ambapo wananchi wa maeneo ya Kata za Ilima, Bujela, Mpuguso na Masoko, wanaona ni mapori makubwa. Je, ni lini yatakamilika hayo mazungumzo ambayo tunaongea na mwekezaji?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, pale inapotokea kuna maeneo ambayo inafanyika shughuli kati ya wawekezaji na shughuli ya wananchi, wakati fulani inajitokeza changamoto mbalimbali hasa kipindi kama hiki ambacho tunakosa wakati fulani, minada haifanyiki kwa wakati. Mfano katika Jimbo la Kyela, mnada Na. 45, wenye kilo 200,045 haukufanyika kabisa. Nini kauli ya Serikali ili wananchi waendelee kupata matumaini ya mazao yao, na kupata soko kwa wakati? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimpongeze Mheshimiwa Baraka Mwamengo, Mbunge wa Kyela, kwa maswali mawili ya msingi. Jambo moja tu, nimhakikishie kwamba mazungumzo yanaendelea kati ya Wizara ya Kilimo pamoja na mwekezaji Mohammed *Enterprises*. Ni kweli, bado kuna baadhi ya kesi ziko Mahakamani na ndiyo ambazo unaona zimechelewesha kidogo mazungumzo, kwa sababu, sehemu ya mazungumzo ni pamoja na mwekezaji kuondoa zile kesi ambazo ziko Mahakamani ili sasa Serikali tuweze kuchukua hatua, ikiwemo kurudi sasa kwenye tathmini, na sisi kununua yale mashamba ili tuweze kuwapatia wakulima pamoja na vile viwanda tuweze kuvikabidhi kwa Vyama vya Ushirika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ninaamini tu, kwa sababu suala likiwa Mahakamani, tunaliacha kule na mchakato unakwenda vizuri, tunaamini ndani ya muda mfupi jambo hilo litakamilika na tutafuata hizi hatua ambazo sisi kama Wizara tunazisimamia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu minada ambayo imekuwa ikichelewa ikiwemo Mnada wa Kyela, ambao ulikuwa ni mnada wa Cocoa, ambao ulitakiwa ufanyike wiki iliyopita, sababu kubwa ya kutokufanyika kwa ule mnada ni kwamba masoko ya bidhaa *(TMX)* huwa wanatafuta ile bei elekezi kwa kutumia bei za soko la dunia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo sasa, wiki iliyopita ukiangalia kwenye yale masoko makubwa kama *London Stock Exchange* ambao wana-*deal* na masoko ya fedha na masoko ya bidhaa; na ukiangalia Soko la *New York* kule walikuwa na siku inayoitwa *Bank Holiday,* yaani Siku ya Benki, ambayo inakuwa ni mapumziko kwa benki, pamoja na taasisi za kifedha, ambazo zinafanya benki na taasisi za kifedha zisifanye kazi. Kwa hiyo, ile ilipelekea kutokuwa na bei elekezi ya dunia, kwa hiyo, huku ikashindikana kufanyika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mnada huo utafanyika siku hii ya leo, na jana ulifanyika kule Morogoro, na utaendelea kwa sababu ile *holiday* ambayo ilisimamisha shughuli za kifedha imekwisha.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Suma Fyandomo.

**MHE. SUMA I. FYANDOMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi niulize swali dogo la nyongeza. Kiwanda cha Chai cha *WATCO* kilichopo Katumba, Serikali iliahidi kwamba kitafunguliwa kwa mara nyingine tarehe 2 Machi, 2026, lakini mpaka sasa hivi hakijafunguliwa. Kiwanda hicho kinategemewa sana na Wananchi wa Wilaya ya Rungwe, hasa wanawake. Sasa je, nini tamko la Serikali kuhusiana na kiwanda hicho?

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninampongeza dada yangu Mheshimiwa Suma Fyandomo. Ni kweli, ile ilikuwa ni ahadi ya kwanza, na bahati nzuri Wizara tulikaa na mwekezaji wa *WATCO,* kwa maana wale pamoja na viongozi wake, ili kuhakikisha kinafunguliwa kwa wakati. Wametuahidi na

kutuhakikishia kwamba, kiwanda kile kinafunguliwa, na wananchi wale watapata hiyo huduma, ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, tunakushukuru kwa majibu yako kwa Waheshimiwa Wabunge.

Tunaendelea na Wizara ya Mifugo na Uvuvi. Ninamwita sasa Mheshimiwa Marirta Gido Kivunge, Mbunge wa Viti Maalum, aulize swali lake.

Na. 396

**Kuendeleza Maeneo ya Wafugaji Longido**

**MHE. MARIRTA G. KIVUNGE** aliuliza:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuyaendeleza maeneo ya wafugaji kwa kutenga maeneo ya malisho na kujenga au kukarabati mabwawa, kwa ajili ya mifugo?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, Dkt. Bashiru Ally.

**WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kujibu Swali Na. 396 la Mheshimiwa Marirta Gido Kivunge, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara kwa kushirikiana na Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi, inaendelea kutekeleza kazi ya kupima na kutenga maeneo kwa ajili ya malisho katika vijiji kwa kuzingatia Sheria ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi ya Vijiji, Sura 116 na Sheria ya Ardhi ya Vijiji, Sura 114.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Halmashauri ya Wilaya ya Longido, jumla ya vijiji 18 vimefanyiwa mipango ya matumizi ya ardhi na jumla ya hekta 119,063.9 zimetengwa kwa ajili ya malisho. Aidha, Wizara itaendelea kutenga fedha kwa kadiri ya bajeti itakavyoruhusu kwa ajili ya kujenga, kukarabati na

kuendeleza miundombinu yote muhimu ikiwemo uchimbaji wa mabwawa katika maeneo yaliyotengwa kwa ajili ya malisho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kutoa rai kwa Halmashauri ya Wilaya ya Longido, wafugaji na wadau wote wa Sekta ya Mifugo, kusimamia utekelezaji wa Mwongozo wa Upatikanaji, Usimamizi na Uendelezaji wa Maeneo ya Malisho kwa Mwaka 2021, unaoelekeza majukumu ya wadau wote wanaohusika katika kuendeleza ardhi iliyotengwa kwa ajili malisho katika vijiji. Ninaomba kuwasilisha.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Asenga.

**MHE. ABUBAKARI D. ASENGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru kwa majibu mazuri ya Serikali. Kutokana na changamoto ya malisho na maji kwa mifugo, kumekuwa na malalamiko makubwa sana ya wafugaji, kama ilivyokuwa Longido na Wilaya ya Kilombero. Sasa je, Mheshimiwa Waziri yuko tayari kutembelea maeneo hayo ili azungumze na wafugaji na kushirikiana nao katika njia za utatuzi wa jambo hilo?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninamshukuru Mheshimiwa Asenga kwa swali lake zuri la nyongeza. Mara baada ya kukamilisha vikao vya bajeti hii, nimepanga kuanza ziara Mkoa wa Arusha na nitaanzia Longido. Lengo langu ni kuwasikiliza wananchi, kama Mheshimiwa Rais ambavyo ametuelekeza sisi wasaidizi wake, na kujibu kero zao na hata Kilombero nitafika. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, tunakushukuru kwa majibu yako kwa Waheshimiwa Wabunge.

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Wizara ya Ujenzi. Namwita sasa Mheshimiwa Dkt. Yahya Esmail Nawanda, Mbunge wa Newala Vijijini, aulize swali lake.

Na. 397

**Taa za Barabarani Katika Mji wa Kitangari**

**MHE. DKT. YAHYA E. NAWANDA** aliuliza:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuweka taa za barabarani katika Mji wa Kitangari?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, kwa niaba yake, Mheshimiwa Naibu Waziri, *Engineer* Godfrey Kasekenya.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi, ninapenda kujibu swali la Mheshimiwa Dkt. Yahya Esmail Nawanda, Mbunge wa Newala Vijijini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imepanga kuweka taa 120 katika maeneo yaliyojengwa kwa kiwango cha lami kwenye Barabara ya Mtama – Mkwiti hadi Newala. Taa hizo zitawekwa katika Vijiji vya Mmowo, Maputa, Amkeni na Kitangari ili kuongeza usalama barabarani na kuchochea shughuli za kiuchumi, ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Dkt. Yahya Nawanda, swali la nyongeza.

**MHE. DKT. YAHYA E. NAWANDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya wananchi wa Jimbo au Majimbo ya Mtama, Newala na Newala Vijijini, tunamshukuru sana Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kutupatia hizo taa 120 katika barabara yetu ya Mtama mpaka Newala.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina swali dogo la nyongeza. Katika barabara hiyo hiyo, kumekuwa na *drift* ambayo wakati wa mvua katika Bonde letu la Mitema, barabara haipitiki kabisa. Je, ni lini sasa Serikali itajenga daraja kuondoa kero katika eneo hilo ili wananchi waweze kupita nyakati zote za masika?

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kwamba, hii barabara iko kwenye hatua za mwisho kabisa za kukamilika usanifu. Kwa hiyo, moja ni kwamba, tutalijenga hilo daraja kulingana na usanifu. Pia, ninachukua nafasi hii kumwelekeza Meneja wa Mkoa wa Mtwara, aweze kufika katika hilo Bonde la Mitema aweze kuangalia kama tayari limeshasanifiwa, aweze kuleta taarifa zake Wizarani ili tuone umuhimu wa kulijenga hilo daraja wakati tunasubiri fedha ya kuijenga barabara yote pamoja na hilo daraja, ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Lucy Mayenga.

**MHE. LUCY T. MAYENGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipatia nafasi ya kumwuliza Mheshimiwa Waziri swali dogo la nyongeza. *TANROADS* wamekuwa na utaratibu wa kuweka taa za barabarani, pia *TARURA* pia, wamekuwa na utaratibu wa kuweka taa barabarani. Sekta zote hizi mbili zimefanya *study* ya kujua *brand* ya taa ambayo hazizimikizimiki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, je, ni kwa nini Wizara hii imekuwa watu wanaweka taa kule, huko katika maeneo mbalimbali, lakini kwa *brand* ambazo zinakuwa tofauti kiasi ambacho leo unakuta kwenye wilaya hii taa zinawaka, baada ya mwaka mmoja zinazima? Kuna maeneo mengine taa zinawaka hazizimiki, kwanini kusiwe na *brand* moja nchi nzima ili kuweza kuweka taa bora ambazo zitaweza kulingana na thamani ya fedha ambazo zinatumika?

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninampongeza sana Mheshimiwa Lucy Mayenga, Mbunge wa Kishapu. Analosema ni kweli, na sisi, kama Wizara, baada ya kuona hilo, ndiyo maana tume-*centralize* sasa hivi kwamba, katika bajeti inayokuja taa zote zitakuwa zinanunuliwa baada ya kuwa zimepitishwa na zimekubalika na zitakuwa zinanunuliwa

kutoka kwa *source* moja ambazo zina ubora, ambazo hazitakuwa tofauti kati ya eneo na eneo, ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Esther Matiko, swali la nyongeza.

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninataka kujua, Serikali haioni umuhimu wa kuweka taa kwenye Mji wa Tarime, ikizingatia ni eneo ambalo liko mpakani, lenye shughuli nyingi za kiuchumi na lango la biashara kati ya Tanzania na Kenya, ili kuweza kuongeza usalama, kuchochea uchumi wa eneo lile na kuweza kuvutia wawekezaji wengi zaidi?

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Tarime ni Makao Makuu ya Wilaya, naamini tu kwamba, taa hazitoshi. Ninamhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba katika bajeti hii, maeneo mengi sana ambayo, hasa tumeweka lami, tunatamani siyo tu kwenye miji mikuu ya wilaya, lakini hata kwenye vijiji ambavyo tayari kuna lami, kuwe na TAA.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ninamhakikishia Mheshimiwa Matiko kwamba, Tarime pia itakuwepo. Kama ataweza kuonana na Meneja wa Mkoa, atamwambia taa ambazo zimepangwa kuwekwa katika Mji wa Tarime, ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Ester Bulaya, kwa kifupi sana.

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru. Barabara ya Bunda – Kisorya mpaka Nyamuswa, kuna baadhi ya maeneo yana taa kutoka Bunda mpaka Bunda Stoo. Kutoka pale Bunda Stoo – Guta mpaka kule kwa Kangi, taa hakuna. Lini sasa mtamalizia hicho kipande ili Mji wa Bunda ung’ae.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, kwa sasa sehemu zote tunazojenga barabara ya lami, na kwenye

miji yote ambayo imekuwa na hadhi ya mji, tunaweka taa. Hiyo barabara kwa kweli, imejengwa kabla, ninamhakikishia Mheshimiwa, nimesema hata kama kwenye barabara za vumbi, lakini kuna kalami, tunaweka taa. Kwa hiyo, nimwambie Mheshimiwa Ester Bulaya, maeneo hayo yatakwenda kuwekewa taa pia, ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa tunaendelea. Bado tuko Wizara ya Ujenzi. Namwita Mheshimiwa Kiza Hussein Mayeye, Mbunge wa Kigoma Kaskazini, aulize swali lake.

Na. 398

**Ujenzi wa Barabara ya Bubango – Chankele – Kagunga kwa Kiwango cha Lami**

**MHE. KIZA H. MAYEYE** aliuliza:-

Je, lini Serikali itakamilisha ujenzi wa Barabara ya Babango – Chankele – Kagunga kwa kiwango cha lami?

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda kujibu swali la Mheshimiwa Kiza Hussein Mayeye, Mbunge wa Kigoma Kaskazini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Barabara ya Bubango – Chankele – Kagunga inajulikana kwa jina la Barabara ya Mkongoro *Junction* – Chankele – Lubona – Mwangonga hadi Kagunga, ambayo ina urefu wa kilomita 65. Barabara hii ni ya wilaya, iliyokasimiwa ili ihudumiwe na *TANROADS,* Mkoa wa Kigoma. Kwa sasa, Serikali inaendelea na kazi ya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sehemu ya barabara hii kuanzia Lubona – Mwamgongo hadi Kagunga, yenye urefu wa kilomita 20, kwa ajili ya kuijenga kwa kiwango cha lami, kazi hiyo

inatarajiwa kukamilika mwezi Aprili, 2027. Mara baada ya kukamilika kwa hatua hiyo na gharama za ujenzi kujulikana, Serikali itaanza ujenzi wa barabara hiyo kwa kiwango cha lami kulingana na upatikanaji wa fedha, ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Kiza Mayeye, swali la nyongeza.

**MHE. KIZA H. MAYEYE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kuuliza maswali ya nyongeza kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, mbali na umuhimu wa barabara hii ambayo inatuunganisha mpaka Burundi, ingeweza kuchochea uchumi wa Jimbo la Kigoma Kaskazini, Kigoma na Tanzania kwa ujumla. Wananchi wa Kata ya Mwandiga, Bubango, Kagunga, Mwamgongo na Ziwani wamekuwa wanateseka sana kwa kukosa barabara iliyo imara toka tumepata uhuru. Je, Mheshimiwa Waziri yuko tayari tuambatane kwenda jimboni ili akaone adha wanayopata wananchi wa Kigoma Kaskazini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili. Ndani ya Jimbo la Kigoma Kaskazini tuna barabara muhimu ambayo ingeweza kuchochea mapato ya jimbo, Barabara ya Pasua – Mahembe – Milinzi – Kwitanga mpaka Kalinzi. Lini Serikali itaona umuhimu wa kukamilisha barabara hii kwa kiwango cha lami? Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza ninakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kwamba, barabara hii ni muhimu sana. Hii barabara haipo, ndiyo kwanza tunaifungua, ninadhani Mheshimiwa Mbunge atakubaliana nami. Ninamhakikishia Mheshimiwa Mbunge, barabara hii mimi nimefika mpaka pale mlimani ikiwa inafunguliwa. Barabara ambayo iko kwenye *terrain* moja ngumu sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan ameamua kuifungua kwa sababu, ili upite kwenye vijiji hivyo ni lazima uzunguke nchi jirani ndiyo uende kwenye vijiji ambavyo viko huko ziwani. Kwa hiyo, tunalijua na ndiyo maana

tunaifanyia usanifu, ikiwa ni pamoja na kuifungua na kuwekewa zege maeneo ambayo ina miinuko mikubwa sana. Mheshimiwa Mbunge nadhani utakuwa unajua, kwa hiyo, niko tayari tena kwenda kuiangalia tumefikia wapi na hasa kwa sababu tumeanza kuifanyia usanifu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu hiyo Barabara ya Pasua – Mahembe, tuna *budget,* bado haijasanifiwa. Kwa hiyo, tutaiweka kwenye mpango wa kuifanyia upembuzi yakinifu na usanifu ili iweze kujengwa na kurahisisha maisha ya wananchi wa Jimbo la Kigoma Kaskazini, ahsante.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa, tunaendelea na swali linalofuata. Ninamwita Mheshimiwa Zuberi Yahya Mfaume, Mbunge wa Morogoro Kusini, aulize swali lake.

Na. 399

**Ujenzi wa Barabara ya Msalabani – Tawa, Morogoro**

**MHE. ZUBERI Y. MFAUME** aliuliza:-

Je, ni lini ujenzi wa Barabara kutoka Msalabani hadi Tawa utaanza?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi, ninapenda kujibu swali la Mheshimiwa Zuberi Yahya Mfaume, Mbunge wa Morogoro Kusini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Barabara ya Msalabani hadi Tawa yenye urefu wa kilometa 10.3 ni barabara ya mkoa inayohudumiwa na *TANROADS* Mkoa wa Morogoro. Kwa sasa Serikali inaendelea kutafuta fedha kwa ajili ya kazi ya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina ili iweze kujengwa kwa kiwango cha lami. Aidha, wakati Serikali ikiendelea na mipango ya kufanya

upembuzi yakinifu na usanifu wa kina, barabara hii imeendelea kufanyiwa matengenezo mbalimbali ili iendelee kupitika majira yote ya mwaka, ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Zuberi Yahya Mfaume.

**MHE. ZUBERI Y. MFAUME:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa fursa tena ya kuuliza maswali madogo mawili ya nyongeza. Kwanza kwa dhati kabisa ninapenda kuipongeza Wizara ya Ujenzi kwa kujenga Daraja linalounganisha Kata ya Konde na Tawa, Daraja la Mto Mfisigo. Kwa sasa liko katika 60% bado 40% kukamilika, ili tuweze kuvuka. Ninamwomba sana Mheshimiwa Naibu Waziri aarakishe, ili tuweze kuvuka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la kwanza, kwa kuwa, sasa Serikali inatafuta fedha kwa ajili ya kutengeneza barabara hii kwa kiwango cha lami, kwa nini fedha hizo chache wanazozipata sasa kwa ajili ya *maintenance* wasitujengee tu yale maeneo korofi yanayosababisha hii barabara ikatike na tusiweze kupita katika kipindi cha masika, walau kwa kutuwekea vipande vya zege?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, barabara hii ndiyo inaunganisha wananchi wa kata hizi zote kuelekea katika Kituo pekee cha afya cha Tawa. *Movement* ya watu katika barabara hii imekuwepo mpaka usiku wa manane kwa ajili ya kwenda kupata huduma za afya pale. Je, Serikali ina mpango gani wa kutuwekea taa za barabarani kwa ajili ya usalama wa watu hawa wanaosafirisha wagonjwa kwenda katika hicho kituo cha afya? Ahsante.

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza ninamshukuru Mheshimiwa Mbunge kwa kutambua kazi kubwa ya Serikali, kwa ku-*respond* haraka kwenye daraja ambalo lilikuwa limekatika la Mfisigo, katika hiyo barabara ambayo amekiri kwamba tuko 60% na tutaitakamilisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, ni kweli kwamba, barabara nyingi ambazo ni za moramu, changamoto inakuwa ni maeneo machache. Tunakokwenda sasa hivi siyo tu kuzikarabati barabara, lakini kuangalia maeneo ambayo huwa ni korofi, kuweza kuyaimarisha kwa lami ama kwa zege, ili sehemu hizo ambazo zinafanya barabara isipitike tunazijenga kwa utaratibu huo. Kwa hiyo, ninamwelekeza pia Meneja wa Mkoa aweze kuipitia hiyo barabara na kuona maeneo ambayo ni korofi, yanayofanya barabara hiyo isipitike na aweze kuleta mahitaji *TANROADS* Makao Makuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suali la pili kuhusu taa za barabarani, kama nilivyojibu katika swali lililokuwa linahusu taa ni kwamba, maeneo yote ambayo ni miji mikubwa ama zimekuwa *center*, tumewaelekeza Mameneja wa mikoa waweze kuziainisha na kuziwekea taa za barabarani. Kwa hiyo, hali kadhalika Meneja wa Mkoa wa Morogoro afike katika hiyo barabara na kuona maeneo yapi yatakuwa yana sifa ya kupewa taa za barabarani, ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Festo Sanga.

**MHE. FESTO R. SANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Naibu Waziri, nimetoka Makete kukagua Barabara kutoka Makete kuelekea Mbeya kwa kiwango cha lami. Licha ya Serikali kumlipa mkandarasi, lakini hadi leo hajaingia *site* kujenga, na mvua haipo. Kwa hiyo, sababu ya mvua, haipo; na mkandarasi hajafika *site*. Yapi maelekezo ya Serikali kwa mkandarasi kurejea kwenye eneo hili ili aweze kujenga barabara yenye maslahi kwa wananchi wa Makete.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninampongeza Mheshimiwa Sanga kwa kufuatilia huo mradi, na ni kweli huo mradi mkandarasi ameshalipwa fedha, ninadhani nitakuwa natoa maelekezo mara ya pili kwa sababu tulishatoa maelekezo kwamba mvua imeshakatika, mkandarasi huyu arudi *site*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa, nina uhakika Meneja ananisikia, pia na Mtendaji Mkuu wa *TANROADS* ananisikia, Makete ni moja ya maeneo ambayo yana muda mfupi sana wa jua. Kwa hiyo, katika kipindi ambacho ni jua, aanze kazi mara moja kwa sababu Serikali imeshamlipa fedha. Ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa tumalizie na Mheshimiwa Agnesta Lambert.

**MHE. AGNESTA L. KAIZA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kuniona. Barabara ya kutoka Kinyerezi - Bonyokwa kwenda Kimara inasuasua sana japokuwa mkandarasi yuko *site* sasa. Kutokana na kusuasua, nyumba nyingi za wananchi zinabomoka, fensi zinabomoka, na Mheshimiwa Naibu Waziri nilishamfikishia taarifa kumweleza jambo hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa kufahamu, nini kauli ya Serikali ambayo itatekelezwa kwa 100% kuhusiana na barabara hii ya Kinyerezi - Bonyokwa kwenda Kimara?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, bahati nzuri hii barabara inaunganisha Jimbo la Segerea na Jimbo la Ubungo. Ninataka nimhakikishe Mheshimiwa Mbunge kwamba mkandarasi huyu ambaye pia ni mzawa wa Nyanza, ameshalipwa fedha ili aweze kuendelea na kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nimwelekeze Meneja wa Mkoa wa Dar es Salaam kwamba kwa kuwa shughuli za barabara za Dar es Salaam mvua imepungua, alikuwa anafanya zaidi kwenye hizi *structure,* sasa arudi kurekebisha barabara ili barabara hiyo iweze kupitika, na pia kutengeneza *diversion* ili wananchi wa Majimbo haya mawili wasikwame, ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri tunakushukuru kwa majibu yako kwa Waheshimiwa Wabunge.

Waheshimiwa Wabunge, tumefika mwisho wa kipindi chetu cha maswali, na kama mnavyoona tumeokoa dakika chache pale. Tunao wachangiaji wengi sana leo.

Nianze na wageni waliopo ndani ya Ukumbi wa Bunge Asubuhi hii. Tunao wageni wa Mheshimiwa Spika. Hawa ni wageni sita wa Mheshimiwa Spika kutoka Jijini Dar es Salaam, nimtaje Mheshimiwa John Mrema, huyu ni Naibu Meya wa Jiji la Dar es Salaam, karibu sana. *(Makofi)*

Tunaye Ndugu Elihuruma Mabelya, ni Mkurugenzi wa Jiji, karibu sana. *(Makofi)*

Yopo Ndugu Haji Manara, ni Diwani wa Kata ya Kariakoo na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Mpango Miji na Mazingira, karibu sana. Naona wana Yanga wanakushangilia. *(Makofi)*

Tunaye Ndugu Saady Khimji, huyu ni Diwani wa Kata ya Ilala na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Uchumi na Huduma za Jamii. *(Makofi)*

Mwingine ni Mheshimiwa Tumike Malilo, huyu ni Diwani wa Kata ya Bonyokwa Ilala. *(Makofi)*

Tunao wageni wengine 54 wa Mheshimiwa Spika, hawa ni Madiwani na viongozi mbalimbali kutoka Jijini Dar es Salaam na Jimbo la Ilala. Watakuwa wamekaa kwenye ukumbi wetu mkubwa, nadhani wanatuona. *(Makofi)*

Tunao wageni waliokaa Jukwaa la Spika, hawa ni wageni wa Mheshimiwa Abdallah Hamis Ulega, Mbunge, na Waziri wa Ujenzi. Nao ni kama ifuatavyo: Tunaye Balozi Mhandisi Aisha Amour, Katibu Mkuu Ujenzi; Dkt. Charles Msonde, Naibu Katibu Mkuu Ujenzi; Mhandisi Amini Mcharo, Mwenyekiti wa Bodi Wakala wa Barabara *TANROADS;* na Dkt. Laurian Ndumbaro, Mwenyekiti wa Bodi ya Wakala wa Majengo Tanzania *TBA*. *(Makofi)*

Wengine ni Dkt. Elisante Ulomi, Makamu Mwenyekiti wa Baraza la Taifa la Ujenzi *NCC; CPA* Vincent Minja, Makamu

Mwenyekiti wa Bodi ya Mfuko wa Barabara *(RFP);* Mhandisi Prof. Bakari Mwinyiwiwa, yeye ni Mwenyekiti wa Bodi ya Usajili wa Wahandisi *(ERB)*; na Dkt. Gemma Garimo, Makamu Mwenyekiti wa Bodi ya Taasisi ya Teknolojia ya Ujenzi (ICoT). *(Makofi)*

Wengine ni Mhandisi Mohamed Besta, Mkurugenzi Mkuu Bodi ya Wakala wa Barabara *TANROADS*; Mhandisi Kheri Mahimbari, Mtendaji Mkuu Wakala wa Ufundi na Umeme TEMESA; na Mhandisi Daudi Kandoro, Mtendaji Mkuu Wakala wa Majengo Tanzania *(TBA)*. *(Makofi)*

Wengine ni Mhandisi Rashid Kalimbaga, Mtendaji Mkuu Mfuko wa Barabara; Mhandisi Bernard Kavishe, Msajili wa Bodi ya Usajili wa Wahandisi *ERB;* Mhandisi Rhoben Nkori, Msajili wa Bodi ya Usajili wa Wakandarasi; Mhandisi Daniel Matondo, Kaimu Msajili, Bodi ya Usajili na Wabunifu wa Majengo na Wakadiriaji Majengo *(EQRB)*; Ndugu Rehema Salim, Meneja Uhusiano wa Kampuni ya *Bakheresa Group. (Makofi)*

Tunao wageni wengine wa Mheshimiwa Ulega, hawa ni familia yake kutoka Mkuranga Mkoani Pwani. Tunaye Alhaj Hamis Ulega, yeye ni Baba wa Mheshimiwa Waziri, yuko pale. *(Makofi)*

Yupo Ndugu Nusura Ali, yeye ni mama wa Mheshimiwa Waziri, karibu sana. *(Makofi)*

Tunaye Ndugu Asha Abdallah, yeye ni Dada wa Mheshimiwa Waziri, karibu sana. *(Makofi)*

Pia tunaye Ndugu Maya Hamis, yeye ni Dada wa Mheshimiwa Waziri. *(Makofi)*

Tunao wageni wengine wa Mheshimiwa Ulega, hawa ni Viongozi wa CCM na Watendaji wa Mkoa wa Pwani wakiongozwa na Ndugu Mwishehe Shabani, Mwenyekiti wa CCM wa Mkoa wa Pwani; tunaye Ndugu David Mramba, Mwenezi wa CCM Mkoa wa Pwani; Ndugu Juma Magahila, Mwenyekiti wa CCM Wilaya ya Mkuranga; na Ndugu Shaban Hassan, Mwenyekiti wa CCM wa Wilaya ya Mafia. *(Makofi)*

Vilevile tunaye Ndugu Juma Ndaruke, Mwenyekiti wa CCM Wilaya ya Kibiti; Mheshimiwa Khadija Nassir, Mkuu wa Wilaya ya Mkuranga; Ndugu Omari Mwanga, Katibu Tawala Wilaya ya Mkuranga; na Ndugu Waziri Kombo, Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya Mkuranga. *(Makofi)*

Wageni wengine wa Mheshimiwa Ulega, Mbunge na Waziri wetu wa Ujenzi, ni Kamati ya Siasa ya Wilaya ya Mkuranga na Mkoa wa Pwani. Watakuwa wanatuona kutoka ukumbi mkuu. Tunao Madiwani wa Halmashauri ya Wilaya ya Mkuranga wakiongozwa na Ndugu Ali Mohamed Dau, na wao wanatuona kutokea kule.

Wageni wengine wa Mheshimiwa Ulega ni viongozi wa dini ambao ni Sheikh Hamis Mtupa, Sheikh wa Mkoa wa Pwani; Sheikh Hamas Mzee, Sheikh wa Wilaya ya Mkuranga; Sheikh Ismail Kilwanda, Mwenyekiti wa BAKWATA Wilaya ya Mkuranga; Ndugu Mohamed Mwinchumu, Katibu wa BAKWATA wa Wilaya ya Mkuranga; na Ndugu Fatma Ali, mke wa Sheikh wa Wilaya ya Mkuranga.

Vilevile, tunaye Mchungaji John Msei wa Kanisa la Anglikana Wilaya ya Mkuranga; Ndugu Kaunda Ibrahim, Mchungaji wa Kanisa la KKKT Wilaya ya Mkuranga; na Mchungaji Beda Stephano, wa Kanisa la *Life Bridge Pentecost* Tanzania la Wilaya ya Mkuranga. Wote kwa ujumla wao tunawakaribisha sana kwenye Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. *(Makofi)*

Wapo wageni wa Waheshimiwa Wabunge. Tunao wageni wa Mheshimiwa Cosmas Mtesigwa Bulala, huyu ni Ndugu Ivon Mwamanda, ni mpigakura wake kutoka Kwimba, Mkoa wa Mwanza. *(Makofi)*

Tunao wageni wa Mheshimiwa Enock Zadock Koola, hawa ni Ndugu Hamisi Sakapala kutoka Jijini Dodoma. *(Makofi)*

Wengine ni wageni 29 wa Mheshimiwa John Francisco Nzilanyingi, hawa ni Madiwani kutoka Nyamagoro Mkoani Mwanza. *(Makofi)*

Wapo wageni wawili wa Mheshimiwa Abdallah Jafari Chaurembo, hawa ni ndugu zake kutoka Temeke, Dar es Salaam. *(Makofi)*

Tunao wageni sita wa Mheshimiwa Neema Gerald Mwandabila, hawa ni wanafunzi na Wajumbe wa Seneti ya Mkoa wa Dodoma. *(Makofi)*

Wapo wageni 26 wa Mheshimiwa Edward Olelekaita Kisau, ni wafanyabiashara kutoka Kiteto Mkoa wa Manyara. *(Makofi)*

Tunao wageni waliotembelea Bunge kwa ajili ya mafunzo. Pia wapo wageni 130 na walimu watano kutoka Shule ya Sekondari wa Wavulana Tengeru Jijini Arusha. *(Makofi)*

Pia, tunao wakuu wa shule 38 na viongozi wa Idara ya Elimu Msingi Wanawake kutoka Halmashauri ya Manispaa ya Morogoro. Hawa wote wanatuona kutoka kwenye ukumbi mkuu. Tunawakaribisha sana Bungeni. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tunayo matangazo mengine mawili. Moja mnakumbushwa kwamba Mbio za Wakili Marathon 2026 zenye kauli mbiu: "Kusogeza Huduma za Msaada wa Kisheria Karibu Zaidi na Mtanzania", bado unaendelea kwenye viwanja vyetu vya Bunge. Mbio zinatarajiwa kufanyika siku ya Jumapili tarehe 31 Mei, 2026 Jijini Dodoma. Waheshimiwa Wabunge, mnaombwa na mnahimizwa kushiriki kwenye mbio hizo.

Tangazo la mwisho kwa muda huu, Waheshimiwa Wabunge na Watumishi wa Bunge mnataarifiwa kuwa siku ya Ijumaa tarehe 22 Mei, 2026 saa 12.30 asubuhi kwenye Uwanja wa Jamhuri Dodoma kutakuwa na mechi ya mpira wa miguu na mpira wa pete kati ya Waheshimiwa Wabunge na Watumishi wa Bunge. Wote mnakaribishwa kuja kuiona timu yenu ya *Bunge Sports Club* ambayo ipo kwenye maandalizi ya michezo ya Mabunge ya Afrika Mashariki *(EALAC)*.

Waheshimiwa Wabunge, haya ndiyo matangazo kwa muda huu. Katibu.

**NDG. ASIA MINJA– KATIBU MEZANI:**

**HOJA ZA SERIKALI**

**Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Ujenzi kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027**

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na ajenda ya hoja za Serikali. Nimwite sasa Waziri wa Ujenzi Mheshimiwa Alhaj Ulega aweze kutoa hotuba yake.

**WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti ... *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, hotuba imesubiriwa kwa hamu sana hiyo, naomba uanze. *(Kicheko/Makofi)*

**WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kutoa hoja kwamba kufuatia taarifa iliyowasilishwa hapa Bungeni na Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu iliyochambua utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya Ujenzi ya mwaka wa fedha 2025/2026, Bunge lako Tukufu sasa likubali kupokea na kujadili utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya Wizara ya Ujenzi kwa mwaka wa fedha 2025/2026. Aidha, ninaliomba Bunge lako Tukufu liridhie na kupitisha Mpango na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Fedha ya Wizara ya Ujenzi kwa mwaka wa fedha 2026/2027.

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, ninapenda kutumia fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu, Mwingi wa Rehema kwa kuijalia nchi yetu amani na utulivu na kutuwezesha kushiriki katika vikao hivi vya Bunge kwa ajili ya kujadili Bajeti ya Wizara ya Ujenzi leo. Kipekee kabisa, ninapenda kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania pamoja na Mheshimiwa Balozi Dkt. Emmanuel John Nchimbi,

Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa kuaminiwa na Watanzania kuiongoza nchi yetu. Hii inadhihirishwa na ushindi wa kishindo walioupata katika uchaguzi mkuu uliofanyika Oktoba, 2025.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninawaombea kwa Mwenyezi Mungu aendelee kuwapa hekima, maarifa na afya njema wanapoendelea kuliongoza Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitoe pongezi za dhati kwa Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, kwa kuchaguliwa kwa mara nyingine kuiongoza Serikali ya Mapinduzi Zanzibar. Ninamwombea afya njema na mafanikio katika uongozi wake ili aendelee kudumisha muungano wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitumie fursa hii pia kutoa pongezi zangu za dhati kwa Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba, Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuaminiwa na Mheshimiwa Rais kushika wadhifa huu muhimu wa uongozi katika Taifa letu. Uteuzi huu unadhihirisha imani kubwa aliyonayo Mheshimiwa Rais katika uzoefu, uwezo na uzalendo wake katika uongozi wa nchi yetu. Ninamwahidi Mheshimiwa Waziri Mkuu kuwa Wizara ya Ujenzi itaendelea kupokea miongozo na kutekeleza maelekezo ya kuimarisha utendaji wa majukumu yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba pia nikupongeze wewe binafsi, Mheshimiwa Spika wa Bunge letu, na Mheshimiwa Naibu Spika kwa kuchaguliwa kwa kishindo kuliongoza Bunge hili la Kumi na Tatu la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Ninawapongeza pia Wenyeviti wengine wote wa Bunge kwa kuchaguliwa na tunawaahidi ushirikiano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, ninawapongeza Waheshimiwa Wabunge wote kwa kuchaguliwa kuingia katika Bunge hili Tukufu. Wizara ya Ujenzi inaahidi kutoa ushirikiano muda wote, na milango ipo wazi kupokea maoni na ushauri ili kuhakikisha miundombinu tunayoitekeleza na kuisimamia nchi

nzima inaendelea kuwa imara, endelevu na yenye kuleta tabasamu kwa wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitumie nafasi hii kumshukuru Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuendelea kuniamini na kuniteua kuwa Waziri wa Ujenzi kwa kipindi kingine tena. Ninaomba kumwahidi Mheshimiwa Rais kuwa, nitatekeleza majukumu haya kwa weledi na uadilifu ili kufikia malengo yaliyokusudiwa kupitia miongozo na mipango mbalimbali ikiwemo dira ya mwaka 2050 na Ilani ya Chama cha Mapinduzi ya 2025.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda kuishukuru Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu inayoongozwa na Mwenyekiti Mheshimiwa Selemani Moshi Kakoso Mbunge na Makamu Mwenyekiti, Mheshimiwa Abubakar Damian Asenga, Mbunge kwa kuchambua kwa kina mpango na bajeti ya Wizara kwa mwaka wa fedha 2026/2027 na kutoa ushauri ambao umezingatiwa katika bajeti hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa masikitiko makubwa, nitumie fursa hii kutoa salamu za pole kwa Bunge lako Tukufu, Chama cha Mapinduzi, wananchi, marafiki na familia kufuatia vifo vya Waheshimiwa Wabunge wenzetu, Mheshimiwa Jenista Joachim Mhagama aliyekuwa Mbunge wa Jimbo la Peramiho, Mheshimiwa William Vangimembe Lukuvi, aliyekuwa Mbunge wa Jimbo la Isimani na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Bunge, Uratibu na Wenye Ulemavu; na Mheshimiwa Halima Idi Nasoro aliyekuwa Mbunge wa Viti Maalum, Wafanyakazi. Tutaendelea kuwaenzi viongozi hawa kwa kuendeleza yale yote mema waliyotenda hususan katika uongozi wao. Tunamwomba Mwenyezi Mungu awapumzishe kwa amani. Amina.

Mheshimiwa Mwenyekiti, saa chache kabla sijaingia kusoma hotuba hii nimepokea simu kutoka kwa Bibi wa Kisukuma aitwaye Helen Mbogoe, mwenye umri wa miaka 70 kutoka Kisesa, Magu, kule Mwanza amenipigia akinipa shukrani kwa Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluh Hassan kwamba kwa miaka mingi safari ya kuvuka Kigongo - Busisi ilichukua saa kadhaa. Leo hii kaniambia

tangu kukamilika kwa Daraja la Magufuli, unakunywa soda na kabla hujaimaliza umeshavuka kwenda upande wa pili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, haya ndiyo maono ya Rais, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwamba wakati tunapojenga barabara, madaraja na vivuko, lengo letu siyo kuongeza tu idadi ya kilomita, tunajenga ili kuunganisha wakulima na masoko, tunajenga ili wagonjwa wafike hospitalini, tunajenga ili wanafunzi wa shule wafike shuleni kwa wakati, vijana wapate ajira na kuiunganisha Tanzania kiuchumi katika ukanda wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maelezo hayo ya utangulizi, ninaomba sasa nitoe taarifa ya mapitio ya utekelezaji wa mpango na bajeti ya Wizara ya Ujenzi kwa mwaka wa fedha 2025/2026 pamoja na Mpango na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka wa fedha 2026/2027.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara imeendelea kutekeleza bajeti iliyoidhinishwa na Bunge lako Tukufu kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026 ambayo ilizingatia mpango mkakati wa Wizara, mipango mingine ya Kitaifa na Maelekezo ya Viongozi Wakuu wa Kitaifa. Utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya Wizara kwa mwaka wa fedha 2025/2026 ni kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara ya Ujenzi ilitengewa shilingi 90,468,270,000 ikiwa ni bajeti ya matumizi ya kawaida kwa mwaka wa fedha 2025/2026. Kati ya fedha hizo shilingi 85,028,585,000 ilikuwa ni bajeti ya mishahara na shilingi 5,439,685,000 ni kwa ajili ya matumizi mengineyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hadi Aprili, 2026 Wizara ilipokea jumla ya shilingi 73,604,735,181.30. Kati ya fedha hizo, shilingi 70,533,041,808.41 ni kwa ajili ya mishahara ya watumishi wa Wizara na taasisi, na shilingi 3,071,693,372.89 ni kwa ajili ya matumizi mengineyo ya Wizara na taasisi zake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bajeti kwa ajili ya miradi ya maendeleo iliyotengwa kwa Wizara ya Ujenzi kwa mwaka wa fedha 2025/2026 ni shilingi 1,813,190,934,000. Kati ya fedha hizo,

shilingi 1,209,223,117,000 ni fedha za ndani, na shilingi 603,967,817,000 ni fedha za nje. Kati ya fedha hizo za ndani, shilingi 688,756,470,000 ni fedha zilizotengwa kwa ajili ya bajeti ya Mfuko wa Barabara, na shilingi 520,466,647,000 ni fedha kutoka katika Mfuko Mkuu wa Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, fedha zilizopokelewa kufikia Aprili, 2026 ni 1,395,658,301,112.09, ambapo kati ya fedha hizo shilingi 786,102,916,695.88 ni fedha za ndani, na shilingi 609,555,384,416.21 ni fedha za nje. Kati ya fedha hizo za ndani, zilizopokelewa, shilingi bilioni 461,173,316,123.56 ni kutoka Mfuko Mkuu wa Serikali na shilingi 324,929,600,572.32 ni za Mfuko wa Barabara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sekta ya ujenzi ni mtambuka na imeendelea kutoa mchango mkubwa katika kuchochea ukuaji wa sekta mbalimbali za kiuchumi na kijamii. Kwa mujibu wa Kitabu cha Hali ya Uchumi wa Taifa cha Mwaka 2024, sekta ya ujenzi imekuwa ni ya pili katika kuchangia kwenye pato la Taifa *(GDP)*, ambapo katika mwaka 2025 imechangia kwa 11.9%.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, sekta hii imeendelea kukua kwa kasi ambapo katika mwaka 2025 sekta ilikua kwa asilimia nne ikilinganishwa na asilimia tatu mwaka 2024. Vilevile sekta ya ujenzi imetoa mchango mkubwa katika kutoa ajira kwa wakandarasi, washauri elekezi, mafundi na wasambazaji wa vifaa, malighafi za ujenzi, ambapo imetoa jumla ya ajira 18,988 kwa mwaka 2025 ikijumuisha vijana na wanawake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mafanikio hayo yametokana na uwekezaji mkubwa unaoendelea kufanywa na Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mtandao wa barabara za Kitaifa unaosimamiwa na Wizara ya Ujenzi kupitia *TANROADS* una jumla ya kilometa 37,734.41. Kati ya hizo kilometa 12,225.26 zimejengwa kwa kiwango cha lami.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati nchi hii inapata uhuru mwaka 1961, mtandao wa barabara za kiwango cha lami ulikuwa na urefu wa kilometa zisizozidi 1,360 tu. Kuanzia Awamu ya Kwanza hadi Awamu ya Tano jumla ya kilometa 9,369.1 zilijengwa. Serikali ya Awamu ya Sita chini ya uongozi thabiti wa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, imefanikiwa kujenga kilometa 1,495.45 na madaraja makubwa 18 ndani ya kipindi cha miaka mitano. Kwa hakika haya ni mafanikio makubwa yaliyopatikana ndani ya muda mfupi kwa upande wa miundombinu ya barabara na madaraja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sote tunakubaliana kwamba kati ya miundombinu yote ya usafiri na usafirishaji, barabara ndicho kiungo muhimu kinachounganisha miundombinu hiyo. Aidha, barabara ndiyo miundombinu inayotumika zaidi nchini kwa kuwa zinafika katika maeneo mengi ikilinganishwa na miundombinu mingine ya usafiri na usafirishaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kutambua umuhimu huo wa barabara katika kipindi cha Julai, 2025 hadi Aprili, 2026 Serikali ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania imefanikiwa ujenzi kwa kiwango cha lami barabara za Kitaifa zinazosimamiwa na *TANROADS* zenye urefu wa kilometa 243.13.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, katika kipindi hicho, Serikali imefanikiwa kukamilisha ujenzi wa madaraja makubwa tisa, ujenzi wa madaraja madogo 11, madaraja mengine 11 unaendelea pamoja na maandalizi ya ujenzi wa madaraja 13. Utekelezaji wa miradi hii umefungua maeneo mbalimbali ya kiuchumi pamoja na kuchangia ufanisi wa miundombinu mingine ya usafiri na usafirishaji ikiwemo reli, bandari na viwanja vya ndege.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utekelezaji wa miradi ya miundombinu ya barabara na madaraja unatumia gharama kubwa na hivyo uwekezaji unahitaji kulindwa. Katika kipindi cha Julai, 2025 hadi Aprili, 2026 Serikali imefanya matengenezo ya kawaida ya barabara zenye urefu wa kilometa 16,782.58,

matengenezo ya muda maalum kilometa 111.12, matengenezo ya sehemu korofi kilometa 147.13, na madaraja 1,383. Lengo ni kuhakikisha kuwa miundombinu inayojengwa inadumu kwa muda mrefu na kuwa salama kwa watumiaji muda wote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mvua za El Nino na Kimbunga Hidaya kilichoikumba nchi yetu mwishoni mwa mwaka 2023 zilisababisha mafuriko ambayo yaliathiri mtandao wa barabara hasa zilizojengwa kwa kiwango cha changarawe. Kwa mujibu wa tathmini ziliofanyika ya uharibifu wa miundombinu iliyotokana na majanga hayo, takribani madaraja 63, kilometa 827 za barabara, mitaro yenye urefu wa jumla ya kilometa 84 na makaravati 225 katika wilaya 139 za Tanzania Bara ziliharibika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara zilizokumbwa na uharibifu mkubwa ni pamoja na Barabara ya Dar es Salaam hadi Lindi. Hali hii iliathiri mtiririko wa kibajeti ambao ulitarajiwa kwenda kwenye matengenezo au ujenzi wa barabara kutumika katika shughuli za dharura.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda kumshukuru tena kwa mara nyingine Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa uamuzi wake wa kuipatia Wizara ya Ujenzi shilingi bilioni 556.93 ili kurejesha miundombinu iliyoharibiwa na mafuriko na mvua kubwa nchi nzima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kupitia fedha hizo, jumla ya miradi 81 ya dharura ya ujenzi wa madaraja yaliyoathiriwa na mvua za El Nino na Kimbunga Hidaya imetekelezwa katika mikoa 22 ya Tanzania Bara kupitia programu ya *CERC*. Kati ya miradi hiyo miradi 70 yenye thamani ya shilingi bilioni 414.481 imetekelezwa na wakandarasi wa ndani na miradi 11 yenye thamani ya shilingi bilioni 142.447 imetekelezwa na wakandarasi wa kigeni. Aidha, utekelezaji wa miradi hii umefikia 97.6%. Utelekelezaji wa miradi hiyo umetatua changamoto zilizokuwepo na kuleta tabasamu kwa wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, haya niliyoyasema siyo maneno yangu, bali ni ushuhuda kutoka kwa wananchi katika maeneo

husika ambao wanashangilia baada ya utekelezaji wa miradi hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mara ya kwanza baada ya miaka mingi, pamoja na mvua kubwa za masika zinazoendelea kunyesha nchini, hatujasikia wananchi wakiwa wamekwama Somanga, wananchi wakiwa wamekwama Mbwemkuru, wananchi wakiwa wamekwama Matandu na wala Mikelengende pale njia nne kwa sababu ya barabara ya Kilwa kutokupitika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo hili halijatokea hivi hivi. Limetokea kwa sababu ya uamuzi wa kimkakati wa Jemedari, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kutenga fedha hii kwa sababu ya kuwanusuru wananchi hawa wa barabara hii ya kimkakati na nyingine nyingi zilizokuwa zimeharibika wakati wa mvua za masika na msimu ule wa El Nino.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuhakikisha wananchi wanaoishi maeneo yaliyotengwa na maji wanapata huduma bora ya usafiri na usafirishaji, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ameendelea kufanya uwekezaji mkubwa katika ujenzi, ukarabati na ujenzi wa maegesho ya vivuko katika maeneo hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara ya Ujenzi kupitia *TEMESA* imefanikiwa kukamilisha miradi ya ujenzi wa vivuko vitakavyotoa huduma katika maeneo ya Kisorya kule Bunda kwenda Rugezi Ukerewe, Bwiro hadi Bukondo kule Ukerewe pamoja na ujenzi wa maegesho ya vivuko katika vituo vya Bwiro hadi Bukondo, Kisorya - Rugezi na Bukimwi kule Ukerewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, ujenzi wa vivuko vipya vinne umefikia katika hatua zifuatavyo: Kivuko cha Ijinga kwenda Kihangala Sengerema 90%, ujenzi wa kivuko cha Nyakaliro kwenda kome kule Geita 91%. Ujenzi wa Kivuko cha Buyagu Mbalika Sengerema umefikia 90%, na ujenzi wa Kivuko cha Nyamisati pale Rufiji kwenda Mafia 65%.

Mheshimiwa Mwenyekiti, miradi mingine ni ujenzi wa maegesho ya Mayenzi - Kanyinya 98%. Ujenzi wa Ijinga - Kahangala 90%, Buyagu kwenda Mbalika 68%, Ilunda kwenda Luchelele - Ilemela 45% na kule Mlimba kwenda Malinyi 40%, Chato kwenda Kikumba - Itale - Zumacheli 95% na Nkome asilimia 60.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa miradi ya kimkakati wa vivuko, Serikali ya Awamu ya Sita chini ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania imefanikiwa kufanya ukarabati mkubwa wa vivuko vifuatavyo: *MV Kilombero Two* tuko 90%, *MV Nyerere* 81%, *MV Magogoni* 90%, *MV Ukara One* 46%, *MV Kigamboni* 45%, *MV Pangani Two* 58%, na ukarabati wa vivuko *MV Mafanikio, MV Malagarasi, MV Ukara Two* na *MV Sabasaba* upo katika hatua za awali za kuanza utekelezaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, ukarabati wa vivuko *MV Mwanza* pamoja na boti ya uokoaji vipo katika hatua ya manunuzi. Utekelezaji wa miradi ya vivuko umeonyeshwa kuanzia aya ya 122 hadi aya ya 127 katika kitabu cha hotuba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kukabiliana na uhaba wa makazi bora unaochochewa na ongezeko la watu, Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, imeendelea kuhakikisha wananchi wanapata makazi bora salama na kwa gharama nafuu. Katika kufanikisha hilo, Wizara ya Ujenzi kupitia *TBA* imeendelea kutekeleza miradi ya nyumba za makazi katika maeneo mbalimbali nchini ikiwa ni pamoja na Nzuguni Dodoma, Magomeni, Temeke na Masaki Jijini Dar es Salaam na Ghana Jijini Mwanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utekelezaji wa miradi ya ujenzi na ukarabati wa nyumba na majengo ya Serikali umeonyeshwa kuanzia aya ya 128 hadi aya ya 132 katika kitabu cha hotuba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kufuatia ongezeko la matukio ya ajali za barabarani nchini yanayosababisha vifo, majeruhi wengi

na upotevu wa mali, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ameendelea kutoa msisitizo kwa taasisi mbalimbali za Serikali kuongeza juhudi za kukabiliana na janga la ajali barabarani nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kufuatia maelekezo hayo, Serikali kupitia Wizara ya Ujenzi kwa kushirikiana na Serikali ya *Japan* kupitia *JICA* imefanikiwa kutekeleza mradi wa ushirikiano wa kitaalamu kati ya Serikali hizi mbili wenye lengo la kuimarisha usalama barabarani na kupunguza vifo pamoja na majeruhi wanaosababishwa na ajali hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuimarisha masuala ya usalama barabarani, Wizara inaendelea kutambua na kurekebisha maeneo yenye ajali nyingi *(black sports)*, upanuzi wa barabara katika maeneo mbalimbali nchini, kuweka taa za barabarani, ambapo jumla ya taa 5,542 zimewekwa katika barabara kuu na za mikoa. Vilevile, ujenzi wa njia za magari makubwa katika maeneo yenye miinuko mikali *(climbing lens)*, kuweka alama na michoro ya usalama barabarani, ujenzi wa maeneo ya maegesho ya magari pamoja na kuweka kingo za barabara katika maeneo hatarishi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili la taa za barabarani tumelivalia njuga kwa uhakika. Ninakumbuka simulizi moja ambayo niliipata kwa watani zangu wa Kisukuma, ambapo kwa mara ya kwanza mara baada ya taa zile za barabarani kufungwa kule Kigongo Busisi katika Daraja la John Pombe Joseph Magufuli, kuna Msukuma mmoja alilala nje ya nyumba yake akidhani usiku haujaingia bado. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatua hizi ni kielelezo dhahiri cha namna Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inayoendelea kuweka kipaumbele katika kuimarisha usalama wa watumiaji wa barabara zetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na malengo ya kupunguza ajali, Wizara inaendelea na majukumu ya udhibiti wa

uzito wa magari kupitia mizani 83 ili kulinda uwekezaji wa Serikali katika mtandao wa barabara. Hadi Aprili, 2026 jumla ya magari 7,900,591 yalikuwa yamepimwa, ambapo kati ya hayo magari 18,343 sawa na asilimia sifuri nukta mbili tatu yalikuwa yamezidisha uzito. Zaidi ya asilimia tano ya uzito unaoruhusiwa kisheria ikilinganishwa na asilimia sifuri nukta mbili saba katika kipindi kama hicho mwaka wa fedha 2024/2025.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utekelezaji wa miradi ya udhibiti wa uzito wa magari, masuala ya usalama barabarani na mazingira umeonyeshwa kuanzia aya ya 133 hadi ya 141 katika kitabu cha hotuba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara kupitia *TANROADS* inasimamia ujenzi, ukarabati, upanuzi na uboreshaji wa jumla ya viwanja vya ndege 10 nchini, ambavyo vimekasimiwa kwa Wizara ya Ujenzi. Mojawapo ya miradi ya viwanja vya ndege inayotekelezwa na Wizara ni ujenzi wa Kiwanja cha Ndege cha Kimataifa cha Msalato, ikiwa ni utekelezaji wa maono ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, wa kukifanya Kiwanja hicho kuwa kitovu cha usafiri na usafirishaji katika ukanda wa kati na wa Kimataifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utekelezaji wa *package* ya kwanza ya mradi huu inahusisha ujenzi wa miundombinu, ambao umefikia 85.17%. Kufuatia kuongezwa kwa mawanda ya mradi na *package* namba mbili inayohusisha ujenzi wa majengo, umefikia 71.52%.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utekelezaji wa miradi mingine ya viwanja vya ndege ni kama ifuatavyo:-

(i) Ujenzi wa Kiwanja cha Ndege cha Tabora, kazi zilizopangwa kufanyika zimekamilika;
(ii) Ujenzi wa Kiwanja cha Ndege cha Kigoma, umefikia 50.16%;
(iii) Kiwanja cha Ndege cha Sumbawanga, 96%;
(iv) Kiwanja cha Ndege cha Shinyanga, 96.5%;
(v) Kiwanja cha Ndege cha Musoma, 67%;

(vi) Kiwanja cha Ndege cha Iringa awamu ya pili, 16%;
(vii) Kiwanja cha Ndege cha Tanga tupo katika hatua ya awali, ambayo ni asilimia mbili nukta moja; na
(viii) Kiwanja cha Ndege cha *Lake Manyara* kazi zake zipo katika hatua ya maandalizi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utekelezaji wa miradi ya ujenzi wa miundombinu ya viwanja vya ndege, umeoneshwa katika aya ya 142 hadi 152 katika kitabu cha hotuba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara ya Ujenzi ina jumla ya taasisi tisa inazozisimamia na utekelezaji wa majukumu yake chini ya Wizara ya Ujenzi. Maelezo ya kina kuhusu utekelezaji wa majukumu ya taasisi hizo hadi kufikia Aprili, 2026 umeoneshwa katika kitabu cha hotuba kuanzia aya ya 154 hadi 189.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara katika utekelezaji wa majukumu yake ya kila siku, imekuwa ikiyajumuisha masuala mtambuka ili kuwezesha kuleta tija na ufanisi katika sekta ya ujenzi. Masuala hayo ni pamoja na ushirikishwaji wa wanawake katika kazi za barabara, matumizi ya teknolojia katika ujenzi, na matengenezo ya barabara ikiwemo teknolojia stahiki ya nguvukazi *(labour-based technologies)*, na ushirikishwaji wa sekta binafsi katika miradi ya ujenzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa usimamizi wa hifadhi ya barabara, Wizara imehuisha kanuni mbili kwa lengo la kuwezesha matumizi na usimamizi endelevu wa hifadhi ya barabara. Aidha, Wizara imetunga kanuni za usimamizi na uendeshaji wa maegesho katika hifadhi za barabara za Kitaifa za mwaka 2025, na kutangazwa kupitia tangazo la Serikali Namba 432 la tarehe 11/7/2025.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile, kupitia Bodi ya Mfuko wa Barabara, Wizara imekamilisha uundwaji wa mfumo wa kielektroniki kwa ajili ya kurahisisha ukusanyaji wa mapato yatokanayo na maegesho ya barabara zetu. Maelezo kuhusu masuala mtambuka yameoneshwa kwenye aya ya 190 hadi 199 katika kitabu cha hotuba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mpango na Bajeti ya Wizara ya Ujenzi kwa mwaka wa fedha 2026/2027 umezingatia mipango ya muda mrefu na kati ya Kitaifa ikiwemo Dira ya Maendeleo 2050, Mpango wa Nne wa Maendeleo wa Taifa wa miaka mitano na Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya Mwaka 2025. Aidha, bajeti imezingatia Mpango Mkakati wa Wizara wa 2026/2027 hadi 2030/2031, Ahadi za Viongozi Wakuu wa Serikali na Mwongozo wa Maandalizi ya Mpango wa Bajeti ya Serikali kwa mwaka wa fedha 2026/2027.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Bajeti ya mwaka 2026/2027 ni bajeti ya kipekee kwa kuwa ndiyo ya kwanza katika utekelezaji wa maono yaliyopo katika Dira ya Taifa ya Maendeleo 2050. Aidha, bajeti hii ni ya kwanza katika kutekeleza Ilani ya Uchaguzi ya CCM 2025 - 2030, pamoja na Mpango wa Nne wa Taifa wa Maendeleo wa Miaka Mitano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kupitia hotuba yangu hii ya bajeti, ninapenda kujibu swali moja kubwa la msingi kwamba ni kwa nini Serikali inafanya uwekezaji mkubwa kwenye ujenzi wa barabara, madaraja, na vivuko?

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi katika Wizara ya Ujenzi tumetambua kwa yakini kwamba kama awamu nyingine zilizopita, Serikali ya Awamu ya Sita inalo jukumu la kipekee la kuliunganisha Taifa letu na hata Mataifa jirani, kama walivyofanya waliotangulia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Awamu ya Kwanza ilijenga nchi, Awamu ya Pili ilifungua milango ya uchumi, Awamu ya Tatu ilisimika misingi ya uchumi wa soko huria, Awamu ya Nne iliongeza kasi ya ujenzi wa miundombinu, Awamu ya Tano ilijenga nidhamu ya utekelezaji, na kazi kubwa ya wakati wetu, ni kuifungua Tanzania kwenye eneo la miundombinu, na kuhakikisha hakuna jamii inayoachwa nyuma kwa sababu ya ubovu wa barabara, madaraja na vivuko. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika dunia ya sasa ya ushindani wa kiuchumi ambayo nguzo yake kubwa ni miundombinu imara,

hatutaweza kushindana kama barabara zetu hazipitiki, na bidhaa maana yake zitachelewa kufika sokoni kwa wakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama ilivyoainishwa kwenye Dira ya 2050, sekta ya ujenzi ni muhimu katika kuwezesha usafirishaji fungamanishi pamoja na kuleta mageuzi katika sekta nyingine. Aidha, kama ilivyotafsiriwa katika Dira 2050, mafanikio ya Dira hii hususan ujenzi wa miundombinu yanategemea ushirikiano thabiti kati ya wadau mbalimbali ikiwemo sekta binafsi, kupitia utaratibu wa ubia kati ya sekta ya umma na sekta binafsi, yaani *PPP*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utekelezaji huo wa miradi ya ujenzi unahitaji fedha nyingi ili kukabiliana na changamoto hizo. Mwelekeo wa Serikali ya Awamu ya Sita chini ya Rais, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, ni kuongeza ushiriki wa wadau, hususan sekta binafsi katika utekelezaji wa miradi ya ujenzi kwa njia ya *PPP*. Lengo ni kupunguza utegemezi wa ugharimiaji wa miradi ya ujenzi kwa kutumia fedha za Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2026/2027, Wizara ya Ujenzi imepanga kutekeleza miradi ya ujenzi wa barabara, majengo, uendeshaji wa vivuko pamoja na karakana kwa maana ya gereji zilizo chini ya *TEMESA*, ikiwemo miradi itakayotekelezwa kwa utaratibu wa *PPP*. Hivyo basi, sekta binafsi, taasisi za kifedha, na wawekezaji wa ndani na nje ya nchi yetu tunawakaribisha kuwekeza katika ujenzi na uendeshaji wa miradi hii kwa njia ya *PPP*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kutekeleza maono ya Dira 2050 na Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano pamoja na Mpango wa Maendeleo wa mwaka 2026/2027, Wizara ya Ujenzi imejipanga kukamilisha kwanza miradi inayoendelea na iliyosainiwa kabla ya kuanza utekelezaji wa miradi mipya. Aidha, vipaumbele vya bajeti katika mwaka wa fedha 2026/2027 ni katika maeneo mahususi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi na wenzangu tulikuwa tunawaza ili bajeti hii tuipende, neno gani la kuitambulisha kwa urahisi? Jibu rahisi ni kwamba, hii ni bajeti ya kuifungua nchi yetu.

Tutatumia rasilimali zetu, tulizonazo kuhakikisha kwamba ujenzi unafanyika katika namna ambayo hakuna watu watakaoachwa nyuma kimaendeleo kwa sababu ya jiografia, foleni na ukosefu wa ubunifu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2026/2027, Wizara ya Ujenzi imepanga kuendelea na utekelezaji wa miradi ya kupunguza msongamano katika majiji ya Dar es Salaam, Arusha, Mwanza, Mbeya, Dodoma na miji mingine nchini. Lengo ni kuboresha mfumo wa usafiri mijini, kuongeza tija ya kiuchumi na kuinua ubora wa maisha ya wananchi, utekelezaji wa miradi katika maeneo hayo ni kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Jiji la Dar es Salaam na mji jirani wa Pwani, miradi inayoendelea kutekelezwa kwa ajili ya kupunguza msongamano wa magari katika jiji la Dar es Salaam, itahusisha ujenzi wa barabara na *flyovers* katika maeneo ya makutano mbalimbali ya barabara. Miradi hiyo ni kama ifuatavyo:-

(i) Ujenzi wa barabara za mabasi yaendayo haraka awamu ya tatu, kutoka Maktaba mpaka Gongo la Mboto;

(ii) Ujenzi wa barabara za mabasi yaendayo haraka awamu ya nne, kutoka Maktaba hadi Morocco - Mwenge, Tegeta - Mwenge na Ubungo;

(iii) Maandalizi ya kuanza ujenzi wa barabara za mabasi yaendayo haraka awamu ya tano, kutoka Ubungo mpaka Bandarini, (barabara hii maarufu kama barabara ya Mandela) ambayo kwa hakika, ni barabara iliyozidiwa sana na foleni;

(iv) Makutano ya Tabata na Tabata Segerea, Tabata mpaka Kigogo, na ujenzi wa *flyover* ya Tabata;

(v) Ujenzi wa *flyovers* mbili katika makutano ya Mwenge na Morocco ambapo Wizara ya Ujenzi tupo katika majadiliano ya hatua ya mwisho na *JICA* ya kuweza kufadhili utekelezaji wa mradi huu;

(vi) Tunakamilisha upanuzi wa barabara ya Ubungo hadi Kimara kutoka njia sita na sasa inakwenda kuwa njia nane;

(vii) Upanuzi wa barabara ya Mbagala - Kongowe hadi Mkuranga, kilometa 17.14, kutoka njia mbili zilizoko leo hadi njia nne, pamoja na daraja la Mzinga;

(viii) Upanuzi wa barabara ya Mwai Kibaki, kilometa 11.77 (kutoka Morocco kupita *Shoppers,* kwa Mwalimu Nyerere, mpaka njia panda ya Kawe, kilometa 11.77) kutoka barabara mbili zilizoko leo na kwenda kuwa njia nne. Ninaomba nirejee kidogo hapa. Kongowe, tunajenga *flyover*. Watu wanaotoka Mtwara kuja Dar es Salaam, hawakutani na watu wanaotoka Kigamboni kuja Dar es Salaam, pale tuna kitu kinaitwa *flyover*. Mama Samia hoyee; *(Makofi)*

(ix) Upanuzi wa barabara ya Kibaha - *TAMCO,* kutoka njia mbili hadi njia nane; na

(x) Ujenzi wa *flyover* kutoka eneo la Faya, Magomeni na Kamata.

Mheshimiwa Mwenyekiti, miradi inayoendelea kutekelezwa kwa ajili ya kupunguza msongamano wa magari katika Jiji la Dodoma ni kama ifuatavyo:-

(i) Ujenzi wa barabara ya mzunguko wa nje kilometa 112 katika Jiji la Dodoma ambao upo katika hatua za mwisho kukamilika;

(ii) Upanuzi wa Barabara ya Dodoma - Morogoro kilometa 70, sehemu ya Kimbinyiko, hapa *roundabout* ya Kimbinyiko hadi Chamwino kilometa 32 tunaitoa kuwa barabara mbili na sasa inakwenda kuwa barabara sita. Tatu, zinakwenda na tatu zinarudi ambapo mkataba wa ujenzi umesainiwa juzi tarehe 16 Mei, 2026. Tumpe nini Mama Samia kama siyo dua na baraka njema?

(iii) Upanuzi wa barabara za Dodoma mpaka Iringa, kilomita 50 awamu ya kwanza ni kutoka *roundabout* ya Bahi

mpaka Mkonze, yaani pale *SGR Station* barabara mbili zinakwenda na mbili zinarejea, msongamano umekwisha;

(iv) Upanuzi wa barabara kutoka *roundabout* ya *Bahi Road* kwenda Kondoa, hii itakuwa ni kilomita 50 ambako hatua ya kwanza tutakwenda mpaka njia panda ya Msalato pale Mipango kilometa 10 kutoka njia mbili na kuwa njia nne, mbili zinakwenda mbili zinarudi, ili uwanja wetu utakapokuwa umekamilika usipate msongamano;

(v) Ujenzi na upanuzi wa barabara ya mzunguko wa ndani katika Jiji la Dodoma. Tutatoka tena *Bahi Road*, tutapitia *Image roundabout*, tutakuja Ntyuka *roundabout*, tutatokea Makulu, kwa njia nne ambayo itakwenda kuungana na ile barabara ya kwenda *Shoppers*, hii na yenyewe itakuwa nne, yaani mbili zinakwenda mbili zinarudi ambazo zitajengwa kwa fedha za washirika wa maendeleo kutoka Serikali ya Japan ambapo mkataba wa ujenzi tayari tumesha-*sign* na tayari tunakwenda kumpa mkandarasi kazi, mara moja inaanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kupunguza msongamano katika Jiji la Arusha:-

(i) Upanuzi wa barabara ya Arusha, Kisongo kutoka njia mbili na kuwa njia nne ambapo mkataba tumesha-*sign* na mkandarasi tumeshampata;

(ii) Ujenzi wa barabara ya Mbauda - Losinyai, ambapo ujenzi unaendelea;

(iii) Upanuzi wa barabara ya Tengeru - Usa-*River* kilometa 11.3 kutoka njia mbili na kwenda kuwa njia nne, inaungana na ile ya Afrika ya Mashariki. Barabara hii tupo katika hatua ya mwisho ya ununuzi; na

(iv) Ujenzi wa barabara ya Tengeru - Mererani kilomita 28, ambapo usanifu umekamilika na tuko tayari kwa ajili ya kutangaza kazi hii tupate mara moja mkandarasi aweze kujenga

barabara hii ambayo itatusaidia pia katika mkakati wetu wa *AFCON* mwakani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mradi wa upanuzi kutoka njia mbili hadi nne wa barabara ya Mwanza - Usagara kilometa 25 ambapo taratibu za manunuzi ya mkandarasi zinaendelea. Pia, mkandarasi wa ujenzi wa barabara ya Mwanza *Airport* - Kayenze hii inakwenda mpaka Magu. Tuko katika hatua za maandalizi ya kuanza kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Jiji la Mbeya, miji ya Iringa, Songwe na Singida. Miradi inayoendelea kutekelezwa kwa ajili ya kupunguza msongamano wa magari katika Jiji la Mbeya, ni pamoja na upanuzi wa barabara sehemu ya Nsalaga – Uyole - Ifisi kilometa 29 ambapo ujenzi unaendelea, na kuendelea na maandalizi ya ujenzi wa barabara ya mchepuko ya Uyole hadi Songwe kilometa 48.9.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, mkandarasi wa upanuzi wa barabara ya Igawa - Tunduma kilometa 218 anaendelea na maandalizi ya kuanza na utaratibu wa *PPP*. Vilevile, katika Mji wa Iringa, ujenzi wa kiwango cha lami wa barabara ya mchepuo wa Iringa kilometa 7.3 unaendelea na kwa mkoa wa Singida Wizara inaendelea na maandalizi ya upanuzi wa barabara ya Singida mjini kilometa 10 kutoka njia mbili hadi kuwa njia nne.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utakubaliana na mimi kwamba sasa hivi Tanzania inapendeza kuliko wakati mwingine. Katika historia ya nchi yetu, ziko picha ukiona Watanzania wamepiga kwenye barabara na madaraja yetu unaweza ukadhani uko nje ya nchi tena Dubai na wala siyo hapa Tanzania. Kwa hakika kazi kubwa sana imefanywa na Serikali ya CCM katika awamu zake zote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, miongoni mwa mikakati ya Wizara ni kuendelea na ujenzi wa barabara zinazounganisha makao makuu ya mikoa, nchi jirani na barabara zinazoelekea katika makao makuu maeneo ya kimkakati kwa kiwango cha lami. Wizara inaendelea kuunganisha mikoa ya Mbeya na Singida,

Mbeya na Tabora, Rukwa na Katavi, Kigoma na Katavi, Arusha na Simiyu, pamoja na Morogoro na Ruvuma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, Wizara inaendelea na ujenzi wa barabara zinazounganisha nchi jirani, ikiwemo barabara ya Tanga – Pangani - Makurunge kilometa 174.5, pamoja na Daraja la Pangani mita 525, inayounganisha Tanzania na Kenya. Ujenzi wa barabara ya kikanda ya Manyovu – Kasulu - Kabingo kilometa 260.6, inayounganisha Tanzania na Burundi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kuna Ujenzi wa Barabara ya Kibondo - Mabamba kilometa 50, inayounganisha Tanzania na Burundi. Ukarabati wa barabara ya Lusahunga - Rusumo kilometa 92, inayounganisha Tanzania, Rwanda na Burundi pamoja na Matai - Kasesya kilometa 50 inayounganisha Tanzania na Zambia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile, Wizara inaendelea na ujenzi wa barabara zinazoelekea katika maeneo ya kimkakati yanayojumuisha bandari, reli, viwanja vya ndege, viwanda, kilimo, migodi, utalii, kongani za viwanda *(EPZ)*, miji mikuu, na ulinzi wa mipaka yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uwekezaji mkubwa uliotokana na maono ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, katika bandari zetu hususan Bandari ya Dar es Salaam umesababisha ongezeko la mizigo inayosafirishwa ndani na nje ya nchi yetu kupitia barabara. Ufanisi huu wa bandari unakumbana na changamoto kadhaa, zikiwemo msongamano pamoja na uchakavu wa miundombinu ya barabara unaohitaji fedha nyingi za kuziboresha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania tayari ametoa maelekezo kwetu ya kutafuta fedha na njia mbadala ya kugharimia miradi ya maendeleo, ukizingatia kwamba mahitaji ni makubwa kama nilivyotamka awali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuzingatia maelekezo hayo, Wizara ya Ujenzi inatarajia kuanza matumizi ya hatifungani katika

bajeti hii kwenye kugharamia matengenezo makubwa na ukarabati wa barabara kuu za kiuchumi ambazo ni Morogoro hadi Dodoma, Dodoma hadi Singida, Singida hadi Tabora, Tabora hadi Shinyanga, Shinyanga hadi Mwanza, Dar es Salaam hadi Kibiti, Kibiti mpaka Lindi Mingoyo, Sirali mpaka Musoma, Musoma mpaka Mwanza, Geita mpaka Bukoba Bukoba mpaka Mutukula, Chalinze mpaka Segera, Segera mpaka Tanga, Tanga mpaka Moshi na hadi Arusha, Babati hadi Singida, Dar es Salaam mpaka Morogoro, Iringa, Makambako na Mbeya mpaka Tunduma. Kutoka njia mbili na kwenda kuwa ni njia nne. Kazi hiyo itafanywa kupitia hati fungani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuendeleza jitihada za kuimarisha miundombinu ya usafiri na usafirishaji majini na kuchochea Uchumi wa Buluu, Serikali imedhamiria kukamilisha ununuzi wa vivuko vipya vitano Kanda ya Ziwa pamoja na uboreshaji wa usafiri Ukanda wa Pwani ambapo kukamilika kwa kivuko kipya cha Nyamisati hadi Mafia kutahakikisha uwepo wa kivuko cha pili cha uhakika kwa safari za kila siku huku kivuko kitakachohudumia Boza, Kuruti, Shungubweni na Kisiju kule Mkuranga kikilenga kutoa huduma rahisi na salama kwa wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inafanya jitihada mbalimbali kuhakikisha wakandarasi wazawa wanashiriki ipasavyo katika shughuli za ujenzi. Jitihada hizo ni pamoja na kutoa mafunzo kwa wakandarasi yanayolenga kukuza ujuzi na wakandarasi katika maeneo ya kiufundi na usimamizi wa miradi, kuendesha mfuko wa kusaidia wakandarasi *(contractors assistance fund)* unaolenga kusaidia wakandarasi wazawa kupata dhamana za kibenki kwa ajili ya zabuni na malipo ya awali, kuhamasisha wakandarasi nguvu kupitia ubia *(joint venture)* na kuendelea kutenga miradi ya kuwajengea uwezo wakandarasi washauri elekezi wazawa kama Sheria ya Ununuzi wa Umma Sura Na. 410 na Kanuni zake zinavyoelekeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara inatambua mchango wa vijana wetu wasomi katika suala zima la ubunifu na maendeleo ya kiteknolojia wa Taifa letu. Februari mwaka huu Wizara ilizindua

chemsha bongo ya foleni *challenge* iliyokuwa na lengo la kuwafanya wanafunzi wa fani ya uhandisi kuumiza vichwa kutafuta suluhu ya changamoto ya foleni mijini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika shindano hilo, mwanafunzi wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Tukay Thomas aliibuka mshindi kwa wazo lake. Zaidi ya washiriki 500 wa ndani na nje ya nchi yetu walijitokeza na Serikali imeongeza katika mipango yake maarifa ya wahandisi watarajiwa hawa zaidi ya 500 kupitia changamoto hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baadhi ya watu waliuponda mpango huu wakati tulipoibuka na wazo hilo. Hata hivyo, tumetiwa nguvu sana na majibu, uzalendo na mapokeo ya vijana wetu kupitia shindano hilo. Wizara yetu na Serikali ya Rais, Mheshimiwa Dkt. Samia itaendelea kusikiliza, itaendelea kuheshimu Mawazo ya vijana wote nchini wenye lengo la kusaidia Taifa letu na kamwe milango yetu haitafungika kwa vijana wa Taifa hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara ya Ujenzi kupitia Wakala wa Majengo Tanzania itaendelea na usimamizi wa miliki ya Serikali ili kutoa makazi bora kwa ajili ya viongozi na watumishi wa umma. Aidha, katika kutekeleza maono ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambayo ni kutoa makazi bora ya gharama nafuu kwa vijana na umma wa Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara imejipanga kukamilisha mradi wa ujenzi wa nyumba za gharama nafuu 144 katika eneo la Temeke Jijini Dar es Salaam na kuanza utekelezaji wa mradi wa nyumba 144 za gharama nafuu utakaotekelezwa hapa Dodoma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, ili kuwezesha Wakala wa Majengo Tanzania kujitegemea na kupunguza utegemezi wake kwa ruzuku ya Serikali, Wizara ya Ujenzi itaendelea kukaribisha sekta binafsi ili kufanya ubia na Serikali kupitia *TBA* kuwekeza katika miradi ya ujenzi na uendeshaji wa nyumba za majengo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, Wizara kupitia *TBA* ipo katika hatua za mwisho za kusaini mkataba wa uendelezaji wa ubia yaani *PPP* katika eneo la Temeke Kota Jijini Dar es Salaam. Vilevile, Wakala umeainisha maeneo 149 mikoa yote nchini Tanzania Bara kwa ajili ya kuyaendeleza kwa njia ya ubia.

Mheshimiwa Mwenyekiti na Waheshimiwa Wabunge, pale Dar es Salaam Magomeni ni eneo ambalo *TBA* imeliandaa kwa ajili ya *PPP*. Masaki tuna eneo kubwa tumeliandaa kwa ajili ya *PPP*. Tunawakaribisha wadau wote karibuni kujenga nasi nyumba za kupangisha kwa ajili ya Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2026/2027 Wizara ya Ujenzi imetengewa shilingi 97,104,935,000 ikiwa ni bajeti ya matumizi ya kawaida. Kati ya fedha hizo, shilingi 92,209,218,000 ni bajeti ya mishahara, na shilingi 4,895,717,000 ni kwa ajili ya matumizi mengineyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bajeti ya maendeleo ya Wizara ya Ujenzi, ni shilingi 2,467,336,476,000. Kati ya fedha hizo, shilingi 1,544,872,147,000 ni fedha za ndani na shilingi 922,464,332,000 ni fedha za nje. Kati ya fedha hizo za ndani, shilingi 1,047,405,500,000 ni fedha zilizotengwa kwa ajili ya fedha za Mfuko wa Barabara, na fedha kutoka katika Mfuko Mkuu wa Serikali ni shilingi 497,466,647,000.

Mheshimiwa Mwenyekiti, miradi itakayotekelezwa na shughuli zake kwa mwaka wa fedha 2026/2027 imeainishwa kuanzia aya ya 219 hadi 361. Aidha, mgawanyo wa fedha za maendeleo pamoja na miradi iliyotengewa fedha ni pamoja na kama ilivyoainishwa katika kiambatanisho namba moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapohitimisha hotuba yangu, ninapenda kwa dhati kabisa kuwashukuru viongozi wenzangu ambao ni Mheshimiwa Mhandisi Godfrey Msongwe Kasekenya, Mbunge wa Ileje, Naibu Waziri, Balozi Mhandisi Aisha Salim Amour, Katibu Mkuu, pamoja na Dr. Charles Enock Msonde, Naibu Katibu Mkuu kwa ushirikiano wanaonipa katika kutekeleza majukumu yangu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, ninaishukuru *management* ya Wizara, Wakuu wa Taasisi zilizo chini ya Wizara na Watumishi wote wa Wizara na taasisi zake kwa kujituma na kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi na kujitolea kwa lengo la kuifanya sekta ya ujenzi izidi kukua na kuimarika na kutoa mchango mkubwa katika maendeleo ya nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa namna ya kipekee kabisa nitumie nafasi hii adhimu kuwashukuru wananchi wa Jimbo langu la Mkuranga kwa kunikubali, kuniamini na kunichagua kwa mara nyingine tena ili kuwawakilisha katika Bunge hili Tukufu kwa kipindi kingine cha miaka mitano. Maneno ninayoweza kuwaambia Wanamkuranga ni machache tu, kwamba, mimi Abdallah sitawaangusha, na ninawapenda sana ndugu zangu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaishukuru pia familia yangu ikiongozwa na mke wangu mpenzi, Mheshimiwa Mariam Abdallah Ibrahim. Ninawashukuru pia watoto wangu kwa kuendelea kuniombea na kunifariji katika utendaji wa majukumu yangu, ahsanteni sana na Mwenyezi Mungu azidi kuwabariki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara inapata ushirikiano mkubwa kutoka kwa wadau mbalimbali wa maendeleo wa ndani na nje. Nitumie fursa hii kuwatambua na kuwashukuru wafuatao: Benki ya Maendeleo ya Afrika *(AFDB)*, Benki ya Dunia, Shirika la Maendeleo la Japan *(JICA)*, *OPEC*, Korea Kusini *(KOICA)*, Abu Dhabi *Fund*, Shirika la Maendeleo la Ufaransa *(AFD)*, Jumuia ya Nchi za Ulaya *(EU)*, Benki ya Uwekezaji ya Ulaya *(EIB)*, Kuwait *Fund*, Barrick, Sekretarieti ya Jumuiya ya Afrika Mashariki, Sekretari ya Jumuiya ya Nchi za Kusini mwa Afrika, Japan, China, Norway na *NSSF*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hawa *NSSF* ndiyo tutakaokwenda kujenga nao barabara nzuri kabisa kutoka Kibaha mpaka Chalinze, na tayari wameonesha nia ya kuendelea hata kutoka Chalinze kwenda Morogoro.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wadau wengine ni taasisi za fedha za *CRDB, NMB, NBC*, Azania *Bank*, *TCB* na asasi mbalimbali

zisizokuwa za kiserikali, sekta binafsi, wanahabari pamoja na wadau wengine wengi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hitimisho. Kwa kutambua umuhimu wa miundombinu katika kuchochea na kuharakisha maendeleo ya kiuchumi na kijamii katika Taifa letu mwaka 2026/2027, Wizara ya Ujenzi itaendelea kuchukua hatua madhubuti za kusimamia, kuimarisha na kuendeleza sekta ya ujenzi. Lengo ni kuhakikisha sekta hii inatoa mchango wa kutosha katika maendeleo ya Taifa na ustawi wa wananchi kama inavyotarajiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninafahamu kwamba katika mvua hizi za masika mwaka huu kuna barabara nyingi zimeharibika na zinahitaji matengenezo. Nimepata salamu za Wabunge wote walioko katika Bunge hili za kuhitaji matengenezo na ukarabati wa barabara zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tulikuwa tunasubiri wakati wa mvua uishe. Ninaomba kuwaahidi Waheshimiwa Wabunge ya kwamba muda siyo mrefu kutoka sasa wataanza kuona makatapila, mafundi na wataalamu wakiwa kwenye maeneo tofauti tofauti wakirekebisha barabara na kuendelea na ujenzi uliokuwa umeanza nchi nzima. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kwa namna ya kipekee nimshukuru sana Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwani ni jana tu Waziri wa Fedha ameniidhinishia fedha za awali shilingi bilioni 20 za kazi hii ya kurekebisha miundombinu iliyoharibika kwa mvua. Fedha hizi zimeshaingia, na haraka zitaenda kuanza kazi. Mtatuona mimi na Mheshimiwa Msongwe Kasekenya na Balozi Aisha na wataalamu wengine wote tumeenea nchi nzima. Hakuna barabara itakayoachwa bila ya kurekebishwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, historia ya Mataifa makubwa duniani inaonesha jambo moja; hakuna maendeleo bila ya miundombinu. Tanzania ya leo inaamua kutokubali tena umbali kuwa kikwazo cha maendeleo. Tutajenga barabara, madaraja

na viwanja vya ndege, lakini zaidi ya yote, tunajenga Taifa lenye kujiamini kuhusu kesho yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara itaweka mkazo mkubwa katika kupunguza msongamano wa magari katika miji na majiji hususan katika barabara za mchepuo, madaraja ya juu pamoja na upanuzi wa barabara zilizopo ili kukidhi mahitaji yatokanayo na ongezeko la watumiaji wa barabara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, Wizara itaendelea kuchukua hatua za haraka kurejesha na kujenga upya miundombinu ya barabara na madaraja iliyoharibiwa na mafuriko pamoja na athari nyingine za mabadiliko ya tabianchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile, jitihada zitaelekezwa katika kuimarisha ubora wa miradi ya ujenzi kwa kusimamia viwango na kutumia teknolojia za kisasa ili miundombinu inayojengwa iwe imara salama na yenye kudumu kwa muda mrefu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hatua nyingine, Wizara inaendelea na maandalizi ya mpango kabambe wa usafiri wa haraka *(Tanzania Express Master Plan)* katika barabara kuu. Mpango huu unatekelezwa kwa kushirikiana na shirika la ushirikiano wa Kimataifa la Korea *(KOICA)*. Lengo ni kuwa na ramani na mwongozo wa kimkakati wa maendeleo ya barabara za haraka nchini. Kazi hii inatarajiwa kukamilika Novemba, 2028.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hatua hizo, Serikali inaendelea na utekelezaji wa miradi ya *expressway* inayohusisha mradi wa Kibaha – Chalinze - Morogoro kilometa 163 ambao upo katika taratibu za ununuzi wa kumpata mwekezaji kama nilivyotangulia kusema, *NSSF* wameonyesha nia ya kufanya kazi hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, taratibu za maandalizi ya kuanza upembuzi yakinifu wa awali, tunao mpango wa kufanya *expressway* ya *airport* yetu ambapo itaunganisha Nyerere *Road,* Mandela *Road* na Sam Nujoma kuelekea Uwanja wa Kimataifa wa Nyerere.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuhakikisha ubora wa miundombinu na kuwezesha miradi kukamilika kwa wakati, Wizara itaendelea kuchukua hatua stahiki kwa wakandarasi na washauri elekezi wanaokiuka masharti ya kimkataba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hadi sasa Wizara imechukua hatua madhubuti kwa wakandarasi wa miradi kadhaa akiwemo kuna mkandarasi wa ibanda Kajunjumele, na Sengerema Nyehunge ambao mikataba yao ilisitishwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, wakandarasi wa miradi ya mabasi yaendayo haraka awamu ya nne pale Dar es Salaam Mwenge - Tegeta tumempa onyo na barabara ya Tungamaa - Mkange tulimpa onyo pia kutokana na kutokutimiza masharti ya kimkataba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hatua hizo, ninazielekeza taasisi zilizo chini ya Wizara ya Ujenzi kusimamia miradi kwa ufanisi ili kuhakikisha thamani ya fedha inapatikana kwenye miradi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hayo, Wizara inakusudia kuanza mchakato wa kuziboresha taasisi zake yaani *TANROADS, TEMESA* na *TBA*. Kwa kuanzia, Wizara katika mwaka huu wa fedha tumekusudia kuifanya *TANROADS* kuwa ni mamlaka kamili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatua hii inakusudia kuongeza uwezo wa Wakala katika kusimamia majukumu yake kwa tija, uwajibikaji na ufanisi unaoendana na kasi ya utendaji ya Mheshimiwa Rais, Dr. Samia Suluhu Hassan.

Mheshimiwa Mwenyekiti, muhtasari wa maombi ya fedha. Katika mwaka wa fedha 2026/2027 Wizara inaliomba Bunge lako Tukufu kuidhinisha jumla ya fedha shilingi 2,564,441,414,000 kwa ajili ya matumizi ya kawaida na matumizi ya miradi ya maendeleo. Katika fedha hizo shilingi 97,104,935,000 ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida ya Wizara na taasisi zake. Shilingi

2,467,336,479,000 ni kwa ajili ya miradi ya maendeleo. Kati ya fedha hizo, matumizi ya kawaida, shilingi 92,209,218,000 ni za mishahara, na shilingi 4,895,710,000 ni matumizi mengineyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Bajeti ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo inajumuisha fedha za ndani shilingi 1,544,872,147,000 na fedha za nje shilingi 922,464,332,000.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hotuba hii, nimeambatanisha mchanganuo wa miradi itakayotekelezwa na Wizara katika mwaka wa fedha 2026/2027. Ninaomba viambatanisho hivyo vyote vichukuliwe kama sehemu ya vielelezo vya hoja yangu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nitoe tena shukrani zangu za dhati kwako na kwa Waheshimiwa Wabunge wote kwa kunisikiliza. Hotuba hii inapatikana pia katika tovuti ya Wizara https://www.mow.go.tz/.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kutoa hoja.

**HOTUBA YA WIZARA YA UJENZI MHESHIMIWA ABDALLAH HAMISI ULEGA (MB), AKIWASILISHA BUNGENI MPANGO WA MAKADIRIO NA MAPATO NA MATUMIZI YA FEDHA KWA MWAKA WA FEDHA 2026/2027 – KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI**

**A.UTANGULIZI**

1. ***Mheshimiwa Spika,*** ninaomba kutoa hoja kwamba, kufuatia taarifa iliyowasilishwa hapa Bungeni na Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu iliyochambua utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya Ujenzi ya mwaka wa fedha 2025/26, Bunge lako Tukufu sasa likubali kupokea na kujadili Utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya Wizara ya Ujenzi kwa mwaka wa fedha 2025/26. Aidha, ninaliomba Bunge lako Tukufu liridhie kupitisha Mpango na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Fedha ya Wizara ya Ujenzi kwa mwaka wa fedha 2026/27.

2. ***Mheshimiwa Spika,*** awali ya yote, nitumie nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu, mwingi wa rehema, kwa kuijaalia

nchi yetu amani na utulivu na kutuwezesha kushiriki katika vikao hivi vya Bunge kwa ajili ya kujadili Bajeti ya Wizara ya Ujenzi.

3. ***Mheshimiwa Spika,*** kipekee kabisa nampongeza Mheshimiwa *Dkt.* Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania pamoja na Mheshimiwa Balozi *Dkt*. Emmanuel John Nchimbi, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuaminiwa na Watanzania kuiongoza nchi yetu. Hii inadhihirishwa na ushindi wa kishindo walioupata katika Uchaguzi Mkuu uliofanyika Oktoba, 2025. Ninawaombea kwa Mwenyezi Mungu aendelee kuwapa hekima, maarifa na afya njema wanapoendelea kuliongoza Taifa letu.

4. ***Mheshimiwa Spika***, nitoe pongezi za dhati kwa Mheshimiwa Dkt Hussein Ally Mwinyi, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa kuchaguliwa kwa mara nyingine kuingoza Serikali ya Mapinduzi Zanzibar. Ninamuombea afya njema na mafanikio ili aendelee kutimiza majukumu yake kwa ustawi wa wananchi wa pande zote mbili za Muungano.

5. ***Mheshimiwa Spika,*** nitumie fursa hii pia kutoa pongezi za dhati kwa Mheshimiwa *Dkt*. Mwigulu Lameck Nchemba, Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuaminiwa na Mheshimiwa Rais kushika wadhifa huu muhimu wa uongozi katika Taifa letu. Uteuzi huu unadhihirisha imani kubwa aliyonayo Mheshimiwa Rais katika uwezo, uzoefu na uzalendo wake katika uongozi wa nchi yetu. Ninamuahidi Mhe. Waziri Mkuu kuwa Wizara ya Ujenzi itaendelea kutekeleza miongozo na maelekezo yake kwa lengo la kuimarisha utendaji wa majukumu yetu.

6. ***Mheshimiwa Spika,*** nitumie nafasi hii kumshukuru Mheshimiwa *Dkt*. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa kuendelea kuniamini na kuniteua kuwa Waziri wa Ujenzi kwa kipindi kingine tena. Naomba kumuahidi Mheshimiwa Rais kuwa, nitatekeleza majukumu haya kwa weledi na uadilifu ili kufikia malengo yaliyokusudiwa kupitia miongozo na mipango mbalimbali ikiwemo Ilani ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2025.

7. ***Mheshimiwa Spika,*** naomba pia kukupongeza wewe binafsi pamoja na Naibu Spika kwa kuchaguliwa kwa kishindo kuliongoza Bunge hili la 13 la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Nawapongeza pia Wenyeviti wote wa Bunge kwa kuchaguliwa na tunawaahidi ushirikiano. Aidha, nawapongeza Waheshimiwa Wabunge wote, wageni na wa zamani kwa kufanikiwa kuingia katika Bunge hili Tukufu. Wizara inaahidi kuwa milango yetu ipo wazi muda wote kwa ajili ya kupokea maoni na ushauri ili kuhakikisha miundombinu tunayoisimamia nchi nzima inaimarika, inakuwa endelevu na kuleta tabasamu na tumaini kwa wananchi wetu.

8. ***Mheshimiwa Spika,*** kipekee napenda kuishukuru Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu chini ya uongozi wa Mwenyekiti, Mheshimiwa Selemani Moshi Kakoso (Mb.) na Makamu Mwenyekiti Mheshimiwa Abubakar Damian Asenga (Mb.) kwa kuchambua kwa kina Mpango na Bajeti ya Wizara kwa mwaka wa fedha 2026/27 na kutoa ushauri ambao umezingatiwa katika bajeti hii.

9. ***Mheshimiwa Spika,*** kwa masikitiko makubwa, nitumie fursa hii pia kutoa salamu za pole kwa Bunge hili Tukufu, Chama cha Mapinduzi, wananchi, marafiki na familia, kufuatia vifo vya Wabunge wenzetu *Mhe*. Jenista Joakim Mhagama aliyekuwa Mbunge wa Jimbo la Peramiho, *Mhe*. William Vangimembe Lukuvi, aliyekuwa Mbunge wa Jimbo la Isimani na Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Bunge, Uratibu na Wenye Ulemavu) na *Mhe*. Halima Idd Nassor aliyekuwa Mbunge wa Viti Maalum (Wafanyakazi). Tutaendelea kuwaenzi Viongozi hawa kwa kuendeleza yale yote mema waliyotenda hususan katika uongozi wao na tunamuomba Mwenyezi Mungu awapumzishe kwa amani.

10. ***Mheshimiwa Spika,*** baada ya maelezo hayo ya utangulizi, naomba sasa nitoe taarifa ya Mapitio ya Utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya Wizara ya Ujenzi kwa mwaka wa fedha 2025/26 pamoja na Mpango na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka wa fedha 2026/27.

## B. MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA MPANGO NA BAJETI YA WIZARA NA TAASISI ZAKE KWA MWAKA WA FEDHA 2025/26

11. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeendelea kutekeleza Bajeti iliyoidhinishwa na Bunge lako Tukufu kwa mwaka wa fedha 2025/26 ambayo ilizingatia Mpango Mkakati wa Wizara, mipango mingine ya Kitaifa na maelekezo ya Viongozi Wakuu wa Kitaifa. Utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya Wizara kwa mwaka wa fedha 2025/26 ni kama ifuatavyo:

### B.1: MATUMIZI YA FEDHA

#### Bajeti ya Matumizi ya Kawaida

12. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara ya Ujenzi ilitengewa **Shilingi 90,468,270,000.00** ikiwa ni Bajeti ya Matumizi ya Kawaida kwa mwaka wa fedha 2025/ 26. Kati ya fedha hizo, **Shilingi 85,028,585,000.00** ilikuwa ni Bajeti ya Mishahara na **Shilingi 5,439,685,000.00** ni kwa ajili ya Matumizi Mengineyo.

13. ***Mheshimiwa Spika***, hadi Aprili, 2026 Wizara ilipokea jumla ya **Shilingi 73,604,735,181.30.** Kati ya fedha hizo, **Shilingi 70,533,041,808.41** ni kwa ajili ya Mishahara ya Watumishi wa Wizara na Taasisi na **Shilingi 3,071,693,372.89** ni kwa ajili ya Matumizi Mengineyo ya Wizara na Taasisi zake.

#### Bajeti ya Miradi ya Maendeleo

14. ***Mheshimiwa Spika,*** Bajeti kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo iliyotengwa kwa Wizara ya Ujenzi kwa mwaka wa fedha 2025/26 ni **Shilingi** 1,813,190,934,000.00. Kati ya fedha hizo, Shilingi **1,209,223,117,000.00** ni fedha za ndani na **Shilingi 603,967,817,000.00** ni fedha za nje. Kati ya fedha za ndani, **Shilingi 688,756,470,000.00** ni fedha zilizotengwa kwa ajili ya bajeti ya Mfuko wa Barabara na **Shilingi 520,466,647,000.00** ni fedha kutoka katika Mfuko Mkuu wa Serikali**.**

15. ***Mheshimiwa Spika,*** fedha zilizopokelewa kufikia Aprili, 2026 ni **Shilingi 1,395,658,301,112.09** Kati ya fedha hizo, **Shilingi 786,102,916,695.88** ni fedha za ndani na **Shilingi 609,555,384,416.21**

ni fedha za nje. Kati ya fedha za ndani zilizopokelewa, **Shilingi 461,173,316,123.56** ni kutoka Mfuko Mkuu wa Serikali na **Shilingi 324,929,600,572.32** ni za Mfuko wa Barabara.

**B.2: UTEKELEZAJI WA MIRADI YA MAENDELEO NA MAFANIKIO YALIYOPATIKANA**

16. ***Mheshimiwa Spika***, Sekta ya Ujenzi ni mtambuka na imeendelea kutoa mchango mkubwa katika kuchochea ukuaji wa sekta mbalimbali za kiuchumi na kijamii. Kwa mujibu wa Kitabu cha Hali ya Uchumi wa Taifa cha mwaka 2025, Sekta ya Ujenzi imekuwa ni ya pili katika kuchangia kwenye Pato la Taifa (GDP) ambapo katika mwaka 2025 imechangia kwa asilimia **11.9.** Aidha, Sekta hii imeendelea kukua kwa kasi ambapo katika mwaka 2025 Sekta ilikua kwa asilimia **4.0** ikilinganishwa na asilimia **3.0** mwaka 2024. Vilevile, Sekta ya Ujenzi imetoa mchango mkubwa katika kutoa ajira kwa Wakandarasi, Washauri Elekezi, mafundi na wasambazaji wa vifaa malighafi za ujenzi ambapo imetoa jumla ya ajira **18,988** kwa mwaka 2025 ikijumuisha Vijana na Wanawake. Mafanikio hayo yametokana na uwekezaji mkubwa unaoendelea kufanywa na Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

**Utekelezaji wa Miradi ya Ujenzi na Ukarabati wa Barabara na Madaraja**

17. ***Mheshimiwa Spika***, Mtandao wa barabara za kitaifa unaosimamiwa na Wizara ya Ujenzi kupitia TANROADS una jumla ya **kilometa 37,734.41**. Kati ya hizo, **kilometa 12,225.26** zimejengwa kwa kiwango cha lami. Wakati nchi inapata uhuru mwaka 1961, mtandao wa barabara za kiwango cha lami ulikuwa na urefu wa **kilometa 1,360.** Kuanzia Awamu ya Kwanza hadi ya Tano jumla ya **kilometa 9,369.81** zilijengwa. Serikali ya Awamu ya Sita chini ya uongozi thabiti wa Mhe. *Dkt*. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania imefanikiwa kujenga **kilometa 1,495.45** na madaraja makubwa **18** ndani ya kipindi cha miaka mitano (5). Kwa hakika haya ni

mafanikio makubwa yaliyopatikana ndani ya muda mfupi kwa upande wa miundombinu ya barabara na madaraja.

18. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2025/26, Wizara ilipanga kutekeleza miradi ya barabara kuu na za mikoa inayohusisha ujenzi na ukarabati kwa kiwango cha lami wa barabara zenye urefu wa kilometa **450** na kilometa **820** kwa kiwango cha changarawe. Aidha, Wizara ilipanga kuendelea na kazi ya Upembuzi Yakinifu na Usanifu wa Kina wa barabara zenye urefu wa kilometa **8,049.67** na madaraja mawili **(2).** Vilevile, miradi mingine iliyopangwa kutekelezwa ni kuendelea na ujenzi na ukarabati wa madaraja makubwa **20** na madaraja madogo/makalvati **78.** Kazi nyingine ni kuanza ujenzi wa madaraja manne **(4)** na kufanya maandalizi ya ujenzi wa madaraja tisa **(9).**

19. ***Mheshimiwa Spika,*** hadi kufikia Aprili, 2026, Wizara imekamilisha ujenzi na ukarabati kwa kiwango cha lami wa barabara zenye urefu wa kilometa **243.13** pamoja na ukarabati wa kilometa **94.36** kwa kiwango cha changarawe. Aidha, kwa upande wa madaraja makubwa, ujenzi wa madaraja **tisa (9)** ambayo ni daraja la Mitomoni (Ruvuma), Mirumba (Katavi), Nzali (Dodoma), Doma (Morogoro), Chakwale (Morogoro), Nguyami (Morogoro), Mkili (Ruvuma), Kalebe (Kagera) na Itembe (Simiyu) umekamilika na ujenzi wa madaraja **11** unaendelea. Maandalizi ya ujenzi wa madaraja **13** yanaendelea. Kwa upande wa ujenzi wa madaraja madogo/makalvati ujenzi umefikia asilimia 6.6. Vilevile, Upembuzi Yakinifu na Usanifu wa Kina wa daraja la Bujonde (Mbeya) na Mkondoa (Morogoro) unaendelea na taratibu za ununuzi wa madaraja ya Sanga (Simiyu) na Kilambo (Mtwara) zinaendelea.

**Matengenezo ya Barabara na Madaraja**

20. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kupitia TANROADS ilipanga kufanya matengenezo ya barabara kuu na barabara za Mikoa ambayo yalihusisha matengenezo ya kawaida (routine and recurrent maintenance) kwa kilometa **35,311.01,** matengenezo ya muda maalum kilometa **2,994.31,** matengenezo ya sehemu

korofi kilometa **305.17** pamoja na matengenezo ya madaraja **2,865** katika mwaka wa fedha 2025/26. Katika kipindi cha Julai 2025 hadi Aprili, 2026 Serikali imefanya matengenezo ya kawaida ya barabara zenye urefu wa **km 16,782.58,** matengenezo ya muda maalum **km 1,101.12,** matengenezo ya sehemu korofi kwa **km 147.13** na madaraja **1,383.** Lengo ni kuhakikisha kuwa miundombinu inayojengwa inalindwa pamoja na kudumu kwa muda mrefu na kuwa salama kwa watumiaji muda wote.

**Matengenezo ya Miundombinu iliyoharibiwa na mvua za El-Nino na Kimbunga Hidaya**

21. ***Mheshimiwa Spika,*** mvua za EL-NINO na Kimbunga Hidaya kilichoikumba nchi yetu mwishoni mwa mwaka 2023 zilisababisha mafuriko ambayo yaliathiri mtandao wa barabara hasa zilizojengwa kwa kiwango cha changarawe. Kwa mujibu wa tathmini iliyofanyika ya uharibifu wa miundombinu uliotokana na majanga hayo, takriban madaraja **63,** kilometa **827** za barabara, mitaro yenye urefu wa kilometa **84** pamoja na Makalavati **225** kutoka kwenye Wilaya 139 za Tanzania bara ziliharibika. Barabara zilizokumbwa na uharibifu mkubwa ni pamoja na barabara ya Dar es Salaam – Lindi. Hali hii iliathiri mtiririko wa kibajeti ambao ulitarajiwa kwenda kwenye matengenezo au ujenzi wa barabara kutumika kushughulikia dharura hizo.

22. ***Mheshimiwa Spika,*** jumla ya Miradi **81** ya Dharura ya Ujenzi wa Madaraja yaliyoathiriwa na Mvua za El-Nino na Kimbunga Hidaya kupitia Programu ya *Contigent Emergency Response Component - CERC* imetekelezwa katika mikoa **22** ya Tanzania bara kwa gharama ya jumla ya **Shilingi bilioni 556.93.** Kati ya miradi hiyo, miradi **70** yenye thamani ya **Shilingi Bilioni 414.481** inatekelezwa na Wakandarasi wa Ndani. Miradi 11 yenye thamani ya **Shilingi Bilioni 142.447** inatekelezwa na wakandarasi wa kigeni. Aidha, utekelezaji wa miradi hii umefikia asilimia **97.6** kama ifuatavyo: Miradi 78 imekamilika na taratibu za kuipokea zinaendelea; na Miradi 3 ipo katika hatua za mwisho za ukamilishaji. Utekelezaji wa Miradi hiyo umetatua changamoto zilizokuwepo na kuleta tabasamu kwa wananchi ambao

wamekuwa wakishuhudia kwa maneno yao wenyewe baada ya utekelezaji wa miradi hiyo.

23. ***Mheshimiwa Spika,*** utekelezaji wa miradi yote ya Ujenzi na Ukarabati wa Barabara na Madaraja iliyotengewa fedha kwa mwaka 2025/26 hadi kufikia Aprili, 2026 ni kama ifuatavyo:

24. ***Mheshimiwa Spika,*** taratibu za ununuzi kwa ajili ya kumpata Mkandarasi na Mhandisi Mshauri kwa ajili ya ujenzi kwa kiwango cha lami wa Barabara ya **Soni – Bumbuli – Dindira – Korogwe (km 74)** sehemu za ***Soni – Bumbuli (km 22)*** na ***Kwameta – Kwashemshi (km 10)*** zinaendelea. Aidha, Serikali inaendelea kutafuta fedha kwa ajili ya ujenzi wa sehemu ya ***Maramba – Mabokweni (km 10)*** na ***Old Korogwe – Kwamndolwa (km 10).***

25. ***Mheshimiwa Spika,*** katika barabara ya **Mtwara – Newala – Masasi (km 210)**, ujenzi kwa kiwango cha lami wa sehemu za ***Mnivata – Mitesa (km 100)*** umefikia asilimia 41 na ***Mitesa – Masasi (km 60)*** umefikia asilimia 65. Vilevile, taratibu za ununuzi wa kuwapata Wakandarasi wa ujenzi wa barabara za ***Mangamba – Madimba - Msimbati (km 35), Mtama –Tandahimba (km 5)*** na ***Namichiga – Ruangwa (km 20.6)*** zinaendelea.

26. ***Mheshimiwa Spika,*** ujenzi wa barabara ya **Likuyufusi – Mkenda (km 122.50)**, sehemu ya ***Likuyufusi – Muhukuru (km 60)*** upo katika hatua za awali.

27. ***Mheshimiwa Spika***, ujenzi wa barabara ya **Nachingwea – Liwale (km 130)** sehemu ya ***Liwale – Kihangara (km 55)*** upo katika hatua za awali.

28. ***Mheshimiwa Spika,*** ujenzi wa barabara ya **Ubena Zomozi – Ngerengere (km 11.6)** unaendelea na umefikia asilimia 27.9.

29. ***Mheshimiwa Spika,*** ujenzi kwa kiwango cha lami wa barabara ya **TAMCO – Vikawe – Mapinga (km 24)** unafanyika kwa awamu ambapo ujenzi wa kilometa 4.7 umekamilika na ujenzi wa kilometa 1.8 unaendelea. Aidha, ujenzi wa sehemu ya ***Pangani – Mapinga (km 13.59)*** umefikia asilimia 13. Vilevile,

Serikali inaendelea kutafuta fedha kwa ajili ya kuanza ujenzi kwa kiwango cha lami barabara ya **Makofia – Mlandizi (km 36.7)**.

30. ***Mheshimiwa Spika,*** katika barabara ya **Musoma – Makojo – Busekela (km 92),** taratibu za ununuzi za kumpata Mkandarasi wa ujenzi wa sehemu ya ***Musoma – Kusenyi (km 40***) kwa kiwango cha lami zinaendelea baada ya kuongezeka kwa mawanda ya mradi.

31. ***Mheshimiwa Spika,*** ujenzi wa barabara ya **Kongwa Jct – Mpwapwa – Gulwe – Kibakwe (km 98)** unafanyika kwa awamu. Ujenzi wa sehemu ya ***Kongwa Jct – Ngambi – Mpwapwa (km 32)*** upo katika hatua za awali za kuanza ujenzi. Vilevile, taratibu za ununuzi za kumpata Mkandarasi wa ujenzi wa sehemu ya ***Mpwapwa – Gulwe – Kibakwe (km 46.9)*** zinaendelea baada ya kufanyika kwa marejeo ya usanifu.

32. ***Mheshimiwa Spika,*** ujenzi wa barabara ya **Muhutwe – Kamachumu – Muleba (km 54)** kwa kiwango cha lami unafanyika kwa awamu ambapo kilometa 43.67 zimekamilika na ujenzi wa sehemu ya Ilambika – Kalela (km 3.8) unaendelea na umefikia asilimia 29.

33. ***Mheshimiwa Spika,*** ujenzi wa barabara ya **Iringa – Ruaha National Park (km 104**) umefikia asilimia 29. Aidha, ujenzi wa barabara ya ***Iringa (Ipogolo) – Kilolo (km 33.2****)* kwa kiwango cha lami umefikia asilimia 95.

34. ***Mheshimiwa Spika,*** ujenzi wa barabara ya **Muheza – Amani (km 36)** kwa kiwango cha lami unafanyika kwa awamu ambapo ujenzi wa sehemu ya ***Kwemhosi – Bombani (km 4)*** umekamilika.

35. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mradi wa ukarabati kwa kiwango cha lami wa **barabara ya Mtwara – Mingoyo – Masasi (km 200.51),** ukarabati wa sehemu ya ***Mtwara – Mingoyo (km 82.27*)** umefikia asilimia 9 na ukarabati wa ***Mingoyo – Nanganga – Masasi (km 118.24)*** umeanza.

36. ***Mheshimiwa Spika,*** kuhusu barabara ya **Kibaoni – Majimoto – Muze – Kilyamatundu (km 189),** hadi kufikia Aprili, 2026, ujenzi wa barabara ya ***Kibaoni – Majimoto – Inyonga (Sehemu ya Kibaoni – Usevya - km 5)*** umefikia asilimia 4; ujenzi wa sehemu ya ***Ntendo – Kizungu (km 25)*** kwa kiwango cha lami unaendelea na umefikia asilimia 52.4. Aidha, maandalizi ya nyaraka za zabuni za kumpata mkandarasi wa ujenzi kwa sehemu ya ***Kizungu – Muze (km 12)*** yanaendelea.

37. ***Mheshimiwa Spika,*** hadi mwezi Aprili, 2026 ujenzi wa **Daraja la J.P. Magufuli (Kigongo – Busisi) na barabara Unganishi** ulikuwa umekamilika. Aidha, taratibu za ununuzi wa Mkandarasi wa ujenzi wa daraja la **Mzinga (Dar es Salaam)** zinaendelea. Vilevile, Serikali inaendelea kutafuta fedha za ujenzi wa daraja la **Ugalla (Katavi)**.

38. ***Mheshimiwa Spika,*** ujenzi wa barabara ya ***Kagera Sugar Jct – Kakunyu; Sehemu ya Kagera Sugar Jct – Kitengule Jct (km 25)*** unaendelea na umefikia asilimia 6. Aidha, upembuzi yakinifu na usanifu wa kina wa barabara ya ***SUA Main Gate – Mzinga Factory Gate (km 11)*** unaendelea.

39. ***Mheshimiwa Spika,*** kuhusu barabara ya **Njombe – Makete – Isyonje (km 157.4),** ujenzi wa sehemu ya ***Kitulo – Iniho (km 36.3)*** unaendelea na umefikia asilimia 30 na ujenzi wa mizani ya Igagala katika barabara hiyo umekamilika. Ujenzi wa barabara ya ***Matamba – Mfumbi (km 33)*** sehemu ya ***Matamba Center (km 1)*** unaendelea. Aidha, Serikali inaendelea kutafuta fedha kwa ajili ya ujenzi wa sehemu za ***Bulongwa – Iyoka - Madihani - Kidope (km 22.15), Madihani – Lufilyo (km 15.1)*** na ***Kitulo - Matamba - Chimala (km 41).***

40. ***Mheshimiwa Spika,*** kuhusu barabara ya **Omugakorongo – Kigarama – Murongo (km 105),** taratibu za ununuzi wa Mkandarasi wa ujenzi wa sehemu za ***Omugakorongo – Businde (km 51.6)*** na ***Businde – Murongo (km 53.4)*** zipo katika hatua za mwisho.

41. ***Mheshimiwa Spika,*** katika barabara ya **Nanganga – Ruangwa – Nachingwea (km 145)**, ujenzi kwa kiwango cha lami wa sehemu ya ***Nanganga – Ruangwa (km 53.2)*** umefikia asilimia 90 na kwa sehemu ya ***Ruangwa – Nachingwea (km 55.7)*** umefikia asilimia 16.14. Kwa sehemu ya ***Nangurukuru – Liwale (km 210),*** ujenzi kwa kiwango cha lami sehemu ya ***Liwale - Choya (km 10)*** upo katika hatua za awali za kuanza ujenzi.

42. ***Mheshimiwa Spika,*** ujenzi kwa kiwango cha lami kwa barabara ya ***Mlowo – Kamsamba (km 10***) upo katika hatua za awali za kuanza ujenzi. Vilevile, taratibu za ununuzi ya Mkandarasi kwa ajili ya ujenzi wa ***Kituo cha Pamoja cha Ukaguzi (Iboya OSIS)*** zinaendelea. Vilevile, kwa sehemu ya ***Chang'ombe – Mkwajuni – Makongolosi (km 61),*** maandalizi ya kuanza ujenzi wa sehemu ya kilometa 5 kuanzia ***Mkwajuni – Makongolosi*** yanaendelea na Serikali inaendelea kutafuta fedha kwa ajili ya ujenzi wa sehemu ya ***Utambalila – Chitete (km17).***

43. ***Mheshimiwa Spika,*** ujenzi kwa kiwango cha lami wa sehemu ya **Ruanda – Iyula – Nyimbili (km 21)** unaendelea katika sehemu 4 tofauti zenye urefu wa takriban kilometa 5 kila moja. Barabara hii inajengwa na Wakandarasi Wanawake ikiwa ni mkakati wa kuwajengea uwezo ambapo Sehemu ya I imefika asilimia 11, Sehemu ya II asilimia 14, Sehemu ya III asilimia 8 na Sehemu ya IV asilimia 9.

44. ***Mheshimiwa Spika,*** katika barabara ya Katumbasongwe – Kasumulu – Ngana – Ndembo (km **90.1),** ujenzi wa sehemu ya ***Isongole II – Ndembo (km 46)*** na ***Ndembo Spur Road (km 6)*** umefikia asilimia 10. Aidha, Serikali inaendelea kutafuta fedha kwa ajili ya ujenzi wa sehemu ya ***Ngana – Ndembo (km 44.10).***

45. ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali inaendelea kutafuta fedha kwa ajili ya ujenzi kwa kiwango cha lami wa **barabara ya Uyogo – Nyamilangano – Nyandekwa – Kahama (km 54)**.

46. ***Mheshimiwa Spika,*** ujenzi kwa kiwango cha lami wa **barabara ya Sengerema – Nyehunge (km 54),** upo katika hatua za awali. Aidha, Serikali inaendelea kutafuta fedha kwa ajili ya

kuanza ujenzi wa barabara ya ***Kamanga – Katunguru – Sengerema (km 35)*** kwa kiwango cha lami.

47. ***Mheshimiwa Spika,*** kwa upande wa barabara ya **Omurushaka – Nkwenda – Murongo (km 125),** ujenzi wa sehemu ya ***Kyerwa – Chonyonyo (km 50***) kwa kiwango cha lami umefikia asilimia 4.9.

48. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mradi wa **Upanuzi wa barabara kuu zinazoingia katikati ya Jiji la Dodoma (km 51.2),** chini ya mradi wa *Dodoma Integrated and Sustainable Transport* (DIST), ununuzi wa Mhandisi Mshauri wa barabara ya ***Dodoma – Morogoro (Kimbinyiko R/ About – Chamwino Jct km 32)*** umekamilika na mkataba kwa ajili ya kuanza ujenzi kwa kiwango cha lami umeshasainiwa. Aidha, sehemu za ***Dodoma – Iringa (Image Rd R/About - Mkonze km 8.5)*** na ***Dodoma – Arusha (Bahi Rd R/About – Msalato Airport Jct km 10.7)*** zipo katika hatua za ununuzi.

49. ***Mheshimiwa Spika,*** ujenzi kwa kiwango cha lami wa barabara ya **Ntyuka Jct – Mvumi Hospital – Kikombo Jct (km 76.07),** sehemu ya ***Ntyuka Jct – Mvumi - Makulu (km 8.6)*** na ***Kikombo Jct – Mapinduzi (km 16.4)*** umefikia asilimia 75.7. Aidha, ujenzi wa barabara ya ***Ntyuka – Mvumi Hospital - Kikombo (km 53)*** umefikia asilimia 2.4. Vilevile, Usanifu wa Kina wa barabara za ***Ihumwa – Hombolo - Mayamaya (km 60)*** upo hatua za mwisho kukamilika. Vilevile, taratibu za ununuzi wa Mkandarasi wa ujenzi wa ***Barabara ya kuingia Hospitali ya Jeshi la Wananchi (JWTZ) Msalato (km 5.5***) zipo katika hatua za mwisho.

50. ***Mheshimiwa Spika,*** ujenzi wa barabara ya **Tarime – Mugumu (km 87.14)** kwa kiwango cha lami, sehemu ya ***Mogabiri – Nyamongo (km 25)*** unaendelea na umefikia asilimia 61. Aidha, Mkandarasi wa ujenzi wa sehemu za ***Tarime – Mogabiri (km 9.3), Nyamongo – Mugumu (km 48.15)*** na ***barabara unganishi ya Mugumu Roundabout (km 3.6)*** anaendelea na maandalizi ya kuanza ujenzi. Kwa upande wa barabara ya **Mika – Utegi – Shirati – Kirongwe (km 56.8),** taratibu za ununuzi wa Mkandarasi wa ujenzi sehemu ya ***Utegi – Shirati (km 27)*** zinaendelea.

51. ***Mheshimiwa Spika,*** Upembuzi Yakinifu na Usanifu wa Kina kwa ajili ya ukarabati kwa kiwango cha lami wa barabara ya **Shelui – Nzega (km 123)** umekamilika. Aidha, taratibu za ununuzi kumpata Mkandarasi na Mhandisi Mshauri kwa ajili ya ujenzi wa sehemu ya ***Shelui – Sekenke – Tulya – Tyegelo (km 62); sehemu ya Shelui – Sekenke – Ntwike (km 20)*** zipo hatua za mwisho.

52. ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali inaendelea kutafuta fedha kwa ajili ya ujenzi wa barabara ya **Nzega – Kagongwa (km 65)**, sehemu ya ***Kagongwa – Sojo (km 18)***. Aidha, ujenzi kwa kiwango cha lami wa barabara ya **Isabdula (Magu) – Bukwimba Station – Ngudu – Ng'hungumalwa (km 50);** sehemu ya ***Isabdula – Bukwimba Station (km 10)*** umefikia asilimia 7. Vilevile, ujenzi kwa kiwango cha lami wa barabara ya **Mwanangwa – Misasi – Salawe – Kahama (km 136);** sehemu ya km 3 kutoka Mwanangwa umefikia asilimia 40.

53. ***Mheshimiwa Spika,*** katika barabara ya **Mafinga – Mgololo (km 81)**, mradi huu unatekelezwa kwa njia ya Sanifu Jenga (Design and Build). Mkandarasi anaendelea na maandalizi ya kuanza ujenzi**.** Aidha, katika barabara ya **Nyololo – Mtwango (km 40.4)** ujenzi wa sehemu ya km 1.1 unaendelea na umefikia asilimia 65.

54. ***Mheshimiwa Spika,*** kuhusu ujenzi kwa kiwango cha lami wa barabara ya **Kongwa – Kibaya - Arusha (km 430),** Mkandarasi wa ujenzi kwa sehemu ya ***Arusha Mjini (Tanganyika Packers/Mbauda Jct) – Losinyai (km 70)*** yupo katika hatua za awali za kuanza ujenzi.

55. ***Mheshimiwa Spika,*** ujenzi kwa kiwango cha lami wa barabara ya **Singida – Sepuka – Ndago (km 77.4**) unaendelea. Aidha, Serikali inaendelea kutafuta fedha kwa ajili ya kujenga kwa kiwango cha lami sehemu ya ***Sepuka – Mlandala – Urugu – Mtoa – Shelui (km 97.6)***.

56. ***Mheshimiwa Spika,*** kuhusu mradi wa ujenzi kwa kiwango cha lami wa barabara ya **Kitai – Lituhi (km 90)** pamoja na **daraja la Mnywamaji,** ujenzi wa barabara hii sehemu ya ***Amanimakoro –***

***Ruanda (km 35)*** unaendelea na umefikia asilimia 41. Aidha, Mkandarasi wa sehemu ya ***Ruanda – Ndumbi Port (km 50)*** pamoja na ***daraja la Mnywamaji*** anaendelea na maandalizi ya kuanza ujenzi.

57. ***Mheshimiwa Spika,*** kuhusu **Barabara za Kuelekea Katika Vituo vya Reli ya Kisasa ya SGR (km 87.6),** ujenzi wa barabara ya Kizota – Zuzu (km 14), sehemu ya Kizota - Zinje (km 6) umekamilika. Vilevile, ujenzi wa barabara za Morogoro – Kihonda SGR Station (km 10) na Rudewa – Kilosa SGR Station (km 3) umefikia asilimia 20. Aidha, Usanifu wa Sehemu ya Pugu – Killtex (km 6) umekamilika na usanifu wa barabara za Gulwe – Gulwe SGR Station (km 2), Igandu – Igandu SGR Station (km 27), Ihumwa – Ihumwa Marshalling Yard (km 5.50) na Bahi – Bahi SGR Station (km 4) upo katika hatua za mwisho kukamilika. Katika barabara ya Mlandizi – Ruvu SGR Station (km 22) Mkandarasi yupo katika hatua za awali za kuanza ujenzi.

58. ***Mheshimiwa Spika,*** katika barabara ya **Tanga – Pangani – Makurunge (km 174.5),** ujenzi wa sehemu ya ***Tanga – Pangani (km 50)*** unaendelea na umefikia asilimia 77. Ujenzi wa sehemu ya ***Pangani – Mkange (km 124.5)*** sehemu ya ***Tungamaa – Mkange (km 95.2)*** umefikia asilimia 60 na ujenzi wa ***daraja la Pangani*** umefikia asilimia 64. Aidha, taratibu za ununuzi kumpata mkandarasi wa ujenzi wa barabara ya ***Mkata – Kwa Msisi (km 36)*** zinaendelea.

59. ***Mheshimiwa Spika,*** ujenzi wa barabara ya **Kisarawe – Maneromango – Mloka (km 150.46)** sehemu ya ***Kisarawe - Maneromango (km 54)*** kwa kiwango cha lami unafanyika kwa awamu ambapo, taratibu za ununuzi kumpata mkandarasi wa ujenzi wa sehemu ya ***Mpuyani – Maneromango (km 34.5)*** zinaendelea na ujenzi wa sehemu ya ***Sungwi – Masaki (km 2.1)*** umefikia asilimia 25. Ujenzi kwa kiwango cha lami sehemu ya ***Kisarawe – Sungwi – Kisanga (km 27.65)*** umekamilika.

60. ***Mheshimiwa Spika,*** kuhusu barabara ya **Geita – Bulyanhulu – Kahama (km 120),** hadi kufikia Aprili, 2026 ujenzi sehemu ya ***Kahama - Bulyanhulu Jct – Kakola (km 73)*** umefikia asilimia 60.

Aidha, Mkandarasi wa ujenzi sehemu ya barabara ya ***Geita – Bukoli – Bulyanhulu Jct (km 57.4) na barabara ya kuingia mji wa Bukoli (km 3.8****)* yupo katika hatua za awali za kuanza kazi. Vilevile, taratibu za ununuzi kwa ajili ya ujenzi kwa kiwango cha lami kwa *sehemu za* ***Nyikonga – Kashelo (km 10.5), Kashelo – Ilolangulu (km 15)*** na ***Ushirombo – Kilimahewa – Nanda (km 15.57)*** zinaendelea. Aidha, Serikali inaendelea kutafuta fedha kwa ajili ya ujenzi wa sehemu za ***Masumbwe – Kashelo (km 60), Kahama - Tulole - Muhulidede - Bukumbi - Mambali -Tabora (km 152.27)*** Sehemu ya ***Kahama - Tulole (km 20)*** na ***Katoro – Nyikonga – Ushirombo (km 47)*** Sehemu ya **Ushirombo – Nyikonga (km 22.5).**

61. ***Mheshimiwa Spika,*** katika barabara ya **Nyamirembe Port – Katoke (km 50);** kwa sehemu ya ***Nyamirembe Port – Nyamirembe Jct (km 1.7)*** ujenzi kwa kiwango cha lami umefikia asilimia 25**.** ***SIDO – Chato Zonal Hospital (km 5.3****)* ujenzi wa sehemu ya barabara yenye urefu wa kilometa 2.4 umefikia asilimia 12 na ***Chato Ginery – Bwina (km 8.1)*** ujenzi wa sehemu ya barabara yenye urefu wa kilometa1 umekamilika.

62. ***Mheshimiwa Spika,*** katika **Barabara ya Geita – Nzera - Nkome (km 54);** sehemu ya ***Sungusila - Nzera – Nkome (km 20.36)*** ujenzi wa barabara hii kwa kiwango cha lami umefikia asilimia 3.

63. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mradi wa **Arusha – Moshi – Himo – Holili (km 199.51)**, ujenzi wa barabara ya ***Mianzini – Ngaramtoni (km 18)*** umefikia asilimia 54. Aidha, taratibu za ununuzi wa Mkandarasi wa ujenzi wa barabara ya ***Tengeru – USA River (km 11.33), Daraja Jipya la Kikafu (m 560) pamoja na Barabara Unganishi (km 4.06)*** na ***Barabara za Moshi Mjini (km 11.7)*** zipo katika hatua za mwisho kukamilika. Kazi ya upanuzi wa barabara ya ***Arusha – Kisongo (km 9.3)*** ipo katika hatua za manunuzi.

64. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mradi wa ujenzi wa **barabara za Kuelekea Kwenye Mradi wa Kufua Umeme Katika Maporomoko ya Mto Rufiji,** ujenzi wa barabara ya ***Bigwa – Matombo – Mvuha (km 78)*** kwa kiwango cha lami umefikia asilimia 2. Aidha,

Upembuzi Yakinifu na Usanifu wa Kina wa barabara za ***Ubena Zomozi – Mvuha – Kisaki – Mtemele Jct (km 178);*** sehemu ya ***Ngerengere – Mvuha – Kisaki – Mtemele Jct (km 166.4)*** kwa ajili ya ujenzi kwa kiwango cha lami upo hatua za mwisho. Vilevile, taratibu za ununuzi kwa ajili ya kumpata Mhandisi Mshauri wa kufanya kazi ya Upembuzi Yakinifu na Usanifu wa Kina katika barabara ya ***Chalinze – Utete (km 354.9)*** zipo katika hatua za mwisho za kusaini mkataba. Aidha, kazi za ukarabati wa barabara za ***Maneromango – Vikumburu – Mloka (km 100)*** na ***Kibiti – Mloka – Mtemele – Rufiji JNHHP (km 203)*** kwa kiwango cha changarawe zinaendelea.

65. ***Mheshimiwa Spika,*** kwa upande wa *expressway* ya **Kibaha – Mlandizi – Chalinze – Morogoro (km 163.8)**, taratibu za ununuzi wa kumpata mwekezaji mpya wa ujenzi wa sehemu ya ***Kibaha - Chalinze (km 78.9)*** zinaendelea kufuatia majadiliano na mwekezaji wa awali kushindikana. Aidha, kwa sehemu ya ***Chalinze – Morogoro (84.9)*** upembuzi yakinifu na usanifu wa awali umekamilika na taratibu za ununuzi wa kumpata mwekezaji zinaendelea. Miradi hii inatekelezwa kwa utaratibu wa PPP.

66. ***Mheshimiwa Spika,*** kazi za ukarabati (overlay) wa sehemu ya ***Mlandizi – Chalinze (km 44.24)*** zinaendelea. Ukarabati kwenye ***Barabara ya Msoga – Msolwa (Chalinze Bypass - km 10.2)*** sehemu ya kilometa 6 umekamilika na kilometa 3.74 unaendelea. Aidha, kwa sehemu ya ***Kibaha – TAMCO (km 4.5)*** maandalizi ya kutafuta Mkandarasi wa upanuzi wa sehemu hii kwa kiwango cha lami zinaendelea. Vilevile, ujenzi wa barabara ya ***Kwa Mathiasi (Morogoro Road) – Msangani (km 10.1)*** unafanyika kwa awamu ambapo ujenzi wa kilometa 8 umekamilika na sehemu iliyobaki yenye urefu wa kilometa 2.1 unaendelea.

67. ***Mheshimiwa Spika,*** kwa upande wa barabara ya **Wazo Hill – Bagamoyo – Msata (km 118.10),** Serikali inaendelea kutafuta fedha za ukarabati na upanuzi wa sehemu ya ***Tegeta/DAWASA–Bagamoyo (km 47).***

68. ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali inaendelea kutafuta fedha za ujenzi wa barabara ya **Nyakahura – Kumubuga – Rulenge –**

**Kabanga Nickel (km 141)** kwa sehemu za ***Rulenge – Kabanga Nickel (km 32), Kumubuga – Rulenge – Murusagamba (km 75)*** na ***Nyakahura – Kumubuga – Murusagamba (km 34),*** kwa kiwango cha lami**.**

69. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mradi wa **Kigoma – Kidahwe – Uvinza – Kaliua – Tabora (km 265),** ujenzi wa sehemu ya ***Uvinza – Malagarasi (km 51.1)*** umekamilika. Aidha, Serikali inaendelea kutafuta fedha kwa ajili ya ujenzi wa barabara ya ***Tabora - Ulyankulu (km 90)*** kwa kiwango cha lami.

70. ***Mheshimiwa Spika,*** katika barabara ya **Ifakara – Kihansi – Mlimba – Madeke – Kibena (km 346.43),** Wakandarasi wa ujenzi kwa kiwango cha lami wa sehemu za ***Ifakara – Mbingu (km 62.5)*** na ***Mbingu – Chita JKT (km 37.5)*** wanaendelea na maandalizi ya kuanza kazi za ujenzi. Katika barabara ya ***Njombe (Kibena) – Lupembe – Madeke (km 126); Sehemu ya Kibena – Kidegembye (km 42)*** taratibu za ununuzi wa Mkandarasi na Mhandisi Mshauri kwa ajili ya ujenzi kwa kiwango cha lami zipo katika hatua za mwisho**.** Aidha, Upembuzi Yakinifu na Usanifu wa Kina wa sehemu ya ***Kihansi – Mlimba – Madeke -Kidegembye (km 181)*** upo katika hatua ya manunuzi ya kumpata Mhandisi Mshauri.

71. ***Mheshimiwa Spika,*** katika barabara ya **Karatu – Mbulu – Haydom – Sibiti River – Lalago – Maswa (km 389**), kazi za ujenzi wa sehemu ya ***Mbulu – Garbabi (km 25***) zimefikia asilimia 42. Vilevile ujenzi kwa kiwango cha lami sehemu ya ***Labay – Haydom (km 25)*** umefikia asilimia 11. Aidha, katika sehemu ya ***Nkoma – Lalago (km 65)*** Mkandarasi anaendelea na maandalizi ya kuanza ujenzi. Serikali inaendelea kutafuta fedha za ujenzi kwa kiwango cha lami wa barabara ya ***Mogitu – Haydom (km 68).***

72. ***Mheshimiwa Spika,*** kuhusu barabara ya Marangu – Tarakea – Rongai – Kamwanga **/Bomang'ombe – Sanya Juu (km 105.16),** sehemu ya ***Kwa Sadala – Masama – Machame Junction (km 16),*** ujenzi wa ***daraja la Kikafu Juu (m 25)*** na barabara unganishi (m 400) upo katika hatua za awali**.** Kwa upande wa barabara ya ***Kiboroloni – Kiharara – Tsuduni – Kidia (km 10.8)*** ujenzi unaendelea kwa awamu ambapo jumla ya km 6 zimekamilika na

kilometa 1.05 ujenzi unaendelea. Aidha, Wakandarasi wa ujenzi wa sehemu ya ***Sanya Juu – Kamwanga (Elerai – Kamwanga: km 39.5****) na* barabara ya ***Tarakea – Holili (km 53); sehemu ya Ikuini – Kirongo Chini (km 10)*** wapo katika hatua za awali za kuanza ujenzi. Vilevile, Serikali inaendelea kutafuta fedha kwa ajili ya ukarabati wa sehemu ya ***Bomang'ombe – Sanya Juu (km 25).***

73. ***Mheshimiwa Spika,*** katika barabara ya **Tukuyu – Mbambo – Katumba (km 60.6),** ujenzi wa sehemu ya ***Katumba – Lupaso (km 35.3)*** umefika asilimia 5 na Mkandarasi wa ***Mbaka – Kibanja (km 20.7)*** yupo katika hatua za awali za ujenzi. Aidha, Serikali inaendelea kutafuta fedha kwa ajili ya ujenzi kwa kiwango cha lami wa sehemu ya ***Mbambo – Ipinda (km 19.7)***.

74. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mradi wa ujenzi wa barabara ya **Dodoma – Manyoni (km 127) na Barabara ya Kuingia Manyoni Mjini (km 4.8),** ujenzi wa ***Kituo cha Pamoja cha Ukaguzi (One Stop Inspection Station – OSIS) cha Muhalala (Manyoni).*** Mkataba wa awali wa utekelezaji wa mradi wa ujenzi wa ***OSIS*** umesitishwa kutokana na changamoto za kimkataba ambapo utekelezaji wake ulikuwa umefikia asilimia 50. Aidha, taratibu za kumpata Mkandarasi mpya wa kumalizia kazi hizo zinaendelea.

75. ***Mheshimiwa Spika,*** ujenzi wa barabara ya **Tabora – Mambali – Bukene – Itobo (km 114)** unafanyika kwa awamu kulingana na upatikanaji wa fedha. Aidha, Serikali inaendelea kutafuta fedha kwa ajili ya ujenzi wa **Barabara ya Namanyere – Katongoro – New Kipili Port (km 64.8)** na **Barabara ya Dumila – Kilosa – Mikumi (km 141)**, sehemu ya ***Kilosa – Ulaya – Mikumi (km 72)*** kwa kiwango cha lami.

76. ***Mheshimiwa Spika,*** ujenzi wa barabara ya***Matai – Kasesya (km 50)*** sehemu ya ***Matai – Tatanda (km 25)*** umefikia asilimia 42. Aidha, ujenzi wa sehemu ya ***Tatanda – Kasesya (km 25***) upo katika hatua za awali. Vilevile, taratibu za ununuzi wa kumpata Mhandisi Mshauri atakaefanya Upembuzi Yakinifu na Usanifu wa Kina wa barabara ya ***Laela – Mwimbi –Kizombwe (km 93)*** zinaendelea.

77. ***Mheshimiwa Spika***, hadi Aprili, 2026, katika mradi wa **Ujenzi wa Madaraja Makubwa**, ujenzi wa madaraja ya Mbangala, Mkili, Nzali, Chakwale na Nguyami umekamilika. Aidha ujenzi wa daraja la Mbambe umefikia asilimia 48, Mirumba asilimia 50, Simiyu asilimia 73, Doma asilimia 80, Suguta asilimia 13, Mwanjiri asilimia 11, Mjonga asilimia 85, Kavuu asilimia 50, Kibakwe asilimia 25, Mitomoni asilimia 85.8 na Sukuma asilimia 76. Vilevile, ujenzi wa barabara unganishi katika Daraja la Sibiti (Singida) umefikia asilimia 6. Taratibu za ununuzi wa Wakandarasi wa ujenzi wa Madaraja ya Mpiji Chini na Kerema Maziwa, zinaendelea. Mikataba ya ujenzi wa madaraja ya Sanza na Godegode ipo katika hatua za mwisho za kusainiwa. Usanifu wa Kina wa daraja la Malagarasi Chini umekamilika. Vilevile, Serikali inaendelea kutafuta fedha kwa ajili ya ukarabati wa daraja la Kirumi na ujenzi wa madaraja ya Mtera Dam, Mnenia, Pahi, Muhuwesi, Kondoa, Suguti, Kisorya, Munguri na Mkenda.

78. ***Mheshimiwa Spika,*** kuhusu barabara ya **Kyaka – Bugene – Kasulo** (**km 183.10**)**,** ujenzi wa sehemu ya ***Bugene – Kasulo – Kumunazi & Kyaka – Mutukula (km 124)*** sehemu ya ***Bugene – Burigi Chato National Park (km 60)*** unaendelea na umefikia asilimia 48.

79. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mradi wa barabara ya **Isaka – Lusahunga (km 242),** kazi za ukarabati wa sehemu ya ***Lusahunga – Rusumo (km 92)*** zinaendelea na zimefikia asilimia 41.16. Kwa upande wa ujenzi wa ***Kituo cha Ukaguzi wa Pamoja (OSIS) cha Nyakanazi,*** ujenzi utaendelea mara baada ya kumpata mkandarasi mpya wa ujenzi. Aidha, Serikali inaendelea kutafuta fedha kwa ajili ya ujenzi kwa kiwango cha lami sehemu ya ***Nyakasanza – Kobero (km 58***).

80. ***Mheshimiwa Spika,*** ujenzi wa Mizani ya Kizengi pamoja na uwekaji wa Taa za Barabarani pamoja na Viakisi mwanga umekamilika na unatumika.

81. ***Mheshimiwa Spika,*** katika barabara ya **Mwanza/Shinyanga Border – Mwanza (km 102)** hatua za ununuzi kwa ajili ya kumpata Mkandarasi wa upanuzi wa sehemu ya ***Mwanza - Usagara (km***

***25)*** kutoka njia mbili hadi njia nne zinaendelea. Aidha, taratibu za ununuzi kwa ajili ya kumpata Mhandisi Mshauri wa kufanya usanifu kwa ajili ya upanuzi wa sehemu ya ***Usagara – Daraja la JPM (km 12)*** zinaendelea.

82. ***Mheshimiwa Spika,*** kazi zilizopangwa kutekelezwa katika mwaka wa fedha 2025/26 kwa ajili ya miradi ya **Barabara za Mikoa (Kasma 4132)** ni ukarabati wa jumla ya kilometa **480** kwa kiwango cha changarawe, kujenga kilometa **45** kwa kiwango cha lami na ujenzi wa Madaraja/ Makalavati **45.** Hadi kufikia Aprili, 2026, kilometa **41.31** za barabara za mikoa zilikuwa zimekarabatiwa kwa kiwango cha changarawe na kilometa **30.65** zimejengwa kwa kiwango cha lami. Aidha, ujenzi wa madaraja/makalavati umefikia asilimia **6.6**.

83. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mradi wa **barabara za kupunguza msongamano wa magari katika jiji la Dar es Salaam**, taratibu za ununuzi wa mkandarasi wa ujenzi wa barabara ya ***Mbezi Victoria – Magoe Mpiji (km 9.55)*** zinaendelea. Aidha, Serikali inaendelea kutafuta fedha za ujenzi wa barabara ya ***Mji Mwema – Kimbiji – Pembamnazi (km 10)*** pamoja na upanuzi wa ***Barabara ya Mwai Kibaki (km 9.1);***

84. ***Mheshimiwa Spika***, ujenzi wa barabara ya ***Goba – Matosa – Temboni* (km 6)** unaendelea kufanyika kwa awamu ambapo kilometa moja (1) imekamilika na ujenzi wa kilometa 5 unaendelea. Vilevile, upanuzi wa barabara ya ***Kongowe – Mjimwema – Kivukoni Ferry (km 25.1)*** km 1.4 umekamilika, ujenzi wa barabara za ***Kipata (m 700), Livingstone (m 350) na Msikitini – Sharif Shamba (km 1)*** umekamilika, ***Kibamba Shule – Mpiji Magoe (km 3.9)*** umekamilika na ujenzi wa km 1 unaendelea***, Chanika – Mbande (km 3.8)*** umefikia asilimia 80***, Mbezi Msakuzi – Makabe Jct (km 8.36)*** ujenzi unaendelea *na* ***Kimara – Bonyokwa – Kinyerezi (km 6.73)*** unaendelea na umefikia asilimia 13. Aidha, Serikali inaendelea kutafuta fedha kwa ajili ya upanuzi wa barabara ya ***Chamazi Centre (km 1.2), Mbande – Chamazi Complex (km 1)*** na ***Gongo la Mboto - Buyuni (km 10).***

85. ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali inaendelea kutafuta fedha kwa ajili ya ujenzi wa barabara ya **Kolandoto – Lalago – Ng'oboko – Mwanhuzi (km 122)*, Nansio – Rugezi (km 12)*** na barabara ya ***Iguguno Shamba – Nduguti - Mkalama (km 89)*** kwa kiwango cha lami.

86. ***Mheshimiwa Spika,*** ujenzi wa barabara ya ***Utete – Nyamwage (km 33.7)*** umefikia asilimia 17. Kwa barabara ya ***Ikwiriri – Mkongo 1 (km 27.74),*** kazi za ujenzi zitaanza mara baada ya Mkataba wa ujenzi kusainiwa. Aidha, Serikali inaendelea kutafuta fedha kwa ajili ya ukarabati wa sehemu za ***Malendego - Tingi (km 50)*** na ***Nangurukuru – Mbwemkuru (km 95)*** pamoja na ujenzi wa barabara ya ***Bungu – Nyamisati (km 40).***

87. ***Mheshimiwa Spika,*** utekelezaji wa mradi wa ujenzi wa barabara ya **Kasulu – Manyovu pamoja na barabara za kuingia Kasulu Mjini *(km 68)*** umekamilika. Aidha, ujenzi wa ***Manyovu/ Mugina OSBP*** umefikia asilimia 5.62.

88. ***Mheshimiwa Spika,*** kwa upande wa mradi wa **barabara ya Mzunguko katika Jiji la Dodoma (Dodoma City Outer Dual Carriageway Ring Road Lot1 & 2 - km 112.3),** ujenzi wa sehemu ya ***Nala – Veyula – Mtumba – Ihumwa Dry Port (km 52.3)*** unaendelea na umefikia asilimia 93 na ujenzi wa sehemu ya ***Ihumwa Dry Port – Matumbulu – Nala (km 60)*** umefikia asilimia 95.

89. ***Mheshimiwa Spika,*** kuhusu ujenzi kwa kiwango cha lami wa **barabara ya Mzunguko wa Ndani katika Jiji la Dodoma: *Bahi R/About – Image R/About – Ntyuka R/About – Makulu R/About (km 6.3),*** mkataba wa ujenzi umesainiwa na mkandarasi anatarajia kuanza kazi hivi karibuni. Upembuzi yakinifu na usanifu wa kina wa barabara ya ***Dodoma City Middle Ring Road*** inayoanzia ***Nanenane – Miyuji – Mnadani Sekondari – Mkonze – Ntyuka – Nanenane (km 47.2)*** unaendelea. Aidha, kazi ya Upembuzi Yakinifu na Usanifu wa Kina wa barabara ya ***Msalato Airport – Mtumba – Chamwino IKULU (km 30)*** inaendelea.

90. ***Mheshimiwa Spika,*** kwa upande wa barabara ya **Kidatu – Ifakara – Lupiro – Malinyi – Londo – Lumecha/Songea (km 499)**,

mkandarasi wa ujenzi kwa kiwango cha lami kwa sehemu ya ***Ifakara – Lupiro – Mtimbira (km 112)*** yupo hatua za maandalizi ya kuanza kazi za ujenzi. Vilevile, Serikali inaendelea kutafuta fedha kwa ajili ya ujenzi wa barabara ya ***Chalinze – Magindu – Lukenge – Seregete B – Kabwe Jct – Mkulazi (km 77.50).***

91. ***Mheshimiwa Spika,*** kuhusu barabara ya **Makutano – Natta – Mugumu/Loliondo – Mto wa Mbu (km 185**), hadi Aprili, 2026, kazi za ujenzi wa sehemu ya ***Sanzate – Natta (km 40)*** zimefikia asilimia 55. Aidha, ujenzi wa barabara ya ***Wasso – Loliondo (km 10)*** Mkandarasi yupo katika hatua za maandalizi ya kuanza kazi. Taratibu za ununuzi za kuwapata Wakandarasi wa barabara za ***Mto wa Mbu – Selela (km 23), Selela – Engaruka (km 27), Ngaresh – Enguik (km 11)*** na ***Ngaresero – Engaruka (km 39)*** kwa kiwango cha lami zinaendelea. Vilevile, Serikali inaendelea kutafuta fedha kwa ajili ya kuanza ujenzi wa barabara ya ***Natta – Mugumu (km 45)***.

92. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mradi wa **Ibanda – Itungi Port/Kajunjumele – Kiwira Port (km 32),** ujenzi wa Kituo cha Pamoja cha Mpakani (OSBP) cha ***Kasumulu/Songwe (Tanzania/ Malawi Border)*** umefikia asilimia 95. Aidha, taratibu za ununuzi wa Mkandarasi wa ukarabati wa barabara ya ***Ibanda – Kajunjumele (km 22)*** na ***Kajunjumele – Kiwira Port (km 6)*** zinaendelea baada ya kusitishwa kwa mkataba wa awali kutokana na utendaji usioridhisha wa Mkandarasi.

93. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mradi wa ujenzi wa barabara ya **Puge – Ziba – Choma (km 109),** sehemu ya kilometa 11 ipo katika hatua ya manunuzi.

94. kuhusu barabara ya **Sumbawanga – Mpanda – Nyakanazi (km 803.6),** ujenzi wa barabara ya ***Mpanda – Mishamo – Uvinza; Sehemu ya Vikonge – Uvinza (km 159)*** kazi za ujenzi wa barabara hii sehemu ya ***Vikonge – Luhafwe (km 25)*** zimefikia asilimia 60.6 na ujenzi wa sehemu ya ***Luhafwe – Mishamo/ Bulamata Jct (km 37.35)*** umefikia asilimia 22.6. Taratibu za ununuzi kwa ajili ya kumpata mkandarasi na Mhandisi Mshauri sehemu ya ***Mishamo – Uvinza (km 100)*** zinaendelea. Kwa barabara ya ***Kibaoni – Sitalike***

***(km 71)*** sehemu ya ***Kibaoni – Mlele Jct (km 50),*** ujenzi umefikia asilimia 16.98 na taratibu za ununuzi kwa ajili ya kumpata Mkandarasi wa ujenzi wa sehemu ya ***Sitalike – Mlele Jct (km 21)*** kwa utaratibu wa sanifu na jenga (design and build) zinaendelea.

95. ***Mheshimiwa Spika***, kwa barabara ya ***Kagwira – Ikola – Karema Port (km 112),*** ujenzi wa sehemu ya ***Kagwira – Kasekese (km 54.14)*** umefikia asilimia 5 na ***Kasekese – Ikola (km 56.91)*** umefikia asilimia 34. Serikali inaendelea kutafuta fedha kwa ajili ya ujenzi wa sehemu za ***Kizi – Lyambalyamfipa – Sitalike (km 86)*** na ***Lyazumbi – Kabwe (km 65).***

96. ***Mheshimiwa Spika,*** katika barabara ya **Nyanguge – Musoma/ Mchepuo wa Usagara – Kisesa (km 202.25)**, Serikali inaendelea kutafuta fedha kwa ajili ya ukarabati wa barabara ya ***Nyanguge – Simiyu/Mara Border (km 100.4)***. Aidha, ujenzi wa barabara ya ***Airport – Nyanguge (km 46)*** sehemu ya ***Airport – Kayenze (km 10)*** umefikia asilimia 20.

97. ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali inaendelea kutafuta fedha za kujenga kwa kiwango cha lami barabara ya **Magole – Mziha – Handeni (km 152.8)**, sehemu ya ***Turiani – Mziha - Handeni (km 104).***

98. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mradi wa Ujenzi wa Barabara za Juu (Flyovers) Jijini DSM na Barabara **Unganishi,** Serikali inaendelea na majadiliano na Shirika la Maendeleo la Japan (JICA) kwa ajili ya ujenzi wa makutano ya barabara kwenye maeneo ya Morocco na Mwenge. Maboresho ya makutano ya Tabata/ Mandela yamejumuishwa katika mradi wa BRT V na Serikali inaendelea kutafuta fedha kwa ajili ya maboresho ya makutano ya barabara kwenye maeneo ya KAMATA, Magomeni, Fire, Selander (Ali Hassan Mwinyi/ UN Roads Jct) na Buguruni.

99. ***Mheshimiwa Spika,*** ujenzi wa barabara ya **Ipole – Rungwa (km 172)** unatekelezwa kwa awamu ambapo, ujenzi wa ***daraja la Msula (m 10) na barabara unganishi mita 600*** umekamilika.

100.***Mheshimiwa Spika,*** kwa upande wa barabara ya **Kidahwe – Kasulu – Kibondo – Nyakanazi (km 341.25),** ujenzi wa sehemu ya ***Mvugwe – Nduta Junction (km 59.35)*** umefikia asilimia 97.01, ***Kanyani Junction – Mvugwe (km 70.5)*** umefikia asilimia 98.5, na ***Nduta Junction – Kibondo (km 25.9)*** umefikia asilimia 53.36. Aidha, ujenzi kwa kiwango cha lami wa barabara ya ***Kibondo – Mabamba (km 48)*** umefikia asilimia 31.5.

101. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mradi wa **Barabara za Maingilio ya Kiwanja cha Ndege cha Mafia,** maandalizi ya nyaraka kwa ajili ya kutangaza zabuni za ujenzi wa barabara ya ***Kilindoni – Ras Mkumbi (km 54.4)*** kwa kiwango cha lami yanaendelea.

102. ***Mheshimiwa Spika,*** kuhusu mradi wa ujenzi wa **Daraja la Nyerere (Kigamboni) na Barabara Unganishi (km 46.3),** ujenzi wa barabara ya ***Kibada – Mwasonga – Tundwisongani Jct/Tundwisongani – Kimbiji (Km 41)*** kwa kiwango cha lami umefikia asilimia 49.

103. ***Mheshimiwa Spika,*** katika barabara ya Mutukula – Bukoba – Muhutwe – Kagoma (km **215.8),** taratibu za ununuzi kwa ajili ya ujenzi kwa kiwango cha lami sehemu ya km 10 barabara ya ***Kanazi (Kyetema) – Ibwera – Katoro – Kyaka II (km 60.7)*** na Mhandisi Mshauri wa kufanya Upembuzi Yakinifu na Usanifu wa Kina wa ***sehemu ya Kyaka - Muhutwe – Kagoma (km 136)*** zinaendelea. Aidha, ujenzi wa kilometa 1 katika barabara ya ***Bukoba – Bukoba Port (km 5)*** umefikia asilimia 75.

104.***Mheshimiwa Spika,*** kuhusu mradi wa ujenzi wa barabara ya **Pugu – Kifuru – Mbezi Mwisho – Mpiji Magoe – Bunju (km 34)**, kazi za Upembuzi Yakinifu na Usanifu wa Kina wa barabara ya mzunguko wa nje wa barabara ya ***Bunju – Kibamba – Pugu Kajiungeni – Mzinga – Tuangoma – Kigamboni (km 61)*** na barabara ya mzunguko wa kati wa ***Mbezi – Mbezi Mwisho – Kifuru – Banana – Kipara – Kigamboni (km 49.0)*** zinaendelea. Aidha, Serikali inaendelea kutafuta fedha za ujenzi wa **Barabara ya Kisarawe – Mlandizi (km 119)** kwa kiwango cha lami.

105.***Mheshimiwa Spika,*** Serikali inatafuta fedha kwa ajili ya ukarabati kwa kiwango cha lami wa barabara ya **Singida – Shelui (km 110)**. Aidha, ujenzi wa ***Barabara ya Ulemo – Kinampanda – Gumanga – Mkalama (km 46)*** kwa kiwango cha lami unafanyika kwa awamu ambapo sehemu ***Kitukutu – Kinampanda (km 7.7)*** umefikia asilimia 67.4**.**

106.***Mheshimiwa Spika,*** kuhusu barabara ya **Dar es Salaam – Mbagala (Kilwa Road),** upanuzi na ukarabati wa sehemu ya ***Mbagala Rangi Tatu – Kongowe (km 3.8)*** kuwa njia nne unaendelea na umefikia asilimia 11. Serikali inaendelea kutafuta fedha za upanuzi na ukarabati wa barabara za **Ikwiriri – Nyamwage – Malendego (km 56)** na ujenzi wa barabara ya **Mkuranga – Kisiju (km 46)**.

107.***Mheshimiwa Spika,*** katika barabara ya **Msimba – Ruaha Mbuyuni/Ikokoto Mafinga (km 535.25),** taratibu za ununuzi kwa ajili ya kumpata Mhandisi Mshauri wa kufanya Upembuzi Yakinifu na Usanifu wa Kina kwa ajili ya ukarabati wa barabara ya ***Morogoro – Iringa (Tumbaku Jct. Mangae/Melela – Mikumi – Iyovi) (km 158.45)*** zinaendelea. Aidha, Serikali inaendelea kutafuta fedha kwa ajili ya ujenzi wa sehemu ya ***Rujewa – Madibira – Mafinga (km 152.0)*** kwa kiwango cha lami.

108.***Mheshimiwa Spika,*** katika barabara ya **Same – Mkumbara – Korogwe (km 172.5),** ujenzi wa sehemu ya ***Ndungu – Mkomazi (km 36)*** umefikia asilimia 8. Aidha, taratibu za ununuzi wa Mkandarasi wa sehemu ya barabara ya ***Same – Kisiwani – Mroyo (km 56.83)*** zinaendelea baada ya Mkandarasi wa kwanza kujitoa kuendelea na hatua za kusaini mkataba. Vilevile, Serikali inaendelea kutafuta fedha za ukarabati kwa kiwango cha lami wa barabara za ***Same – Himo (km 76), Mombo – Lushoto (km 32)*** na ujenzi wa barabara ya ***Lushoto – Magamba – Mlola (km 34.5).***

109.***Mheshimiwa Spika,*** katika mradi wa barabara ya **Mbeya – Chunya - Makongolosi (km 267.9),** ujenzi wa barabara ya ***Noranga – Itigi – Mkiwa (km 56.9)*** sehemu ya ***Noranga – Itigi (Mlongoji) (km 25)*** umefikia asilimia 79.8, ujenzi wa ***barabara za Itigi Mjini (km 10.7)*** umefikia asilimia 93 kufuatia ongezeko la

mawanda ya mradi na ujenzi wa sehemu ya ***Noranga – Doroto (km 6)*** na ***Itigi – Mkiwa (km 25.6)*** umefikia asilimia 6. Aidha, Serikali inaendelea kutafuta fedha za ujenzi kwa kiwango cha lami wa barabara za ***Makongolosi – Rungwa – Noranga (km 356)*** na ***Mbalizi – Makongolosi (km 50)***.

110.***Mheshimiwa Spika,*** katika barabara ya **Itoni – Ludewa – Manda (km 211),** ujenzi wa sehemu ya ***Itoni – Lusitu (km 50)*** kwa kiwango cha zege umefikia asilimia 23.4. Aidha, Serikali inaendelea kutafuta fedha za ujenzi kwa kiwango cha lami wa barabara za **Mawengi – Ludewa – Manda (km 161)** na **Nkomang'ombe – Mchuchuma (km 7).**

111.***Mheshimiwa Spika,*** kuhusu barabara ya **Handeni – Kibirashi – Kibaya – Njoro – Goima - Chambalo – Chemba – Kwa Mtoro – Singida (km 424.24)**, ujenzi wa sehemu ya ***Handeni – Mafuleta (km 20)*** umefikia asilimia 52.53, ujenzi wa sehemu ya ***Mafuleta – Kileguru (km 30)*** na ***Kisima – Kibaya (km 50)*** upo katika hatua za awali. Kwa sehemu ya taarifa ya awali (Baseline Study) imeshakamilika na imewasilishwa *Tanzania Port Authority (TPA)* kwa ajili ya kutekeleza mradi huu kwa utaratibu wa PPP.

112.***Mheshimiwa Spika,*** kuhusu barabara ya **Makambako – Songea (km 295) na Barabara ya Mchepuo wa Songea *(km 11)***, Mkandarasi wa ujenzi wa sehemu ya ***Lutukila – Songea (km 95)*** na ***Mchepuo wa Songea (km 11)*** yupo katika hatua za awali za kuanza kazi. Aidha, Serikali inaendelea kutafuta fedha kwa ajili ya ujenzi wa barabara ya ***Ramadhani – Ilembula Hospital – Iyayi (km 75)*** na ukarabati wa barabara ya ***Makambako – Lutukila (km 200)*** kwa kiwango cha lami.

113.***Mheshimiwa Spika,*** kuhusu mradi wa barabara ya **Dodoma – Iringa (km 264),** ujenzi wa ***Barabara ya Mchepuo wa Iringa (km 7.3)*** umefikia asilimia 35. Kazi za uimarishaji wa matabaka ya barabara katika barabara ya ***Iringa – Dodoma (km 264)*** zinaendelea kwa awamu ambapo jumla ya km 25.3 zimekamilika na uimarishaji wa sehemu zingine zilizoharibika unaendelea. Vilevile, taratibu za ununuzi ya kumpata Mkandarasi wa ujenzi wa

barabara ya ***Iringa – Pawaga (km 71.93); sehemu ya Pawaga Jct – Ikonongo (km 5)*** na ***Itundu – Ilolo Mpya (km 20)*** zinaendelea.

114.***Mheshimiwa Spika,*** katika mradi wa ujenzi wa barabara ya **Dodoma – Babati (km 263.4)** ujenzi wa barabara ya ***Dareda – Dongobesh (km 60)*** sehemu ya ***Dareda Mjini – Dareda Mission (km 8)*** umefikia asilimia 10. Ujenzi wa barabara ya ***Miteremko ya Magara (Magara Escarpment - km 15)*** kwa kiwango cha zege unaendelea ambapo jumla ya kilometa **5.615** zimekamilika na ujenzi wa sehemu ya kilometa **1.55** unaendelea.

115.***Mheshimiwa Spika***, Serikali inatafuta fedha kwa ajili ya Ujenzi wa barabara ya **Mtwara Pachani – Nalasi – Tunduru (km 300)** na barabara za **Chuo cha Uongozi** (Uongozi Institute) kilometa 8.8 kwa ajili ya ujenzi wa barabara hizi kwa kiwango cha lami.

116.***Mheshimiwa Spika,*** kuhusu mradi wa **Barabara za Igawa – Songwe – Tunduma na Mchepuo wa Mbeya (km 266.9),** upanuzi wa sehemu ya ***Uyole – Ifisi (km 29)*** umefikia asilimia 41. Aidha, Serikali inaendelea kutafuta fedha kwa ajili ya ujenzi wa barabara ya Mchepuo wa ***Iwambi – Mbalizi (Bypass) (km 6.5)*** kwa kiwango cha lami.

117. *Mheshimiwa Spika,* kuhusu mradi wa ujenzi wa Miundombinu ya Mabasi Yaendayo Haraka **Awamu ya Pili hadi Tano (km 69.8),** kazi za ujenzi wa barabara ya ***Mabasi Yaendayo Haraka Awamu ya Pili*** (CBD – Mbagala, **km 20.3**) zimekamilika na ujenzi wa miundombinu ya ***Mabasi Yaendayo Haraka Awamu ya Tatu*** (CBD – Gongolamboto **km 23.33**) umefikia asilimia 99. Aidha, ujenzi wa Barabara za ***Mabasi Yaendayo Haraka Awamu ya Nne (Ali Hassan Mwinyi – Morocco – Mwenge - Ubungo (km 13.5)*** umefikia asilimia 53, ***Mwenge – Tegeta/Basihaya (km 15.63)*** umefikia asilimia 46 na ujenzi wa ***Miundombinu ya Majengo ya Mbuyuni, Simu 2000 na Kivukoni*** umefikia asilimia 28.

117.***Mheshimiwa Spika,*** kazi za maboresho ya miundombinu ya **Mabasi Yaendayo Haraka Awamu ya Kwanza,** zimefikia asilimia 74. Aidha, ujenzi wa ***Daraja la Jangwani (m 390) pamoja na barabara unganishi (m 710)*** umefikia asilimia 33. Taratibu za

kumpata Mkandarasi kwa ajili ya ujenzi wa barabara za ***Mabasi Yaendayo Haraka Awamu ya Tano,*** unaohusisha ujenzi wa barabara ya Nelson Mandela kuanzia ***Ubungo hadi daraja la Mwalimu Nyerere*** pamoja na barabara ya Tabata kutoka Segerea kupitia Tabata Dampo hadi Mzunguko wa Kigogo katika barabara ya ***Kawawa (km 27.6)*** zinaendelea.

118.*Mheshimiwa Spika,* katika mradi wa Ujenzi wa Jengo la Makao Makuu ya Taasisi ya Teknolojia ya Ujenzi (Institute of Construction Technology – **ICoT),** ujenzi wa jengo jipya la Taaluma na Utawala ICoT Morogoro unaendelea na umefikia asilimia 76. Aidha, **Ujenzi wa Makao Makuu ya Wakala wa Barabara Tanzania (TANROADS),** umefikia asilimia **80**. Vilevile, Serikali inaendelea kutafuta fedha kwa ajili ya ujenzi wa Ofisi za TANROADS Mikoa ya Dar es Salaam, Katavi, Geita, Simiyu, Njombe, Lindi na Songwe.

120. ***Mheshimiwa Spika***, fedha za Mfuko wa Barabara zinatumika kutekeleza miradi mbalimbali ya barabara nchini ikiwemo miradi ya Upembuzi Yakinifu na Usanifu wa Kina. Katika Mwaka wa Fedha 2025/26 Wizara ilipanga kufanya Upembuzi Yakinifu na Usanifu wa Kina wa **kilometa 8,049.67** za barabara kuu kwa kutumia fedha za Mfuko wa Barabara. Hadi Aprili, 2026 Upembuzi Yakinifu na Usanifu wa Kina wa miradi minne (**4)** yenye jumla ya **kilometa 404** umekamilika. Miradi mingine **79** ipo katika hatua mbalimbali za utekelezaji, ambapo miradi **42** yenye jumla ya **kilometa 2,283.32** ipo katika hatua ya Upembuzi Yakinifu na Usanifu wa Kina na miradi **38** yenye jumla ya **kilometa 3,805.1** ipo katika hatua ya ununuzi kama ifuatavyo:-

***a.* Miradi ambayo Upembuzi Yakinifu na Usanifu wa Kina umekamilika:**

*i. Barabara ya Mbalizi - Mkwajuni (Sehemu ya Galula – Mkwajuni - Makongolosi) (km 61);*
*ii. Barabara ya Ngopito - Kimotorok - Singe (Babati) (km 255);*
*iii. Barabara ya Babati (Dareda) - Dongobesh (km 60); na*
*iv. Barabara ya Tengeru – Mererani (km 28).*

**b. Miradi ambayo Upembuzi Yakinifu na Usanifu wa Kina unaendelea:**

i. *Sehemu ya Barabara ya Mlima Kitonga (km 10);*
ii. *Sehemu ya Barabara ya Kizuka – Ngerengere (SGR) (km 9);*
iii. *Barabara ya Bariadi – Salama – Ng'haya – Magu (km 76);*
iv. *Daraja la Bujonde;*
v. *Barabara ya Old Korogwe – Kwandolwa – Magoma -Mabokweni (km 127.54);*
vi. *Barabara ya Longido - Siha (km 56), (Sehemu ya Longido – Tingatinga, (km 38);*
vii. *Barabara ya Katesh - Haydom (km 68);*
viii. *Barabara ya Kimotorok - Sukuro - Terati/Rotiana (km128);*
ix. *Barabara ya Mzunguko wa Kati wa Dodoma (km 47.2);*
x. *Barabara ya Nyankanga - Rung'abure (km 91);*
xi. *Barabara za Mjini Geita (Mtakuja - Buhalahala) sehemu ya barabara kuu ya Nyamuhama - Bwanga - Ibanda (T003) (km 24);*
xii. *Barabara ya Nyakahanga - Nyabiyonza - Nyakakika (km 96);*
xii. *Barabara ya Isongole - Itumba - Shigamba - Ibaba - Katengele Kafwafwa road (138.46km) Including Katengele - Ibungu Spur Road (17km) and Katengele - Isoko Spur Road (6km);*
xiii. *Barabara ya Mbalizi - Shigamba road (52km) and Kyimo - Kafwafwa (21.98km);*
xiv. *Barabara ya Ihumwa - Hombolo - Mayamaya (km55);*
xv. *Barabara ya Sanya Juu (Nyumba Moja) - Longido (km 56) (Sehemu ya Nyumba Moja - Tingatinga (km 15);*
xvi. *Barabara ya Ngongo - Mandawa - Chukuani (km 85);*
xvii. *Barabara ya Gairo – Nongwe (km 55.54);*
xviii. *Barabara ya Miyombo - Lumuma – Kidete (km 71);*

xix. *Barabara ya Mtama - Mkwiti - Newala (km 74);*
xx. *Barabara ya Fulo – Nyambiti – Mallya (km73);*
xxi. *Barabara ya Busisi – Nyang'wale (km 55);*
xxii. *Barabara ya Inyonga – Ilunda – Kishelo – Kitunda (km163);*
xxiii. *Barabara ya Mandera – Mkange - Saadani (km 63);*
xxiv. *Barabara ya Katumbasongwe - Kasumulu - Ngana - Ileje (km 60);*
xxv. *Barabara ya Kalambanzite - Ilemba (km 26);*
xxvi. *Barabara ya Katoma - Kanyigo - Bukwali (km 38.83);*
xxx. *Barabara ya Newala - Makong'onda - Mbuyuni (km 42);*
xxxi. *Barabara ya Rwamishenye - Kyakailabwa (km 3.06);*
xxxii. *Barabara ya Kigarama - Mabira - Kyerwa (km 50.95);*
xxxiii. *Barabara ya Rutenge - Rubale – Kishoju (km74.06);*
xxxii. *Barabara ya Mutukula - Kakunyu (Barabara ya Usalama) (km56);*
xxxiv. *Barabara ya Kwasadala - Kware - Lemira (km 15);*
xxxv. *Barabara ya Mugumu - Fort Ikoma (km 30);*
xxxvi. *Barabara ya Kitama - Litehu - Matipa (km 58);*
xxxvii. *Barabara ya Magu - Mahaha (km 51.3);*
xxxviii. *Barabara ya Bukonyo - Murutunguru - Bukongo (km 14);*
xxxix. *Barabara ya Ngudu – Mallya (km 24);*
xl. *Barabara ya Mchepuo wa Njombe (km 22);*
xli. *Barabara ya Tutuo - Usoke (km 69); na*
xlii. *Barabara ya Balili - Mugeta Chini (km 41.4).*

**c. Miradi ambayo ipo katika taratibu za ununuzi kwa ajili ya kumpata Mhandisi Mshauri wa kufanya Upembuzi Yakinifu na Usanifu wa Kina:**

i. *Barabara ya Mpanda - Ugalla - Kaliua - Ulyankulu – Kahama (Usanifu wa Kina) (km 457);*

ii. *Barabara ya Morogoro (Tumbaku Jct) - Mangae/Melela - Mikumi - Iyovi (km156);*
iii. *Barabara ya Omurushaka - Murongo Sehemu ya Kyerwa - Murongo) (km 75);*
v. *Barabara ya Kibaha - Mlandizi - Chalinze (km 75);*
vi. *Barabara ya Chalinze-Manga (km 93);*
vii. *Barabara ya Ikungi (Singida) - Londoni - Kilimatinde (Solya) (R431) (km117.9);*
viii. *Barabara ya Nyankumbu - Kharumwa - Nyang'holongo - Kahama (km 149);*
ix. *Mpango Kabambe wa Mtandao wa Barabara (National Road Network Master Plan);*
x. *Barabara ya Bariadi - Kisesa - Mwandoya - Ngh'oboko (km 102);*
xi. *Daraja la Sanga;*
xii. *Barabara ya Kisarawe - Bwawa la Mwalimu Nyerere (km 187);*
xiii. *Barabara ya Longido - Kitumbeine – Oldonyolengai (km 98);*
xiv. *Barabara ya Makutano (Zerozero) - Sirari (km 83) na Barabara ya Maingilio ya Tarime (5.4Km);*
xv. *Barabara ya Nachingwea - Liwale - Ilonga - Mwaya - Mahenge (km 345);*
xvi. *Barabara ya Usagara – Kigongo na Busisi – Sengerema (km 56);*
xvii. *Barabara ya Manyoni - Heka - Ikasi – Chaliingongo (Singida/Dodoma Brd) - Kipanga - Kidiho - Bihawana Junction (km 192);*
xviii. *Barabara ya Singida (Magereza) - Mtunduru - Iyumbu (km 113);*
xix. *Barabara ya Mambali – Bukumbi - Ishilimulwa – Shitage – Kahama (km105);*
xx. *Barabara ya Makutano ya Umba – Makutano ya Mkomazi Junction (km 82.24);*
xxi. *Barabara ya Bombomtoni – Makutano ya Umba (km 46.33);*
xxii. *Barabara ya Chimala - Matamba – Kitulo (km 51);*
xxiii. *Barabara ya Maneromango - Vikumburu - Mloka – Geti la Mtemela (km 105);*

xxiv. *Barabara ya Mwandiga - Chankele - Mwangogo – Kagunga (km 60);*
xxv. *Barabara ya Laela - Mwimbi – Kizombwe (km 98);*
xxvi. *Barabara ya Simbo - Ilagala – Kalya (km 234);*
xxvii. *Barabara ya Chenene - Itiso – Izava R.464 (km 72.81);*
xxviii. *Barabara ya Musoma - Makutano Chini (T17) Kuondoa Mafuriko Daraja la Nyasho (km 0.5);*
xxix. *Barabara ya Ilula - Kilolo (km 91);*
xxx. *Barabara ya Ilongo - Usangu (km 36.85);*
xxxi. *Barabara ya Iyogwe - Chakwale - Ngilori (km 41.7);*
xxxii. *Barabara ya Ikonda - Lupila – Mlangali (km 78.84);*
xxxiii. *Barabara ya Kasansa - Muze (km 31.3);*
xxxiv. *Barabara ya Segera - Tanga Harbours (km 74);*
xxxv. *Barabara ya Ngiloli - Chakwale - Iyogwe - Tunguli - Kwekivu (km 70);*
xxxvi. *Barabara ya Bulamata - Mishamo (km 90);*
xxxvii. *Barabara ya Kwaluguru - Songe – Kiberashi (km125.13);*
xxxviii. *Barabara ya Mwembe - Myamba - Ndungu (km 90.10); na*
xxxix. *Daraja la Kilambo na barabara unganishi (TZ/Mozambique Brd).*

121. ***Mheshimiwa Spika***, kupitia Mradi wa **Kuimarisha Uwezo wa Kitengo cha Utafiti na Maendeleo (Research and Development Unit - RDU) katika kupima vifaa vya ujenzi na kuanzisha Teknolojia ya kisasa ya Asphalt Mix Design,** katika mwaka wa fedha 2025/26, Serikali imeendelea kutekeleza shughuli za kuimarisha uwezo wa Kitengo hicho kwa kuboresha mifumo ya usimamizi wa maabara za upimaji (Laboratory Management system), kuendeleza huduma za udhibiti ubora wa vifaa vya ujenzi (Quality Control/Quality Assurance), kuimarisha uwezo wa upimaji wa kazi za barabara za lami, pamoja na kuendeleza/kuhuisha matumizi ya teknolojia na miongozo ya kisasa ya usanifu na uhakiki wa ubora wa majenzi.

**Utekelezaji wa Miradi ya Ujenzi na Ukarabati wa Vivuko na Maegesho ya Vivuko**

122.***Mheshimiwa Spika,*** Katika kuhakikisha wananchi wanaoishi maeneo yaliyotengwa na maji wanapata huduma bora ya usafiri na usafirishaji, Serikali kupitia Wakala wa Ufundi na Umeme Tanzania (TEMESA) imeendelea kufanya uwekezaji mkubwa katika ujenzi, ukarabati na ujenzi wa maegesho ya vivuko katika maeneo hayo. Hadi Aprili, 2026, Wizara imekamilisha baadhi ya miradi na miradi mingine ina endelea kutekelezwa kama ifuatavyo:

123.***Mheshimiwa Spika,*** miradi iliyokamilika ni Ujenzi wa vivuko vitakavyotoa huduma katika maeneo ya Kisorya – Rugezi na Bwiro – Bukondo. Miradi mingine iliyokamilika ni Ujenzi wa maegesho ya Vivuko katika vituo vya Bwiro – Bukondo, Kisorya – Rugezi, na Bukimwi.

124.***Mheshimiwa Spika,*** miradi mingine inayoendelea ni pamoja na maandalizi ya utekelezaji wa awamu ya pili ya upanuzi wa maegesho ya Magogoni – Kigamboni upande wa Kigamboni. Mradi wa usimikaji mfumo wa kielektroniki wa udhibiti matumizi ya mafuta katika vivuko 19 umefikia asilimia 83.

125.***Mheshimiwa Spika,*** miradi mingine inayoendelea kutekelezwa ni ujenzi wa maegesho ya Mayenzi – Kanyinya (asilimia 98), Ijinga – Kahangala (asilimia 90), Buyagu – Mbalika (asilimia 68), Ilunda – Luchelele (asilimia 45), Mlimba – Malinyi (asilimia 40), Chato – Kikumbaitale - Zumacheli (asilimia 95) na Nkome (asilimia 60). Aidha, ujenzi wa maegesho ya NyakaliroKome na miundombinu ya vituo vya Nyakarilo – Kome na Bugorola – Ukara ipo hatua za awali za utekelezaji. Vilevile, miradi ya ujenzi wa maegesho ya Magogoni – Kigamboni, Muleba – Ikuza, Kilambo – Namoto na Kamanga – Kirumba Mwaloni ipo kwenye hatua za ununuzi.

Vilevile, ujenzi wa maegesho ya Rusumo – Nyakiziba na Rugasa pamoja na ukarabati wa maegesho ya Kasharu – Buganguzi upo katika hatua ya usanifu. Aidha, ujenzi/ukarabati wa miundombinu katika vituo vya Ilunda – Luchelele, Buyagu – Mbalika, Ijinga – Kahangala, Kahunda – Maisome na Bezi – Bukimwi ipo katika hatua ya usanifu.

126.***Mheshimiwa Spika,*** kwa upande wa miradi ya ***ununuzi/ujenzi wa vivuko,*** ujenzi wa vivuko vipya vinne (4) umefikia hatua zifuatazo; Ijinga - Kahangala (asilimia 90), Nyakaliro-Kome (asilimia 91), Buyagu – Mbalika (asilimia 90) na Nyamisati – Mafia (asilimia 65).

127.***Mheshimiwa Spika,*** kuhusu miradi ya ***Ukarabati wa Vivuko***, Ukarabati mkubwa wa vivuko uko katika hatua zifuatazo: MV Kilombero II (asilimia 90), MV Nyerere (asilimia 81), MV Magogoni (asilimia 90), MV Ukara I (asilimia 46), MV Kigamboni (asilimia 45) na MV Pangani II (asilimia 58). Ukarabati wa vivuko MV Mafanikio, MV Malagalasi, MV Ukara II na MV Sabasaba upo hatua za awali za kuanza utekelezaji. Aidha, ukarabati wa kivuko MV Mwanza pamoja na boti ya uokoaji (Rescue Boat SAR II) vipo katika hatua ya ununuzi. Utekelezaji wa mradi wa ukarabati wa MV Kome II unasubiri kupatikana kwa kivuko mbadala.

**Utekelezaji wa Miradi ya Ujenzi na Ukarabati wa Nyumba na Majengo ya Serikali**

128.***Mheshimiwa Spika,*** katika kukabiliana na uhaba wa makazi bora unaochochewa na ongezeko kubwa la watu, Serikali imeendelea kuhakikisha wananchi wanapata makazi bora, salama na yenye gharama nafuu. Katika kutekeleza hayo Wizara kupitia Wakala wa Majengo Tanzania (TBA) imeendelea kutekeleza miradi mbalimbali ya ujenzi na ukarabati wa nyumba na majengo ya Serikali.

129.***Mheshimiwa Spika***, utekelezaji wa Awamu ya II ya ***ujenzi wa nyumba nyingine 150 za watumishi wa Umma jijini Dodoma*** eneo la Nzuguni unaendelea. Mradi huu unatekelezwa kwa kuanzia na ujenzi wa nyumba 110 zinazojumuisha nyumba 50 za chini (asilimia 70) na majengo mawili (2) ya ghorofa yenye nyumba 30 kila moja (asilimia 15).

130.***Mheshimiwa Spika***, ujenzi wa nyumba za ***makazi ya watumishi katika eneo la Magomeni Kota Awamu ya II*** jengo C umefikia asilimia 63 na jengo D umefikia asilimia 48. Aidha, ujenzi wa nyumba za ***makazi ya gharama nafuu eneo la Temeke Kota***

Jijini Dar es Salaam umefikia asilimia 47 na ***Ghana Kota*** "Block II", Jijini Mwanza umefikia asilimia 50. Vilevile ujenzi wa nyumba za makazi eneo la Kaloleni Kota Jijini Arusha umefikia asilimia 24.

131.***Mheshimiwa Spika***, mradi wa ***ukarabati wa nyumba 40 za Viongozi jijini Dodoma*** ulihusisha nyumba 13 ambapo, hadi kufikia Aprili, 2026 ukarabati upo katika hatua mbalimbali za utekelezaji. Utekelezaji wa mradi wa ***ukarabati wa nyumba 30 za Viongozi Jijini Dar es Salaam*** unaendelea ambapo hadi kufikia Aprili, 2026 ukarabati wa nyumba kumi (10) unaendelea na upo katika hatua mbalimbali za utekelezaji katika maeneo ya Mikocheni, Oysterbay na Kijitonyama. Aidha, mradi wa ***ukarabati wa nyumba zilizokuwa zinamilikiwa na TAMISEMI*** katika mikoa 20 na kuhamishiwa TBA unaendelea katika mikoa sita (6). Utekelezaji wa miradi hiyo unahusisha mikoa ya Iringa nyumba 61 (asilimia 56), Mara nyumba 18 (asilimia 16), Simiyu nyumba 10 (asilimia 10), Ruvuma nyumba 5 (asilimia 5), Katavi nyumba 12 (asilimia 75), na Tanga nyumba 11 (asilimia 10). Vilevile, mradi wa ukarabati wa nyumba 644 za awamu ya kwanza ya Magomeni Kota Jijini Dar es Salaam unaendelea ambapo hadi kufikia Aprili, 2026 umefikia asilimia 25.

132. ***Mheshimiwa Spika,*** mradi mwingine unaotekelezwa ni ***Ujenzi na Ukarabati wa Karakana za TEMESA na TBA.*** Kwa upande wa TBA, ukarabati wa karakana za samani unatekelezwa katika mikoa ya Mwanza, Mbeya, Dar es Salaam, Tabora, Morogoro na Arusha. Hadi Aprili, 2026, ukarabati wa karakana mbili (2) katika Mikoa ya Mwanza na Dar es Salaam umekamilika. Aidha, ukarabati unaendelea katika mikoa ya Morogoro (asilimia 5), Tabora (asilimia 12), Mbeya (asilimia 8) na Arusha (asilimia 15). Kwa upande wa miradi ya ***ukarabati wa Karakana za Matengenezo ya Magari za TEMESA*** utekelezaji umefikia hatua ifuatayo; karakana ya Mkoa wa Tabora (asilimia 88), Kigoma (asilimia 80), Mwanza (asilimia 78), Arusha (asilimia 65), Mara (asilimia 48), Mtwara (asilimia 45), Dodoma (asilimia 32) na Ruvuma (asilimia 7).

**Udhibiti Uzito wa Magari, Masuala ya Usalama Barabarani na Mazingira**

133.***Mheshimiwa Spika,*** kufuatia ongezeko la matukio ya ajali za barabarani nchini yanayosababisha vifo na majeruhi wengi, Wizara inaendelea kuimarisha usalama na ubora wa miundombinu ya barabara kuu na za mikoa, ili kufikia lengo la Umoja wa Mataifa (UN Decade of Action 2021-2030) la kupunguza ajali kwa asilimia 50 ifikapo mwaka 2030. Hadi kufikia Aprili 2026, kazi zilizofanyika ni pamoja na kufanya ukaguzi wa usalama barabarani kwenye barabara nne **(4)** za Uvinza-Malagarasi, Kazilambwa-Chagu, Iringa-Kilolo na Barabara ya TANZAM Highway inayoanzia mkoa wa Dar es Salaam hadi mkoa wa Songwe kwenye mpaka wa Tunduma ili kutambua maeneo hatarishi. Aidha, ili kuboresha usalama katika Mlima Kitonga mkoani Iringa, umefanyika upanuzi kwa kuongeza njia moja na kuweka vioo (Concave Mirror) maeneo matano **(5)** yenye kona kali ili kuongeza uono na kuwezesha gari kulipita jingine kwa usalama ikiwa ni maboresho ya muda mfupi.

134.***Mheshimiwa Spika,*** kazi nyingine za kuimarisha usalama na ubora wa barabara ni kuendelea na maandalizi ya Mwongozo wa uwekaji wa taa za barabarani, kwa lengo la kuhakikisha uwepo wa viwango vinavyofanana na mwonekano unaolingana nchini kote. Aidha, Wizara imeendelea kuimarisha usalama barabarani kwa kufunga taa za kuongoza magari katika makutano **42**, pamoja na kufunga taa maalum katika vivuko vya waenda kwa miguu vinne (**4)** ili kuwawezesha watembea kwa miguu kuvuka barabara kwa usalama katika majiji ya Dar es Salaam na Dodoma. Jumla ya taa za barabarani **5,542** katika barabara kuu na za mikoa zimefungwa ili kuboresha mwonekano nyakati za usiku na kuongeza usalama, hatua inayochangia kupunguza ajali na vitendo vya uhalifu. Mikoa iliyofunga taa hizo ni Tanga (82), Ruvuma (28), Kilimanjaro (124), Rukwa (98), Dodoma (572), Pwani (160), Songwe (318), Mbeya (176), Simiyu (47), Mwanza (77), Shinyanga (102), Kagera (257), Morogoro (94) Dar es Salaam (182), Geita (320), Arusha (214), Mtwara (725), Lindi (995), Kigoma (179), Katavi (10), Njombe (18), Manyara (70),

Iringa (135), Singida (50) na Tabora (509). Vilevile, njia za waenda kwa miguu zenye urefu wa mita **8,344** zimejengwa katika mikoa yote nchini, ikiwa ni sehemu ya jitihada za kuboresha miundombinu na kulinda usalama wa watumiaji wa barabara.

135. **Mheshimiwa Spika,** Wizara ilipanga kuendelea na majukumu ya udhibiti wa uzito wa magari kupitia mizani **83** ili kulinda uwekezaji wa Serikali katika mtandao wa barabara. Hadi Aprili, 2026 jumla ya magari **7,900,591** yalikuwa yamepimwa ambapo kati ya hayo, magari **18,343** sawa na asilimia **0.23** yalikuwa yamezidisha uzito zaidi ya asilimia 5 ya uzito unaoruhusiwa kisheria ikilinganishwa na asilimia **0.27** katika kipindi hicho mwaka wa fedha 2024/25. Uzidishaji wa uzito wa magari yanayotumia barabara zetu umeendelea kupungua mwaka hadi mwaka kutokana na usimamizi thabiti wa Sheria ya Udhibiti Uzito wa Magari ya Jumuiya ya Afrika Mashariki ya mwaka 2016. Vilevile, Wizara imeendelea kutoa elimu kuhusu Sheria ya Udhibiti Uzito wa Magari ya Jumuiya ya Afrika Mashariki ya mwaka 2016 na kanuni zake za mwaka 2018 kwa wasafirishaji mbalimbali na watumishi wa mizani katika mikoa ya Dar es Salaam na Mwanza.

136. ***Mheshimiwa Spika***, katika Mradi wa ***Usalama Barabarani,*** Taratibu za ununuzi kwa ajili ya kupata Mkandarasi atakayefunga mizani ya kisasa 32 yenye uwezo wa kupima uzito wa magari yakiwa kwenye mwendo (Weighing in Motion System - WIMS) zinaendelea. Awali taratibu za ununuzi wa Mkandarasi zilisitishwa kutokana na gharama za Mkandarasi aliyekidhi vigezo kuwa kubwa zaidi ya bajeti, hivyo kulazimu zabuni hiyo kutangazwa upya. Mizani hiyo itajengwa katika mikoa ya Njombe, Mbeya, Singida, Tabora, Shinyanga, Mwanza, Manyara, Kilimanjaro, Tanga, Pwani, Lindi, Ruvuma na Kagera.

137. ***Mheshimiwa Spika***, Wizara kupitia TANROADS inaendelea na maboresho ya vituo vya mizani kutoka kwenye mizani inayopima mtaimbo mmoja mmoja (Single Axle Weighbridge) na kufunga mizani inayopima kundi la mitaimbo kwa wakati mmoja (Group of Axles Weighbridge). Utekelezaji wa maboresho hayo unafanyika katika vituo vya mizani ya Ilolangulu (Tabora) na umefikia asilimia 60, Makambako (Njombe) asilimia 95, Mkuranga

(Pwani) asilimia 85, Mdori (Manyara) asilimia 80 na Nangurukuru (Lindi) asilimia 95. Aidha, Wizara inaendelea na usanifu na ufungaji wa mifumo ya TEHAMA kwa ajili ya usimamizi wa utendaji kazi wa mizani 83 kwa kutumia wataalam wa ndani.

138.***Mheshimiwa Spika,*** malipo ya fidia ili kupisha ujenzi wa Kituo cha Ukaguzi wa Pamoja (OSIS) cha Iboya (Songwe) yamefanyika na kwa sasa Serikali inatafuta fedha za malipo ya fidia kupisha ujenzi wa OSIS ya Himo (Kilimanjaro). Aidha, Usanifu wa Kina wa miradi ya OSIS ya Idofi (Njombe) na Iboya (Songwe) umekamilika. Serikali inaendelea kutafuta fedha kwa ajili ya ujenzi wa vituo hivyo. Aidha, uthamini kwa ajili ya kulipa fidia ili kupisha ujenzi wa Kituo cha Mizani Kidyama (Kigoma) unaendelea. Serikali inaendelea kutafuta fedha kwa ajili ya Ujenzi wa Kituo hicho pamoja na Kituo cha Mizani Malolegwa (Kigoma).

139.***Mheshimiwa Spika,*** Serikali kupitia Wizara ya Ujenzi na Serikali ya Japan kupitia Shirika la Maendeleo la Japan (JICA) inaendelea kutekeleza mradi wa ushirikiano (Technical Cooperation) katika uimarishaji wa usalama barabarani hapa nchini. Mradi huu unalenga kuboresha mfumo wa usimamizi wa masuala ya usalama barabarani nchini na kuhakikisha taarifa za usalama barabarani zinasimamiwa kikamilifu na kujumuishwa ipasavyo katika Sera.

Aidha, katika kutekeleza mradi huu taasisi mbalimbali zinazohusika na masuala ya usalama barabarani kama vile Wizara ya Elimu Sayansi na Teknolojia, Wizara ya Afya kupitia Hospitali ya Rufaa ya Amana, Jeshi la Polisi Kikosi cha Usalama Barabarani, Jeshi la Zimamoto, Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhi (LATRA), Wakala ya Barabara Vijijini na Mijini (TARURA), Wakala wa Barabara Nchini (TANROADS) pamoja na wadau wengine waamehusishwa. Maboresho ya mfumo wa ukusanyaji wa Taarifa za ajali za barabarani (RAMIS) yanaendelea. Aidha,Wataalam 24 kutoka taasisi zinazohusika na masuala ya usalama barabarani wamepata mafunzo nchini Japan kuhusu masuala ya usalama barabarani.

140.***Mheshimiwa Spika,*** mradi wa ***menejimenti ya usimamizi wa mazingira*** una lengo la kuelimisha na kuwezesha utekelezaji wa Sheria ya Mazingira ya mwaka 2004 katika Sekta ya Ujenzi. Wizara kwa kushirikiana na Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Bunge, Uratibu na wenye Ulemavu) inaendelea na maandalizi ya Mkakati wa Wizara wa Usimamizi wa Maafa. Aidha, maandalizi ya Mpango Tekelezi wa mazingira Sekta ya Ujenzi wa miaka mitano yanaendelea. Vilevile, Wizara kupitia TANROADS imepata vyeti vya tathmini za athari kwa mazingira (EIA Certificate) katika miradi tisa (9) na miradi 16 ya barabara imesajiliwa NEMC kwa ajili ya mapitio ili kupata vyeti vya mazingira.

141.***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeendelea kutoa elimu kwa lengo la kuwajengea uelewa wananchi kuhusu uhifadhi wa mazingira, masuala ya kijamii, usalama na afya mahali pa kazi katika maeneo mbalimbali ya miradi 108 ya ujenzi wa barabara. Aidha, ili kupendezesha mazingira ya barabara na kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi miti 65,728 imepandwa katika hifadhi za barabara za mikoa yote 26 ya Tanzania Bara ikiwemo miti iliyopandwa kupitia mradi wa Kukijanisha Dodoma (Green Solution Project - GSP).

**Utekelezaji wa Miradi ya Ujenzi, Upanuzi na Ukarabati wa Miundombinu ya Viwanja vya Ndege**

142.***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kupitia TANROADS inasimamia ujenzi, ukarabati, upanuzi na uboreshaji wa jumla ya viwanja vya ndege kumi (10) nchini ambavyo imekasimiwa. Utekelezaji wa miradi hiyo hadi kufikia Aprili, 2026 ni kama ifuatavyo:

143.***Mheshimiwa Spika,*** katika mradi wa ujenzi wa **Kiwanja cha Ndege cha Kimataifa cha Msalato,** utekelezaji wa *Package I* unaohusisha ujenzi wa barabara ya kuruka na kutua ndege (runway), barabara ya viungio (taxiway), maegesho ya ndege (apron) pamoja na usimikaji wa taa za usalama na kuongozea ndege umefikia asilimia 85.17 kufuatia ongezeko la mawanda ya mradi. Aidha, utekelezaji wa *Package II* unaohusisha ujenzi wa jengo la abiria, jengo la kuongozea ndege, Kituo cha Zimamoto,

Kituo cha Hali ya Hewa na vituo vidogo nane (8) vya kufua umeme unaendelea na umefikia asilimia 71.52.

144.***Mheshimiwa Spika,*** katika **Kiwanja cha Ndege cha Kigoma,** kazi za ujenzi wa Jengo la Abiria pamoja na miundombinu yake, ukarabati na upanuzi wa maegesho ya ndege, maegesho ya magari na barabara ya kuingia na kutoka kiwanjani, usimikaji wa taa na mitambo ya kuongozea ndege, ujenzi wa uzio wa usalama, jengo la kuongozea ndege na jengo la uchunguzi wa hali ya hewa zinaendelea na utekelezaji umefikia asilimia **50.16**.

145.***Mheshimiwa Spika,*** katika **Kiwanja cha Ndege cha Tabora,** kazi za ujenzi wa Jengo la Abiria na miundombinu yake, jengo la kuongozea ndege, barabara ya kuingia kiwanjani, maegesho ya magari, uzio wa usalama pamoja na jengo la uchunguzi wa hali ya hewa zimekamilika.

146.***Mheshimiwa Spika,*** mradi wa uboreshaji na ukarabati wa **kiwanja cha Ndege cha Sumbawanga** unaohusisha kazi za ujenzi wa barabara ya kutua na kuruka ndege na kiungio chake, maegesho ya ndege, jengo la abiria, jengo la kuongozea ndege, jengo la uchunguzi wa hali ya hewa, uzio wa usalama, barabara ya kuingia na kutoka kiwanjani, maegesho ya magari pamoja na usimikaji wa taa na mitambo ya kuongozea ndege umefikia asilimia 96.

147.***Mheshimiwa Spika,*** kazi za ujenzi wa barabara ya kutua na kuruka ndege na kiungio chake, maegesho ya ndege, jengo la abiria, jengo la kuongozea ndege, jengo la uchunguzi wa hali ya hewa, uzio wa usalama, barabara ya kuingia na kutoka kiwanjani, maegesho ya magari pamoja na usimikaji wa taa na mitambo ya kuongozea ndege katika **Kiwanja cha ndege cha Shinyanga** zimefikia asilimia 96.5.

148.***Mheshimiwa Spika,*** kazi ya upanuzi na ukarabati wa barabara ya kutua na kuruka ndege, maegesho ya ndege, barabara ya kiungio na uzio wa usalama katika **kiwanja cha Ndege cha Musoma** inaendelea na utekelezaji umefikia asilimia 67.

149.***Mheshimiwa Spika,*** katika **kiwanja cha Ndege cha Iringa,** utekelezaji wa Awamu ya II unaohusisha ujenzi wa Jengo la Abiria, mnara wa kuongozea ndege, pamoja na maegesho ya magari umefikia asilimia 16.

150.***Mheshimiwa Spika,*** kazi ya ujenzi wa uzio wa usalama na barabara ya mzunguko katika **Kiwanja cha Ndege cha Geita** imekamilika.

151.***Mheshimiwa Spika,*** kazi za ukarabati na uboreshaji wa barabara ya kuruka na kutua ndege, ujenzi wa maegesho ya ndege, barabara za viungio, jengo la umeme na jengo la abiria lenye mnara wa kuongozea ndege na usimikaji wa taa za kuongozea ndege na taa za usalama katika **Kiwanja cha ndege cha Lake Manyara** zipo katika hatua za maandalizi.

152.***Mheshimiwa Spika,*** kazi za ukarabati na upanuzi wa barabara ya kutua na kuruka ndege, barabara ya kiungio, maegesho ya ndege, ujenzi wa uzio wa usalama, jengo la abiria na barabara ya kuingia kiwanjani, kituo cha zimamoto, ununuzi na usimikaji wa taa na mitambo ya kuongozea ndege pamoja na ununuzi wa gari la zimamoto katika **Kiwanja cha ndege cha Tanga** zimefikia asilimia 2.1

**B.3 UTENDAJI WA TAASISI ZILIZO CHINI YA WIZARA YA UJENZI**

153. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara ya Ujenzi ina Taasisi tisa (9) inazosisimamia ambazo zinatekeleza majukumu ya Sekta ya Ujenzi. Utekelezaji wa majukumu ya Taasisi hizo hadi kufikia Aprili, 2025 ni kama ifuatavyo:

**Bodi ya Mfuko wa Barabara**

154.***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2025/26, Bodi ilipanga kukusanya jumla ya Shilingi **945,794,956,001**. Kati ya fedha hizo, Shilingi **688,756,470,000** ni kwa ajili ya kazi zinazosimamiwa na Wizara ya Ujenzi. Aidha, kiasi cha **Shilingi 257,038,486,001** zilitengwa kwa ajili ya kugharamia kazi zinazosimamiwa na Ofisi ya Waziri Mkuu – TAMISEMI. Hadi Aprili,

2026 Bodi imekusanya jumla ya **Shilingi 682,595,140,010** sawa na asilimia **69** ya bajeti ya mwaka.

155.***Mheshimiwa Spika,*** Bodi imefanya ukaguzi wa ubora wa kazi za matengenezo ya barabara ili kupata thamani halisi ya fedha katika miradi inayotekelezwa. Hadi kufikia Aprili, 2026, jumla ya miradi 189 yenye thamani ya **Shilingi 166,100,603,634.15** ilifanyiwa ukaguzi kwa kutumia wataalam washauri na miradi 40 kwa kutumia wataalam wa ndani. Aidha, Bodi imeendelea kufanya tathmini juu ya vyanzo vipya vya mapato ya Mfuko ambapo hadi kufikia Aprili, 2026 rasimu ya mapendekezo ya vyanzo vipya viwili (2) imeandaliwa na kuwasilishwa Wizara ya Fedha. Kazi nyingine ni kuratibu na kutekeleza zoezi la kuchukua takwimu na taarifa za hali ya barabara (road inventory and condition survey) kwa lengo la kuzitumia katika kuandaa mipango kazi na utekelezaji wa kazi za barabara.

156.***Mheshimiwa Spika,*** vilevile, Bodi imekamilisha utengenezaji wa mfumo wa kidijitali unaoitwa *Tanzania Roads Database Management System (TRDMS)* kwa ajili ya kukusanya, kuhifadhi, kusimamia, kuchambua na kuonesha taarifa za mtandao wa barabara nchini. Mfumo huu utatumika katika kuweka vipaumbele vya matengenezo, kufuatilia matumizi ya fedha na kuboresha uwajibikaji. Aidha, Bodi kwa kushirikiana na TANROADS na TARURA imetengeneza mfumo wa *Roads eRevenue Management System (ReRIS).* Mfumo huu umelenga kurahisisha na kuweka kidijitali taarifa za ukusanyaji wa mapato yatokanayo na matumizi ya hifadhi ya barabara.

**Wakala wa Majengo Tanzania**

157.***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2025/26, Wakala wa Majengo Tanzania (TBA) umeendelea kutekeleza majukumu yake kwa kutumia fedha za ruzuku ya Serikali pamoja na mapato ya ndani ya Wakala. Kazi zinazotekelezwa ni pamoja na kutoa huduma za ushauri kwa miradi ya ujenzi wa majengo ya Serikali, kujenga majengo ya Washitiri mbalimbali pamoja na kuuza na kupangisha nyumba na majengo ya Serikali ili kuongeza uwezo wa Wakala kujiendesha.

158.***Mheshimiwa Spika,*** miradi iliyotekelezwa kwa kutumia fedha za ndani za Wakala ni pamoja na ujenzi wa majengo mawili ya ghorofa kwa watumishi wa Umma eneo la Canadian Masaki, Dar es Salaam ''Block II" na III ambao umekamilika; Ujenzi wa ofisi ya TBA Mkoa wa Geita umefikia asilimia 60 na ujenzi wa Ghorofa za Watumishi wa Umma za Ghana Kota ''Block I" jijini Mwanza ambao umefikia asilimia 74. Ukarabati wa Majengo mbalimbali nchini umefanyika katika Mikoa ya Dar es Salaam (13), Dodoma (5), Katavi (12), Arusha (1), Shinyanga (1), Geita (1), Mara (2), Mwanza (1), Mbeya (8), Lindi (2), Iringa (1), Tabora (1), Kigoma (1) na Njombe (5). Aidha, Wakala umekarabati ofisi za TBA katika mikoa ya Songwe na ofisi ndogo ya Makao Makuu Jijini Dar es Salaam.

159.***Mheshimiwa Spika,*** Wakala pia umetekeleza miradi 95 ya Washitiri. Miradi hiyo ni pamoja na miradi nane (8) ya Buni Jenga (Design and Build) ambayo ni ujenzi wa nyumba ya makazi ya Mkuu wa Mkoa wa Geita, ujenzi wa jengo la Ofisi ya Halmashauri ya mji wa Bariadi mkoani Simiyu na ujenzi wa Ofisi ya Mkuu wa Wilaya Butiama Mkoa wa Mara ambayo imekamilika. Miradi mingine ni ujenzi wa wodi na Jengo la Mionzi katika Hospitali ya Rufaa ya Kanda ya Buigiri – Chato awamu ya II ambao umefikia asilimia 91, ujenzi wa ofisi ya Mkuu wa Wilaya ya Nkasi ambao umefikia asilimia 95, ujenzi wa jengo la ofisi ya Tanesco Mkoa wa Kilimajaro ambao umefikia asilimia 65, ujenzi wa ofisi za Bodi ya Tumbaku Mkoa wa Tabora Wilaya ya Kaliua ambao umefikia asilimia 55 na ujenzi wa Jengo la Utawala Halmashauri ya Ifakara awamu ya II ambao umefikia asilimia 3.

160.***Mheshimiwa Spika,*** Wakala pia umeendelea kutoa huduma ya ushauri katika miradi ya ujenzi wa majengo ya Ofisi za Wizara 13 na Taasisi sita (6) katika Mji wa Serikali eneo la Mtumba Dodoma ambapo utekelezaji wa miradi hii upo katika hatua mbalimbali.

161.***Mheshimiwa Spika,*** vilevile, Wakala umetekeleza miradi 61 ya Ushauri (Consultancy). Miongoni mwa miradi hiyo, 12 imekamilika. Aidha, miradi inayoendelea ni pamoja na kutoa huduma za ushauri katika Ukarabati mkubwa wa viwanja vya

Benjamin Mkapa na Uhuru Jijini Dar es Salaam ambao umefikia asilimia 90 na asilimia 62 mtawalia, ujenzi wa miundombinu katika Soko la Bunazi Kagera ambao umefikia asilimia 70, ujenzi wa Ofisi za Makao Makuu ya Ruwasa Jijini Dodoma umefikia asilimia 78 na ujenzi wa Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Morogoro umefikia asilimia 80.

162. ***Mheshimiwa Spika,*** Wakala vilevile umetekeleza miradi tisa (9) ya ujenzi na ukarabati. Miradi iliyotekelezwa ni pamoja na ujenzi wa jengo la Utawala Halmashauri ya Wilaya ya Serengeti umefikia asilimia 32, ujenzi wa Jengo la Halmashauri ya Wilaya ya Kilosa umefikia asilimia 73, upanuzi na ukarabati wa jengo la utawala katika Hospitali ya Magonjwa Ambukizi Kibong'oto mkoani Kilimanjaro umefikia asilimia 80 na ukarabati wa jengo la NIDA Kibaha umefikia asilimia 70.

163. ***Mheshimiwa Spika,*** Wakala pia ulitekeleza mradi mmoja (1) wa Usimamizi (Project Management) ambao ulihusisha usimamizi wa mifumo ya joto, hewa na viyoyozi; mifumo ya umeme; mifumo ya vitambua moto na vitoa sauti; mifumo ya majisafi na majitaka; mitambo ya kangavuke (generators) na transfoma pamoja na usimamizi wa samani katika Ukumbi wa Bunge Dodoma.

**Wakala wa Ufundi na Umeme Tanzania**

164. ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka wa fedha 2025/26, Wakala wa Ufundi na Umeme Tanzania (TEMESA) ulipanga kufanya matengenezo ya magari, pikipiki na mitambo ya Serikali; kusimika na kufanya matengenezo na kutoa ushauri katika mifumo ya umeme, elektroniki, majokofu na viyoyozi kwenye majengo ya Serikali. Kazi nyingine ni uendeshaji wa shughuli za usafiri wa vivuko vya Serikali zinazohusisha ujenzi na ukarabati wa vivuko, maegesho na miundombinu ya vivuko (majengo na uzio).

165. ***Mheshimiwa Spika,*** hadi Aprili, 2026, utekelezaji wa miradi ya ***maegesho ya vivuko***, ***Ukarabati wa Vivuko, Ujenzi wa Vivuko Vipya*** na ***Ujenzi na Ukarabati wa Karakana*** kwa kutumia fedha za ruzuku ni kama inavyooneshwa katika **Aya 122-127.**

166.***Mheshimiwa Spika,*** Wakala pia ulipanga kutekeleza ***Miradi ya Washitiri na Ushauri*** iliyohusisha kufanya matengenezo ya magari **40,235**, matengenezo na usimikaji wa mifumo **741** ya umeme, **744** ya majokofu na viyoyozi na mifumo **173** ya elektroniki. Aidha, Wakala ulipanga kutoa ushauri wa Kihandisi kwa miradi ya usimikaji wa mifumo **146** ya umeme, mitambo, elektroniki, viyoyozi na majokofu na kusimamia mifumo hiyo. Wakala pia ulipanga kuendelea na usimamizi wa vivuko vya Serikali **32** na ukodishaji wa mitambo ya ujenzi wa barabara.

167.***Mheshimiwa Spika,*** hadi Aprili, 2026, Wakala umefanya matengenezo ya magari **8,067** ikilinganishwa na lengo la matengenezo ya magari 40,235. Hali hii imetokana na kuanzishwa kwa matumizi ya Mfumo wa Usimamizi wa Matengenezo (MUM), unaomlazimu Mshitiri kulipia gharama za matengenezo kabla. Matumizi ya mfumo huu yamewezesha Wakala kukabiliana na changamoto ya kutolipwa au kucheleweshewa malipo ya matengenezo ya magari ya washitiri.

168.***Mheshimiwa Spika,*** Wakala pia umefanya kazi ya usimikaji wa mifumo ya umeme **332**, elektroniki **14**, viyoyozi na majokofu **331**. Miradi **40** ya usanifu wa kazi za umeme, mitambo na elektroniki imetekelezwa. Aidha, Wakala kupitia huduma za vivuko umevusha abiria wapatao **3,283,482**, tani za mizigo **68,462** na magari **339,076**. Vilevile, Wakala unaendelea na usimamizi vivuko **32** katika vituo **22** nchi nzima. na ukodishaji wa mitambo kwa ajili ya kazi za ujenzi.

**Bodi ya Usajili ya Wabunifu Majengo na Wakadiriaji Majenzi (AQRB)**

169.***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kupitia Bodi ya Usajili wa Wabunifu Majengo na Wakadiriaji Majenzi (AQRB) inatekeleza majukumu ya kusajili, kusimamia na kuratibu mienendo ya Wabunifu Majengo (Architects) na Wakadiriaji Majenzi (Quantity Surveyors), Wasimamizi wa Miradi (Project Managers) pamoja na Kampuni za Ushauri Elekezi katika fani zilizotajwa hapo juu. Aidha, Bodi ina jukumu la kukagua sehemu ambazo shughuli za ujenzi

zinafanyika ili kuhakikisha kuwa ubunifu, ukadiriaji na usimamizi wa ujenzi unafanywa na wataalam waliosajiliwa na Bodi.

170.***Mheshimiwa Spika,*** Katika kutekeleza majukumu hayo AQRB imefanikiwa kusajili wataalam 163 sawa na asilimia 72.4 ya lengo la mwaka na Wataalam wa Kati (semi-professionals) 174 sawa na asilimia 55.6. Kwa upande wa kampuni za ushauri, Bodi imesajili kampuni 42 sawa na asilimia 117 ya lengo. Bodi imesajili miradi 1,416 sawa na asilimia 79 ya lengo na kukagua miradi 4,480 sawa na asilimia 105.5 ya lengo, hatua inayoonesha kuimarika kwa usimamizi wa sekta.

171.***Mheshimiwa Spika,*** kati ya miradi iliyokaguliwa, miradi 727 ilibainika kuwa na dosari. Hatua zilizochukuliwa kwa wavunjaji wa sheria ni pamoja na kutozwa faini, kusimamishwa au kufutiwa usajili kwa wataalam husika, pamoja na kufikishwa mahakamani pale ilipobidi. Aidha, waendelezaji 126 wamefikishwa mahakamani kwa kutokufuata matakwa ya sheria. Bodi itaendelea kuchukua hatua kali zaidi kwa wavunjaji wa sheria ili kuhakikisha uzingatiaji wa viwango, ubora na usalama wa miradi ya ujenzi.

**Baraza la Taifa la Ujenzi (NCC)**

172.***Mheshimiwa Spika,*** Wizara ya Ujenzi kupitia Baraza la Taifa la Ujenzi ina jukumu la kutoa ushauri wa kitalaam katika Sekta ya Ujenzi. Kazi zilizofanyika hadi kufikia Aprili, 2026 ni pamoja na kutoa huduma za ushauri wa kitaalam katika Mradi wa Kuimarisha Elimu ya Sekondari (SEQUIP), kwenye miradi 30 katika mikoa 10. Ushauri huu umewezesha kuboresha ujenzi wa majengo mbalimbali katika mradi wa SEQUIP.

173.***Mheshimiwa Spika,*** kazi nyingine ni kutoa ushauri wa kiufundi na kitalaam kwa wadau wa sekta ya ujenzi ikiwemo NSSF na Wizara ya Fedha; kuendelea kuandaa Mwongozo wa Usimamizi wa Mikataba ya Ujenzi wa Barabara (Contract Management and Administration Manual). Aidha, Baraza liliendelea kuratibu utatuzi wa migogoro 24 inayojumuisha migogoro 18 ya usuluhishi (Arbitration) na migogoro sita (6) ni ya usuluhishi wa awali

(Adjudication). Usimamizi huu umewezesha miradi hii ya ujenzi kuendelea na utekelezaji wake badala ya kusimama.

174.***Mheshimiwa Spika,*** vilevile, Baraza limeendelea kutoa mafunzo (training) kwa kozi za majadiliano ya kimkataba katika miradi ya ujenzi (Construction Contract Negotiation) na kozi maalum kwa wafanyakazi wa TANROADS katika usimamizi wa mabadiliko ya bei katika mikataba (Management of Price Adjustment Clause). Mafunzo haya yamejenga uwezo kwa wataalam 160 katika usimamizi wenye tija wa mikataba ya ujenzi.

175.***Mheshimiwa Spika,*** Baraza pia limeandaa Fahirisi za bei za vifaa, mitambo na ujira wa mafundi ujenzi (Construction Resources Price Indices) kwa kila mwezi kwa kipindi husika pamoja na kuendelea na maandalizi ya Miongozo ya Gharama za Ujenzi na Matengenezo ya Barabara kwa kila mkoa (Base Unit Rates for Road Construction and Maintenance Works). **Taasisi ya Teknolojia ya Ujenzi (ICoT).**

176.***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kupitia Taasisi ya Teknolojia ya Ujenzi (ICoT) imeendelea kutoa mafunzo katika fani za Uhandisi (Ujenzi, Umeme na Mitambo) kwa ngazi ya Stashahada na Elimu ya Ufundi Stadi. Kazi zilizofanyika hadi Aprili, 2026 ni pamoja na kudahili wanafunzi 112 wapya kwa ngazi ya cheti 'NTA Level 4' na kutoa mafunzo kwa wanafunzi 197 wa 'NTA Level 5 & 6' ambao wanaendelea na masomo katika fani za uhandisi Ujenzi, Umeme na Mitambo. Hivyo, jumla ya wanafunzi wanaoendelea na masomo ni 309 katika ngazi ya Stashahada (NTA Level 4 – 6).

177.***Mheshimiwa Spika,*** Taasisi pia imedahili wanafunzi wapya 152 wa 'VET Level I' na 74 'VET Level III' na kutoa mafunzo kwa wanafunzi 162 wa 'VET Level II' wanaondelea na masomo. Hivyo, jumla ya wanafunzi 388 wa Elimu ya Mafunzo ya Ufundi Stadi (VET Level I-III) wanaendelea na masomo. Kazi nyingine ni pamoja na kuhuisha mitaala ya ICoT kwa ngazi za NTA Level 4 – 6 kwa fani za uhandisi ujenzi, umeme, na mitambo.

178.***Mheshimiwa Spika,*** kazi nyingine ni kutoa mafunzo ya Udereva wa awali na Umma kwa awamu tano (5) ambapo jumla

ya washiriki 346 walipata mafunzo. Aidha, Taasisi imeeendesha kozi tatu (3) kuhusu matumizi ya Teknolojia Stahiki ya Nguvukazi katika Ujenzi, Ukarabati na Matengenezo ya Barabara za udongo na changarawe kwa washiriki 68.

**Bodi ya Usajili wa Wakandarasi (CRB)**

179.***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kupitia Bodi ya Usajili wa Wakandarasi ilisajili wakandarasi 1,258 hadi Aprili, 2026 sawa na asilimia 78 ya lengo na hivyo kufanya jumla ya wakandarasi waliosajiliwa katika rejesta ya Bodi kufikia **12,573**. Kati ya hao, wakandarasi **12,317** sawa na asilimia **98** ni wa ndani. Ongezeko la wakandarasi waliosajiliwa linaongeza ushindani katika soko na hivyo kuwezesha waajiri, ikiwemo Serikali kupata bei zenye ushindani zaidi. Hii inasaidia Serikali kupata thamani ya fedha (value for money) kwa miradi inayotekelezwa. Aidha wakandarasi wanatoa fursa za ajira (za kudumu na za muda mfupi) kwa wananchi katika utekelezaji wa miradi ya ujenzi.

180.***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi hicho, jumla ya miradi 2,402 sawa na asilimia 69.6 ya malengo ya mwaka ilikaguliwa. Miradi 1,385 ambayo ni sawa na asilimia 58 ya miradi yote iliyokaguliwa haikuwa na mapungufu na miradi 1,017 sawa na asilimia 42 ilipatikana na mapungufu mbalimbali yakiwemo, kutozingatia usalama kazini, kutosajili miradi na kufanya kazi za thamani inayozidi kiwango kinachoruhusiwa kwa daraja husika.

181.***Mheshimiwa Spika,*** ukaguzi wa miradi unaiwezesha Serikali kuhakikisha kwamba miradi ya ujenzi nchini inatekelezwa na Wakandarasi waliosajiliwa kwa kukidhi vigezo vya kisheria. Hii inasaidia miradi kutekelezwa kwa viwango na muda uliokubalika. Kupitia ukaguzi wa miradi, Serikali inanufaika kwa sababu miradi itatekelezwa kwa kuzingatia usalama wa wafanyakazi na umma kwa ujumla na pia miradi inatekelezwa kwa wakati hivyo wananchi kupata huduma iliyokusudiwa na Serikali yao kwa wakati na kwa viwango vilivyokusudiwa.

Aidha, miradi inapotekelezwa na wakandarasi waliosajiliwa, Serikali inapata taarifa sahihi za miradi husika na hivyo kurahisisha

upatikanaji wa taarifa zinazosaidia kwa namna mbalimbali ikiwemo ufuatiliaji wa ulipaji kodi sahihi.

182.***Mheshimiwa Spika,*** vilevile, Bodi iliendesha kozi za mafunzo tatu (3) katika vituo vitatu (3) kupitia Mpango Maalum wa Mafunzo Endelevu kwa Wakandarasi (Sustainable Structured Training Programme – SSTP) katika mikoa ya Dodoma, Iringa na Mwanza. Jumla ya wakandarasi 256 walishiriki katika mafunzo hayo.

Mafunzo kwa wakandarasi yanalenga kuongeza ushindani wa wakandarasi kwa kuboresha ujuzi wao katika maeneo ya kiufundi na kiusimamizi hivyo kuboresha uwezo wa kutekeleza miradi yao kwa ufanisi zaidi. Serikali inanufaika kwa sababu miradi yake itatekelezwa kwa wakati na kwa viwango vilivyokubalika na hivyo huduma iliyokusudiwa kuwafikia wananchi.

183.***Mheshimiwa Spika,*** Bodi pia iliendelea kuendesha mfuko wa kuwezesha wakandarasi (Contractors Assistance Fund - CAF) unaotoa dhamana za zabuni na malipo ya awali kwa wakandarasi wa ndani 'Advance Payment Guarantee' ili kuwezesha ushiriki wa wakandarasi hao katika zabuni na utekelezaji wa miradi mbalimbali. Mtaji wa mfuko huu umekua kutoka shilingi Bilioni 4.4 kwa mwaka wa fedha 2024/25 hadi kufikia shilingi Bilioni 4.5 kwa mwaka wa fedha 2025/26. Aidha, idadi ya wanachama wa mfuko imeongezeka kutoka 1,466 mwaka wa fedha 2024/25 hadi kufikia wanachama 1,479 mwaka wa fedha 2025/26.

Kupitia dhamana zinazotolewa na Mfuko, wakandarasi wengi zaidi wanashiriki zabuni na hivyo kuongeza ushindani hivyo Serikali inafaidika kwa kupata bei shindani zaidi na miradi yake kutekelezwa kwa wakati. Vilevile kwa kupata malipo ya awali kupitia dhamana zitolewazo na mfuko, Serikali inawapunguzia wakandarasi adha ya kutafuta dhamana za mikopo (collateral) ili kupata fedha za kuanzia utekelezaji. Pia inawawezesha wakandarasi kuanza utekelezaji wa miradi kwa wakati.

**Bodi ya Usajili wa Wahandisi (ERB)**

184.***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kupitia Bodi ya Usajili wa Wahandisi, imesajili wahandisi 2,429 sawa na asilimia 64 ya lengo, mafundi sanifu 317 sawa na asilimia 63.4, makampuni ya ushauri wa kihandisi saba (7) sawa na asilimia 39 na maabara moja (1) ya vifaa vya ujenzi na uhandisi sawa na asilimia 20 ya lengo la mwaka. Usajili huu umefikisha jumla ya wahandisi waliosajiliwa katika ngazi mbalimbali kuwa 46,084, makampuni ya ushauri wa kihandisi kuwa 476 na maabara za kihandisi kuwa 56. Kati ya jumla ya wahandisi waliosajiliwa 42,606 ni Watanzania na 3,478 ni wageni. Makampuni ya ushauri wa kihandisi ya Kitanzania ni 331 na ya kigeni ni 145. Aidha, Bodi imesajili miradi 1,215 kati ya miradi 3,500 iliyopangwa. Pia imekagua viwanda na Majengo 341 kati ya 130 yaliyopangwa.

185.***Mheshimiwa Spika,*** Mafunzo elekezi kwa Wahandisi Wahitimu na kwa Mafundi Sanifu yalitolewa kwa awamu mbili (2). Vilevile, Bodi iliendelea kuwaapisha Wahandisi Wataalam Kiapo cha Utii kwa Taaluma (Professional Oath) ambapo jumla ya wahandisi 555 wameapishwa katika mwaka wa fedha 2025/26.

186.***Mheshimiwa Spika,*** vilevile, Bodi iliendelea kusimamia utekelezaji wa Mpango wa Mafunzo kwa Vitendo kwa Wahandisi Wahitimu 3,857. Jumla ya wahandisi wahitimu 15,689 wamepitia Mpango huu tangu uanzishwe mwaka 2003.

Bodi iliandaa na kuadhimisha Siku ya Wahandisi (Annual Engineers Day 2025) ambapo wahandisi na wadau wengine wa tasnia 4,578 walishiriki. Mada iliyojadiliwa katika siku hiyo ilikuwa ni Dira ya Maendeleo 2025 iliyotimizwa na kusonga mbele kuelekea Dira ya Maendeleo 2050 (Achieved Vision 2025 and Advancing Towards Vision 2050; The Role of Engineers).

**Kituo cha Usambazaji wa Teknolojia Katika Sekta ya Ujenzi na Usafirishaji (Tanzania Transportation Technology Transfer Centre)**

187.***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2025/ 26, Kituo kwa kushirikiana na TARA kiliandaa na kuendesha mafunzo kwa

wadau wa Sekta ya Ujenzi na Usafirishaji yaliyofanyika Septemba, 2025 na Disemba, 2025 kwa ajili ya kujenga uwezo katika sekta. Aidha, Kituo kimeendelea na taratibu za kuboresha Maktaba Mtandao (e-library) kupitia Taasisi ya Teknolojia ya Ujenzi (ICoT) ili kuendeleza huduma za usambazaji wa teknolojia kwa njia ya kidijitali.

188. ***Mheshimiwa Spika,*** vilevile, Wizara kupitia Kituo imeendelea kuratibu uanzishwaji na uendeshaji wa Taasisi ya Teknolojia ya Ujenzi (ICoT) kwa kuwezesha hatua mbalimbali za uanzishwaji; kuwezesha mafunzo ya kujenga uwezo kwa wahandisi ndani ya Wizara na kufanikisha kuhamisha maktaba yake (Physical Library) kutoka Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kwenda Dodoma.

189. ***Mheshimiwa Spika,*** Kituo pia kimeendelea kushirikiana na Kitengo cha Utafiti na Maendeleo (Research Development Unit - RDU) cha Wakala wa Barabara Tanzania (TANROADS) kufanya tafiti na tathmini kuhusu matumizi ya teknolojia mpya/ mbadala. Lengo ni kuwezesha Wizara kupata teknolojia stahiki zenye ufanisi na gharama nafuu kwenye utekelezaji wa miradi.

1. ***Mheshimiwa Spika***, katika kuimarisha uwezo na kubadilishana uzoefu, Kituo kimeshiriki katika mkutano wa kikanda wa Kamati ya Kujenga Uwezo na Usambazaji wa Teknolojia ya Usafirishaji ya SADC chini ya Shirikisho la Barabara la nchi za Kusini mwa Afrika (ASANRA) uliofanyika mwezi Novemba, 2025 nchini Namibia, ambao ulihusu masuala ya kuendeleza na kusambaza teknolojia katika sekta za Ujenzi na Usafirishaji pamoja na kujadili kuhusu maandalizi ya Mkutano wa 10 wa Vituo vya Usambazaji wa Teknolojia Afrika (10th $T^2$ Centre Conference) ambao utafanyika mwezi Oktoba, 2026 nchini Malawi.

## B.4. MASUALA MTAMBUKA

### Ushirikishwaji wa Wanawake katika Kazi za Barabara

190.***Mheshimiwa Spika***, katika kuimarisha ushiriki wa wanawake katika kazi za barabara, mwaka wa fedha 2025/26, Wizara kupitia Kitengo cha Ushirikishwaji wa Wanawake imeendelea kutekeleza majukumu yanayojumuisha maboresho ya kanzi data ya ushirikishwaji wa wanawake, ambayo sasa inahifadhi na kufuatilia taarifa za ushiriki wa wanawake katika miradi ya barabara kwa ufanisi zaidi. Vilevile, Kitengo kimeendelea na maboresho ya muongozo wa ushirikishwaji wa wanawake katika sekta ya ujenzi, ili kutoa mwongozo thabiti kwa wadau wote kuhusu namna bora ya kuwashirikisha wanawake katika miradi ya ujenzi.

191.***Mheshimiwa Spika,*** sambamba na maboresho hayo, Kitengo kimeendelea kufanya ukaguzi wa kazi zinazotekelezwa na wakandarasi wanawake katika mikoa mbalimbali, kwa lengo la kuhakikisha ubora wa kazi na usawa wa fursa katika utekelezaji wa miradi. Hatua hizi zimeimarisha uwezo wa Wizara kufuatilia maendeleo ya wakandarasi wanawake na kutoa msingi thabiti wa kuendeleza ushiriki wao katika sekta ya barabara.

### Matumizi ya Teknolojia Mpya katika Ujenzi na Matengenezo ya Barabara

192.***Mheshimiwa Spika***, Wizara inaendelea na matumizi ya teknolojia mpya katika ujenzi na matengenezo ya barabara ili kuongeza uimara, ubora na ufanisi wa gharama za miundombinu ya barabara nchini. Kupitia Kitengo cha Utafiti na Maendeleo (RDU), cha TANROADS Serikali imeendelea kufanya tafiti na tathmini za vifaa vya ujenzi, mchanganyiko wa lami, pamoja na mbinu mbalimbali za kisasa zinazowezesha barabara kudumu zaidi chini ya mizigo mikubwa na hali tofauti za mazingira.

193.***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka huu, Wizara imeendelea kuhimiza matumizi ya teknolojia za kisasa za lami ikiwemo *Stone Mastic Asphalt* (SMA), *Dense Graded Asphalt* (DGA), na matumizi ya miongozo ya kitaalam iliyoandaliwa na RDU kwa ajili ya

kuboresha usanifu wa mchanganyiko wa lami na kuongeza ubora wa kazi za barabara. Teknolojia hizi zinasaidia kupata tabaka za lami zenye uhimili mkubwa zaidi, matumizi bora ya malighafi, na huduma ya muda mrefu kwa barabara zinazopokea mizigo mikubwa.

194.***Mheshimiwa Spika***, sambamba na hilo, Wizara inaendelea kutumia teknolojia za kisasa za uchunguzi na tathmini ya miundombinu ya barabara, ikiwemo *Falling Weight Deflectometer* (FWD), *Ground Penetrating Radar* (GPR), *Laser Cracking Measurement System* (LCMS) na vifaa vingine vya kisasa vinavyowezesha kupata taarifa sahihi za hali ya tabaka za barabara wakati wa ujenzi na matengenezo. Matumizi ya teknolojia hizi yanaimarisha maamuzi ya kiuhandisi, hupunguza makosa ya utekelezaji, na kuongeza ufanisi wa usimamizi wa miradi.

195.***Mheshimiwa Spika***, aidha, Wizara kupitia RDU imeendelea kuimarisha matumizi ya teknolojia za kisasa katika usimamizi wa ubora wa maabara na kazi za barabara kwa kutumia *Laboratory Quality Performance Index* (LQPI), tafiti za ubora wa vifaa vya ujenzi, pamoja na maboresho ya mifumo ya upimaji na udhibiti wa ubora. Hatua hizi zinaweka msingi imara wa matumizi ya sayansi, teknolojia na ubunifu katika kuhakikisha barabara zinazojengwa na kutunzwa zinakuwa salama, imara na zenye kudumu kwa muda mrefu.

**Ushirikishwaji wa Sekta Binafsi Katika Miradi ya Ujenzi**

196. ***Mheshimiwa Spika***, katika kukuza ushiriki wa Sekta Binafsi, Wizara ipo katika hatua mbalimbali za utekelezaji wa miradi ya ushirikiano wa Sekta ya Umma na Sekta Binafsi (PPP). Hadi kufikia Aprili, 2026 Wizara imeendelea na maandalizi ya utekelezaji wa miradi minne (4) ya barabara kwa utaratibu wa PPP kama ifuatavyo;-. Kibaha – Chalinze (km 78.9) na Chalinze – Morogoro (km 84.9) mradi upo katika taratibu za manunuzi, barabara ya Handeni-Kiberashi-Singida (km 384) taarifa ya Upembuzi Yakinifu na Usanifu wa Kina wa barabara hii imeshakamilika na tayari imewasilishwa TPA kwa ajili ya hatua za kutafuta Mbia

atakaetekeleza mradi huu kwa PPP. Vilevile, Wizara ipo kwenye hatua ya Upembuzi Yakinifu na Usanifu wa Kina wa Barabara ya Igawa-Songwe-Tunduma (km 218) na Uyole - Songwe Bypass (km 48.9) na barabara ya Mzunguko wa Kati (km 50.9) (Inner Ring Road) na Mzunguko wa Nje (km 77.5) (Outer Ring Road) Dar es Salaam kwa utaratibu wa PPP.

**Matumizi ya Hifadhi ya Barabara**

197.***Mheshimiwa Spika,*** kwa upande wa usimamizi wa hifadhi ya barabara, Wizara imehuisha Kanuni mbili kwa lengo la kuwezesha matumizi na usimamizi endelevu wa hifadhi ya barabara. Aidha, Wizara imetunga Kanuni za Usimamizi na Uendeshaji wa Maegesho katika Hifadhi za Barabara za Kitaifa za Mwaka 2025 na kutangazwa kupitia Tangazo la Serikali Na. 432 la tarehe 11/7/2025. Vilevile, kupitia Bodi ya Mfuko wa Barabara, Wizara imekamilisha uundwaji wa mfumo wa kielektroniki kwa ajili ya kurahisisha ukusanyaji wa mapato yatokanayo na maegesho. Marekebisho haya yanakusudia kuleta matokeo chanya ikiwa ni pamoja na kukidhi mahitaji ya rasilimali zinazotumika katika matengenezo ya miundombinu ya barabara, kuongeza mapato ya Mfuko wa Barabara kwa ajili ya kugharamia matenegenezo ya barabara na hivyo kulinda miundombinu hiyo, kuondoa msongamano na kupunguza ajali zitokanazo na uegeshaji holela unaofanywa na watumiaji wa vyombo vya moto katika barabara kuu na kuendeleza miundombinu ya barabara yenye kuchangia katika nyanja mbalimbali za uchumi na jamii (multiplier effect).

198.***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kupitia TANROADS imekamilisha ujenzi wa maegesho ya malori kwenye eneo la Mtanana mkoani Dodoma na inaendelea na ujenzi wa manegesho mengine eneo la Tunduma mkoani Songwe. Taratibu za ujenzi wa maegesho kwenye maeneo mengine zinaendelea. Hivyo, Wadau kutoka sekta binafsi wameonyesha nia ya kushiriakiana na Serikali katika kuwekeza kwenye hifadhi ya barabara. Baadhi wameshawasilisha maombi yao ikiwa ni pamoja na ujenzi wa maegesho na maduka makubwa.

199. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imechukua hatua hizi ili kuimarisha usalama barabarani, kupunguza msongamano wa magari, kupendezesha maeneo ya miji, kuongeza fursa za ajira na kipato kwa wananchi na kuongeza mapato kwa ajili ya kugharamia matengenezo ya barabara. Wizara itashirikiana na wadau wote kuhakikisha hifadhi ya barabara inatumika kwa mujibu wa Sheria na Kanuni zinazosimamia matumizi yake.

## B.5. CHANGAMOTO ZILIZOIKABILI WIZARA NA MIKAKATI YA KUZITATUA

200. ***Mheshimiwa Spika,*** changamoto kadhaa zimechangia kutokufikiwa malengo ya utekelezaji wa majukumu ya Wizara. Changamoto hizo ni pamoja na:

**a)** Uvamizi wa maeneo ya hifadhi ya barabara na hivyo kusababisha usumbufu na gharama wakati wa ujenzi wa barabara

***Mkakati:***
Kuweka alama na kuzuia uendelezaji katika maeneo ya hifadhi za barabara sambamba na kutoa elimu kwa umma kuhusu kuepuka kuvamia maeneo ya hifadhi za barabara

**b)** Mabadiliko ya tabianchi yanasababisha mafuriko kwa baadhi ya maeneo nchini na hivyo kusababisha uharibifu wa miundombinu ya barabara na madaraja.

***Mkakati***
Wizara inaboresha miongozo ya usanifu na matumizi ya malighafi za ujenzi kwa kuzingatia uhimilivu (Resilience) wa miundombinu.

## C. MPANGO NA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA FEDHA KWA MWAKA WA FEDHA 2026/27

201. ***Mheshimiwa Spika,*** Mpango na Bajeti wa Wizara ya Ujenzi kwa mwaka wa fedha 2026/27 umezingatia mipango ya muda mrefu na ya kati ya kitaifa ikiwemo Dira ya Taifa ya Maendeleo 2050 (DIRA 2050); Mpango wa Nne wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano *(*FYDP IV*)* na Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya Mwaka 2025. Aidha, bajeti imezingatia Mpango Mkakati wa Wizara (2026/27 – 2030/31); Ahadi za Viongozi Wakuu wa Serikali na Mwongozo wa Maandalizi ya Mpango na Bajeti ya Serikali kwa mwaka wa fedha 2026/27.

**Mwelekeo wa Bajeti katika Utekelezaji wa Mipango ya Kitaifa**

202. ***Mheshimiwa Spika,*** Bajeti ya mwaka 2026/ 27 ni ya kipekee kwa kuwa ndiyo ya kwanza katika utekelezaji wa maono yaliyopo katika DIRA 2050. Aidha, Bajeti hii ni ya kwanza katika utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi ya mwaka 2025 pamoja na *FYDP IV*. Kutokana na hali hii, bajeti ya mwaka huu imejikita katika kujenga msingi wa miundombinu ya kisasa, imara na inayoweza kuhimili changamoto za mahitaji makubwa ya miundombinu, hususan ya barabara na madaraja pamoja na mabadiliko ya tabianchi.

203. ***Mheshimiwa Spika,*** katika Dira 2050, Sekta ya Ujenzi imetambuliwa kama mojawapo ya sekta zenye fursa za kuleta **mageuzi** kuelekea mwaka 2050. Aidha, "Usafirishaji Fungamanishi" ni mojawapo ya maeneo matano (5) yaliyoainishwa kama **Vichocheo** katika kuharakisha kufikia malengo ya DIRA 2050 ambao utaifanya Tanzania kuwa kitovu cha biashara kikanda. Kwa kuzingatia hayo, miradi iliyopangwa katika bajeti hii inalenga kuimarisha na kuchochea ukuaji wa sekta nyingine ili kuleta mageuzi ya kiuchumi kufikia mwaka 2050. Miradi iliyopangwa kutekelezwa na Wizara kwa mwaka wa fedha 2026/27 imeangalia fursa za kimaendeleo na mabadiliko yanayoweza kujitokeza kwa kipindi cha muda mrefu hususan katika suala la kero ya msongamano wa magari mijini, kuongezeka kwa mahitaji ya kuimarishwa kwa barabara ili

kuendana na kasi ya ufanisi wa bandari zetu pamoja na kukua kwa shughuli za viwanda, kilimo, utalii pamoja na sekta nyingine za kiuchumi. Vilevile, msisitizo umewekwa katika ujenzi wa miundombinu inayostahimili mabadiliko ya tabianchi pamoja na matumizi ya teknolojia za kisasa ili kuongeza ubora na ufanisi.

204.***Mheshimiwa Spika,*** kupitia utekelezaji wa dhima ya "Uboreshaji wa Ukuaji wa Uchumi Shirikishi na Uzalishaji wa Ajira", msisitizo ni kufanya mageuzi ya kuleta tija, ushindani na jumuishi katika sekta zote. Aidha, kupitia FYDP IV, Sekta ya Ujenzi imetambuliwa kuwa muhimu katika kusaidia maendeleo ya miundombinu, ukuaji wa miji na viwanda na kuzalisha ajira. Vile vile, katika kutekeleza dhima ya DIRA 2050 kwa mafanikio msisitizo umewekwa katika kushirikisha Sekta Binafsi kupitia utaratibu wa Ubia kati ya Sekta ya Umma na Binafsi (PPP).

205.***Mheshimiwa Spika,*** kwa upande mwingine, Ilani ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi ya mwaka 2025, inasisitiza utekelezaji wa miradi ya kimkakati kwa maendeleo ya nchi na watu, ikiwa ni pamoja na huduma za ujenzi. Bajeti ya Wizara imelenga kutekeleza miradi kulingana na vipaumbele pamoja na mpangokazi wa utekelezaji wa Ilani ili kuhakikisha kuwa ifikapo mwaka 2030 maelekezo ya Ilani yanayohusu Wizara na Sekta ya Ujenzi kwa ujumla yawe yametekelezwa kwa mafanikio makubwa.

**Vipaumbele vya Wizara ya Ujenzi kwa Mwaka 2026/27**

206.***Mheshimiwa Spika,*** kama ilivyoainishwa kwenye Dira 2050, Sekta ya Ujenzi ni muhimu katika kuwezesha usafirishaji fungamanishi pamoja na kuleta Mageuzi katika sekta zingine. Aidha, kama ilivyotafsriwa katika DIRA 2050, mafanikio ya Dira hii hususan ujenzi wa miundombinu yanategemea ushirikiano thabiti kati ya wadau mbalimbali ikiwemo Sekta Binafsi kupitia utaratibu wa Ubia kati ya Sekta ya Umma na Binafsi (PPP).

207.***Mheshimiwa Spika,*** utekelezaji wa miradi ya Ujenzi unahitaji fedha nyingi. Ili kukabiliana na changamoto hizo, mwelekeo wa Serikali ya Awamu ya Sita chini ya Mhe. Dkt Samia Suluhu Hassan

ni kuongeza ushiriki wa wadau hususan Sekta Binafsi katika utekelezaji wa miradi ya ujenzi kwa njia ya PPP. Lengo ni kupunguza utegemezi wa ugharamiaji wa miradi ya ujenzi kwa kutumia fedha za Serikali. Katika mwaka wa fedha 2026/27, Wizara ya Ujenzi imepanga kutekeleza miradi ya ujenzi wa barabara, majengo, uendeshaji wa vivuko pamoja na karakana ikiwemo miradi itakayo tekelezwa kwa utaratibu wa PPP. Hivyo Sekta binafsi, Taasisi za kifedha na wawekezaji wa ndani na nje ya nchi wanakaribishwa kuwekeza katika ujenzi na uendeshaji wa miradi hii.

208. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kutekeleza maono ya Dira 2050 na Mpango wa Maendeleo wa miaka mitano (2026/27 – 2030/31) pamoja na Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2026/27, Wizara ya Ujenzi imejipanga kukamilisha kwanza miradi inayoendelea na iliyosainiwa kabla ya kuanza utekelezaji wa miradi mipya. Aidha, vipaumbele vya bajeti katika mwaka 2026/27 ni katika maeneo mahsusi yafuatayo:

**a) Kuendelea na ujenzi wa barabara za kupunguza msongamano hususan katika majiji na miji inayokua kwa kasi:**

209. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2026/27 Wizara ya Ujenzi imepanga kuendelea na utekelezaji wa miradi ya kupunguza msongamano katika majiji ya Dar es Salaam, Arusha, Mwanza, Mbeya, Dodoma na katika miji ya Pwani, Iringa na Singida. Lengo ni kuboresha mfumo wa usafiri mijini, kuongeza tija ya kiuchumi, na kuinua ubora wa maisha ya wananchi. Utekelezaji wa miradi katika maeneo hayo ni kama ifuatavyo:

Jiji la Dar es Salaam na Mji wa Pwani Miradi itakayoendelea kutekelezwa kwa ajili ya kupunguza msongamano wa magari katika jiji la Dar es Salaam itahusisha ujenzi wa barabara na *flyovers* katika makutano mbalimbali ya Barabara. Miradi hiyo ni:

(i) Ujenzi wa Barabara za Mabasi Yaendayo Haraka Awamu ya tatu (3) kutoka Maktaba – JNIA - Gongolamboto (km 23.3);

(ii) Ujenzi wa Barabara za Mabasi Yaendayo Haraka Awamu ya nne (4) kutoka Maktaba – Morocco – Mwenge - Tegeta na Mwenge - Ubungo (km 30.1);
(iii) Maandalizi ya kuanza ujenzi wa Barabara za Mabasi Yaendayo Haraka Awamu ya Tano (5) kutoka Ubungo – Bandarini, Makutano ya Tabata – Tabata Segerea na Tabata – Kigogo (km 27.6) na ujenzi wa *Flyover* ya Tabata;
(iv) Ujenzi wa *Flyovers* mbili katika makutano ya Mwenge na Morocco; ambapo Wizara ya Ujenzi inaendelea na majadiliano na JICA ili kuweza kufadhili utekelezaji wa mradi huo;
(v) Kukamilisha Upanuzi wa Barabara ya Ubungo – Kimara kutoka njia sita (6) kuwa njia nane (8);
(vi) Upanuzi wa barabara ya Mbagala – Kongowe - Mkuranga (km 17.14) kutoka njia mbili (2) hadi njia nne (4) pamoja na Daraja la Mzinga;
(vii) Upanuzi wa barabara ya Mwai Kibaki (km 11.77) kutoka njia mbili (2) kuwa njia nne (4);
(viii) Upanuzi wa Barabara ya Kibaha – TAMCO (km 4.5) kutoka njia mbili (2) hadi njia nane (8); na
(ix) Ujenzi wa *Flyover* katika eneo la Fire, Magomeni na KAMATA.

**Jiji la Dodoma**

Miradi inayoendelea kutekelezwa kwa ajili ya kupunguza msongamano wa magari katika jiji la Dodoma ni pamoja na:

(i) Ujenzi wa barabara ya Mzunguko wa Nje kilometa 112.3 katika jiji la Dodoma ambao upo katika hatua za mwisho kukamilika;
(ii) Upanuzi wa barabara ya Dodoma – Morogoro (km 70); sehemu ya Kimbinyiko R/ About – Chamwino Jct (km 32) kutoka njia mbili (2) kuwa njia sita (6) ambapo mkataba wa ujenzi umesainiwa tarehe 18 Mei, 2026.
(iii) Upanuzi wa barabara za Dodoma – Iringa (km 50) Awamu ya I; sehemu ya Bahi Rd R/About – Mkonze/SGR Station (km 8.5) kutoka njia mbili (2) kuwa njia nne (4) na Dodoma – Arusha (km 50) Awamu ya I; sehemu ya Bahi

Rd R/About – Msalato Airport Jct (km 10.7) kutoka njia mbili (2) kuwa njia njia nne (4) ambapo taratibu za manunuzi zinaendelea.

(iv) Ujenzi na upanuzi wa barabara ya mzunguko wa ndani katika jiji la Dodoma: Bahi R/About – Image R/About – Ntyuka R/About – Makulu (km 6.4) kwa njia nne (4) ambazo zitajengwa kwa fedha za Washirika wa Maendeleo kutoka Japan ambapo mkataba wa ujenzi umesainiwa.

**Jiji la Arusha**

Miradi ya kupunguza msongamano katika Jiji la Arusha ni pamoja na:

(i) Upanuzi wa barabara ya Arusha – Kisongo (km 9.3) kutoka njia mbili (2) kuwa njia nne (4) ambapo mkataba umesainiwa;
(ii) Ujenzi wa barabara ya Mbauda – Losinyai (km 70) ambapo ujenzi unaendelea;
(iii) Upanuzi wa barabara ya Tengeru – USA River (km 11.3) kutoka njia mbili (2) kuwa njia nne (4) ambayo ipo katika hatua za mwisho za ununuzi wa Mkandarasi; na
(iv) Ujenzi wa barabara ya Tengeru - Mererani (km 28) ambapo usanifu umekamilika.

**Jiji la Mwanza**

Mradi wa upanuzi kutoka njia mbili (2) hadi nne (4) wa barabara ya Mwanza – Usagara (km 25) ambapo taratibu za manunuzi ya Mkandarasi zinaendelea na Mkandarasi wa ujenzi wa Barabara ya Mwanza Airport – Kayenze (km 10) yupo katika hatua za maandalizi ya kuanza kazi.

**Jiji la Mbeya, Miji ya Iringa, Songwe na Singida**

Miradi itakayoendelea kutekelezwa kwa ajili ya kupunguza msongamano wa magari katika jiji la Mbeya ni pamoja na upanuzi wa sehemu ya Nsalaga – Uyole - Ifisi (km 29) ambapo ujenzi unaendelea na kuendelea na maandalizi ya ujenzi wa barabara ya mchepuo ya Uyole – Songwe (km 48.9). Aidha,

Mkandarasi wa upanuzi wa barabara ya Igawa – Tunduma (km 218) anaendelea na maandalizi ya kuanza mradi kwa utaratibu wa PPP. Vilevile, katika mji wa Iringa, ujenzi kwa kiwango cha lami wa Barabara ya Mchepuo wa Iringa (km 7.3) unaendelea na kwa mkoa wa Singida, Wizara inaendelea na maandalizi ya upanuzi wa Barabara ya Singida Mjini (km 10) kutoka njia mbili (2) kuwa njia nne (4).

**c) Kuendelea na Ujenzi wa barabara zinazounganisha makao makuu ya mikoa, Tanzania na nchi jirani na maeneo ya kimkakati**

210. ***Mheshimiwa Spika,*** miongoni mwa mikakati ya Wizara ni kuendelea na ujenzi wa barabara zinazounganisha makao makuu ya mikoa, nchi jirani na barabara zinazoelekea katika maeneo ya kimkakati kwa kiwango cha lami. Wizara inaendelea kuunganisha mikoa ya Mbeya na Singida, Mbeya na Tabora, Rukwa na Katavi, Kigoma na Katavi, Arusha na Simiyu pamoja na Morogoro na Ruvuma.

Aidha, Wizara inaendelea na ujenzi wa barabara zinazounganisha nchi jirani ikiwemo barabara ya Tanga – Pangani – Makurunge (km 174.5) pamoja na daraja la Pangani (m 525) inayounganisha Tanzania na Kenya; Ujenzi wa barabara ya kikanda ya Manyovu – Kasulu – Kabingo (km 260.6) inayounganisha Tanzania na Burundi, Ujenzi wa barabara ya Kibondo – Mabamba (km 50) inayounganisha Tanzania na Burundi; Ukarabati wa barabara ya Lusahunga – Rusumo (km 92) inayounganisha Tanzania, Rwanda na Burundi na Matai – Kasesya (km 50) inayounganisha Tanzania na Zambia. Vilevile, Wizara inaendelea na ujenzi wa barabara zinazoelekea katika maeneo ya kimkakati yanajumuisha bandari, reli, viwanja vya ndege, viwanda, kilimo, migodi, utalii, kongani za viwanda (EPZ), miji mikuu na ulinzi wa mipakani.

**d) Kuendelea na ukarabati na matengenezo makubwa ya maeneo yenye changamoto katika barabara kuu na za mikoa**

211.***Mheshimiwa Spika,*** uwekezaji mkubwa uliotokana na maono ya Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, katika bandari zetu hususan bandari ya Dar es Salaam umesababisha ongezeko la mizigo inayosafirishwa ndani na nje ya nchi kupitia barabara. Ufanisi huu wa bandari unakumbana na changamoto kadhaa zikiwemo msongamano pamoja na uchakavu wa miundombinu ya barabara unaohitaji fedha nyingi kuziboresha.

212.***Mheshimiwa Spika,*** wakati wa hafla ya kupokea gawio na michango kutoka mashirika ya Umma, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania alisisitiza umuhimu wa matumizi ya Hati Fungani (Bond) kama njia mbadala ya kugharamia miradi ya maendeleo ya Serikali. Kwa kuzingatia maelekezo hayo, Wizara ya Ujenzi inatarajia kuanza matumizi ya Hati Fungani (Infrastracture bond) katika kugharamia matengenezo makubwa na ukarabati wa barabara kuu za Kiuchumi ambazo ni Morogoro – Dodoma - Singida – Tabora – Shinyanga – Mwanza/ Tinde – Rusumo; Kibiti – Lindi – Mingoyo; Sirari – Musoma – Mwanza – Geita – Bukoba - Mutukura na Dar es Salaam – Morogoro – Iringa – Makambako - Mbeya – Tunduma kutoka njia mbili (2) kwenda njia nne (4).

**d) Kuendelea na kuimarisha usafiri na miundombinu ya vivuko;**

213.***Mheshimiwa Spika,*** katika kuendeleza jitihada za kuimarisha miundombinu ya usafiri na usafirishaji majini na kuchochea Uchumi wa Buluu, Serikali imedhamiria kukamilisha ununuzi wa vivuko vipya vitano (5) Kanda ya Ziwa pamoja na uboreshaji wa usafiri katika ukanda wa Pwani, ambapo kukamilika kwa kivuko kipya cha Nyamisati – Mafia kutahakikisha uwepo wa kivuko cha pili cha uhakika kwa safari za kila siku, huku kivuko kitakachohudumia Boza, Kuruti, Shungumbweni (Ngwevu) na Kisiju kikilenga kutoa huduma rahisi na salama kwa wananchi.

**e) Kuendelea kuwajengea uwezo wataalam na wakandarasi wa ndani katika masuala ya ujenzi**

214. ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali inafanya jitihada mbalimbali kuhakikisha wakandarasi wazawa wanashiriki ipasavyo katika shughuli za ujenzi. Jitihada hizo ni pamoja na kutoa mafunzo kwa wakandarasi unaolenga kukuza ujuzi wa wakandarasi katika maeneo ya kiufundi na usimamizi wa miradi; kuendesha mfuko wa kusaidia wakandarasi (Contractors Assistance Fund – CAF) unaolenga kusaidia Wakandarasi Wazawa kupata dhamana za benki kwa ajili ya zabuni na malipo ya awali; kuhamasisha wakandarasi kuunganisha nguvu kupitia ubia (Joint Venture); na kuendelea kutenga miradi ya kuwajengea uwezo Wakandarasi na Washauri Elekezi Wazawa kama Sheria ya Ununuzi wa Umma, Sura ya 410 na kanuni zake inavyoelekeza.

**f) Kuendelea na ujenzi wa majengo ya Serikali na nyumba za gharama nafuu.**

215. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara ya Ujenzi kupitia Wakala wa Majengo Tanzania (TBA) itaendelea na usimamizi wa milki ya Serikali ili kutoa makazi bora kwa ajili ya Viongozi na watumishi wa umma. Aidha, katika kutekeleza maono ya Mhe. Rais ambayo ni kutoa makazi bora ya gharama naafuu kwa vijana na umma kwa ujumla, Wizara imejipanga kukamilisha Mradi wa ujenzi wa nyumba za gharama nafuu 144 unaoendelea katika eneo la Temeke Jijini Dar es Salaam na kuanza utekelezaji wa Mradi nyumba 144 za gharama nafuu utakaotekelezwa jijini Dodoma.

216. ***Mheshimiwa Spika,*** ili kuuwezesha Wakala wa Majengo Tanzania kujitegemea na kupunguza utegemezi wake kwa Ruzuku ya Serikali, Wizara ya Ujenzi itaendelea kukaribisha Sekta Binafsi ili kufanya ubia na Serikali kupitia TBA, kuwekeza katika miradi ya ujenzi na uendeshaji wa nyumba na majengo. Aidha, Wizara kupitia TBA, ipo katika hatua za mwisho za kusaini mkataba wa uendelezaji kwa ubia (PPP) wa eneo la Temeke Kota jijini Dar es Salaam. Vilevile Wakala umeainisha maeneo yake oevu 149 katika mikoa yote Tanzania Bara kwa ajili ya kuyaendeleza kwa njia ya ubia (PPP).

## C.1 MAKADIRIO YA BAJETI

### Makadirio ya Bajeti ya Matumizi ya Kawaida

217. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2026/27 Wizara ya Ujenzi imetengewa **Shilingi 97,104,935,000.00.** ikiwa ni Bajeti ya Matumizi ya Kawaida. Kati ya fedha hizo, **Shilingi 92,209,218,000.00** ni Bajeti ya Mishahara na **Shilingi 4,895,717,000.00** ni kwa ajili ya Matumizi Mengineyo.

### Makadirio ya Bajeti ya Miradi ya Maendeleo

218. ***Mheshimiwa Spika,*** Bajeti ya Maendeleo kwa Wizara ya Ujenzi ni **Shilingi 2,467,336,479,000.00.** Kati ya fedha hizo, **Shilingi 1,544,872,147,000.00** ni fedha za ndani na **Shilingi 922,464,332,000.00.** ni fedha za nje. Kati ya fedha za ndani, **Shilingi 1,047,405,500,000.00** ni fedha zilizotengwa kwa ajili ya bajeti ya Mfuko wa Barabara na fedha kutoka katika Mfuko Mkuu wa Serikali ni **Shilingi 497,466,647,000.00.** Mgawanyo wa fedha za maendeleo pamoja na miradi iliyotengewa fedha umeoneshwa katika ***Kiambatisho Na. 1.*** Maelezo kuhusu Miradi ya Maendeleo iliyotengewa fedha katika mwaka wa fedha 2026/27 ni kama ifuatavyo:

## C.2 MPANGO WA UTEKELEZAJI WA MIRADI

### a) Miradi ya Barabara na Madaraja

219. ***Mheshimiwa Spika,*** miradi ya barabara na madaraja itakayotekelezwa katika mwaka wa fedha 2026/27 ni kama ifuatavyo:

#### Barabara ya Soni – Bumbuli – Dindira – Korogwe

220. ***Mheshimiwa Spika,*** mradi huu umetengewa jumla ya **Shilingi milioni 5,550.00** kwa ajili ya kuanza ujenzi wa barabara hii kwa kiwango cha lami, sehemu za Soni – Bumbuli - Funta (km 22) na Kwameta – Kwashemshi (km 10). Kazi nyingine ni kuendelea na maandalizi ya ujenzi wa barabara ya Old Korogwe – Kwamndolwa – Magoma – Mashewa – Bombomtoni –

Mabokweni (km 127.69) sehemu ya Old Korogwe – Kwamndolwa (km 10) na sehemu ya Maramba – Mabokweni (km 10) pamoja na kuanza maandalizi ya ujenzi wa sehemu ya Maramba - Bombomtoni (km 28). **Barabara ya Mtwara – Newala – Masasi**

221.***Mheshimiwa Spika,*** jumla ya **Shilingi milioni 68,699.85** zinazojumuisha **Shilingi milioni 1,760.00** fedha za ndani na **Shilingi milioni 66,939.85** fedha za nje zimetengwa kwa ajili ya kulipa madeni ya Mkandarasi wa barabara ya Mtwara – Newala – Masasi: sehemu ya Mtwara – Mnivata (km 50) na kuendelea na ujenzi wa sehemu za Mnivata – Mitesa (km 100) na Mitesa – Masasi (km 60) kwa kiwango cha lami. Kazi nyingine ni kuanza ujenzi wa barabara ya Namichiga – Ruangwa (km 20.6), Magamba – Madimba – Msimbati (km 35) na Mtama – Tandahimba (km 5) kwa kiwango cha lami.

**Barabara ya Likuyufusi – Mkenda**

222. ***Mheshimiwa Spika,*** jumla ya **Shilingi milioni 2,800.00** zimetengwa kwa ajili ya kuanza ujenzi wa barabara hii sehemu ya Likuyufusi – Mhukuru (km 60) kwa kiwango cha lami.

**Barabara ya Nachingwea – Liwale**

223. ***Mheshimiwa Spika,*** jumla ya **Shilingi milioni 3,050.00** zimetengwa kwa ajili ya kuanza ujenzi wa barabara ya hii kwa kiwango cha lami, sehemu ya Liwale – Kihangara (km 55) na kuendelea na maandalizi ya ujenzi wa sehemu ya Masasi – Nachingwea (km 45) kwa kiwango cha lami.

**Barabara ya Ubena Zomozi – Ngerengere**

224. ***Mheshimiwa Spika,*** jumla ya **Shilingi milioni 2,000.00** zimetengwa kwa ajili ya kuendelea na ujenzi sehemu ya Ubena Zomozi – Kizuka (km 11.6) kwa kiwango cha lami.

**Barabara za TAMCO – Vikawe – Mapinga**

225. ***Mheshimiwa Spika,*** mradi huu umetengewa jumla ya **Shilingi milioni 2,200.00** kwa ajili ya kuendelea na ujenzi sehemu ya Pangani – Mapinga (km 14.5) na Kibaha - Kiluvya – Kisarawe (km 22) kwa kiwango cha lami.

**Barabara ya Makofia – Mlandizi**

226. ***Mheshimiwa Spika,*** barabara hii imetengewa jumla ya **Shilingi milioni 500.00** kwa ajili ya kuendelea na maandalizi ya ujenzi wa km 36.7 kwa kiwango cha lami.

**Barabara ya Musoma – Makojo – Busekela**

227. ***Mheshimiwa Spika,*** barabara hii imetengewa jumla ya **Shilingi milioni 2,810.00** kwa ajili ya kuanza ujenzi wa sehemu ya Musoma – Kusenyi (km 40) kwa kiwango cha lami na kulipa deni la Mkandarasi wa ujenzi wa sehemu ya Suguti – Kusenyi (km 5).

**Barabara ya Kongwa Jct – Mpwapwa – Gulwe –** Kibakwe

228. ***Mheshimiwa Spika,*** barabara hii imetengewa jumla ya **Shilingi milioni 3,500.00** kwa ajili ya kuendelea na ujenzi wa sehemu ya Kongwa Jct – Ngambi – Mpwapwa (km 32) na kuendelea na maandalizi ya ujenzi wa sehemu ya Mpwapwa – Gulwe – Kibakwe (km 46.9) kwa kiwango cha lami.

**Barabara ya Muhutwe – Kamachumu – Muleba**

229. ***Mheshimiwa Spika,*** jumla ya **Shilingi milioni 500.00** zimetengwa kwa ajili ya kuendelea na ujenzi wa km 3.8 kwa kiwango cha lami.

**Barabara ya Iringa – Ruaha National Park**

230. ***Mheshimiwa Spika,*** barabara hii imetengewa jumla ya **Shilingi milioni 41,328.40** zinazojumuisha Shilingi **milioni 400.00** fedha za ndani na **Shilingi milioni 40,928.40** fedha za nje kwa ajili ya kuendelea na ujenzi wa barabara za Iringa – Ruaha National

Park (km 104) na Iringa (Ipogolo) – Kilolo (km 33.2) kwa kiwango cha lami.

**Barabara ya Muheza – Amani**

231. ***Mheshimiwa Spika,*** jumla ya **Shilingi milioni 800.00** zimetengwa kwa ajili ya kuendelea maandalizi ya ujenzi wa km 28 kwa kiwango cha lami.

**Barabara ya Mtwara – Mingoyo – Masasi**

232. ***Mheshimiwa Spika,*** jumla ya **Shilingi milioni 90,923.84** zinazojumuisha **Shilingi milioni 500.00** fedha za ndani na **Shilingi milioni 90,423.84** fedha za nje zimetengwa kwa ajili ya kuendelea na ukarabati wa sehemu za Mtwara – Mingoyo (km 82.27) na Mingoyo – Nanganga – Masasi (km 118.24) kwa kiwango cha lami.

**Barabara ya Kibaoni – Majimoto – Muze – Kilyamatundu**

233. ***Mheshimiwa Spika,*** jumla ya Shilingi milioni 3,000.00 zimetengwa kwa ajili ya kuendelea na ujenzi kwa kiwango cha lami wa barabara ya Ntendo – Muze – Kilyamatundu; sehemu ya Ntendo – Kizungu (km 25) na kuanza ujenzi wa barabara ya Kibaoni – Majimoto – Inyonga (km 152); sehemu ya Kibaoni – Usevya (km 5) kwa kiwango cha lami. Kazi nyingine ni kuendelea na maandalizi ya ujenzi wa barabara ya Kizungu – Muze (km 12) kwa kiwango cha lami.

**Daraja la Kigongo – Busisi (J.P. Magufuli) na Barabara Unganishi**

234. ***Mheshimiwa Spika,*** jumla ya **Shilingi milioni 11,346.57** zimetengwa kwa ajili ya kazi zilizoongezeka kwenye mradi huu ikiwemo ufungaji wa vifaa vya kieletroniki vya usalama wa daraja.

**Daraja la Mzinga**

235. ***Mheshimiwa Spika,*** jumla ya **Shilingi milioni 300.00** zimetengwa kwa ajili ya kuanza ujenzi wa daraja la Mzinga katika Barabara ya Mbagala Rangi Tatu – Kongowe Jijini Dar es Salaam.

**Daraja la Ugalla**

236. ***Mheshimiwa Spika,*** jumla ya **Shilingi *milioni* 500.00** zimetengwa kwa ajili ya kuendelea na maandalizi ya ujenzi wa daraja hili lililopo katika mkoa wa Katavi.

**Daraja la Kitengule na Barabara Unganishi**

237. ***Mheshimiwa Spika,*** jumla ya **Shilingi milioni 2,010.00** zimetengwa kwa ajili ya kuendelea na ujenzi wa barabara ya Kagera Sugar Jct – Kakunyu; sehemu ya Kagera Sugar Jct – Kitengule Jct (km 25) na malipo ya Mkandarasi na Mhandisi Mshauri wa ujenzi wa Daraja la Kitengule.

**Barabara ya Morogoro – Dodoma pamoja na Daraja la Mkundi**

238. ***Mheshimiwa Spika,*** jumla ya **Shilingi milioni 1,300.00** zimetengwa kwa ajili ya sehemu ya malipo ya Mhandisi Mshauri aliyefanya Upembuzi Yakinifu na Usanifu wa Kina wa barabara hii pamoja na Daraja hilo ili kuikarabati kwa kiwango cha lami. Kazi nyingine ni kuendelea na maandalizi ya ujenzi wa barabara ya SUA Main Gate – Mzinga Factory Gate (km 11) kwa kiwango cha lami.

**Daraja Jipya la Wami**

239. ***Mheshimiwa Spika,*** jumla ya **Shilingi milioni 10.00** zimetengwa kwa ajili ya sehemu ya malipo ya Mkandarasi na Mhandisi Mshauri wa ujenzi wa Daraja hili lililopo katika barabara ya Chalinze – Segera.

**Barabara ya Njombe – Makete – Isyonje**

240. ***Mheshimiwa Spika,*** jumla ya **Shilingi milioni 4,170.00** zimetengwa kwa ajili ya kuendelea na ujenzi wa barabara ya Isyonje – Makete; sehemu ya Kitulo – Iniho (km 36.3), barabara ya Njombe – Njombe Referral Hospital (km 3) kwa kiwango cha lami na sehemu ya malipo ya Wakandarasi na Wahandisi Washauri kwa sehemu za Njombe – Moronga (km 53.90), Moronga – Makete (km 53.50) na Mizani ya Igagala. Kazi nyingine ni kuanza maandalizi ya ujenzi kwa kiwango cha lami wa barabara za Bulongwa – Iyoka – Madihani – Kidope (km 22), Madihani – Lufilyo (km 15.1), Kitulo – Matamba – Chimala (km 41) na Matamba – Mfumbi (km 33).

**Barabara ya Omugakorongo – Kigarama – Murongo**

241. ***Mheshimiwa Spika,*** jumla ya **Shilingi milioni 5,600.00** zimetengwa kwa ajili ya kuanza ujenzi kwa kiwango cha lami wa sehemu za Businde – Murongo (km 53.4) na Omugakorongo – Businde (km 51.6) kwa kiwango cha lami.

**Barabara ya Nanganga – Ruangwa – Nachingwea**

242. ***Mheshimiwa Spika,*** jumla ya Shilingi **milioni 6,800.00** zimetengwa kwa ajili ya kuendelea na ujenzi wa sehemu za Nanganga – Ruangwa (km 53.2), Nachingwea – Ruangwa (km 55.7) na kuanza ujenzi wa barabara ya Choya – Liwale (km 72) kwa kiwango cha lami.

**Barabara ya Mpemba – Isongole**

243. ***Mheshimiwa Spika,*** jumla ya **Shilingi milioni 2,610.00** zimetengwa kwa ajili ya kuanza ujenzi wa barabara za Mlowo – Kamsamba (km 15), Chang'ombe – Mkwajuni – Makongolosi (km 61) sehemu yenye urefu wa kilometa ~~5~~ 10 kuanzia Mkwajuni kwa kiwango cha lami na ujenzi wa kituo cha pamoja cha ukaguzi cha Iboya (One Stop Inspection Station – OSIS). Kazi nyingine ni kuanza maandalizi ya ujenzi wa barabara ya Utambalila - Chitete

(km 17) kwa kiwango cha lami na sehemu ya malipo ya Mkandarasi wa barabara ya Mpemba – Isongole (km 50.3).

**Barabara ya Ruanda – Iyula – Nyimbili**

244. ***Mheshimiwa Spika,*** jumla ya **Shilingi milioni 500.00** zimetengwa kwa ajili ya kuendelea na ujenzi wa barabara hii yenye urefu wa km 21 kwa kiwango cha lami.

**Barabara ya Katumbasongwe – Kasumulu – Ngana – Ndembo**

245. ***Mheshimiwa Spika,*** jumla ya **Shilingi milioni 3,300.00** zimetengwa kwa ajili ya kuendelea na ujenzi wa sehemu ya Isongole II – Ndembo (km 52) na barabara ya kuingia Mji wa Ndembo (Ndembo Spur Road) kwa kiwango cha lami na kuendelea na maandalizi ya ujenzi wa barabara ya Katumbasongwe – Kasumulu – Ngana – Ndembo (km 44.10) kwa kiwango cha lami.

**Barabara ya Uyogo – Nyamilangano – Nyandekwa – Kahama**

246. ***Mheshimiwa Spika,*** jumla ya **Shilingi milioni 500.00** zimetengwa kwa ajili ya kuendelea na maandalizi ya ujenzi wa barabara hii yenye urefu wa km 54 kwa kiwango cha lami.

**Barabara ya Sengerema – Nyehunge – Kahunda**

247. ***Mheshimiwa Spika,*** jumla ya **Shilingi milioni 3,300.00** zimetengwa kwa ajili ya kuendelea na ujenzi wa barabara ya Sengerema – Nyehunge (km 54). Kazi nyingine ni kuendelea na maandalizi ya ujenzi wa sehemu ya Kamanga – Katunguru – Sengerema (km 35) kwa kiwango cha lami.

**Barabara ya Omurushaka – Nkwenda – Murongo**

248. ***Mheshimiwa Spika,*** jumla ya **Shilingi milioni 2,800.00** zimetengwa kwa ajili ya kuendelea na ujenzi wa barabara hii sehemu ya Kyerwa – Chonyonyo (km 50) kwa kiwango cha lami.

**Upanuzi wa Barabara Kuu zinazoingia atikati ya Jiji la Dodoma**

249. ***Mheshimiwa Spika,*** jumla ya **Shilingi milioni 40,922.91** zimetengwa zikijumuisha **Shilingi milioni 250.00** fedha za ndani na **Shilingi milioni 40,672.91** fedha za nje kwa ajili ya kuanza upanuzi wa barabara kuu zinazoingia katika Jiji la Dodoma (km 51.2) zinazohusisha barabara ya Dodoma – Morogoro (km 32), Dodoma – Iringa (km 8.5) na Dodoma – Arusha (km 10.7).

**Barabara ya Ntyuka Jct – Mvumi Hospital – Kikombo Jct**

250. ***Mheshimiwa Spika,*** jumla ya **Shilingi milioni 6,300.00** zimetengwa kwa ajili ya kuendelea na ujenzi wa barabara hii sehemu za Ntyuka Jct – Mvumi Makulu (km 8.6), Kikombo Jct – Mapinduzi (km 16.4) na Ntyuka – Mvumi Hospital - Kikombo (km 53) na kuanza maandalizi ya ujenzi kwa kiwango cha lami wa barabara ya kuingia Hospitali ya JWTZ Msalato (km 5.5). Kazi nyingine ni kuendelea na Upembuzi Yakinifu na Usanifu wa Kina wa barabara ya Ihumwa – Hombolo - Mayamaya (km 60) ili kuijenga kwa kiwango cha lami.

**Barabara ya Tarime – Mugumu**

251. ***Mheshimiwa Spika,*** jumla ya **Shilingi milioni 7,000.00** zimetengwa kwa ajili ya kuendelea na ujenzi kwa kiwango cha lami wa barabara za Mogabiri – Nyamongo (km 25), Tarime – Mogabiri (km 9.3), Nyamongo – Mugumu (km 48.15) pamoja na barabara ya kuelekea Mugumu Roundabout (km 3.6). Kazi nyingine ni kuanza ujenzi wa barabara ya Mika – Utegi – Shirati – Kirongwe (km 56.8); Sehemu ya Utegi – Shirati (km 27).

**Barabara ya Shelui – Nzega**

252. ***Mheshimiwa Spika,*** jumla ya Shilingi milioni **850.00** zimetengwa kwa ajili ya sehemu ya malipo ya Mhandisi Mshauri wa kazi ya Upembuzi Yakinifu na Usanifu wa Kina kwa ajili ya ukarabati kwa kiwango cha lami wa barabara ya Shelui – Nzega (km 123). Kazi nyingine ni kuanza maandalizi ya ujenzi wa barabara ya Shelui – Sekenke – Tulya – Tyegelo (km 62); sehemu ya Shelui – Sekenke – Ntwike (km 20) kwa kiwango cha lami.

**Barabara ya Nzega – Kagongwa**

253. ***Mheshimiwa Spika,*** jumla ya **Shilingi milioni 800.00** zimetengwa kwa ajili ya kuendelea na maandalizi ya ujenzi wa barabara ya Nzega – Kagongwa (km 65), sehemu ya Kagongwa – Bukooba (km 18) kwa kiwango cha lami.

**Barabara ya Isabdula (Magu) – Bukwimba Station – Ngudu – Ng'hungumalwa**

254. ***Mheshimiwa Spika,*** jumla ya **Shilingi milioni 3,800.00** zimetengwa kwa ajili ya kuanza ujenzi wa barabara ya Isabdula (Magu) – Bukwimba Station – Ngudu – Ng'hungumalwa sehemu ya km 10 na kuendelea na ujenzi wa barabara ya Mwanangwa – Misasi – Salawe – Kahama (km 136); sehemu ya km 3 kwa kiwango cha lami.

**Barabara ya Mafinga – Mgololo**

255. ***Mheshimiwa Spika,*** jumla ya **Shilingi milioni 2,800.00** zimetengwa kwa ajili kuanza ujenzi wa barabara hii yenye urefu wa km 81 kwa kiwango cha lami.

**Barabara ya Nyololo – Mtwango**

256. ***Mheshimiwa Spika,*** jumla ya **Shilingi milioni 2,000.00** zimetengwa kwa ajili kuendelea na ujenzi wa barabara ya Nyololo – Mtwango (km 40.4); sehemu ya km 15 kwa kiwango cha lami.

**Barabara ya Kongwa – Kibaya- Arusha**

257. ***Mheshimiwa Spika,*** jumla ya **Shilingi milioni 2,800.00** zimetengwa kwa ajili kuendelea na ujenzi wa barabara hii sehemu ya Tanganyika Packers/ Mbauda Jct - Losinyai (km 70) kwa kiwango cha lami.

**Barabra ya Singida – Sepuka – Ndago – Kizaga**

258. ***Mheshimiwa Spika,*** jumla ya **Shilingi milioni 3,300.00** zimetengwa kwa ajili ya kuendelea na ujenzi wa barabara ya Singida – Sepuka – Ndago – Kizaga (km 77.4) kwa kiwango cha lami na kuanza maandalizi ya ujenzi wa barabara ya Sepuka – Mlandala – Urugu – Mtoa – Shelui (km 97.6).

**Barabara ya Kitai – Lituhi pamoja na Daraja la Mnywamaji**

259. ***Mheshimiwa Spika,*** jumla ya **Shilingi milioni 5,500.00** zimetengwa kwa ajili ya kuanza maandalizi ya ujenzi kwa kiwango cha lami wa barabara ya Kitai – Lituhi (km 90) pamoja na daraja la Mnywamaji; sehemu za Amanimakoro – Ruanda (km 35), Ndumbi – Mbamba Bay (km 98) na Ruanda – Ndumbi Port (km 50) kwa kiwango cha lami.

**Barabara za Kuelekea Katika Vituo vya Reli ya Kisasa ya SGR**

260. ***Mheshimiwa Spika,*** jumla ya **Shilingi milioni 12,950.00** zimetengwa kwa ajili ya kuanza maandalizi ya ujenzi kwa kiwango cha lami wa barabara za Zinje – Zuzu (km 8), barabara za kuelekea katika vituo vya reli ya kisasa (SGR) ambazo ni Morogoro – Kihonda SGR Station (km 10), Rudewa – Kilosa SGR Station (km 3), Gulwe – Gulwe SGR Station (km 2), Igandu – Igandu SGR Station (km 27), Ihumwa – Ihumwa *Marshalling Yard* (km 5.5), Bahi – Bahi SGR Station (km 4), Mlandizi – Ruvu SGR Station (km 22) na barabara ya Pugu – Kiltex (km 6.7). Kazi nyingine ni kuanza Upembuzi Yakinifu na Usanifu wa Kina wa barabara za Ipuli - Tabora SGR Station (km 4.6), Ikungu - Malampaka SGR Station (km 15), Mwigerezi - Mabama SGR Station (km 2.74), Urambo Sec. - Urambo SGR Station (km 2.58), Kintinku - Makutupora SGR Station (km 12) na Manyoni - Manyoni SGR Station (km 1.2).

**Barabara ya Tanga – Pangani – Makurunge**

261. ***Mheshimiwa Spika,*** jumla ya **Shilingi milioni 66,355.68** zinazojumuisha **Shilingi milioni 3,750.00** fedha za ndani na **Shilingi**

**milioni 62,605.68** fedha za nje zimetengwa kwa ajili ya kuendelea na ujenzi kwa kiwango cha lami wa barabara za Tanga – Pangani (km 50), daraja la Pangani (m 525) pamoja na barabara unganishi (km 25.6) na Pangani (Tungamaa) – Mkwaja – Mkange (km 95.2). Kazi nyingine ni kuanza ujenzi kwa kiwango cha lami wa barabara ya Mkata – Kwa Msisi (km 36).

**Barabara ya Kisarawe – Maneromango – Mloka (km 150.46)**

262. ***Mheshimiwa Spika,*** jumla ya **Shilingi milioni 2,200.00** zimetengwa kwa ajili ya kuendelea na maandalizi ya ujenzi wa sehemu ya Mpuyani - Maneromango (km 34.5) kwa kiwango cha lami.

**Barabara ya Geita – Bulyanhulu – Kahama**

263. ***Mheshimiwa Spika,*** jumla ya **Shilingi milioni 46,654.83** zinazojumuisha **Shilingi milioni 5,300.00** fedha za ndani na **Shilingi milioni 41,354.83** fedha za nje zimetengwa kwa ajili ya kuendelea na ujenzi kwa kiwango cha lami wa sehemu ya Kahama – Bulyanhulu Jct – Kakola (km 73.9), Geita – Bulyanhulu Jct (km 58.3). Kazi nyingine ni kuanza ujenzi wa barabara za Nyikonga – Kashelo (km 10.5), Kashelo – Ilolangulu (km 15) na Ushirombo – Kilimahewa – Nanda (km 15.7). Aidha, maandalizi ya ujenzi wa barabara ya Katoro – Nyikonga – Ushirombo (km 47): sehemu ya Ushirombo – Nyikonga (km 22.5), Masumbwe – Kashelo (km 60) na Kahama – Tulole – Muhulidede - Bukumbi – Mambali – Tabora (km 152.27): sehemu ya Kahama - Tulole (km 20) kwa kiwango cha lami yanaendelea.

**Barabara ya Nyamirembe Port – Katoke**

264. ***Mheshimiwa Spika,*** jumla ya **Shilingi milioni 1,500.00** zimetengwa kwa ajili ya kuendelea na ujenzi wa barabara za Chato Ginery – Bwina (km 8.1) na SIDO – Chato Zonal Hospital (km 5.3) kwa kiwango cha lami. Kazi nyingine ni kuendelea na maandalizi ya ujenzi kwa kiwango cha lami wa barabara ya Nyamirembe Port – Katoke (km 50).

**Barabara ya Geita – Nzera – Nkome**

265. ***Mheshimiwa Spika,*** jumla ya **Shilingi milioni 2,000.00** zimetengwa kwa ajili ya kuendelea na ujenzi kwa kiwango cha lami wa barabara hii sehemu ya Nzera – Nkome (km 20.36).

**Barabara ya Arusha – Moshi – Himo – Holili**

266. ***Mheshimiwa Spika,*** jumla ya **Shilingi milioni 83,937.58** zinazojumuisha **Shilingi 76,127.58** fedha za nje na **Shilingi 7,810.00** fedha za ndani zimetengwa kwa ajili ya kuendelea na ujenzi wa barabara ya Mianzini – Ngaramtoni (km 18) na upanuzi wa sehemu ya Tengeru – USA River (km 9.3), Arusha – Kisongo (km 9.3), daraja jipya la Kikafu (m 560) pamoja na barabara unganishi (km 4.06) na barabara za Moshi Mjini (km 8.4).

Kazi nyingine ni kuanza ujenzi wa barabara ya Tengeru – Mererani (km 28) pamoja na maandalizi ya ujenzi wa barabara ya USA River – Ngarenanyuki – Oldonyosambu sehemu ya km 10 na upanuzi wa barabara ya Kijenge – USA River (km 11.3). Aidha, sehemu ya fedha hizi zitatumika kwa ajili ya malipo ya Mkandarasi na Mhandisi Mshauri wa mradi wa ujenzi wa barabara ya Sakina – Tengeru (km 14.1) na barabara ya mchepuo ya Arusha (km 11.7).

**Barabara za kuelekea kwenye Mradi wa Kufua Umeme katika Maporomoko ya Mto Rufiji (Access Roads to Rufiji Hydropower Project)**

267. ***Mheshimiwa Spika,*** mradi huu umetengewa jumla ya **Shilingi milioni 4,050.00** kwa ajili ya kuendelea na ujenzi kwa kiwango cha lami wa barabara ya Bigwa – Matombo – Mvuha (km 78). Aidha, mradi huu utahusisha kuendelea na Upembuzi Yakinifu na Usanifu wa Kina wa barabara za Chalinze – Utete (km 354.9) na Ngerengere – Mvuha – Kisaki – Mtemele Jct (km 166.4) ikiwa ni mandalizi ya kuijenga kwa kiwango cha lami.

**Barabara ya Dar es Salaam – Chalinze – Morogoro – Expressway**

268. ***Mheshimiwa Spika,*** mradi huu umetengewa jumla ya **Shilingi milioni 4,160.00** kwa ajili ya kuendelea na ukarabati wa barabara ya Mlandizi – Chalinze (km 44), Msoga – Msolwa (Chalinze Bypass km 10) na ujenzi wa barabara ya Kwa Mathiasi – Msangani sehemu ya (km 2.1). Kazi nyingine ni kuanza maandalizi ya upanuzi wa barabara ya Kibaha – TAMCO – Picha ya Ndege (km 4.5) na kuendelea na maandalizi ya ujenzi wa barabara ya Kibaha – Mlandizi – Chalinze – Morogoro Expressway (km 163.8) kwa utaratibu wa PPP. Aidha, fedha hizi zitatumika kwa ajili ya malipo ya Mkandarasi wa kazi ya kuboresha maeneo hatarishi (Assorted Accident Blackspots) katika barabara ya Dar es Salaam – Morogoro na ujenzi wa Kituo cha Pamoja cha Ukaguzi (One Stop Inspection Station – OSIS) cha Vigwaza. Vilevile, fedha hizi zinahusisha kuanza kazi ya upembuzi Yakinifu na Usanifu wa awali sehemu ya Ubungo – Kibaha Expressway (km 34.29).

**Barabara ya Wazo Hill – Bagamoyo – Msata**

269. ***Mheshimiwa Spika,*** mradi huu umetengewa jumla ya **Shilingi milioni 500.00** kwa ajili ya kuanza ukarabati na upanuzi wa barabara hii (sehemu ya Tegeta/DAWASA – Bagamoyo (km 46.9).

**Barabara ya Usagara – Geita – Buzirayombo – Kyamyorwa**

270. ***Mheshimiwa Spika,*** mradi huu umetengewa jumla ya **Shilingi milioni 10.00** kwa ajili ya malipo ya Wakandarasi kwa sehemu za Uyovu – Bwanga (km 43) na Bwanga – Biharamulo (km 67).

**Barabara ya Nyakahura – Kumubuga – Rulenge – Kabanga Nickel**

271. ***Mheshimiwa Spika,*** mradi huu umetengewa jumla ya **Shilingi milioni 1,500.00** kwa ajili ya kuendelea na maandalizi ya ujenzi kwa kiwango cha lami wa barabara za Nyakahura – Kumubuga – Murusagamba (km 34), Kumubuga – Rulenge – Murugarama (km 75) na Rulenge – Kabanga Nickel (km 32).

**Barabara ya Kigoma – Kidahwe – Uvinza – Kaliua – Tabora (km 265)**

272. ***Mheshimiwa Spika,*** mradi huu umetengewa jumla ya **Shilingi milioni 2,839.16** zinazojumuisha **Shilingi milioni 2,500.00** fedha za ndani na **Shilingi milioni 339.16** fedha za nje kwa ajili ya malipo ya Wakandarasi waliojenga barabara za Tabora – Ndono (km 42), Ndono – Urambo (km 52), Kaliua – Kazilambwa (km 56), Urambo – Kaliua (km 28), Malagarasi – Uvinza (km 51.1), Kazilambwa – Chagu (km 36) na Urambo Roundabout. Kazi nyingine ni kuendelea na usanifu wa barabara ya Tabora – Ulyankulu (km 90).

**Barabara ya Ifakara – Kihansi – Mlimba – Madeke – Kibena (Njombe)**

273. ***Mheshimiwa Spika,*** mradi huu umetengewa jumla ya **Shilingi milioni 7,313.72** zinazojumuisha **Shilingi milioni 6,350.00** fedha za ndani na **Shilingi milioni 963,721.56** fedha za nje kwa ajili ya kuendelea na ujenzi wa barabara ya Ifakara – Kihansi (km 124) sehemu za Ifakara – Mbingu (km 62.5) na Mbingu – Chita (km 37.5) na kuanza ujenzi wa barabara ya Kibena – Lupembe – Madeke (km 126); sehemu ya Kibena – Kidegyembe (km 42) kwa kiwango cha lami. Kazi nyingine ni kuendelea na Upembuzi Yakinifu na Usanifu wa Kina wa sehemu ya Kihansi – Mlimba – Madeke - Kidegyembe (km 181) ili iweze kujengwa kwa kiwango cha lami.

**Barabara ya Karatu – Mbulu – Haydom – Sibiti River – Lalago – Maswa**

274. ***Mheshimiwa Spika,*** mradi huu umetengewa jumla ya **Shilingi milioni 7,050.00** kwa ajili ya kuendelea na ujenzi kwa kiwango cha lami wa barabara hii sehemu za Mbulu – Garbabi (km 25) na Labay – Haydom (km 25) na kuanza ujenzi wa Nkoma – Lalago (km 65). Aidha, kazi nyingine ni kuendelea na maandalizi ya ujenzi kwa kiwango cha lami wa barabara ya Mogitu – Haydom (km 68).

**Barabara ya Marangu – Tarakea – Rongai – Kamwanga /Bomang'ombe – Sanya Juu**

275.***Mheshimiwa Spika,*** mradi huu umetengewa ***jumla*** ya **Shilingi milioni 5,230.00** kwa ajili ya kuendelea na ujenzi wa barabara za Kwa Sadala – Masama – Machame Junction (km 16) na Kiboroloni – Kiharara – Tsuduni – Kidia (km 10.8). Kuanza ujenzi wa barabara za Sanya Juu – Kamwanga: sehemu ya Elerai – Kamwanga (km 39.5) na Tarakea – Holili (km 53): sehemu ya Ikuini – Kirongo chini (km 10). Aidha, mradi huu utahusisha kuendelea na maandalizi ya ukarabati wa barabara ya Bomang'ombe – Sanya Juu (km 25) pamoja na malipo ya Wakandarasi na Wahandisi Washauri wa barabara za Marangu – Rombo Mkuu – Tarakea (km 64), Sanya Juu – Kamwanga (sehemu ya Sanya Juu – Elerai, km 32) na KIA – Mererani (km 26).

**Barabara ya Tukuyu – Mbambo – Katumba**

276.***Mheshimiwa Spika,*** mradi huu umetengewa jumla ya **Shilingi milioni 4,460.00** kwa ajili ya kuendelea na ujenzi wa sehemu za Katumba – Lupaso (km 35.3), Mbaka – Kibanja (km 20.7) pamoja na kuendelea na maandalizi ya ujenzi wa barabara ya Mbambo – Ipinda (km 19.7) na malipo ya Mkandarasi wa barabara ya Bujesi – Mbambo (km 10).

**Barabara ya Dodoma – Manyoni**

277. ***Mheshimiwa Spika,*** mradi huu umetengewa jumla ya **Shilingi milioni 1,800.00** kwa ajili ya kuendelea na ujenzi wa Kituo cha Pamoja cha Ukaguzi (One Stop Inspection Station – OSIS) cha Muhalala (Manyoni) na kuanza maandalizi ya ujenzi wa mizani ya Segu.

**Barabara ya Tabora – Mambali – Bukene – Itobo**

278. ***Mheshimiwa Spika,*** mradi huu umetengewa jumla ya **Shilingi milioni 500.00** kwa ajili ya kuendelea na maandalizi ya ujenzi kwa kiwango cha lami wa barabara hii yenye urefu wa km 114.

**Barabara ya Namanyere – Katongoro – New Kipili Port**

279. ***Mheshimiwa Spika,*** mradi huu umetengewa jumla ya **Shilingi milioni 500.00** kwa ajili ya kuendelea na maandalizi ya ujenzi wa barabara ya Namanyere – Katongoro – New Kipili Port (km 64.8); sehemu ya Namanyere – Mfili II Bridge (km 20) kwa kiwango cha lami.

**Barabara ya Dumila – Kilosa – Mikumi**

280. ***Mheshimiwa Spika,*** mradi huu umetengewa jumla ya **Shilingi milioni 270.00** kwa ajili ya malipo ya Wakandarasi na Mhandisi Mshauri wa sehemu za Dumila – Rudewa (km 45) na Rudewa – Kilosa (km 24). Kazi nyingine ni kuendelea na maandalizi ya ujenzi wa barabara ya Kilosa – Ulaya – Mikumi (km 72) kwa kiwango cha lami; sehemu ya Ulaya (km 2).

**Barabara ya Sumbawanga – Matai – Kasanga Port**

281. ***Mheshimiwa Spika,*** mradi huu umetengewa jumla ya **Shilingi milioni 4,510.00** kwa ajili ya kuendelea na ujenzi wa barabara ya Matai – Kasesya (km 50) pamoja na malipo ya Mkandarasi na Mhandisi Mshauri wa ujenzi wa barabara ya Sumbawanga – Matai – Kasanga Port (km 107). Aidha, mradi huu utahusisha kuendelea na maandalizi ya ujenzi wa barabara ya Laela – Mwimbi – Kizombwe (km 93) kwa kiwango cha lami.

**Ujenzi wa Madaraja Makubwa**

282. ***Mheshimiwa Spika,*** mradi huu umetengewa jumla ya **Shilingi milioni 15,030.00** kwa ajili ya malipo ya Wakandarasi na Wahandisi Washauri wa ujenzi wa daraja la Magufuli (Morogoro), Ruhuhu (Ruvuma), Momba (Rukwa), Mara (Mara), Magara (Manyara), Msingi (Singida), Mpwapwa (Dodoma), Itembe (Simiyu) na Kiyegeya (Morogoro). Kazi nyingine ni kuendelea na maandalizi ya kuanza ukarabati wa daraja la Kirumi (Mara), kuendelea na ujenzi wa barabara unganishi za Daraja la Sibiti (Singida), kuendelea na ujenzi wa Madaraja ya Mbambe (Pwani), Kavuu (Katavi), Sukuma (Mwanza), Mwanjiri, Suguta,

Kerema Maziwa na Kibakwe (Dodoma); Mpiji Chini (Dar es Salaam), Simiyu (Mwanza) na Mkenda (Ruvuma).

283.***Mheshimiwa Spika,*** Vilevile, fedha hizi zitahusisha kuendelea na maandalizi ya ujenzi wa Madaraja ya Mtera, Kondoa, Godegode, Pahi, Munguri, Mnenia na Mjonga (Dodoma); Kisorya - Rugezi (MaraMwanza), Suguti (Mara), Sanza (Singida) na Malagarasi Chini (Kigoma). Fedha hizi pia zitahusisha kuendelea na Upembuzi Yakinifu na Usanifu wa Kina wa daraja la Muhuwesi (Ruvuma).

**Barabara ya New Bagamoyo (Kawawa Jct – Tegeta)**

284. ***Mheshimiwa Spika,*** jumla ya **Shilingi milioni 10.00** zimetengwa kwa ajili ya malipo ya Mkandarasi na Mhandisi Mshauri wa ujenzi wa barabara ya Morocco – Mwenge (km 4.3).

**Barabara ya Kyaka – Bugene – Kasulo**

284.***Mheshimiwa Spika,*** jumla ya **Shilingi milioni 3,810.00** zimetengwa kwa ajili ya kuendelea na ujenzi kwa kiwango cha lami wa barabara ya Kumunazi – Kasulo – Bugene (km 133); sehemu ya Bugene – Burigi Chato National Park (km 60) pamoja na maandalizi ya ujenzi wa sehemu za Burigi Chato – Kimisi (km 15) na Nyakahanga – Nyabiyonza – Nyakakika (km 96): sehemu ya Nyakahanga – Nyabiyonza – Chabalisa (km 22.5) pamoja na malipo ya Mkandarasi wa sehemu ya Kyaka – Bugene (km 59.1).

**Barabara ya Isaka – Lusahunga**

286. ***Mheshimiwa Spika,*** jumla ya **Shilingi milioni 29,341.43** zinazojumuisha **Shilingi milioni 2,560.00** fedha za ndani na **Shilingi milioni 26,781.43** fedha za nje zimetengwa kwa ajili ya kuendelea na ujenzi wa Kituo cha Pamoja cha Ukaguzi – OSIS cha Nyakanazi pamoja na ukarabati wa sehemu ya Lusahunga – Rusumo (km 92). Mradi huu utahusisha pia maandalizi ya ujenzi wa barabara ya Nyakasanza – Kobero (km 58) kwa kiwango cha lami pamoja na malipo ya Wakandarasi na Mhandisi Mshauri wa sehemu ya Ushirombo – Lusahunga (km 110).

**Barabara ya Manyoni – Itigi – Tabora**

287.***Mheshimiwa Spika,*** jumla ya **Shilingi milioni 6,482.09** zinazojumuisha **Shilingi milioni 130.00** fedha za ndani na **Shilingi milioni 6,352.09** fedha za nje zimetengwa kwa ajili ya malipo ya Wakandarasi na Wahandisi Washauri wa ujenzi wa sehemu za Manyoni – Itigi – Chaya (km 89.35), Nyahua – Chaya (km 85.4), Tabora – Nyahua (km 85) na Mizani ya Kizengi.

288.***Mheshimiwa Spika,*** jumla ya **Shilingi milioni 61,585.00** zimetengwa kwa ajili ya **Barabara za Mikoa** na madaraja katika mikoa yote 26 ya Tanzania Bara. Kazi zilizopangwa kutekelezwa ni ukarabati wa jumla ya kilometa **421.62** kwa kiwango cha changarawe, kujenga kilometa **59** kwa kiwango cha lami na ujenzi wa Madaraja/Makalavati **51.** Aidha, fedha hizi zitatumika kwa ajili ya programu ya mafunzo kwa vitendo (Structured Engineers Apprentinceship Programme – SEAP) kwa wahandisi wahitimu. **Orodha ya miradi ya barabara za Mikoa itakayotekelezwa kwa kutumia fedha za Bajeti ya Maendeleo kutoka Mfuko Mkuu wa Serikali imeoneshwa katika Kiambatisho Na. 2.**

**Barabara ya Mwanza/Shinyanga Border – Mwanza**

289. ***Mheshimiwa Spika,*** jumla ya **Shilingi milioni 3,050.00** zimetengwa kwa ajili ya kuanza maandalizi ya ukarabati wa barabara hii pamoja na upanuzi wa barabara ya Mwanza - Usagara - JPM Bridge kwa njia nne (km 37); Sehemu ya Mwanza – Usagara (km 25).

**Mradi wa Kupunguza Msongamano Barabara za Dar es Salaam**

290. ***Mheshimiwa Spika,*** mradi huu umetengewa jumla ya **Shilingi milioni 9,440.00** kwa ajili ya kuendelea na ujenzi wa barabara za Kimara – Bonyokwa – Kinyerezi (km 6.73), Goba – Matosa – Temboni (km 6), Kibamba Shule – Mpiji Magoe (km 9.2), Mbezi Msakuzi – Makabe Jct (km 8.36) na Chanika – Mbande – Rangi Tatu (km 3.8). Aidha, fedha hizi zitahusisha kuanza ujenzi wa barabara za Kibamba – Kisopwa – Kwembe – Makondeko (km

14.66), Kongowe – Mjimwema – Kivukoni Ferry (One Lane Widening: km 25.1) na Mbezi Victoria – Mpiji Magoe – Bunju (km 9.55). Kazi nyingine ni maandalizi ya upanuzi wa barabara ya Mwai Kibaki (km 9.1), Mbagala Rangi Tatu - Nzasa Jct (km 2.00), Chamazi Centre (km 6.00), Mbande - Chamazi Complex (km 2.00) na Gongo la Mboto - Buyuni (km 10) na kuendelea na maandalizi ya ujenzi wa barabara ya Mji Mwema – Kimbiji – Pembamnazi (km 10). Aidha, fedha hizi zitatumika kwa ajili ya malipo ya Wakandarasi wa barabara za Kipata (m 700), Livingstone (m 350), Msikitini – Sharif Shamba (km 1), Tangi Bovu – Goba (km 9), Kimara Baruti – Msewe – Changanyikeni (km 2.6), Wazo Hill – Madale (km 6) pamoja na Ardhi – Makongo – Goba; sehemu ya Ardhi – Makongo (km 5).

**Barabara ya Nyamuswa – Bunda – Kisorya**

291. ***Mheshimiwa Spika,*** jumla ya **Shilingi milioni 820.00** zimetengwa kwa ajili ya kuendelea na ujenzi wa barabara ya Nansio – Rugezi (km 6) pamoja na malipo ya Mkandarasi na Mhandisi Mshauri wa ujenzi wa sehemu za Kisorya – Bulamba (km 51) na Nyamuswa – Bunda – Bulamba (km 56.4).

**Barabara ya Kolandoto – Lalago – Ng'oboko – Mwanhuzi**

292. ***Mheshimiwa Spika,*** jumla ya **Shilingi milioni 1,650.00** zimetengwa kwa ajili ya kuendelea na maandalizi ya ujenzi kwa kiwango cha lami wa barabara za Kolandoto – Kishapu – Lalago (km 64); Sehemu ya Kolandoto – Kola Bridge (km 10) na Iguguno Shamba – Nduguti – Mkalama (km 89); Sehemu ya Iguguno Shamba – Mnolo (km 10).

**Barabara ya Ndundu – Somanga**

293. ***Mheshimiwa Spika,*** jumla ya Shilingi **milioni 4,010.00** zimetengwa kwa ajili ya kuendelea na ujenzi wa barabara ya Utete – Nyamwage (km 33.7), kuendelea na maandalizi ya ukarabati wa barabara za Malendego – Tingi (km 50), Bungu – Nyamisati (km 40.03) na Nangurukuru – Mbwemkuru (km 95). Kazi nyingine ni kuendelea na maandalizi ya ujenzi wa barabara ya

Ikwiriri – Mkongo (km 27.74) na malipo ya Mkandarasi wa ujenzi wa barabara ya Ndundu – Somanga (km 60).

**Barabara ya Kasulu – Manyovu**

294.***Mheshimiwa Spika,*** jumla ya **Shilingi milioni 19,377.27** zinazojumuisha **Shilingi milioni 300.00** fedha za ndani na **Shilingi milioni 19,077.27** fedha za nje zimetengwa kwa ajili ya malipo ya Mkandarasi wa barabara ya Kasulu – Manyovu pamoja na barabara za kuingia Kasulu mjini (km 68) na kuendelea na ujenzi wa Kituo cha Pamoja Mpakani (OSBP) cha Manyovu/Mugina.

**Barabara ya Dodoma *City Outer Dual Carriageway Ring Road Lot1 & 2***

295.***Mheshimiwa Spika,*** mradi huu umetengewa jumla ya **Shilingi milioni 50,004.28** zinazojumuisha **Shilingi milioni 1,500.00** fedha za ndani na **Shilingi milioni 48,504.28** fedha za nje kwa ajili ya malipo ya Wakandarasi wa ujenzi wa Barabara ya Mzunguko wa Nje katika Jiji la Dodoma (Dodoma City Outer Dual Carriageway Ring Road) sehemu za Nala – Veyula – Mtumba – Ihumwa Dry Port (km 52.3) na Ihumwa Dry Port – Matumbulu – Nala (km 60). Kazi nyingine ni kuanza ujenzi wa barabara ya Mzunguko wa Ndani katika Jiji la Dodoma (Dodoma Inner Ring Road) kwa sehemu ya Bahi R/About – Image R/About – Ntyuka R/About – Makulu R/About (km 6.3) na kuendelea na maandalizi ya ujenzi wa barabara ya Mzunguko wa Kati katika Jiji la Dodoma (Dodoma City Middle Ring Road) inayoanzia Nanenane – Miyuji – Mnadani Sekondari – Mkonze – Ntyuka – Nanenane (km 47.2) na *Msalato Airport* – Mtumba – Chamwino IKULU (km 30) kwa kiwango cha lami.

**Barabara ya Kidatu – Ifakara – Lupilo – Malinyi – Londo – Lumecha/Songea**

296. ***Mheshimiwa Spika,*** mradi huu umetengewa jumla ya **Shilingi milioni 4,200.00** kwa ajili ya malipo ya Mkandarasi na Mhandisi Mshauri wa ujenzi wa sehemu ya Kidatu – Ifakara (km 66.9) na kuendelea na maandalizi ya ujenzi wa barabara ya

Chalinze – Magindu – Lukenge – Seregete B – Kabwe Jct – Mkulazi (km 77.5). Aidha, mradi huu utahusisha ujenzi kwa kiwango cha lami wa barabara ya Ifakara – Lupilo – Malinyi – Londo – Lumecha/Songea (km 396) sehemu ya Ifakara – Lupilo – Mtimbira (km 112) pamoja na Barabara ya Lupilo – Mahenge (km 42.00).

**Barabara ya Tabora – Ipole – Koga – Mpanda**

297. ***Mheshimiwa Spika,*** jumla ya **Shilingi milioni 50.00** zimetengwa kwa ajili ya malipo ya Wakandarasi na Wahandisi Washauri wa ujenzi wa sehemu za Usesula – Komanga (km 115), Komanga – Kasinde (km 120), Kasinde – Mpanda (km 118), Tabora – Sikonge (km 30) na *Mpanda Airport* – Kasimba Jct (km 3) kwa kiwango cha lami.

**Barabara ya Makutano – Natta – Mugumu/Loliondo – Mto wa Mbu**

298. ***Mheshimiwa Spika,*** mradi huu umetengewa jumla ya **Shilingi milioni 9,820.00** kwa ajili ya kuendelea na ujenzi kwa kiwango cha lami kwa sehemu ya Sanzate – Natta (km 40), kuanza ujenzi wa sehemu za Waso – Loliondo (km 10), Mto wa Mbu – Selela (km 23) na Monduli – Engaruka (km 115): sehemu ya Ngarashi - Enguik (km 11) pamoja na kuendelea na maandalizi ya kuanza ujenzi kwa kiwango cha lami wa sehemu ya Natta – Mugumu (km 45), Selela – Engaruka (km 27) na Engaruka - Ngaresero (km 39). Aidha fedha hizo zitatumika kwa ajili ya malipo ya Wakandarasi na Wahandisi Washauri wa barabara za Makutano – Sanzate (km 50) na Waso – Sale Jct (km 49).

**Barabara ya Ibanda – Itungi Port**

299. ***Mheshimiwa Spika,*** mradi huu umetengewa jumla ya **Shilingi milioni 4,770.00** kwa ajili ya kuendelea na ukarabati wa barabara za Ibanda – Kajunjumele (km 22) na ujenzi wa sehemu ya Kajunjumele – Kiwira Port (km 6). Kazi nyingine ni kukamilisha ujenzi wa Kituo cha Pamoja Mpakani Kasumulu/Songwe (Kasumulu/Songwe– Tanzania/ Malawi Border OSBP) pamoja na malipo ya Mkandarasi na Mhandisi Mshauri wa ujenzi wa

barabara ya Kikusya – Ipinda – Matema Beach (km 39.1) na barabara ya Uyole – Kasumulu sehemu ya Ilima *Escarpment* (km 3).

**Barabara ya Nzega – Tabora**

300. ***Mheshimiwa Spika,*** mradi huu umetengewa jumla ya **Shilingi milioni 820.00** kwa ajili ya kuanza ujenzi kwa kiwango cha lami wa barabara ya Puge – Ziba – Choma (km 109) sehemu za Ziba – Choma (km 1), Ziba – Nkinga (km 5) na Puge – Ndala (km 5) pamoja na malipo ya Wakandarasi na Wahandisi Washauri wa ujenzi wa sehemu za Nzega – Puge (km 58.6) na Puge – Tabora (km 56.1).

**Barabara ya Sumbawanga – Mpanda – Nyakanazi**

301. ***Mheshimiwa Spika,*** mradi huu umetengewa jumla ya **Shilingi milioni 58,947.10** zinazojumuisha **Shilingi milioni 12,740.00.00** fedha za ndani na **Shilingi milioni 46,207.10** fedha za nje kwa ajili ya kuendelea na ujenzi kwa kiwango cha lami wa barabara za Kibaoni – Mlele Jct (km 50), Mpanda – Mishamo – Uvinza sehemu ya Vikonge – Luhafwe (km 25), Luhafwe – Mishamo/Bulamata Jct (km 37), Kagwira – Ikola – Karema Port Lot 1: Kagwira – Kasekese (km 54.14) na Lot 2: Kasekese – Karema Port (km 59.3). Kazi nyingine ni kuendelea na maandalizi ya ujenzi wa barabara za Mishamo – Uvinza (km 100), Kizi – Lyambalyamfipa – Sitalike (km 86.31), Mlele Junction – Sitalike (km 23.5) na Lyazumbi – Kabwe (km 65). Aidha, fedha hizi zitatumika kwa ajili ya malipo ya Wakandarasi na Wahandisi Washauri wa sehemu za Sumbawanga – Kanazi (km 75), Kanazi – Kizi – Kibaoni (km 76.6), Sitalike – Mpanda (km 36) na Mpanda – Ifukutwa – Vikonge (km 37.65).

**Barabara ya Nyanguge – Musoma/Usagara – Kisesa Bypass**

302. ***Mheshimiwa Spika,*** mradi huu umetengewa jumla ya **Shilingi milioni 2,520.00** kwa ajili ya kuendelea na maandalizi ya ukarabati wa sehemu ya Nyanguge – Simiyu/Mara Border (km 100.4) na kuanza ujenzi wa barabara ya *Airport* – Kayenze –

Nyanguge (Airport Bypass) (km 46) sehemu ya Airport Jct – Igombe (km 10) pamoja na malipo ya Mkandarasi wa barabara ya Simiyu/Mara Border – Musoma (km 85.5).

**Barabara ya Magole – Mziha – Handeni**

303. ***Mheshimiwa Spika,*** mradi huu umetengewa jumla ya **Shilingi milioni 510.00** kwa ajili ya kuendelea na maandalizi ya ujenzi wa sehemu ya Handeni – Kang'ata (km 30) na malipo ya Mkandarasi wa barabara ya Magole – Turiani (km 48.8).

**Ujenzi wa Barabara za Juu (Flyovers) Jijini DSM na Barabara Unganishi**

304. ***Mheshimiwa Spika,*** mradi huu umetengewa jumla ya **Shilingi milioni 1,510.00** zinazojumuisha **Shilingi milioni 510.00** fedha za ndani na **Shilingi milioni 1,000.00** fedha za nje kwa ajili ya kuendelea na maandalizi ya kuboresha makutano ya barabara katika maeneo ya KAMATA, Magomeni, Mwenge, Tabata/Mandela, Morocco, Buguruni, Mbezi Mwisho, Fire pamoja na makutano ya barabara za Kinondoni/Ali Hassan Mwinyi na Selander (Ali Hassan Mwinyi/UN Road Jct) pamoja na malipo ya Wakandarasi na Wahandisi Washauri wa ujenzi wa barabara za juu katika makutano ya Ubungo (Ubungo Interchange).

**Barabara ya Mwigumbi – Maswa – Bariadi – Lamadi**

305. ***Mheshimiwa Spika,*** mradi huu umetengewa jumla ya **Shilingi milioni 30.00** kwa ajili ya malipo ya Wakandarasi na Wahandisi Washauri wa barabara za Mwigumbi – Maswa (km 50.3), Maswa – Bariadi (km 49.7) na barabara ya Mchepuo wa Maswa (Maswa Bypass; km 11).

**Barabara ya Tabora – Ipole – Rungwa (Sehemu ya Ipole – Rungwa)**

306. ***Mheshimiwa Spika,*** mradi huu umetengewa jumla ya **Shilingi milioni 1,000.00** kwa ajili ya kuendelea na maandalizi ya

ujenzi wa barabara hii yenye urefu wa km 172 kwa kiwango cha lami.

**Barabara ya Kidahwe – Kasulu – Kibondo – Nyakanazi (km 341.25)**

307. ***Mheshimiwa Spika,*** mradi huu umetengewa jumla ya **Shilingi milioni 33,227.14** zinazojumuisha **Shilingi milioni 6,020.00** fedha za ndani na **Shilingi milioni 27,207.14** fedha za nje kwa ajili ya kuendelea na ujenzi wa sehemu za Mvugwe – Nduta Jct. (km 59.35), Nduta Jct. – Kibondo (km 25.9) na Kibondo – Mabamba (km 48.0) pamoja na malipo ya Wakandarasi na Wahandisi Washauri wa barabara za Kidahwe – Kasulu (km 63.0) na Nyakanazi – Kakonko (km 50.0), Kanyani Jct. – Mvugwe (km 70.5), Nduta Jct. – Kibondo Jct. – Kabingo (km 62.5).

**Barabara ya Kwenda Kiwanja cha Ndege cha Mafia (Mafia Airport Access Road**

308. ***Mheshimiwa Spika,*** mradi huu umetengewa jumla ya **Shilingi milioni 1,000.00** kwa ajili ya kuendelea na maandalizi ya ujenzi wa barabara ya Kilindoni – Ras Mkumbi (km 54.4).

**Daraja la Kigamboni (Nyerere) na Barabara Unganishi**

309. ***Mheshimiwa Spika,*** mradi huu umetengewa jumla ya **Shilingi milioni 2,530.00** kwa ajili ya kuendelea na ujenzi wa barabara ya Kibada – Mwasonga – Tundwisongani Jct/Tundwisongani – Kimbiji (Kibada – Mwasonga – Songani Jct Section (km 41) pamoja na malipo ya Wakandarasi na Wahandisi Washauri wa barabara za Daraja la Nyerere – Vijibweni (km 1.5) na Tungi – Kibada (km 3.8).

**Barabara ya Mutukula – Bukoba – Muhutwe – Kagoma**

310. ***Mheshimiwa Spika,*** mradi huu umetengewa jumla ya **Shilingi milioni 2,300.00** kwa ajili ya kuendelea na maandalizi ya ujenzi kwa kiwango cha lami wa barabara za Kanazi (Kyetema) – Ibwera – Katoro – Kyaka II (km 60.7) sehemu ya Kanazi (Kyetema) – Kalebe Bridge (km 10) pamoja na malipo ya Mkandarasi wa

kazi ya upanuzi wa barabara ya Bukoba – Bukoba Port (km 5). Kazi nyingine ni kuendelea na Upembuzi Yakinifu na Usanifu wa Kina wa barabara za Bukoba Mjini – Busimbe – Maruku – Kanyangereko – Ngongo (km 19.1) na Kyaka - Bukoba – Muhutwe – Kagoma (km 101).

**Fedha za Matengenezo na Ukarabati wa Barabara**

311. ***Mheshimiwa Spika,*** jumla ya **Shilingi milioni 1,047,405.50** kwa ajili ya matengenezo na ukarabati wa barabara, Upembuzi Yakinifu na Usanifu wa Kina, udhibiti wa uzito wa magari, usalama barabarani na mazingira, matengenezo na ukarabati wa vivuko pamoja na kujenga uwezo wa Wizara na Taasisi zinazosimamia masuala ya barabara na vivuko. Fedha hizi zinasimamiwa na Bodi ya Mfuko wa Barabara.

**Ujenzi wa Njia za Magari Mazito na Maegesho ya Dharura Katika Barabara Kuu ya Ukanda wa Kati**

312. ***Mheshimiwa Spika,*** mradi huu umetengewa jumla ya **Shilingi milioni 250.00** kwa ajili ya maandalizi ya Upembuzi Yakinifu na Usanifu wa Kina wa maeneo ya kujenga njia za magari mazito kwenye miinuko na kujenga maegesho ya dharura katika Barabara Kuu ya Ushoroba wa Kati.

**Upanuzi wa Barabara ya Kimara – Kibaha Ikijumuisha Upanuzi wa Madaraja ya Kibamba, Kiluvya na Mpiji**

313. ***Mheshimiwa Spika,*** mradi huu umetengewa jumla ya **Shilingi milioni 500.00** kwa ajili ya malipo ya Mkandarasi na Mhandisi Mshauri wa barabara ya Kimara – Kibaha (km 25.7) sehemu ya Kimara – Kibaha Mizani (km 19.2) na madaraja ya Kibamba, Kiluvya na Mpiji.

**Barabara ya Kisarawe – Mlandizi**

314. ***Mheshimiwa Spika,*** mradi huu umetengewa jumla ya **Shilingi milioni 500.00** kwa ajili ya kuendelea na maandalizi ya

ujenzi wa barabara hii yenye urefu wa km 119 kwa kiwango cha lami.

**Barabara ya Pugu – Kifuru – Mbezi Mwisho – Mpiji Magoe – Bunju**

315. ***Mheshimiwa Spika,*** jumla ya **Shilingi milioni 500.00** zimetengwa kwa ajili ya kuendelea na Upembuzi Yakinifu na Usanifu wa Kina wa barabara ya mzunguko wa nje unaojumuisha sehemu za Bunju – Kibamba – Pugu Kajiungeni – Mzinga – Tuangoma – Kigamboni (km 61) na mzunguko wa kati sehemu ya Mbezi Mwisho (Kwa Msuguri) – Kifuru – Banana – Kipara – Kigamboni (km 49).

**Barabara ya Kagoma – Lusahunga**

316. ***Mheshimiwa Spika,*** jumla ya **Shilingi milioni 10.00** zimetengwa kwa ajili ya malipo ya Mkandarasi na Mhandisi Mshauri wa barabara ya Muleba – Kanyambogo – Rubya (km 18.5).

**Barabara ya Singida – Shelui**

317. ***Mheshimiwa Spika,*** jumla ya **Shilingi milioni 2,600.00** zimetengwa kwa ajili ya kuanza ujenzi wa barabara ya Singida Urban – Ilongero – Haydom (km 93) sehemu ya Singida Urban (Igauri) – Ilongero (km 11), kuendelea na ujenzi wa barabara ya Ulemo – Kinampanda – Gumanga – Mkalama (km 46) na kuanza upanuzi wa barabara za Singida Mjini (km 10). Aidha, fedha hizi zitatumika kwa ajili ya malipo ya Mhandisi Mshauri wa kazi ya Usanifu wa Kina wa barabara ya Singida – Shelui (km 110) na upanuzi wa barabara hii eneo la Mlima Sekenke (km 6).

**Barabara ya Dar es Salaam – Mbagala (Kilwa Road)**

318. ***Mheshimiwa Spika,*** jumla ya **Shilingi milioni 3,810.00** zimetengwa kwa ajili ya kuendelea na upanuzi wa sehemu za Mbagala Rangi Tatu – Kongowe (km 3.8) kutoka njia mbili kuwa njia sita. Kazi nyingine ni kuendelea na maandalizi ya ukarabati wa sehemu ya Ikwiriri - Nyamwage – Malendego (km 56) na

ujenzi wa barabara ya Mkuranga – Kisiju (km 46) na Vikindu - Vianzi – Sangatini (km 20) pamoja na malipo ya Mkandarasi na Mhandisi Mshauri wa ujenzi wa daraja la Gerezani.

**Barabara ya Msimba – Ruaha Mbuyuni/Ikokoto Mafinga**

319. ***Mheshimiwa Spika,*** jumla ya **Shilingi milioni 1,210.00** zimetengwa kwa ajili ya kuendelea na maandalizi ya ujenzi wa barabara ya Rujewa – Madibira – Mafinga (km 152) pamoja na kuanza Upembuzi Yakinifu na Usanifu wa Kina kwa ajili ya ukarabati wa barabara ya Morogoro – Iringa sehemu ya Tumbaku Jct – Mangae/Melela – Mikumi – Iyovi (km 158.45). Kazi nyingine ni kuendelea na upanuzi wa eneo la Mlima Kitonga kutoka njia mbili kuwa njia nne (km 10). Aidha, fedha hizi zitatumika kwa ajili ya malipo ya Mkandarasi na Mhandisi Mshauri wa ukarabati wa sehemu ya Mafinga – Igawa (km 137.9).

**Barabara ya Korogwe – Mkumbara – Same**

320. ***Mheshimiwa Spika,*** jumla ya **Shilingi milioni 4,700.00** zimetengwa kwa ajili ya kuendelea na ujenzi wa barabara ya Same – Kisiwani – Mkomazi (km 100.5) sehemu ya Ndungu – Mkomazi (km 36) na kuanza ujenzi wa sehemu ya Same – Kisiwani – Mroyo (km 56.83). Kazi nyingine ni kuendelea na maandalizi ya ukarabati wa sehemu za Same – Himo (km 76) na Mombo – Lushoto (km 32) pamoja na maandalizi ya ujenzi wa barabara ya Lushoto – Magamba – Mlola (km 34.5).

**Barabara ya Mbeya – Makongolosi – Manyoni**

321. ***Mheshimiwa Spika,*** jumla ya **Shilingi milioni 6,230.00** zimetengwa kwa ajili ya kukamilisha ujenzi wa barabara za Itigi Mjini (km 10.7), kuendelea na ujenzi sehemu za Noranga (Doroto) – Itigi (Mlongoji) (km 25), Noranga – Doroto & Itigi – Mkiwa (km 31.6) pamoja na maandalizi ya ujenzi wa barabara ya Mbalizi – Makongolosi (km 56), Manyoni East – Heka – Sanza – Bihawana (km194) na Makongolosi – Rungwa - Noranga (km 256). Aidha, fedha hizi zitatumika kwa ajili ya malipo ya Wakandarasi na Wahandisi Washauri wa sehemu za Mbeya – Lwanjilo (km 36), Lwanjilo – Chunya (km 36) na Chunya – Makongolosi (km 39).

**Barabara ya Itoni – Ludewa – Manda**

322. ***Mheshimiwa Spika,*** jumla ya **Shilingi milioni 4,110.00** zimetengwa kwa ajili ya kuendelea na ujenzi kwa kiwango cha zege wa sehemu ya Itoni – Lusitu (km 50). Kazi nyingine ni kuendelea na maandalizi ya ujenzi wa barabara ya Nkomang'ombe – Mchuchuma (km 7) na sehemu ya tatu ya Mawengi - Ludewa – Manda (km 111) kwa kiwango cha lami. Aidha, fedha hizi zitatumika kwa ajili ya malipo ya Mkandarasi na Mhandisi Mshauri wa ujenzi wa barabara ya Lusitu – Mawengi (km 50).

**Ujenzi wa Daraja Jipya la Selander (Tanzanite)**

323. ***Mheshimiwa Spika,*** jumla ya **Shilingi milioni 10.00** zimetengwa kwa ajili ya malipo ya Mkandarasi na Mhandisi Mshauri wa ujenzi wa Daraja Jipya la Selander (km 1.03) na barabara unganishi zenye jumla ya urefu wa kilometa 5.2.

**Handeni – Kibirashi – Kibaya – Njoro – Goima – Chambalo – Chemba – Kwa Mtoro – Singida**

324. ***Mheshimiwa Spika,*** jumla ya **Shilingi milioni 8,000.00** zimetengwa kwa ajili ya kuendelea na ujenzi kwa kiwango cha lami wa barabara hii kwa sehemu za Handeni – Mafuleta (km 20), Mafuleta – Kileguru (km 30), kuanza kazi za ujenzi wa sehemu ya Kisima – Kibaya (km 50). Kazi nyingine ni kuendelea na maandalizi ya ujenzi wa sehemu ya Kileguru – Kibirashi – Kibaya – Singida (km 324) kwa utaratibu wa PPP.

**Barabara ya Makambako – Songea na Barabara ya Mchepuo ya Songea (Songea Bypass)**

325. ***Mheshimiwa Spika,*** jumla ya **Shilingi milioni 42,313.56** zinazojumuisha **Shilingi milioni 1,500.00** fedha za ndani na **Shilingi milioni 40,813.56** fedha za nje zimetengwa kwa ajili ya kuendelea na ukarabati wa barabara ya Makambako – Songea sehemu ya Lutukila – Songea (km 95.18) na Mchepuo wa Songea (km 11). Kazi nyingine ni kuendelea na maandalizi ya ujenzi wa barabara

ya Ramadhani – Iyayi - Ilembula Hospital (km 75) sehemu ya Ramadhani – Itulike (km 10), OSIS ya Idofi na ukarabati wa sehemu ya Makambako – Lutikila (km 184).

**Barabara ya Dodoma – Iringa**

326. ***Mheshimiwa Spika,*** jumla ya **Shilingi milioni 5,510.00** zimetengwa kwa ajili ya kuendelea na ujenzi kwa kiwango cha lami wa barabara ya mchepuo ya Iringa (km 7.3), kuimarisha matabaka ya barabara ya Iringa – Dodoma (km 20), kuanza maandalizi ya ujenzi wa mizani ya Mlowa na ujenzi wa barabara ya Iringa – Pawaga (km 71.9) sehemu ya Pawaga Jct – Ikonongo (km 5) na Itunundu – Ilolo mpya (km 20). Aidha, fedha hizi zitatumika kwa ajili ya malipo ya Mkandarasi wa ujenzi wa Mizani kwenye barabara ya Iringa – Dodoma.

**Barabara ya Dodoma – Babati**

327. ***Mheshimiwa Spika,*** jumla ya **Shilingi milioni 2,730.00** zimetengwa kwa ajili ya kuendelea na ujenzi wa barabara ya Dareda – Dongobesh (km 60): sehemu ya Dareda Mjini – Dareda Mission (km 8) kwa kiwango cha lami pamoja na ujenzi wa barabara mlima Magara (Magara Escapement) kwa zege na maandalizi ya ujenzi wa barabara ya Olbolot – Dalai – Mnenia – Kolo (km 117) sehemu ya Kolo – Mnenia (Kiteo) km 20. Aidha, fedha hizi zitatumika kwa ajili ya malipo ya Wakandarasi na Wahandisi Washauri wa ujenzi wa sehemu za Dodoma – Mayamaya (km 43.65), Mayamaya – Mela (km 99.35) na Mela – Bonga (km 88.8).

**Barabara ya Masasi – Songea – Mbamba Bay**

328. ***Mheshimiwa Spika,*** mradi huu umetengewa jumla ya **Shilingi milioni 1,740.00** kwa ajili ya kuendelea na maandalizi ya ujenzi wa barabara ya Mtwara Pachani – Nalasi – Tunduru (km 300), Nangombo – Chiwindi (km 40), Namtumbo – Mtonya (km 11.74) na Mtonya – Mgombasi – Naikesi (km 44.06) kwa kiwango cha lami. Aidha, fedha hizi zitatumika kwa ajili ya malipo ya Wakandarasi na Wahandisi Washauri wa ujenzi wa sehemu za

Tunduru – Matemanga (km 59), Matemanga – Kilimasera (km 68.2), Kilimasera – Namtumbo (km 60) na Mbinga – Mbamba Bay (km 66). Aidha, mradi huu unahusisha

**Ujenzi wa Barabara za Chuo cha Uongozi (Uongozi Institute)**

329. ***Mheshimiwa Spika,*** jumla ya **Shilingi milioni 300.00** zimetengwa kwa ajili ya maandalizi ya ujenzi wa barabara hii yenye urefu wa kilometa 8.8 kwa kiwango cha lami.

**Barabara ya Igawa – Songwe – Tunduma na Mbeya *Bypass***

330. ***Mheshimiwa Spika,*** jumla ya Shilingi **milioni 4,060.00** zimetengwa kwa ajili ya kuendelea na upanuzi wa sehemu ya Nsalaga - Uyole - Ifisi (km 29) na kuendelea na maandalizi ya ujenzi wa barabara ya mchepuo ya Uyole – Songwe (km 48.9) na Igawa – Songwe – Tunduma (km 218) kwa kiwango cha lami kwa utaratibu wa PPP. Aidha, mradi huu utahusisha kuanza maandalizi ya ujenzi kwa kiwango cha lami wa barabara ya Iwambi – Mbalizi Bypass (km 6.5).

**Miundombinu ya Mabasi Yaendayo Haraka (BRT Phase I – V)**

331. ***Mheshimiwa Spika,*** jumla ya **Shilingi milioni 213,843.91** zinazojumuisha **Shilingi milioni 2,500.00** fedha za ndani na **Shilingi milioni 211,343.91** fedha za nje zimetengwa kwa ajili ya kuendelea na ujenzi wa Miundombinu ya Mabasi Yaendayo Haraka Awamu ya Tatu na Nne, kukamilisha maboresho ya miundombinu ya Mabasi Yaendayo Haraka iliyojengwa katika Awamu ya Kwanza, kuendelea na ujenzi wa daraja la Jangwani pamoja na kuanza ujenzi wa Miundombinu ya Mabasi Yaendayo Haraka Awamu ya Tano pamoja na malipo ya Wakandarasi wa ujenzi wa miundombinu ya Mabasi Yaendayo Haraka Awamu ya Pili na Tatu.

**Ujenzi wa Jengo la Makao Makuu ya Taasisi ya Teknolojia ya Ujenzi (Institute of Construction Technology – ICoT)**

332. ***Mheshimiwa Spika,*** jumla ya **Shilingi milioni 2,000.00** zimetengwa kwa ajili ya kuendelea na ujenzi wa jengo la Makao Makuu ya Taasisi ya Teknolojia ya Ujenzi (Institute of Construction Technology – ICoT) Mkoani Morogoro pamoja na kuanza maandalizi ya ujenzi wa majengo ya ICoT *Campus* ya Mbeya.

**Ujenzi wa Makao Makuu ya Wakala wa Barabara Tanzania**

333. ***Mheshimiwa Spika,*** jumla ya **Shilingi milioni 3,000.00** zimetengwa kwa ajili ya kukamilisha ujenzi wa jengo la Makao Makuu ya Wakala ya Barabara (TANROADS) pamoja na kuendelea na maandalizi ya ujenzi wa Ofisi za Mikoa ya Dar es Salaam, Katavi, Geita, Simiyu, Njombe, Lindi na Songwe.

b) **Udhibiti Uzito wa Magari, Masuala ya Usalama Barabarani na Mazingira**

334. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2026/27, mradi wa Usalama Barabarani umetengewa jumla ya **Shilingi milioni 1,037.101** kwa ajili ya ujenzi wa vituo vya mizani vya Buhigwe katika barabara kuu ya Kasulu-Manyovu, Kidyama katika barabara kuu ya Kasulu- Kibondo na Marolegwa katika barabara kuu ya Kibondo – Kakonko. Kazi nyingine ni kuendelea na maandalizi ya ujenzi wa mizani 32 ya kisasa inayopima uzito wa magari yakiwa kwenye mwendo. Vilevile, fedha za mradi huu zitatumika kuwezesha usanifu na ufungaji wa mifumo ya TEHAMA kwa ajili ya usimamizi wa utendaji kazi wa mizani 58 pamoja na kuwezesha ujenzi wa Vituo vya Ukaguzi wa Pamoja (OSIS) vya Ruaha Mbuyuni (Morogoro) na Himo (Kilimanjaro).

335. ***Mheshimiwa Spika,*** mradi wa Kujenga Uwezo wa Taasisi katika masuala ya usalama barabarani na mazingira umetengewa **Shilingi milioni 180.5** kwa ajili ya kuwezesha huduma za ukaguzi wa usalama wa barabara kwa miradi mipya mitano (5) ya barabara za mikoa na miradi mipya mitano (5) ya barabara kuu. Kazi nyingine ni kufanya tathmini ya hadhi ya

barabara zenye urefu wa km 1,500 katika barabara zinazotumika (iRAP Star rating road safety assessment) na ukaguzi wa barabara kubaini maeneo hatarishi katika ushoroba wa kati.

336. ***Mheshimiwa Spika,*** mradi wa Menejimenti ya Usimamizi wa Mazingira umetengewa **Shilingi milioni 152.54** kwa ajili ya kuandaa mkakati wa Wizara ya Ujenzi wa kupunguza vihatarishi vya maafa pamoja na maandalizi ya mpango wa kujiandaa kukabiliana na maafa. Aidha, Wizara imepanga kufanya mapitio ya miongozo ya tathmini na usimamizi wa mazingira na kuandaa mpango tekelezi wa mazingira wa miaka mitano wa Sekta ya Ujenzi (Works Sector Environment Action Plan). Vilevile, Wizara imepanga kupanda miti 40,000 katika barabara kuu na barabara za mikoa na kuanza maandalizi ya mpango wa kuhimili mabadiliko ya Tabianchi wa Sekta ya Ujenzi.

c) **Ujenzi na Ukarabati wa Vivuko na Maegesho ya Vivuko**

337. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2026/27 mradi wa **Ujenzi na Ukarabati wa Vivuko, Maegesho na miundombinu ya maegesho** umetengewa jumla ya **Shilingi milioni 28,409.07** kwa ajili ya kazi zifuatazo: Ujenzi wa maegesho mapya kumi na nne (14), Ukarabati wa maegesho nane (8), Ujenzi wa miundombinu katika vituo sita (6) vya maegesho, kukamilisha ujenzi wa vivuko sita (6) na kuanza ujenzi wa kivuko kipya kimoja (1), ukarabati wa vivuko 14 pamoja na miradi ya karakana za TEMESA.

338. ***Mheshimiwa Spika,*** mradi wa ***Maegesho ya Vivuko na Miundombinu,*** umetengewa jumla ya **Shilingi milioni 5,222.86** kwa ajili ya ujenzi na ukarabati wa maegesho ya Bugolora - Ukara, Iramba - Majita, Nyakarilo - Kome, Musoma - Kinesi, Kahunda - Maisome, Ijinga – Kahangala, Mayenzi – Kanyinya, Buyagu – Mbalika, Ilunda – Luchelele, na Chato – Muharamba – Kikumbaitale - Zumacheli - Nkome katika kituo cha Chato – Nkome. Vilevile fedha hizi zitatumika kulipa fidia kwa wakazi wa Kigamboni watakaopisha eneo la upanuzi wa maegesho upande wa Kigamboni pamoja na malipo ya Mkandarasi wa

ujenzi wa maegesho ya Kisorya – Rugezi, Bwiro – Bukondo na Bukimwi.

339.***Mheshimiwa Spika,*** kazi nyingine ni ujenzi wa miundombinu ya vivuko: ofisi, majengo ya abiria na uzio kwenye vituo sita (6) vya vivuko ambavyo ni Kisorya – Rugezi, Bugolora - Ukara, na Nyakarilo - Kome.

340.***Mheshimiwa Spika,*** mradi wa ***Ujenzi wa Vivuko Vipya*** umetengewa **Shilingi milioni 9,626.63** kwa ajili ya kukamilisha ujenzi wa vivuko vinne (4) vya Ijinga – Kahangala, Nyakarilo – Kome, Nyamisati – Mafia, Buyagu – Mbalika na kuanza ujenzi wa kivuko kimoja (1) kwa ajili ya kutoa huduma katika maeneo ya Boza – Kuruti, Shungubweni (Ngwevu) na Kisiju Pwani – Kisiwa cha Kwale pamoja na malipo ya Mkandarasi wa Vivuko Viwili vya Kisorya – Rugezi na Bwiro – Bukondo.

341.***Mheshimiwa Spika,*** mradi wa ***Ukarabati wa Vivuko*** umetengewa jumla ya **Shilingi milioni 8,859.58** kwa ajili ya kukamilisha ukarabati wa vivuko 14 ambavyo ni MV Tanga, MV Kome II, MV Nyerere, MV Mafanikio, MV Kitunda, MV Malagalasi, MV Kazi, MV Magogoni, MV Kigamboni, MV Ukara I, MV Ukara II, MV Sabasaba, MV Pangani II pamoja na ukarabati wa MV Kilombero II kabla ya kukihamishia eneo la Mlimba – Malinyi.

342.***Mheshimiwa Spika,*** jumla ya **Shilingi milioni 4,700.00** zimetengwa kwa ajili ya kukamilisha ukarabati wa karakana nane (8) za magari na mitambo zilizopo katika mikoa ya Mwanza, Arusha, Mtwara, Kigoma, Mara, Ruvuma, Dodoma na Mororgoro pamoja na ujenzi wa karakana mpya mbili (2) katika mikoa ya Dodoma na Simiyu. Kazi nyingine ni pamoja na ununuzi wa vifaa wezeshi vya karakana, na kuwezesha utekelezaji wa Mkakati wa Maboresho ya Utendaji Kazi wa TEMESA (TEMESA Transformation Strategy).

**d) Ujenzi na Ukarabati wa Nyumba na Majengo ya Serikali**

343. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2026/27, jumla ya **Shilingi milioni 24,696.14** zimetengwa kwa ajili ya mradi wa Ujenzi na Ukarabati wa Nyumba na Majengo ya Serikali ikiwemo ifuatayo:-

344. ***Mheshimiwa Spika,*** jumla ya **Shilingi milioni 5,255.41** zimetengwa kwa ajili ya Ujenzi wa jengo la makazi kwa ajili ya Watumishi wa Umma katika eneo la Temeke Kota. Aidha, **Shilingi milioni 600.00** zimetengwa kwa ajili ya kuendelea na ujenzi wa jengo la makazi kwa ajili ya Watumishi wa Umma katika eneo la Magomeni Kota Wilaya ya Kinondoni.

345. ***Mheshimiwa Spika,*** jumla ya **Shilingi milioni 3,722.75** zimetengwa kwa ajili ya kuendelea na ujenzi wa Jengo la Makazi kwa ajili ya watumishi wa Umma katika eneo la Kaloleni Kota (Block I) mkoani Arusha. Aidha, kiasi cha **Shilingi milioni 2,032.86** kimetengwa kwa ajili ya ununuzi wa nyumba (Chimala Apartments) za Watumishi wa Umma, jijini Dar es Salaam na **Shilingi milioni 5,013.48** kwa ajili ya ujenzi wa nyumba 110 za Watumishi wa Umma eneo la Nzuguni 'B' jijini Dodoma. Vilevile, **Shilingi milioni 1,811.16** ni kwa ajili ya maandalizi ya ujenzi wa nyumba 144 za gharama nafuu.

346. ***Mheshimiwa Spika,*** jumla ya **Shilingi milioni 1,600.00** zimetengwa kwa ajili ukarabati wa nyumba 40 za watumishi wa umma jijini Dodoma na nyumba 30 za Viongozi Dar es Salaam na nyumba za makazi 644 Magomeni Kota. Kazi nyingine ni ukarabati wa nyumba nyingine 66 zilizokuwa zinamilikiwa na iliyokuwa Mamlaka ya Ustawishaji Makao Makuu Dodoma (CDA) na nyumba zilizo katika mikoa 20 zilizokuwa zinamilikiwa na TAMISEMI zilizohamishiwa TBA. Vilevile, karakana sita (6) za TBA zitakarabatiwa katika mikoa ya Arusha, Mwanza, Dodoma, Tabora, Dar es Salaam na Mbeya.

347. ***Mheshimiwa Spika,*** jumla ya **Shilingi milioni 935.79** zimetengwa kwa ajili ya kazi za kutengeneza na kusimika Mfumo wa Usimamizi wa Vivuko, Mfumo wa usimamizi wa magari na

mitambo ya Serikali na Mfumo wa Usimamizi wa Nyumba na Majengo ya Serikali.

348. ***Mheshimiwa Spika,*** **jumla ya Shilingi milioni 840.00** zimetengwa kwa ajili ya kuwajengea uwezo wahitimu wa fani za Ubunifu Majengo na Ukadiriaji Majenzi. Aidha, **Shilingi milioni 486.56** zimetengwa kwa ajili ya kazi ya kutunga Sheria na Kanuni za Majengo na **Shilingi milioni 430.00** kwa ajili ya kuwajengea uwezo Wakandarasi wa Ndani waliosajiliwa kutekeleza kazi za Majengo na Vivuko.

e) **Miradi ya Ujenzi wa Miundombinu ya Viwanja vya Ndege**

349. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2026/27, miradi ya ujenzi na ukarabati wa miundombinu ya viwanja vya ndege imetengewa jumla ya **Shilingi milioni 119,884.807.** Kati ya fedha hizo, **Shilingi milioni 45,843.350** ni fedha za ndani na **Shilingi milioni 74,041.458** ni fedha za nje. Miradi ifuatayo imepangwa kutekelezwa:

**Ujenzi wa Kiwanja cha Ndege cha Kigoma**

350. ***Mheshimiwa Spika,*** mradi huu umetengewa jumla ya **Shilingi milioni 19,613.79** zinazojumuisha **Shilingi milioni 8,573.34** fedha za ndani na **Shilingi milioni 11,040.45** fedha za nje. Fedha hizi ni kwa ajili ya kuendelea na ujenzi wa jengo la abiria pamoja na miundombinu yake (ukarabati na upanuzi wa maegesho ya ndege, maegesho ya magari na barabara ya kuingia na kutoka kiwanjani). Kazi nyingine ni ujenzi wa uzio wa usalama, jengo la kuongozea ndege na jengo la uchunguzi wa hali ya hewa na usimikaji wa taa na mitambo ya kuongozea ndege

**Ujenzi wa Kiwanja cha Ndege cha Tabora**

351. ***Mheshimiwa Spika,*** mradi huu umetengewa jumla ya **Shilingi milioni 3,401.57.** Kati ya fedha hizo, **Shilingi milioni 2,301.54** ni fedha za ndani na **Shilingi milioni 1,100.03** ni fedha za nje kwa ajili ya malipo ya Mkandarasi na Mshauri Elekezi kwa kazi za ujenzi wa jengo la abiria na miundombinu yake, jengo la kuongozea

ndege, barabara ya kuingia kiwanjani, maegesho ya magari, uzio wa usalama pamoja na jengo la uchunguzi wa hali ya hewa.

**Ujenzi wa Kiwanja cha Ndege cha Songwe**

352. ***Mheshimiwa Spika,*** jumla ya **Shilingi milioni 4,549.11** zimetengwa kwa ajili ya malipo ya Wakandarasi na Washauri Elekezi kwa kazi za ukarabati wa barabara ya kutua na kuruka ndege pamoja na eneo la usalama (Runway End Safety Area-RESA), usimikaji wa taa za usalama na taa za kuongozea ndege na umaliziaji wa jengo la abiria.

**Ukarabati wa Kiwanja cha Ndege cha Mwanza**

353. ***Mheshimiwa Spika,*** jumla ya **Shilingi milioni 4,518.63** zimetengwa kwa ajili ya malipo ya Mkandarasi na Mshauri Elekezi kwa kazi za upanuzi na ukarabati wa barabara ya kuruka na kutua ndege, maungio ya ndege, maegesho ya ndege, jengo la kuongozea ndege, jengo la mizigo pamoja na ujenzi wa mifumo ya maji safi na majitaka.

**Ukarabati wa Kiwanja cha Ndege cha Mtwara**

354. ***Mheshimiwa Spika,*** jumla ya **Shilingi milioni 1,889.20** zimetengwa kwa ajili ya malipo ya Mkandarasi na Mshauri Elekezi kwa kazi za ukarabati wa barabara ya kuruka na kutua ndege, viungio vyake, maegesho ya ndege, kusimika taa za kuongozea ndege, ujenzi wa barabara ya kuingia na kutoka kiwanjani, maegesho ya magari pamoja na uzio wa usalama.

**Ujenzi wa Kiwanja cha Ndege cha Sumbawanga**

355. ***Mheshimiwa Spika,*** jumla ya **Shilingi milioni 3,894.23** zinazojumuisha **Shilingi milioni 2,066.31** fedha za ndani na **Shilingi milioni 1,827.92** fedha za nje kwa ajili ya malipo ya Mkandarasi na Mshauri Elekezi kwa kazi za ujenzi wa barabara ya kutua na kuruka ndege na kiungio chake, maegesho ya ndege, jengo la abiria, jengo la kuongozea ndege, jengo la uchunguzi wa hali ya hewa, barabara ya kuingia kiwanjani na maegesho ya magari.

Kazi nyingine ni usimikaji wa taa na mitambo ya kuongozea ndege na ujenzi wa uzio wa usalama.

**Ujenzi wa Kiwanja cha Ndege cha Shinyanga**

356. ***Mheshimiwa Spika,*** jumla ya **Shilingi milioni 5,805.26** zinazojumuisha **Shilingi milioni 3,031.97** fedha za ndani na **Shilingi milioni 2,773.29** fedha za nje zimetengwa kwa ajili ya utekelezaji wa mradi huu. Kazi zitakazotekelezwa ni kuendelea na ujenzi wa barabara ya kutua na kuruka ndege na kiungio chake, maegesho ya ndege, jengo la abiria, jengo la kuongozea ndege, jengo la uchunguzi wa hali ya hewa, barabara ya kuingia kiwanjani, maegesho ya magari na usimikaji wa taa. Aidha, kazi nyingine ni usimikaji wa mitambo ya kuongozea ndege pamoja na ujenzi wa uzio wa usalama.

**Uendelezaji wa Viwanja vya Ndege vya Mikoa**

357. ***Mheshimiwa Spika,*** mradi huu umetengewa jumla ya **Shilingi milioni 42,076.64** zinazojumuisha **Shilingi milioni 16,355.10** fedha za ndani na **Shilingi milioni 25,721.54** fedha za nje. Fedha hizi zimetengwa kwa ajili ya kuendelea na ujenzi wa viwanja vya ndege vya Iringa (Awamu ya pili), Musoma, Lake Manyara, Tanga pamoja na malipo ya Wakandarasi na Washauri Elekezi wa kazi za uboreshaji wa Kiwanja cha Ndege cha Geita, Iringa (Awamu ya kwanza) na Songea.

**Ujenzi wa Kiwanja cha Ndege cha Kimataifa cha Msalato**

358. ***Mheshimiwa Spika***, mradi huu umetengewa jumla ya **Shilingi milioni 34,081.98** zinazojumuisha **Shilingi milioni 2,503.75** fedha za ndani na **Shilingi milioni 31,578.23** fedha za nje kwa ajili ya kuendelea na ujenzi wa kiwanja kipya cha ndege cha Kimataifa cha Msalato mkoani Dodoma.

**Ujenzi wa Jengo la Tatu la Abiria Katika Kiwanja cha Ndege cha Kimataifa cha Julius Nyerere (JNIA)**

359. ***Mheshimiwa Spika,*** mradi huu umetengewa jumla ya **Shilingi milioni 54.40** kwa ajili ya malipo ya Mkandarasi na Mshauri Elekezi kwa kazi za ujenzi wa jengo la tatu la abiria.

f) **Fedha za Mfuko wa Barabara**

360. ***Mheshimiwa Spika,*** fedha za Mfuko wa Barabara zilizotengwa kwa ajili ya Wizara ya Ujenzi katika mwaka wa fedha 2026/27 ni jumla ya **Shilingi milioni 1,047,405.50** Kati ya fedha hizo, TANROADS imetengewa **Shilingi milioni 926,919.55** kwa ajili ya kazi za matengenezo na ukarabati wa barabara kuu na za mikoa, madaraja na uendeshaji wa mizani na Wizara ya Ujenzi imetengewa **Shilingi milioni 102,991.06** kwa ajili ya kazi za ukarabati wa barabara za mikoa, Upembuzi Yakinifu na Usanifu wa Kina wa barabara, ukarabati na ununuzi wa vivuko, usalama barabarani pamoja na usimamizi na ufuatiliaji wa miradi hiyo. Aidha, **Shilingi milioni 17,494.89** zitatumika kugharamia uendeshaji wa Bodi ya Mfuko wa Barabara.

361. ***Mheshimiwa Spika,*** **Shilingi 102,991,060,605.73** zilizotengwa kwa ajili ya Wizara zimegawanywa kama ifuatavyo: **Shilingi 20,800,000,000.00** ni kwa ajili ya kufanya Upembuzi Yakinifu na Usanifu wa Kina wa barabara zenye urefu wa kilometa **7,601.8** na **Shilingi 62,607,120,000.00** zimetengwa kwa ajili ya miradi ya barabara za mikoa itakayohusisha ukarabati wa jumla ya kilometa **271.59** kwa kiwango cha changarawe, ujenzi wa kilometa **76.51** kwa kiwango cha lami pamoja na ujenzi na ukarabati wa madaraja/ makalavati **22** katika mikoa mbalimbali nchini. Aidha, **Shilingi 6,622,026,826.39** ni kwa ajili ya ununuzi na ukarabati wa vivuko pamoja na ujenzi wa maegesho na miundombinu ya vivuko; **Shilingi 5,438,974,976.85** ni kwa ajili ya miradi ya usalama Barabarani na Mazingira na **Shilingi 7,622,938,802.49** ni kwa ajili ya kazi za usimamizi na ufuatiliaji wa miradi inayotekelezwa na Wizara pamoja na kujenga uwezo wa watumishi. *Mchanganuo wa miradi itakayotekelezwa kwa fedha za Mfuko wa Barabara zilizotengwa kwa ajili ya Wizara ya Ujenzi*

*umeoneshwa katika **Viambatisho Na. 3** na **4.** Mchanganuo wa matumizi ya fedha hizo umeoneshwa katika **Viambatisho Na. 5, 5A - 5D.***

**C.3 MPANGO WA KAZI ZA TAASISI ZILIZO CHINI YA WIZARA YA UJENZI KWA MWAKA WA FEDHA 2026/27**

**Wakala wa Barabara Tanzania (TANROADS)**

362.***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2026/27, Wakala wa Barabara Tanzania umepanga kujenga barabara kuu zenye urefu wa **kilometa 260.5** kwa kiwango cha lami, ukarabati wa **kilometa 87.5** kwa kiwango cha lami, ujenzi wa **madaraja 16,** ukarabati wa **daraja moja (1)** na kuendelea na maandalizi ya ujenzi wa **madaraja 11.** Kazi nyingine ni kufanya Upembuzi Yakinifu na Usanifu wa Kina wa barabara zenye urefu wa **kilometa 7,020.79** na **madaraja matatu (3)** ambayo ni Bujonde (Mbeya), Kilambo (Mtwara) na Sanga (Simiyu).

363.***Mheshimiwa Spika,*** miradi ya barabara za mikoa iliyopangwa kutekelezwa na Wakala ni ujenzi kwa kiwango cha lami wa barabara zenye urefu wa **kilometa 135.51.** Kati ya hizo, **kilometa 59** zitajengwa kwa kutumia fedha za Mfuko Mkuu wa Serikali na **kilometa 76.51** zitajengwa kwa fedha za Mfuko wa Barabara. Vile vile, Wakala umepanga kufanya ukarabati kwa kiwango cha changarawe wa barabara zenye urefu wa **kilometa 693.21**. Kati ya hizo, **kilometa 421.62** zitakarabatiwa kwa kutumia fedha za Mfuko Mkuu wa Serikali na **kilometa 271.59** zitakarabatiwa kwa kutumia fedha za Mfuko wa Barabara. Aidha, Wakala umepanga kujenga na kufanya ukarabati wa madaraja/ makalavati **73,** ambapo kati ya hayo, madaraja/ makalavati **51** yatatumia fedha za Mfuko Mkuu wa Serikali na **22** yatatumia fedha za Mfuko wa Barabara.

364.***Mheshimiwa Spika,*** Wakala pia umepanga kufanya matengenezo ya barabara kuu na barabara za Mikoa ambayo yatahusisha matengenezo ya kawaida (routine and recurrent maintenance) kwa **kilometa 35,356.36** matengenezo ya muda maalum **kilometa 3,390.92,** matengenezo ya sehemu korofi

**kilometa 382.47** pamoja na matengenezo ya madaraja **3,863**. Mpango huu pia unajumuisha shughuli za udhibiti wa uzito wa magari na hifadhi za barabara, kazi za dharura pamoja na mradi wa matengenezo ya barabara kwa mikataba ya muda mrefu.

365. ***Mheshimiwa Spika,*** vilevile, Wakala utaendelea na majukumu ya kusimamia miradi ya ujenzi na ukarabati wa Viwanja vya Ndege vilivyokasimiwa Wizara ya Ujenzi. Miradi iliyopangwa kutekelezwa imeainishwa katika **Aya 354-364.**

Wakala wa Majengo Tanzania (TBA)

366. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2026/27, Wakala wa Majengo Tanzania (TBA) utaendelea kutekeleza majukumu yake kwa kutumia fedha za ruzuku ya Serikali pamoja na mapato ya ndani ya Wakala. Kazi zitakazotekelezwa ni pamoja na kutoa huduma za ushauri kwa miradi ya ujenzi wa majengo ya Serikali, kujenga majengo ya Washitiri mbalimbali, kuuza na kupangisha nyumba zinazojengwa na TBA kwa Watumishi wa Umma na wasio watumishi wa Umma ili kuongeza uwezo wa Wakala kujiendesha.

367. ***Mheshimiwa Spika,*** miradi iliyopangwa kutekelezwa kwa kutumia fedha za ruzuku imeoneshwa katika **Aya 346-353**.

368. ***Mheshimiwa Spika,*** miradi itakayotekelezwa kwa kutumia mapato ya ndani ya Wakala ni:-Ununuzi wa mitambo na mashine kumi; ujenzi wa nyumba 72 za watumishi wa umma Mikoani (Mtwara, Iringa, Rukwa, Songwe, Katavi na Simiyu); ujenzi wa jengo la ghorofa kwa ajili ya watumishi wa umma eneo la Ghana Kota Jijini Mwanza (Block I); ujenzi wa jengo la ghorofa kwa ajili ya watumishi wa umma eneo la Mission Kota mkoani Geita; ujenzi wa maabara ya kupima ubora wa vifaa vya ujenzi Jijini Dodoma; ujenzi wa ofisi za TBA katika mikoa ya Njombe na Geita pamoja na ujenzi wa vyumba 93 vya biashara eneo la Nzuguni Dodoma.

369. ***Mheshimiwa Spika,*** miradi mingine ni:-

Ukarabati wa Majengo mbalimbali mikoani; Ukarabati wa ofisi za mikoa za TBA katika mikoa 12 (Iringa, Kagera, Kigoma, Manyara, Mtwara, Mara, Mbeya, Morogoro, Pwani, Rukwa, Tabora na

Tanga) na ukarabati wa Karakana katika mikoa ya Lindi, Rukwa, Tanga na Ruvuma.

370.***Mheshimiwa Spika,*** Wakala pia umepanga kutekeleza miradi 102 ya Washitiri ambapo miradi 27 ni ya ujenzi na miradi 75 ni ya ushauri. Aidha, kati ya miradi ya ujenzi, miradi 17 ni ya Buni-Jenga ambapo miradi minne (4) inaendelea kutekelezwa na miradi 10 ni ya ujenzi ambapo miradi nane (8) inaendelea. Vilevile, kati ya miradi 75 ya Ushauri iliyopangwa kutekelezwa miradi 51 inaendelea.

**Wakala wa Ufundi na Umeme Tanzania (TEMESA)**

371.***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2026/27, Wakala umepanga kuboresha huduma za usimamizi na uendeshaji wa vivuko vya Serikali, ukodishaji wa mitambo ya ujenzi pamoja na kufanya matengenezo ya magari, usimikaji wa mifumo ya umeme, majokofu, viyoyozi na elektroniki. Aidha, kazi nyingine ni kuendelea na utekelezaji wa Mpango Mkakati wa maboresho ya Utendaji kazi wa TEMESA (TEMESA Transformation Strategy).

372.***Mheshimiwa Spika,*** miradi ya Ruzuku itakayotekelezwa na Wakala katika mwaka wa fedha 2026/27 inahusisha ujenzi wa maegesho katika vituo 17 na miundombinu ya vivuko katika vituo vitatu (3), ukarabati wa Vivuko 14, kumalizia ujenzi wa Vivuko vitano (5) na kuanza ujenzi wa Kivuko kimoja (1) kipya. Aidha, miradi mingine iliyopangwa kutekelezwa na Wakala ni kama inavyoonekana kwenye **Aya 326-331**.

373.***Mheshimiwa Spika,*** Katika uendeshaji wa vivuko vya Serikali, Wakala umepanga kutoa huduma ya kuvusha abiria **20,818,604,** magari **674,220** na tani za mizigo **729** kwa mwaka 2026/ 27. Aidha Wakala umepanga kufanya matengenezo ya magari **43,880**, na usimikaji wa mifumo **55** ya umeme, **312** ya majokofu na viyoyozi na mifumo **17** ya elektroniki. Vilevile, Wakala umepanga kutoa ushauri wa kihandisi kwa miradi ya usimikaji wa mifumo **37** ya umeme na usimikaji wa mifumo **58** ya mitambo, kielektroniki,

viyoyozi na majokofu. Wakala pia utaendelea kutoa huduma ya ukodishaji wa mitambo ya magari na mitambo ya ujenzi.

**Bodi ya Mfuko wa Barabara (RFB)**

374. ***Mheshimiwa Spika,*** Mfuko wa Barabara unatarajia kukusanya jumla ya **Shilingi 1,362,677,278,926.95** kwa ajili ya kugharamia matengenezo ya barabara nchini. Kati ya fedha hizo, **Shilingi 1,047,405,500,383.73** ni kwa ajili ya matengenezo ya barabara za Kitaifa (Barabara Kuu na Barabara za Mikoa) zinazosimamiwa na Wizara ya Ujenzi (Fungu 98). Aidha, **Shilingi 315,271,778,543.22** ni kwa ajili ya kugharamia barabara za Wilaya zinazosimamiwa na Ofisi ya Waziri Mkuu –TAMISEMI (Fungu 56). Mgawanyo wa fedha za Mfuko wa Barabara kwa kila taasisi kwa mwaka wa fedha 2026/27 ni kama ifuatavyo: Wizara ya Ujenzi **Shilingi 102,991,060,605.727**; TANROADS **Shilingi 926,919,545,451.54**; Ofisi ya Waziri Mkuu TAMISEMI **Shilingi 31,000,576,986.97**; TARURA **Shilingi 279,005,192,882.72**; na Bodi ya Mfuko wa Barabara **Shilingi 22,760,903,000.00**.

375. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2026/27 Bodi ya Mfuko wa Barabara itaendelea kufanya tafiti za vyanzo vipya vya mapato ili kuongeza uwezo wa Mfuko kugharamia matengenezo ya Barabara, kufanya ukaguzi wa ubora wa kazi za barabara katika mikoa yote nchini ili kuhakikisha kuwa miradi inayotekelezwa inakidhi thamani ya fedha zilizotumika (*value for money*). Vilevile, Bodi itaimarisha makusanyo yatokanayo na matumizi ya hifadhi za barabara baada ya kukamilisha mapitio ya kanuni zinazosimamia matumizi ya hifadhi za barabara na kuunda mfumo wa kusimamia makusanyo yatokanayo na matumizi hayo.

376. ***Mheshimiwa Spika,*** ili kuimarisha usimamizi wa matengenezo ya Barabara, Bodi itagharamia maboresho ya Mifumo ya Usimamizi wa Rasilimali za Barabara (RAMs) inayotumika kusimamia mtandao wa Barabara za Kitaifa na Wilaya. Hatua hii itawezesha Mifumo ya Wakala wa Barabara na wa Bodi (TRDMS) kusomana na hivyo mipango ya matengenezo na usimamizi wake kufanyika kwa ufanisi. Aidha, ili kupata fedha

za kutosha kugharamia matengenezo maalum ya barabara za kimkakati (*strategic corridors*), Bodi inaendelea kutafuta fedha kutoka katika soko la mitaji na dhamana kupitia Hatifungani. Vilevile, Bodi kwa kushirikiana na wadau mbalimbali itaendelea kufanya utafiti katika maeneo mbalimbali ili kuhamasisha matumizi ya teknolojia ya gharama nafuu ya matengenezo ya barabara.

**Bodi ya Usajili wa Wahandisi (ERB)**

377. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2026/27, Bodi ya Usajili wa Wahandisi (ERB) imeweka malengo ya kusajili wahandisi 3,297, mafundi sanifu 500, Kampuni za Ushauri wa Kihandisi 18, Maabara za vifaa vya ujenzi na uhandisi tano (5), kusimamia mafunzo ya kujiendeleza kitaaluma kwa wahandisi wataalam na wahandisi washauri (CPD), kusimamia utekelezaji wa Mpango wa Mafunzo kwa Vitendo kwa Wahandisi Wahitimu (SEAP) 1,200. Aidha, Bodi itafanya ukaguzi wa miradi 3,500 ya kihandisi nchini ili kuhakikisha kuwa shughuli zote za kihandisi zinafanywa na wahandisi waliosajiliwa na wenye kuzingatia maadili ya utendaji kazi za kihandisi

**Bodi ya Usajili wa Wabunifu Majengo na Wakadiriaji Majenzi (AQRB)**

378.***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka wa fedha 2026/27, Bodi ya Usajili wa Wabunifu Majengo na Wakadiriaji Majenzi imepanga kusajili Wataalam 250 na Wataalam wa Kati 350 katika fani za Ubunifu Majengo, Ukadiriaji Majenzi, Usanifu Teknolojia ya Majengo, Ubunifu wa Mandhari ya Ndani ya Majengo, Ubunifu wa Mandhari ya Nje ya Majengo, Utathmini Majengo, Usimamizi Ujenzi na Usimamizi Miradi.

379.***Mheshimiwa Spika***, Bodi imepanga kusajili kampuni 40 za Ubunifu Majengo na Ukadiriaji Majenzi. Bodi pia imepanga kuwajengea uwezo wahitimu 370 na kuendesha mitihani ya kitaalam kwa wahitimu 350 katika fani za Ubunifu Majengo, Ukadiriaji Majenzi, Ubunifu wa Ndani wa jengo, Ubunifu wa Mandhari ya Nje ya Jengo, Usanifu Teknolojia ya Majengo,

Utathmini Majengo, Usimamizi Ujenzi na Usimamizi Miradi. Mafunzo hayo yatatolewa kupitia mpango maalum wa Mafunzo kwa Vitendo (AQIP). Aidha, Bodi imepanga kufanya ukaguzi wa miradi ya ujenzi 4,900 na kusajili miradi 1,800.

**Bodi ya Usajili wa Wakandarasi (CRB)**

380. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2026/27, Bodi imepanga kusajili jumla ya Wakandarasi wapya 1,600 na kukagua jumla ya miradi ya ujenzi 3,450. Aidha, Bodi imepanga kuendesha kozi za mafunzo ya ushirikiano wa ubia na kuratibu mkutano wa mashauriano wa wadau wa sekta ya ujenzi. Aidha, Bodi itaendelea kuendesha Mfuko Maalum wa Kuwawezesha Wakandarasi (CAF) kwa kutoa dhamana za zabuni na malipo ya awali. Vilevile, Bodi itaendelea na jitihada za kuhamasisha Wakandarasi wa Ndani kujiunga ili kuomba zabuni kwa mfumo wa ubia.

**Baraza la Taifa la Ujenzi (NCC)**

381. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2026/27, Baraza limepanga kutekeleza kazi mbalimbali ikiwemo kuratibu utatuzi wa migogoro inayotokea katika miradi ya ujenzi kwa njia ya *Adjudicationa* na *Arbitration* sambamba na kuwaendeleza watalaam wanaohusika katika utatuzi wa migogoro pamoja na kutunga kanuni mpya za usimamizi wa utatuzi wa migogoro. Aidha, Baraza limepanga kutoa Ushauri wa kitaalam kwa wafyatua matofali ili kufikia viwango vya ubora unaotakiwa katika matofali kwa matumizi mbalimbali ya ujenzi, usimamizi wa miradi na mikataba ya ujenzi pamoja na kupanga gharama za ujenzi kwa taasisi za umma na sekta binafsi.

382. ***Mheshimiwa Spika,*** Vilevile, Baraza litaendelea kuchakata na kuchapisha fahirisi za bei (price indices) za vifaa na nguvukazi katika miradi ya ujenzi kila mwezi pamoja na kuchakata na kuchapisha miongozo ya gharama ya kazi mbalimbali za ujenzi wa barabara na majengo. Aidha, Baraza litaendelea kujenga uwezo wa kitalaam kwa wadau wa sekta ya ujenzi, kutoa mafunzo yapatayo 12 katika maeneo ya usimamizi bora wa

miradi na mikataba ya ujenzi pamoja na kuandaa Miongozo ya Kisheria ya Ujenzi. Kazi nyingine ni kuandaa miongozo ya Mikataba ya Ujenzi wa Majengo inayotumika na waendelezaji wa Sekta Binafsi, pamoja na kuratibu na kusimamia tafiti mbili (2) katika maeneo ya *Local Content* na Usimamizi wa Makampuni ya Ndani yanayojihusisha na Ujenzi.

Kituo cha Usambazaji wa Teknolojia Katika Sekta ya Ujenzi na Usafirishaji Tanzania (Tanzania Transportation Technology Transfer – TanT$^2$ Centre)

383.***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2026/27, Kituo kimepanga kuendelea kusambaza teknolojia katika Sekta ya Ujenzi na Usafirishaji hapa nchini kupitia majarida, semina na mafunzo mbalimbali. Aidha, kituo kitaendelea kushirikiana na Kitengo cha Utafiti na Maendeleo (RDU) cha Wakala wa Barabara Tanzania (TANROADS) kufanya tathmini na ufuatiliaji wa teknolojia mbalimbali mpya na mbadala nje na ndani ya nchi katika ujenzi na matengenezo ya barabara ili kuwezesha Wizara kupata teknolojia stahiki zenye ufanisi na gharama nafuu; Kuandaa, kuchapisha na kusambaza majarida yake yanayoandaliwa kwa ajili ya usambazaji teknolojia kwa wadau na kutafuta maarifa na taarifa mbalimbali muhimu katika Sekta za Ujenzi na Usafirishaji; na Kukamilisha kuboresha Maktaba Mtandao (e-library) kupitia Taasisi ya Teknolojia ya Ujenzi (ICoT) ili kuimarisha huduma za usambazaji wa teknolojia kwa njia ya kidijitali. Vilevile, kituo kitaendelea kupokea na kusambaza majarida kutoka kwa wadau mbalimbali yanayohusu teknolojia, maarifa na taarifa muhimu katika Sekta za Ujenzi na Usafirishaji.

384.***Mheshimiwa Spika,*** kazi nyingine zilizopangwa ni kuandaa na kuendesha mafunzo kwa wadau yanayolenga kutatua changamoto zinazoikabili Sekta za Ujenzi na Usafirishaji; Kuratibu shughuli mbalimbali za uanzishwaji wa Taasisi ya Teknolojia ya Ujenzi (ICoT); Kushiriki katika kuandaa na kufanyika kwa Mkutano wa Vituo vya usambazaji wa Teknolojia Afrika (yaani 10$^{th}$ T$^2$ Centre Conference) utakaofanyika mwezi Oktoba, 2026; na kuendesha makongamano ya Watalaam wa taasisi mbalimbali zinazohusika na miundombinu na usafirishaji ili kujadili na kutafuta

majibu ya changamoto mbalimbali zinazoikabili Sekta za Ujenzi na Usafirishaji. Pia kituo kitashiriki katika kufanya tafiti za matumizi ya teknolojia mpya mbalimbali ndani na nje ya nchi katika ujenzi wa barabara. Vilevile, kituo kitashiriki katika Kamati za Kujenga Uwezo za SADC chini ya Shirikisho la Barabara la Nchi za Kusini mwa Afrika (ASANRA), Shirikisho la Barabara Duniani (PIARC) na Shirikisho la Barabara la Kimataifa (IRF) katika kubadilishana Teknolojia na maarifa mapya.

**Taasisi ya Teknolojia ya Ujenzi (Institute of Construction Technology – ICoT)**

385.***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2026/27 Taasisi ya Teknolojia ya Ujenzi imepanga kutekeleza majukumu yafuatayo: Kudahili wanafunzi wapya wa Stashahada katika ngazi ya cheti yaani 'NTA level 4' wapatao 150; na kutoa mafunzo kwa wanafunzi wa 'NTA Level 4 – 6' katika fani za Uhandisi Ujenzi, Umeme na Mitambo; kudahili wanafunzi wapya 200 wa Elimu ya Mafunzo ya Ufundi Stadi (VET) daraja la kwanza na daraja la tatu; kuendelea kutoa mafunzo kwa wanafunzi wa daraja la kwanza, la pili na la tatu.

386.***Mheshimiwa Spika,*** vilevile, Taasisi ya Teknolojia ya Ujenzi imepanga kuendesha kozi fupi za udereva wa awali na udereva wa magari ya umma kwa awamu 10 na awamu mbili (2) kwa kozi za madereva wa mitambo. Kazi nyingine ni kuendesha mafunzo kwa kozi za Kompyuta, Ufundi magari na Umeme wa majumbani. Aidha, Taasisi itaendelea kusimamia ujenzi wa jengo jipya la Taaluma, kufanya ukarabati na matengenezo katika miundombinu ya Taasisi, kutangaza shughuli za Taasisi kupitia maonesho ya nanenane, semina/ mikutano ya kitaaluma inayoandaliwa na ERB, CRB, AQRB, IET na TARA pamoja na kushiriki katika michezo ya SHIMIWI.

387.***Mheshimiwa Spika,*** Taasisi inatarajia kuhuisha mikataba ya watumishi wa muda na kuwajengea uwezo watumishi pamoja na kuhuisha sheria na kanuni mbalimbali za uendeshaji wa mafunzo ya Astashahada na Stashahada.

## C.4. MASUALA MTAMBUKA

### Uwezeshaji wa Wakandarasi Wazawa katika kazi za Ujenzi

388. ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali inatambua ushiriki usioridhisha wa Wakandarasi wazawa katika miradi mikubwa unaosababishwa na changamoto mbalimbali kama udogo wa mitaji na upungufu wa vifaa na mitambo ya ujenzi. Aidha, Serikali inafanya jitihada mbalimbali kuhakikisha wakandarasi wazawa wanashiriki ipasavyo katika shughuli za ujenzi kama ifuatavyo;-

i. Kutoa mafunzo kwa Wakandarasi kupitia mpango mahsusi wa mafunzo (Sustainable Structured Training Programme – SSTP) unaolenga kukuza ujuzi wa Wakandarasi katika maeneo ya kiufundi na usimamizi wa miradi;
ii. Kuendesha mfuko wa kusaidia wakandarasi (Contractors Assistance fund – CAF) unaolenga kusaidia Wakandarasi wazawa kupata dhamana za benki kwa ajili ya zabuni na malipo ya awali;
iii. Kuwahamasisha Wakandarasi kuunganisha nguvu kupitia ubia (Joint Venture) kwa lengo la kushiriki zabuni na kutekeleza miradi mikubwa pamoja na Wakandarasi hupatiwa mafunzo ya namna bora ya kuunda ushirikiano wa ubia wenye tija katika utekelezaji wa miradi; na
iv. Kuendelea kutenga miradi ya kuwajengea uwezo Wakandarasi na Washauri Elekezi Wazawa kama Sheria ya Ununuzi wa Umma, Sura ya 410 na kanuni zake inavyoelekeza.

389. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kupitia Bodi ya Usajili wa Wahandsi imeweka utaratibu rahisi wa usajili wa Makampuni ya Ushauri wa kihandisi ili kuongeza ushindani wenye usawa kati ya makampuni ya wazawa na yale ya kigeni. Aidha, Bodi imeanzisha utaratibu wa kukusanya na kuchambua taarifa za makampuni ya ushauri kila mwaka kwa lengo la kubaini maeneo yenye mapungufu na kuwezesha utoaji wa mafunzo na kujenga uwezo wa kiushindani.

**Ushirikishwaji wa Makundi Maalum katika miradi ya Ujenzi**

390.***Mheshimiwa Spika***, Wizara imeendelea kutoa fursa za mafunzo kazini (Internship & Graduate field Attachment) kwa kutumia program mbalimbali kama vile program ya "*Structured Engineers Apprenticeship Programme – SEAP*" kwa wahitimu kutoka vyuo mbalimbali nchini kwa lengo la kuimarisha maendeleo ya kitaaluma ya Wahandisi wanawake nchini kupitia uzoefu wa vitendo na kuongeza ushiriki wa Wahandisi wanawake katika utekelezaji wa miradi ya ujenzi. Aidha, Wizara imetenga asilimia 20 ya mikataba ya Matengenezo ya Barabara kwa ajili ya makundi maalumu ambapo makundi haya yameendelea kupatiwa mafunzo maalumu juu ya namna ya kuomba na kujaza zabuni kwa ufanisi, kutoa mafunzo ya matengenezo na ukarabati wa barabara kwa kutumia Teknolojia Stahiki ya nguvu kazi sambamba na kuwasadia kusajili kampuni zao za Ujenzi.

391.**Mheshimiwa Spika,** katika mwaka wa fedha 2026/27 Wizara itaendelea kujikita katika kuendeleza jitihada za kuwajengea uwezo wanawake ili kuongeza ushiriki wao katika sekta ya barabara. Hatua zilizopangwa ni pamoja na kutoa mafunzo kwa wakandarasi wanawake juu ya namna ya kuomba na kujaza zabuni kwa ufanisi, kutoa mafunzo ya matengenezo na ukarabati wa barabara kwa kutumia Teknolojia Stahiki ya Nguvu Kazi sambamba na kuwasaidia kusajili kampuni zao za ujenzi. Aidha, Wizara itatenga miradi maalum ya matengenezo na maendeleo kwa ajili ya wakandarasi wanawake ili kukuza kampuni za wazawa na kuongeza ushindani wao katika zabuni, huku ikifuatilia kwa karibu kazi zinazotekelezwa na wakandarasi wanawake ili kuhakikisha usawa wa fursa na ubora wa kazi.

392.**Mheshimiwa Spika,** sambamba na hatua hizo, Wizara kupitia kitengo cha Wanawake imepanga kutembelea vyuo vya elimu ya juu ili kuhamasisha wanawake kujiunga na fani za uhandisi, kuendeleza kampeni za kuhamasisha wasichana wa sekondari kusoma masomo ya sayansi na hisabati, na kuendelea kutoa elimu kwa umma kuhusu umuhimu wa ushirikishwaji wa wanawake katika masuala ya barabara. Vilevile, Wizara itahakikisha inakamilisha maboresho ya muongozo wa

ushirikishwaji wa wanawake katika sekta ya ujenzi ili wadau wote wapate mwongozo thabiti wa namna bora ya kuwashirikisha wanawake katika tasnia. Hatua hizo zinalenga kuimarisha usawa wa kijinsia, kuongeza idadi ya wanawake wanaojihusisha na shughuli za ujenzi na kujenga msingi thabiti wa ushiriki wao katika maendeleo ya miundombinu.

393.***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kupitia TEMESA imeendelea kutoa ajira za mikataba kwa vijana katika fani mbalimbali ambapo Wakala umeajiri wahitimu vijana 115 kwa Mkataba. Vilevile imeajiri mafundi 13 kwa Mkatababa maalum kwa lengo la kuwajengea uwezo na uzoefu katika kuendeleza fani ya ufundi katika karakana za Wakala na watumishi 70 ajira za kudumu.

394.***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kupitia TBA itaendelea na ujenzi wa nyumba za watumishi za gharama nafuu ambapo kipaumbele kitakuwa ni kwa ajili ya vijana walioajiriwa pamoja na vijana walioanza ajira hivi karibuni. Aidha, Wizara inaendelea kukamilisha ujenzi wa nyumba za gharama nafuu 144 eneo la TEMEKE Jijini Dar es Salaam ili kuweza kutatua changamoto ambazo vijana wanazipitia kwenye kupata nyumba za gharama nafuu za kuishi. Vilevile, Wizara imetenga fedha kiasi cha **Shilingi 1,811.164.00** kwa ajili ya kuanza ujenzi wa nyumba za bei nafuu Jijini Dodoma. Hata hivyo, bajeti hii itazalisha ajira takribani **815** kwa vijana na wanawake (Mama na Baba lishe) pamoja na kuzingatia miundombinu kwa watu wenye ulemavu.
Ushirikishwaji wa Sekta Binafsi katika miradi ya Ujenzi

395.***Mheshimiwa Spika,*** Wizara inaendelea kushirikisha wadau mbalimabli kutoka Sekta Binafsi ikijumuisha kampuni za Kitanzania na za kigeni ili kuwezesha miradi ya ujenzi inatekelezwa kwa ubia kati ya Serikali na Sekta Binafsi. Hadi kufikia Aprili, 2026 Wizara imekamilisha taarifa ya Upembuzi Yakinifu wa miradi miwili (2) ya barabara za mwendokasi za Kibaha – Chalinze (km 78.9) na Chalinze – Morogoro (km 84.9) kwa utaratibu wa PPP. Aidha, manunuzi ya kumpata mbia barabara ya Kibaha – Chalinze (km 78.9) yanaendelea na inarajiwa mkataba utasainiwa mwaka wa fedha 2026/27. Vilevile, taarifa ya Upembuzi Yakinifu na Usanifu wa kina wa barabara ya HandeniKiberashi-Singida (km 384)

imeshakamilika na tayari imewasilishwa TPA kwa ajili ya hatua za kutafuta Mbia atakaetekeleza mradi huu kwa PPP. Pia Wizara ipo katika hatua ya Upembuzi Yakinifu na Usanifu wa Kina wa Barabara ya Igawa-Songwe-Tunduma (km 218) na Uyole - Songwe Bypass (km 48.9) na barabara ya Mzunguko wa Kati (km 50.9) (Inner Ring Road) na Mzunguko wa Nje (km 77.5) (Outer Ring Road) Dar es Salaam kwa utaratibu wa PPP.

396.***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kupitia TBA ipo katika hatua za mwisho za kusaini mkataba kwa njia ya ubia (PPP) katika eneo la Temeke Kota kwa kushirikiana na sekta binafsi, ambapo kwa sasa Wakala unasubiri uhakiki wa mwisho (Vetting) kutoka kwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali kabla ya mkataba kusainiwa. Aidha, mradi wa uendelezaji wa eneo la Mpemba mkoani Songwe upo katika hatua ya upembuzi yakinifu (feasibility study) ukiratibiwa na Kituo cha Ubia baina ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi (PPPC). Aidha, Wakala tayari umeainisha maeneo yake oevu 149 katika mikoa yote Tanzania Bara kwa ajili ya kuyaendeleza kwa njia ya ubia (PPP). Utekelezaji wa miradi hiyo utachangia kupunguza changamoto za makazi kwa Watumishi wa Umma na kuiwezesha TBA kupata mapato yatakayopelekea TBA kujiendesha na kupunguza utegemezi wa ruzuku kutoka Serikalini katika utekelezaji wa miradi.

397.***Mheshimiwa Spika,*** Vilevile, Wizara imefanya maboresho ya karakana za kutengeneza magari pamoja na kuweka vifaa vya kisasa ili kuendana na mabadiliko ya teknolojia yanayobadilika kwa kasi. Uboreshaji unalenga kuvutia ushirikishwaji wa sekta binafsi kwa ufanisi. Aidha, katika kituo cha kivuko cha Magogoni-Kigamboni unaendelea kukodisha eneo kwa Azam Marine ili kuendelea na utoaji huduma kwa wananchi wakati ukisubiri mchakato wa taratibu za PPP kukamilika. Wizara pia inaendelea na taratibu za kupata wabia wa matengenezo ya magari kwa utaratibu wa PPP ili kutoa huduma za kwa ufanisi zaidi.

**Maboresho ya Sera, Miongozo, Sheria na Kanuni**

398.***Mheshimiwa Spika,*** Wizara itaendelea na mapitio na uhuishaji wa sera, miongozo, sheria na kanuni ili ziendane na

mabadiliko ya teknolojia na maendeleo endelevu. Maboresho yanajumuisha Mwongozo wa usanifu (Pavement and Materials Design Manual 1999) na Mwongozo wa Viwango Msawazo vya Ujenzi wa Barabara (Standard Specifications for Road Works 2000), ili pamoja na mambo mengine kuweka mwongozo wa namna ya kukabiliana na mabadiliko ya tabia ya nchi na ukuaji wa teknolojia duniani. Aidha, Wizara inaendelea kufanya maboresho ya sheria na kanuni zikiwemo Sheria ya NCC na Sheria CRB.

399.***Mheshimiwa Spika,*** maboresho ya Sheria ya NCC yanalenga kulipatia Baraza mamlaka ya udhibiti na usimamizi wa sekta ya ujenzi hususan usimamizi na udhibiti wa Sekta ndogo ya Majengo. Matokeo chanya yanayotarajiwa ni kuimarisha udhibiti wa ubora wa kazi za majenzi nchini, kusimamiwa kwa sekta ya majengo nchini. Aidha, maboresho ya Sheria ya CRB yanakusudia kuleta unafuu zaidi kwa wakandarasi au kampuni za wazawa.

**Matumizi ya Teknolojia Mpya katika Ujenzi na Matengenezo ya Barabara**

400. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara itaendelea na matumizi ya teknolojia mbalimbali katika ujenzi na matengenezo ya barabara ambazo zinafanya zidumu kwa muda mrefu. Lengo ni kukabiliana na changamoto za upatikanaji wa materials hasa changarawe zenye ubora unaotakiwa. Teknolojia zinazotumika kwa sasa ni geo-polymer (sementi mbadala), ecoroads (chemical stabilizers) na armaseal (lami).

**Mapambano dhidi ya VVU na Magonjwa Yasiyoambukiza**

401. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara itaendelea kutoa elimu kuhusu kujikinga na maambukizi ya VVU na magonjwa yasiyoambukiza kwa watumishi wa Wizara. Aidha, Wizara itaendelea kuwahudumia watumishi waliotoa taarifa ya kuathirika na virusi vya UKIMWI kwa kuwapatia posho ya chakula ili waweze kupata lishe bora kwa lengo la kupunguza makali ya virusi hivyo.

**Mapambano dhidi ya Rushwa**

402. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2026/27, Wizara itaendelea kutekeleza mikakati mbalimbali katika mapambano dhidi ya Rushwa kwa lengo la kukuza uwajibikaji, uwazi na uadilifu katika matumizi ya rasilimali za umma. Aidha, mafunzo yanayohusu maadili na kuzuia vitendo vya rushwa yataendelea kutolewa kupitia semina na mabaraza ya wafanyakazi.

**Rasilimali Watu na maendeleo ya Watumishi**

403. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2026/ 27,
Wizara itaendelea kuzingatia taratibu za Utumishi wa Umma na kuwajali wastaafu kwa kuwagharamia mafunzo ya muda mfupi ya kujiandaa na maisha baada ya kustaafu kazi wakati mafao yao yakiwa yanaendelea kuandaliwa na mfuko wa Hifadhi ya Jamii kwa Watumishi wa Umma PSSF. Aidha, Wizara itaendelea kuwaendeleza Watumishi kitaaluma kwa kuwapeleka katika mafunzo ya muda mrefu na muda mfupi.

**C.SHUKRANI**

404.***Mheshimiwa Spika,*** ninapohitimisha hotuba yangu, napenda kwa dhati kabisa kuwashukuru viongozi wenzangu wa Wizara ambao ni Mheshimiwa Mhandisi **Godfrey Msongwe Kasekenya (Mb.),** Naibu Waziri, Balozi Mhandisi **Aisha Salim Amour,** Katibu Mkuu pamoja na Dkt. **Charles Enock Msonde,** Naibu Katibu Mkuu kwa ushirikiano wanaonipa katika kutekeleza majukumu yangu. Aidha, naishukuru Menejimenti ya Wizara, Wakuu wa Taasisi zilizo chini ya Wizara na Watumishi wote wa Wizara na Taasisi kwa kujituma na kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi na kujitolea lengo likiwa ni kuifanya Sekta ya Ujenzi izidi kuimarika na kutoa mchango mkubwa katika maendeleo ya nchi yetu.

405.***Mheshimiwa Spika,*** kipekee kabisa nitumie nafasi hii adhimu kuwashukuru wananchi wa Jimbo langu la Mkuranga kwa kunikubali, kuniamini na kunichagua kwa mara nyingine tena ili kuwawakilisha katika Bunge hili Tukufu kwa kipindi kingine cha

miaka mitano. Maneno ninayoweza kuwaambia ni machache tu - *Sitawaangusha*.

406.***Mheshimiwa Spika,*** naishukuru pia familia yangu, mke na watoto wangu kwa kuendelea kuniombea na kunifariji katika utendaji wa majukumu yangu. Ahsanteni sana, na Mwenyezi Mungu awabariki.

407.***Mheshimiwa Spika,*** Wizara inapata ushirikiano mkubwa kutoka kwa wadau mbalimbali wa maendeleo wa ndani na wa nje. Nitumie fursa hii kuwatambua na kuwashukuru wafuatao: Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB), Benki ya Dunia (WB), Shirika la Kimataifa la Maendeleo la Japan (JICA), OPEC Fund, Korea Kusini (KOICA), Abu Dhabi Fund, Shirika la Maendeleo la Ufaransa (AFD), Jumuiya ya Nchi za Ulaya (EU), Benki ya Uwekezaji ya Ulaya (EIB), Kuwait Fund, Barrick, Sekretarieti ya Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC), Sekretarieti ya Jumuiya ya Nchi za Kusini mwa Afrika (SADC), Japan, China, Norway, NSSF, Taasisi za fedha za CRDB, NMB, NBC na TCB na Asasi mbalimbali zisizokuwa za Serikali; Sekta Binafsi; wanahabari pamoja na wadau wengine wengi.

**E. HITIMISHO**

408.***Mheshimiwa Spika,*** kwa kutambua umuhimu wa miundombinu ya usafirishaji katika kuchochea na kuharakisha maendeleo ya kiuchumi na kijamii kwa Taifa letu, katika mwaka 2026/27 Wizara ya Ujenzi itaendelea kuchukua hatua madhubuti za kusimamia, kuimarisha na kuendeleza Sekta ya Ujenzi. Lengo ni kuhakikisha sekta hii inatoa mchango wa kutosha katika maendeleo ya Taifa na ustawi wa wananchi wake kama inavyotarajiwa.

409.***Mheshimiwa Spika,*** Wizara itaweka mkazo mkubwa katika kupunguza changamoto ya msongamano wa magari katika miji na majiji, hususan kwa kujenga barabara za mchepuo, madaraja ya juu pamoja na upanuzi wa barabara zilizopo ili kukidhi mahitaji yanayotokana na ongezeko la watumiaji wa barabara hizo. Aidha, Wizara itaendelea kuchukua hatua za haraka kurejesha

na kujenga upya miundombinu iliyoharibiwa na mafuriko pamoja na athari nyingine za mabadiliko ya tabianchi. Barabara na madaraja yaliyoathirika yatajengwa kwa viwango vinavyoweza kuhimili majanga hayo, ili kuepuka kuongeza mzigo kwa Serikali kugharamia uharibifu unaojitokeza kila msimu wa mvua kubwa na kuhakikisha barabara zetu zinapitika majira yote ya mwaka hata wakati wa changamoto za hali ya hewa.

410. ***Mheshimiwa Spika***, katika hatua nyingine, Wizara inaendelea na maandalizi ya Mpango Kabambe wa Usafiri wa Haraka (Tanzania Expressway Master Plan) katika barabara kuu. Mpango huu unatekelezwa kwa kushirikiana na Shirika la Ushirikiano wa Kimataifa la Korea (KOICA). Lengo ni kuwa na ramani na mwongozo wa kimkakati wa maendeleo ya barabara za haraka nchini. Sambamba na hatua hizo, Serikali inaendelea na utekelezaji wa miradi ya Expressway inayohusisha mradi wa Kibaha – Chalinze – Morogoro (km 163.8), ambao uko katika hatua za ununuzi wa kumpata mwekezaji kwa utaratibu wa PPP. Aidha, taratibu za maandalizi ya kuanza kazi ya upembuzi yakinifu wa awali zinaendelea kwa miradi ya *Expressway* katika barabara ya Nyerere (DSM CBD – Airport - km 12.49), barabara ya Mandela na Sam Nujoma (Mfugale Flyover (TAZARA)) – Ubungo – Mwenge; (km 11.52) na KIA – Arusha (km 45).

411. ***Mheshimiwa Spika***, jitihada zitaelekezwa katika kuimarisha ubora wa miradi ya ujenzi kwa kusimamia viwango na kutumia teknolojia za kisasa ili miundombinu inayojengwa iwe imara, salama na yenye kudumu kwa muda mrefu Wizara pia itaendelea kuimarisha utoaji wa huduma kupitia taasisi zake kwa kuhakikisha zinatoa huduma kwa weledi, uwazi na kwa kuzingatia mahitaji halisi ya wananchi. Aidha, Taasisi zitaendelea kuhimizwa kubuni vyanzo vipya vya mapato sambamba na kuongeza ushiriki wa Sekta Binafsi katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo inayosimamiwa na taasisi hizo.

412. ***Mheshimiwa Spika***, katika kuhakikisha ubora wa miundombinu na kuwezesha miradi kukamilika kwa wakati, Wizara itaendelea kuchukua hatua stahiki kwa Wakandarasi na Washauri Elekezi wanaokiuka masharti ya kimkataba. Hadi sasa,

Wizara imechukua hatua madhubuti kwa wakandarasi wa miradi kadhaa wakiwemo wa barabara ya Ibanda – Kajunjumele, Sengerema – Nyehunge ambao mikataba yao ilisitishwa. Aidha, Wakandarasi na miradi ya mabasi yaendayo haraka (BRT) awamu ya nne (4) na barabara ya Tungamaa – Mkange wamepewa onyo kutokana na kutokutimiza masharti ya mkataba. Sambamba na hatua hizo, ninazielekeza Taasisi zilizo chini ya Wizara ya Ujenzi kusimamia miradi kwa ufanisi ili kuhakikisha thamani ya fedha inapatikana kwenye miradi.

## F. MUHTASARI WA MAOMBI YA FEDHA YA WIZARA YA UJENZI KATIKA MWAKA WA FEDHA 2026/27

413.***Mheshimiwa Spika,*** kwa mwaka wa fedha 2026/27, Wizara ya Ujenzi inaliomba Bunge lako Tukufu liidhinishe jumla ya **Shilingi, 2,564,441,414,000.00** kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo. Kati ya fedha hizo, **Shilingi 97,104,935,000.00** ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida ya Wizara na Taasisi na **Shilingi 2,467,336,479,000.00** kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo. Kati ya fedha za Matumizi ya Kawaida, **Shilingi 92,209,218,000.00** ni za Mishahara ya Watumishi na **Shilingi 4,895,717,000.00** ni za Matumizi Mengineyo. Bajeti ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo inajumuisha fedha za ndani **Shilingi 1,544,872,147,000.00** na fedha za nje ni **Shilingi 922,464,332,000.00.** Fedha za ndani zinajumuisha **Shilingi 1,047,405,500,000.00** kutoka Mfuko wa Barabara na **Shilingi 497,466,647,000.00** ni fedha kutoka Mfuko Mkuu wa Serikali.

414.***Mheshimiwa Spika***, pamoja na Hotuba hii, nimeambatisha mchanganuo wa miradi itakayotekelezwa na Wizara katika mwaka wa fedha 2026/27 **(Kiambatisho Na. 1 – 5)**. Naomba viambatisho hivyo vichukuliwe kama sehemu ya vielelezo vya hoja yangu.

415.***Mheshimiwa Spika,*** naomba nitoe tena shukrani zangu za dhati kwako na kwa Waheshimiwa Wabunge wote kwa kunisikiliza. Hotuba hii inapatikana pia katika tovuti ya Wizara (**www.mow.go.tz**).

416. ***Mheshimiwa Spika,*** naomba kutoa hoja.

**WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaafiki.

*Hoja ilitolewa iamuliwe*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana, hoja imetolewa na kuungwa mkono. Ahsante sana Mheshimiwa Alhaji Abdallah Hamis Ulega. Nimwite sasa Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu, Mheshimiwa Selemani Kakoso.

**MHE. MOSHI S. KAKOSO - MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA MIUNDOMBINU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ifuatayo ni taarifa ya Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu kuhusu Utekelezaji wa Majukumu ya Fungu Na. 98, Wizara ya Ujenzi kwa mwaka wa fedha 2025/2026 pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa mwaka wa fedha 2026/2027.

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote ninaomba taarifa yote ya Kamati iingie katika Taarifa Rasmi za Bunge kama ilivyowekwa Mezani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Kanuni ya 121(9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge 2025 ninaomba kuwasilisha taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu kuhusu Utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya Ujenzi Fungu 98 kwa mwaka wa fedha 2025/2026 pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa mwaka wa fedha 2026/2027.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bila kuathiri masharti yanayopatikana katika Kanuni ya 145 Kanuni za Bunge, taarifa hii imegawanyika katika sehemu zifuatazo: Sehemu ya kwanza ni utangulizi ambao unaeleza kuhusu muundo wa taarifa pamoja na namna Kamati ilivyotekeleza majukumu yake. Sehemu ya pili inahusu uchambuzi na utekelezaji wa bajeti kwa mwaka wa fedha 2025/2026 kwa kutathmini uzingatiaji na ushauri wa maoni

ya Kamati, makusanyo ya maduhuli, mwenendo na upatikanaji wa fedha, na utekelezaji wa miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sehemu ya tatu inahusu uchambuzi wa Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka wa fedha 2026/2027, na sehemu ya nne ni majumuisho ya Maoni na Ushauri wa Kamati na mwisho ni hitimisho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu utekelezaji wa maoni na ushauri wa Kamati. Ninapenda kulijulisha Bunge lako Tukufu kwamba kwa sehemu kubwa ya Serikali imeyafanyia kazi maoni ya Kamati na ushauri uliotolewa na Kamati wakati wa kujadili Bajeti kwa mwaka wa fedha 2025/2026. Hata hivyo, katika baadhi ya maeneo ushauri uliotolewa haukufanyiwa kazi kwa ukamilifu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfano ni ushauri wa Kamati kuhusu Serikali kufanya malipo ya fidia kwa wananchi ambao wamepisha miradi katika sekta ya ujenzi. Serikali imetekeleza ushauri kwa kulipa shilingi bilioni 30.6 sawa na 25.41% tu ya shilingi bilioni 120.94 zinazodaiwa na wananchi kwa kuwalipa fidia. Hali hii inaweza kusababisha malalamiko na kudumaza hali ya kiuchumi kwa sababu wananchi hao hawawezi kutumia ardhi hiyo katika shughuli za uzalishaji mali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2025/2026 Wizara ya Ujenzi ilipangiwa kukusanya maduhuli ya jumla ya shilingi milioni 80 ambapo hadi kufikia Machi, 2025 Wizara ilikuwa imekusanya jumla ya shilingi milioni 78.23 sawa na 97.80% ya lengo. Kamati inaipongeza Wizara kwa makusanyo hayo na kuitaka kubuni vyanzo vipya vya mapato kwa ajili ya kuhudumia sekta ya ujenzi nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mwenendo na upatikanaji wa fedha. Katika mwaka wa fedha 2025/2026 Wizara ya Ujenzi iliidhinishiwa kutumia jumla ya shilingi trilioni 1.903 kwa ajili ya matumizi ya kawaida na utekelezaji wa miradi ya maendeleo. Hadi kufikia Machi, 2025 Wizara ilikuwa imepokea shilingi trilioni 1.378 sawa na 72.38% ya bajeti. Taarifa zaidi kuhusu mwenendo wa matumizi inapatikana katika ukurasa wa 5 - 8 wa taarifa hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ukaguzi na utekelezaji wa miradi ya maendeleo. Kwa mujibu wa Kanuni ya 120(2) ya Kanuni ya Kudumu za Bunge, Kamati ilifanya ukaguzi wa miradi ya maendeleo iliyotengewa fedha katika mwaka wa fedha 2025/2026 kwenye mikoa ya Morogoro, Tanga na Dar es Salaam kati ya tarehe 12 na tarehe 19 Machi, 2026. Taarifa zaidi kuhusu miradi hiyo inapatikana katika ukurasa wa 8 - 19 wa taarifa hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, masuala mahususi yaliyobainika. Katika mwaka wa fedha 2025/2026 Bodi ya Mfuko wa Barabara iliidhinishiwa bajeti ya shilingi bilioni 945.80 kwa ajili ya matengenezo na ukarabati wa barabara nchini. Hata hivyo, Kamati ilibaini kwamba hadi kufikia tarehe 24 Machi, 2026 kiasi cha shilingi bilioni 418.88 pekee sawa na 44% tu ya bajeti ya Mfuko wa Barabara ndicho kilichokuwa kimehamishwa katika akaunti kupelekwa akaunti za Mfuko wa Barabara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inalikumbusha Bunge lako Tukufu kuwa fedha za Mfuko wa Barabara ni fedha zinazolindwa kwa mujibu wa sheria. Kwa hiyo, Serikali kushindwa kuhamisha fedha hizo katika akaunti ya Mfuko wa Barabara kwa wakati inachelewesha matengenezo na ukarabati wa barabara nchini ambazo zimeathirika na hali ya mvua nyingi. Aidha, hali hii pia imekuwa ikiripotiwa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali *(CAG)* mara kwa mara bila Serikali kuchukua hatua ya kuirekebisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile, Kamati imebaini kuwa Serikali ina mpango wa kuchukua asilimia tano ya fedha za Mfuko wa Barabara kwa ajili ya kugharamia miradi mingine ya maendeleo. Pamoja na nia njema ya Serikali, Kamati haikubaliani na uamuzi huo na inaliomba Bunge lako Tukufu kuiunga mkono kwa ajili ya kunusuru sekta ya barabara hapa nchini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii inatokana na ukweli kuwa mahitaji ya fedha katika kufanya matengenezo na kukarabati barabara na kujenga madaraja nchini ni makubwa kuliko kiasi cha fedha kinachopatikana. Kwa hiyo, uamuzi huo utapunguza

ufanisi na tija katika kukabiliana na ubovu pamoja na uchakavu wa miundombinu ya barabara na madaraja hapa nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu hali ya miundombinu ya barabara na madaraja nchini, taarifa ya *TANROADS* ya tarehe 30 Machi, 2026 inaonyesha kuwa ni 30% tu ya barabara za Kitaifa ndiyo iko katika hali nzuri wakati 70% zikiwa katika hali ya wastani au mbaya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile, taarifa ya Wizara ya tarehe 24 Machi, 2026 iliyowasilishwa katika Kamati, inaonesha kuwa 39.4% ya mtandao wa barabara zote za lami zinazosimamiwa na *TANROADS* zimefikia mwisho wa uhai wake na kupelekea uchakavu. Aidha, kwa misimu ya hivi karibuni, nchi yetu imepokea mvua nyingi za juu ya wastani ambazo zimechangia uharibifu wa miundombinu ya barabara na madaraja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara nyingi zilizoathirika ni zile zinazopita katika shoroba za kiuchumi huku zikiunganisha mikoa kwa mikoa na nyingine zikiunganisha wilaya kwa wilaya na nyingine zikiunganisha nchi yetu na nchi jirani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baadhi ya barabara hizo ni pamoja na barabara ya Dar es Salaam – Mkuranga – Kibiti – Lindi; Barabara ya Igawa – Tunduma; Barabara ya Ifakara – Mlimba – Njombe; Barabara ya Ifakara – Malinyi – Namtumbo; Barabara ya Morogoro – Dodoma; Barabara ya Dodoma – Iringa; Barabara ya Singida – Igunga – Nzega – Mwanza na Barabara ya Babati – Singida. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hali hii imesababisha baadhi ya maeneo kushindwa kufikika kwa urahisi na kuzua malalamiko miongoni mwa wananchi na wawakilishi wao katika maeneo hayo. Ili kuboresha miundombinu hiyo, Serikali inahitaji kuwekeza kiwango kikubwa cha fedha ambapo kupitia uratibu wa bajeti ya Serikali pekee changamoto hii haitaweza kutatuliwa kwa wakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu hali ya miradi ya zamani ya barabara, miradi viporo. Ibara ya 40 ya Ilani ya Uchaguzi wa

Chama cha Mapinduzi ya Mwaka 2025/2030 inaeleza kuhusu Serikali kukamilisha kwa kiwango cha lami ujenzi wa barabara na kukarabati zinazounganishwa na makao makuu ya mikoa yote hapa nchini na zile zinazounganisha Tanzania na nchi jirani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uamuzi wa kujenga baadhi ya barabara hizo ulifanywa na Serikali kwa sababu ya umuhimu wake katika uchumi wa nchi yetu. Mathalani, baadhi ya barabara hizo na sababu ya Serikali kuamua kuzijenga ni kama ifuatavyo: Magole – Mziha – Handeni; lengo lake ni kupitisha malori ya mizigo kutoka Bandari ya Tanga kwa ajili ya kupunguza foleni ya malori yanayotoka Bandari ya Dar es Salaam kupitia Chalinze. Barabara ya Nzega – Itobo – Bukene, lengo lake ni kuunganisha Wilaya ya Nzega na Igunga kuelekea katika Mradi wa Reli ya Kisasa *SGR* eneo la Isaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Barabara ya Nsimbo – Kalia - pamoja na Daraja la Mto Maragarasi, lengo lake ni kuunganisha nchi yetu ya Tanzania kupitia Mkoa wa Kigoma na nchi jirani ya Burundi, hivyo kurahisisha biashara baina ya maeneo hayo. Barabara ya Tarime – Serengeti – Mugumu, lengo lake ni kurahisisha usafiri wa watalii wanaotoka katika Hifadhi ya Maasai Mara nchini Kenya kuja katika Hifadhi ya Taifa ya Serengeti nchini Tanzania kupitia katika mpaka wa Sirari. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, tathmini ya Kamati inaonesha kuwa miradi mingi ya zamani ambayo ni viporo haijatengewa fedha za kutosha kwa ajili ya kuendeleza ujenzi wake. Aidha, katika miradi hiyo, fedha zilizotengwa zimeelekezwa katika kulipa madeni ya nyuma ya wakandarasi na siyo katika kuendeleza shughuli za ujenzi kukamilisha miradi hiyo husika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara ya Ujenzi inakabiliwa na changamoto ya madeni makubwa ya wakandarasi na wahandisi washauri. Madeni haya kwa kiasi kikubwa yanatokana na utekelezaji wa miradi ya barabara iliyofanyika kwa zaidi ya miaka 10.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hali hii imechangia kuathiri moja kwa moja ufanisi katika utekelezaji wa bajeti ya Wizara na mathalani katika utekelezaji wa bajeti ya mwaka wa fedha 2025/2026. Hadi kufikia Machi, 2026, Wizara ilikuwa imepokea jumla ya shilingi trilioni 1.32 sawa na 72.80% ya fedha yote ya maendeleo. Kama fedha hizi zingeelekezwa katika vipaumbele na mpango wa bajeti kama ilivyoidhinishwa na Bunge, zingeweza kuleta tija iliyokusudiwa katika sekta ya barabara nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, uchambuzi wa Kamati umebaini kuwa sehemu kubwa ya fedha hizi zilielekezwa katika malipo ya madeni, hivyo kuathiri matokeo ya utekelezaji wa bajeti ya Wizara kwa ujumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ilitoa ahadi ya kulipa jumla ya shilingi bilioni 800 kwa madeni yaliyohakikiwa ya wakandarasi na wazabuni kupitia Wizara ya Fedha, Fungu Namba 21 ili kupunguza tatizo hilo. Kamati ina maoni ya kuwa juhudi hizi zinaweza zisilete matokeo yanayotarajiwa kwa sababu madeni hayo ni ya Wizara mbalimbali na siyo ya Wizara ya Ujenzi peke yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, muundo wa taasisi za *TANROADS*, *TBA* na *TEMESA*. Katika kupitia utekelezaji wa majukumu ya taasisi hizo, Kamati ilibaini kuwa sheria zinazounda taasisi zimepitwa na wakati. Aidha, taasisi zimekuwa na mchango mkubwa katika sekta ya ujenzi wa barabara, nyumba na ufundi nchini. Hata hivyo, taasisi hizi zinakabiliwa na changamoto ya kuingiliwa kiutendaji na kukosa uhuru wa kutekeleza majukumu yake yote kwa ufanisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kupitia sheria ya uanzishwaji wa wakala, taasisi hizi zimekosa bodi madhubuti ya usimamizi, kwani zinasimamiwa na bodi za ushauri. Aidha, changamoto ya muundo wa taasisi hizi, inachangia bodi ya ushauri kukosa mamlaka ya kisheria katika kuwasimamia na kuwajibisha watendaji wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati imefanya uchambuzi wa kina wa hali ya vivuko na kubaini kuwa vivuko vingi nchini ni vya muda mrefu, hivyo kukabiliwa na hali ya uchakavu na ubovu wa mitambo. Hali hii imesababisha kuwa na huduma duni za usafiri wa wananchi wanaotegemea kutumia vivuko hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kukabiliana na hali hiyo Serikali imechukua hatua ya ununuzi na ukarabati wa vivuko katika maeneo mbalimbali nchini. Hata hivyo, Kamati imebaini kuwa utekelezaji wa hatua hiyo umekuwa ukichukua muda mrefu kiasi cha kuwakatisha tamaa wananchi wanaotegemea huduma kupitia vivuko hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2025/2026 Serikali imefanikiwa kukamilisha ujenzi wa kivuko kimoja tu pekee cha Kisorya – Rugezi kati ya vivuko vitano ambavyo vilitakiwa kununuliwa. Aidha, katika vivuko saba vilivyokuwa vinakarabatiwa, hakuna hata kimoja kilichokamilika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uchambuzi wa mpango wa makadirio na mapato ya matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027. Katika mwaka wa fedha 2026/2027, Wizara imepanga kukusanya jumla ya shilingi 87,001,000 sawa na ongezeko la asilimia mbili nukta tatu tano ikilinganishwa na mwaka wa fedha 2025/2026. Kamati inaitaka Wizara iweke mikakati na kuongeza vyanzo vya mapato kwa ajili ya kuendeleza sekta ya ujenzi nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, makadirio ya matumizi. Katika mwaka wa fedha 2026/2027, Wizara ya Ujenzi (Fungu Namba 98) inaomba kuidhinishiwa jumla ya shilingi 2,564,000,000,000 sawa na ongezeko la 34.71% ukilinganisha na bajeti ya mwaka wa fedha 2025/2026.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa fedha za kugharamia matengenezo na ukarabati wa barabara kupitia fedha za Mfuko wa Barabara, zimeongezeka kwa 52.14%. Hata hivyo, Kamati imebaini kuwa mara nyingi mwenendo wa upatikanaji wa fedha hizo siyo wa kuridhisha. Kwa mfano, hadi kufikia robo tatu ya utekelezaji wa bajeti katika mwaka wa fedha

2024/2025 na 2025/2026 fedha zilipatikana kwa 35.37% na 42.66% kwa fedha ambazo zimepatikana mtawalia wa bajeti iliyokuwa imeidhinishwa na Bunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kufuatia mwenendo huu, Kamati kupitia Bunge lako Tukufu inaitaka Serikali kuhakikisha upatikanaji wa fedha za Mfuko wa Barabara ni kama zinavyoidhinishwa. Kamati ina maoni kuwa upatikanaji usioridhisha wa fedha za Mfuko wa Barabara unachangia ufanisi mdogo katika matengenezo ya ukarabati wa miundombinu ya barabara na madaraja nchini. Taarifa zaidi kuhusu makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara ya Ujenzi inapatikana katika ukurasa wa 28-34.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maoni na ushauri wa Kamati. Baada ya uchambuzi wa kina kuhusu utekelezaji wa bajeti pamoja na makadirio na mapato na matumizi Wizara ya Ujenzi (Fungu Namba 98) kwa mwaka wa fedha 2026/2027, sasa ninaomba kuwasilisha maoni na ushauri wa Kamati kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, maoni ya jumla. Serikali isimamie kikamilifu miradi inayotekelezwa na Wizara ili iweze kukamilika kwa wakati na kwa kuzingatia ubora pamoja na thamani ya fedha. Serikali kupitia Wizara ya Ujenzi, ibuni vyanzo vya mapato na kuweka mikakati itakayoongeza ufanisi katika ukusanyaji wake ili kuifanya Wizara ya Ujenzi kuwa na taasisi zake kupunguza utegemezi wa ruzuku kutoka Mfuko Mkuu wa Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia Serikali ihakikishe kuwa taasisi zilizo chini ya Wizara ya Ujenzi zinatoa huduma bora kwa wadau wa sekta ya ujenzi nchini, hivyo kuchangia katika kuleta ustawi wa maisha ya wananchi; na Serikali iongeze ubunifu na matumizi ya teknolojia kwenye sekta ya ujenzi nchini kwa ajili ya kuendelea kuchochea maendeleo ya uchumi wa kisasa na kuzalisha ajira kwa vijana nchini na kufikia malengo yaliyowekwa katika Dira ya Taifa ya Maendeleo ya 2050.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maoni mahsusi. Kamati inashauri kuwa katika mapato ya Bodi ya Mfuko wa Barabara, Serikali

ihakikishe inahamisha fedha zote kwenda kwenye akaunti ya Mfuko wa Barabara kama zilivyoidhinishwa na Bunge ili kutekeleza miradi ya maendeleo na ukarabati wa barabara na madaraja nchini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali isitishe mara moja mpango wake wa kupunguza asilimia tano ya fedha za Mfuko wa Barabara kwa ajili ya kuzihamisha katika shughuli nyingine kwa sababu, mpango huo utazorotesha maendeleo ya sekta ya barabara nchini. Aidha, mpango huo ukitekelezwa ni wazi kuwa utakuwa unavunja sheria, kwani fedha hizi zinalindwa kwa mujibu wa Sheria ya *Ringfence*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kupitia Bodi ya Mfuko wa Barabara, ibuni vyanzo vipya vya mapato kwa ajili ya kuwezesha mfuko huo kuhudumia matengenezo na ukarabati wa miundombinu ya barabara na madaraja nchini. Aidha, Serikali ifanye tathmini ya kina kuhusu kuweka tozo maalumu ya maendeleo ya miundombinu ya barabara katika mapato ghafi ya madini, vibali vya ujenzi, muda wa maongezi kwenye simu, sekta ya mawasiliano pamoja na kulipia Daraja la Tanzanite kwa watumiaji wa daraja hilo. Daraja la Tanzanite lipo mbadala wake wa *Selander Bridge*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kukamilisha miradi ya zamani na barabara viporo. Kamati inashauri kuwa Serikali iweke kipaumbele na kuongeza kasi katika kukamilisha miradi yote ya zamani na miradi viporo ya ujenzi wa barabara na madaraja nchini ili kuchochea uchumi na kupata tija iliyokusudiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ipitie na kufanya upya mgawanyo wa fedha katika miradi hiyo kwa kutoa kipaumbele katika miradi viporo ili ikamilike na kuleta tija iliyokusudiwa na kufanya ukaguzi maalumu kupitia kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali *(CAG)* kwenye miradi yote ya ujenzi wa barabara na madaraja iliyochukua muda mrefu kwa ajili ya kujiridhisha na matumizi ya fedha za umma katika miradi hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, madeni ya wakandarasi na wahandisi washauri. Kamati inaishauri Serikali kuweka kipaumbele katika kulipa madai ya wakandarasi na wahandisi washauri ili kupunguza gharama ya miradi hiyo inayotokana na riba na ucheleweshaji wa malipo katika miradi kwenye sekta ya ujenzi; na Serikali ifanye uhakiki kuhusu madeni ya nyuma ya wakandarasi katika sekta ya ujenzi kulipwa Wizara ya Fedha (Hazina) ili bajeti ya maendeleo ya Wizara ya Ujenzi itekeleze majukumu yake na vipaumbele vyake kama ilivyokuwa imeidhinishiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nirudie kwenye eneo hili. Serikali ifanye uhakiki kuhusu madeni ya nyuma ya wakandarasi katika sekta ya ujenzi na kulipwa Wizara ya Fedha (Hazina) ili bajeti ya maendeleo ya Wizara ya Ujenzi itekeleze majukumu na vipaumbele vyake kama itakavyokuwa imeidhinishwa na Bunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hali ya miundombinu na barabara hapa nchini. Kamati inashauri kuwa Serikali ichukue hatua za haraka za kuhuisha barabara zinazopita katika shoroba za kiuchumi ambazo zimefikia mwisho wake wa uhai kwa sababu barabara hizi zina mchango mkubwa katika kukuza uchumi na kuongeza pato la Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia Serikali ifanye tathmini ya kina kubainisha barabara na madaraja ya kipaumbele yaliyo katika hali mbaya na kuandaa mpango wa kudumu katika kuboresha na kukarabati miundombinu hiyo; na Serikali ifanye upembuzi yakinifu na usanifu na kupata gharama halisi kwa ajili ya kuivutia na kuingia ubia na sekta binafsi *(PPP)* kwenye ujenzi na uendeshaji wa miundombinu ya barabara na madaraja hapa nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, upanuzi wa Barabara ya Dar es Salaam – Chalinze – Morogoro na ile ya Tanga – Handeni – Kibirashi ziingizwe katika utekelezaji kwa njia ya *PPP* kwani *TPA* na *NSSF* wameonesha nia ya kuzijenga. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, malipo ya fidia kwa wananchi waliopisha miradi ya maendeleo katika sekta ya ujenzi nchini. Kamati inashauri kuwa Serikali iongeze kasi katika kulipa wananchi

ambao maeneo yao yametwaliwa kwa mujibu wa sheria kwa ajili ya miradi ya barabara, viwanja vya ndege na vituo vya mabasi ili waweze kutafuta mahali pengine pa makazi na kuendelea na shughuli zao za kiuchumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ifanye tathmini ya kina kuhusu maeneo ambayo yanahitajika na inayoweza kulipa kwa sasa ikiwa ni pamoja na kuangalia uwezekano wa kurejesha baadhi ya maeneo kwa wananchi ili waweze kuyatumia katika shughuli za kiuchumi; na Serikali isizalishe madai mapya kwa kutwaa maeneo bila kuwa na fedha za kulipa fidia kwa wananchi ambao ardhi yao inachukuliwa kwa ajili ya miradi ya maendeleo ya sekta ya ujenzi hapa nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, muundo wa taasisi ya *TANROADS*, *TEMESA* na *TBA*. Kamati inashauri kuwa, Serikali iandae na kuleta Bungeni mabadiliko ya Sheria ya Muundo wa Taasisi hizi kutoka kuwa wakala na kuwa mamlaka, ili kuongeza ufanisi na uwajibikaji katika utekelezaji wa majukumu yao. Serikali iongeze usimamizi wa taasisi hizi, ili ziweze kubuni vyanzo vya mapato kupitia mali zake *(asset)* kwani taasisi zina mali nyingi ambazo hazitumiki katika kuzalisha mapato na ihakikishe taasisi hizi, hasa *TEMESA* na *TBA,* zinakusanya madeni kutokana na huduma ambazo wanazitoa kwa taasisi za umma na zile za binafsi. Kwenye eneo hili, Taasisi za Umma huwa hazilipi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hali ilivyo ya vivuko nchini. Kamati inashauri kuwa, Serikali iongeze kasi katika kukamilisha miradi yote ya ununuzi na ukarabati wa vivuko nchini, ili wananchi wapate huduma bora za usafiri kupitia vivuko hivyo. Serikali ihakikishe ununuzi wa vivuko vya Nyamisati, Mafia, *MV Kigamboni,* pamoja na ukarabati wa Kivuko cha *MV Pangani,* ili ukamilike kufikia tarehe 30 Juni, 2027 kwa ajili ya kutoa huduma kwa wananchi wanaotegemea vivuko hivyo. Aidha, Serikali ikamilishe vivuko vilivyopo Mwanza vilivyojengwa kwa Mkandarasi *Songoro Marine*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hitimisho na shukrani. Ninaendelea kukushukuru wewe binafsi kwa kuendelea kuliongoza vyema Bunge letu. Kwa namna ya kipekee ninamshukuru Mheshimiwa

Spika kwa maelekezo yake ambayo yamekuwa msaada mkubwa katika uendeshaji bora wa shughuli za kila siku. Kamati ya kudumu ya Bunge ya Miundombinu inamshukuru sana. Aidha, ninamshukuru Mheshimiwa Naibu Spika kwa namna anavyosaidia kutekeleza majukumu yake pamoja na Wenyeviti wa Bunge kwa kukusaidia kuendesha vikao vya Bunge kwa ufanisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kutumia fursa hii kumshukuru Waziri wa Ujenzi, Mheshimiwa Abdallah Hamis Ulega, Mbunge na Naibu Waziri wa Ujenzi, Mheshimiwa Godfrey Msongwe Kesekenya, kwa ushirikiano ambao wameipatia Kamati katika kipindi chote cha utekelezaji wa majukumu ya Kamati. Aidha, ninawashukuru watendaji wote wa Wizara ya Ujenzi pamoja na taasisi zote chini ya uongozi wa Katibu Mkuu wa Wizara hiyo, Balozi Mhandisi Aisha Amour, kwa ushirikiano wao kwa Kamati hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa moyo wa dhati kabisa ninawashukuru sana Waheshimiwa Wajumbe wote wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu ambao wamekuwa mstari wa mbele katika kuendeleza na kuisimamia Wizara ya Ujenzi, pamoja na taasisi zilizo chini yake kwa niaba ya Bunge hili Tukufu. Kwa hakika maoni, ushauri na mapendekezo yao vina mchango mkubwa katika kuboresha utendaji wa Serikali. Ninaomba kuwatambua Wajumbe hao ili majina yao yaingie katika kumbukumbu za Taarifa Rasmi za Bunge *(Hansard)*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, lakini siyo kwa umuhimu ninawashukuru sana watendaji wote wa Ofisi ya Bunge chini ya uongozi wa Katibu wa Bunge, Bwana Baraka Leonard, kwa kuisaidia Kamati kutekeleza majukumu yake hadi kukamilika kwa taarifa hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Msimamo wa Kamati. Baada ya maelekezo hayo, ninaomba Bunge lako likubali kupokea na kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Ujenzi, Fungu Namba 98, kwa mwaka wa fedha 2026/2027, kama yalivyowasilishwa na mtoa hoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kuwasilisha. Ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

**TAARIFA YA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA MIUNDOMBINU KUHUSU UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU YA FUNGU 98 - WIZARA YA UJENZI KWA MWAKA WA FEDHA 2025/2026 PAMOJA NA MAONI YA KAMATI KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA WIZARA HIYO KWA MWAKA WA FEDHA 2026/2027 – KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI**

**SEHEMU YA KWANZA**

**1.0 UTANGULIZI**

**1.1 Maelezo ya Awali**

**Mheshimiwa Spika,** kwa mujibu wa **Kanuni ya 121 (9)** ya Kanuni za Kudumu za Bunge, 2025 [Kanuni za Bunge] naomba kuwasilisha taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu kuhusu utekelezaji wa bajeti ya Wizara ya Ujenzi **(Fungu 98)** kwa mwaka wa fedha 2025/2026 pamoja na maoni ya Kamati kuhusu makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara hiyo kwa mwaka wa fedha 2026/2027.

**Mheshimiwa Spika,** bila kuathiri masharti yanayopatikana katika Kanuni ya 145 ya Kanuni za Bunge, taarifa hii imegawanyika katika sehemu zifuatazo:-

a) Sehemu ya kwanza ni utangulizi ambayo inaeleza kuhusu muundo wa taarifa pamoja na namna Kamati ilivyotekeleza majukumu yake;

b) Sehemu ya pili inahusu uchambuzi wa utekelezaji wa Bajeti kwa mwaka wa fedha 2025/2026 kwa kutathimini uzingatiaji wa ushauri na maoni ya Kamati, makusanyo ya maduhuli, mwenendo wa upatikanaji wa fedha na utekelezaji wa miradi ya maendeleo;

c) Sehemu ya tatu inahusu uchambuzi wa makadirio ya mapato na matumizi kwa mwaka wa fedha 2026/2027;

d) Sehemu ya nne ni majumuisho ya maoni na ushauri wa Kamati; na

e) Sehemu ya tano ni hitimisho.

### 1.2 Namna Kamati Ilivyotekeleza Majukumu Yake

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu hutekeleza majukumu yake kwa kuzingatia masharti yaliyoainishwa katika Katiba, Sheria mbalimbali pamoja na Kanuni za Kudumu za Bunge.

**Mheshimiwa Spika,** katika kufanya uchambuzi wa utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya **Ujenzi (Fungu 98)** kwa mwaka wa fedha 2025/2026 pamoja na makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara hiyo kwa mwaka wa fedha 2026/2027, Kamati ilifanya yafuatayo: -

a) Kupokea dondoo (extracts) na randama ya Wizara kwa ajili ya Uchambuzi wa Bajeti [Kanuni ya 118 (1)];

b) Kupokea taarifa na kukagua utekelezaji wa miradi ya maendeleo iliyotengewa fedha katika mwaka wa fedha 2025/2026 [Kanuni ya 120 (1)]; na

c) Kuchambua utekelezaji wa Bajeti ya Wizara na taasisi zake kwa mwaka wa Fedha 2025/2026, pamoja na kufanya ulinganisho wa makadirio ya mapato na matumizi kwa mwaka wa fedha 2026/2027 [Kanuni ya 120 (2)].

## SEHEMU YA PILI

## 2.0 UCHAMBUZI WA UTEKELEZAJI WA BAJETI YA MWAKA WA FEDHA 2025/2026

### 2.1 Utekelezaji wa Maoni na Ushauri wa Kamati

**Mheshimiwa Spika,** tarehe 5 Mei, 2025, Bunge lilipokea, kujadili na kuidhinisha makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara ya Ujenzi

**(Fungu 98)** kwa mwaka wa fedha 2025/2026. Katika kikao hicho, Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu iliwasilisha maoni yake kuhusu Bajeti ya Wizara hiyo ili kutimiza masharti yaliyowekwa na **Kanuni ya 121 (9).**

**Mheshimiwa Spika,** napenda kulijulisha Bunge lako Tukufu kwamba, kwa sehemu kubwa Serikali imeyafanyia kazi maoni na ushauri uliotolewa na Kamati. Hata hivyo, katika baadhi ya maeneo ushauri uliotolewa haukufanyiwa kazi kwa ukamilifu. Kamati inapenda kuweka msisitizo kuhusu umuhimu wa utekelezaji wake kama ifuatavyo: -

a) Kamati ilishauri Serikali kuhakikisha inafanya malipo kwa madai ya Makandarasi na Wahandisi Washauri katika sekta ya Ujenzi. Pamoja na jitihada za Serikali kupunguza madai hayo, kasi ya ulipaji wake ni ndogo ukilinganisha na ukubwa wa deni sambamba na ongezeko la riba inayotokana na kuchelewesha malipo ya madai hayo; na

b) Kamati ilishauri Serikali kufanya malipo ya fidia kwa wananchi ambao ardhi yao imetwaliwa ili kupisha miradi katika sekta ya Ujenzi. Hadi kufikia tarehe 24 Machi, 2026, Serikali ilikuwa imelipa **Shilingi 30,669,633,870.54** sawa na **asilimia 25.41** tu ya **Shilingi 120,694,171,449.31** zinazodaiwa na wananchi kama fidia. Hali hii inaweza kusababisha malalamiko na kudumaza hali ya kiuchumi kwa sababu wananchi hao hawawezi kutumia ardhi hiyo katika shughuli za uzalishaji mali.

### 2.2 Makusanyo ya Maduhuli

**Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2025/2026 Wizara ya Ujenzi ilipangiwa kukusanya maduhuli ya jumla ya **Shilingi 80,001,000/=.** Hadi kufikia Machi, 2025 Wizara ilikuwa imefanikiwa kukusanya jumla ya **Shilingi 78,237,500.00,** sawa na **asilimia 97.80** ya lengo kama inavyoonekana katika **Kielelezo Na. 1.**

**Kielelezo Na. 1: Makusanyo ya Mapato kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026 kwa kipindi cha Julai hadi Machi, 2026**

| Kifungu | Jina la Kifungu | Makadirio 2025/2026 (Shilingi) | Makusanyo hadi Machi, 2026 (Shilingi) | Asilimia (%) |
|---|---|---|---|---|
| 1001 | Utawala | 1,000 | 0.00 | 0.00 |
| 2002 | Huduma za Ufundi | 78,000,000.00 | 71,572,500.00 | 91.8 |
| 5002 | Usalama na Mazingira | 2,000,000.00 | 6,664,500.00 | 333 |
| **JUMLA** | | ***80,001,000.00*** | ***78,237,000.00*** | ***97.8*** |

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inaipongeza Wizara kwa ufanisi katika ukusanyaji wa maduhuli. Vilevile, Kamati inaitaka Wizara na taasisi zake kuendelea kubuni vyanzo vipya vya mapato ili kuongeza mchango wa sekta ya ujenzi katika pato la Taifa.

**2.3 Mwenendo wa Upatikanaji wa Fedha**

**Mheshimiwa Spika,** utekelezaji wa vipaumbele na majukumu ya Wizara unategemea upatikanaji wa fedha zilizoidhinishwa na Bunge kutoka hazina. Katika mwaka wa fedha 2025/2026, Wizara ya Ujenzi iliidhinishiwa kutumia jumla ya **Shilingi 1,903,659,204,000/=** kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo.

Mheshimiwa Spika, hadi kufikia Machi, 2025, Wizara ilikuwa imepokea **Shilingi 1,377,854,457,522.07** sawa na asilimia **72.38** ya Bajeti. Kamati inaipongeza Serikali kwa kutoa kiasi hicho cha fedha kwa ajili ya utekelezaji wa vipaumbele na majukumu ya Wizara.

### 2.3.1 Matumizi ya Kawaida

**Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2025/2026, Wizara ya Ujenzi **(Fungu 98)** iliidhinishiwa **Shilingi 90,468,270,000**/= ikiwa ni fedha za matumizi ya kawaida. Hadi kufikia Machi, 2025, Wizara ilipokea **Shilingi 57,881,873,458.90** sawa na **asilimia 63.98** ya bajeti iliyoidhinishwa kama inavyoonekana katika **Kielelezo Na. 2.**

**Kielelezo Na. 2: Mwenendo wa Mapokezi ya Fedha za Matumizi ya Kawaida toka Hazina hadi kufikia Machi, 2026**

| Bajeti (Matumizi) | Kiasi Kilichoidhinishwa 2025/2026 (Shilingi) | Kiasi Kilichopokelewa (Shilingi) | Asilimia (%) |
|---|---|---|---|
| Mishahara (P.E) | 85,028,585,000.00 | 55,438,930,600.17 | 65.20 |
| Matumizi Mengineyo (O.C.) | 5,439,685,000.00 | 2,442,942,798.70 | 44.91 |
| **JUMLA KUU** | **90,468,270,000.00** | **57,881,873,458.90** | **63.98** |

**Mheshimiwa Spika,** katika uchambuzi wake, Kamati imebaini kuwa hali ya mapokezi ya fedha za Matumizi ya Kawaida ipo chini ya wastani kulinganisha na mpango kazi wa utekelezaji wa Bajeti. Aidha, Kamati haikuridhika na mwenendo wa upatikanaji wa fedha za Matumizi Mengineyo (O.C.), kwa sababu Wizara ilikuwa imepokea **asilimia 44.91** tu ya Bajeti iliyoidhinishwa na Bunge ukilinganisha na **asilimia 75** ya mpango kazi wa utekelezaji wake.

### 2.3.2 Fedha za Miradi ya Maendeleo

**Mheshimiwa Spika,** katika mwaka wa fedha 2025/2026, Wizara ya Ujenzi iliidhinishiwa jumla ya **Shilingi 1,813,190,934,000/=** kwa ajili ya utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo. Hadi kufikia Machi, 2026 Wizara ilikuwa imepokea **Shilingi 1,319,972,584,063.17** sawa na **asilimia 72.80** ya makadirio. **Kielelezo Na. 3** kinatoa mchanganuo wa hali ya mapokezi ya fedha za bajeti ya maendeleo.

**Kielelezo Na. 3: Mwenendo wa Mapokezi ya Fedha za Miradi ya Maendeleo hadi kufikia Machi, 2026**

| Matumizi | Chanzo | Kilichoidhinishwa 2025/2026 (Shilingi) | Kilichopokelewa (Shilingi) | Asilimia (%) |
|---|---|---|---|---|
| Ndani | Mfuko Mkuu | 520,466,647,000.00 | 416,567,351,247.80 | 80.03 |
| | Mfuko wa Barabara | 688,756,470,000.00 | 293,849,848,399.16 | 42.66 |
| | Jumla (A) | 1,209,223,117,000.00 | 710,417,199,646.96 | 58.75 |
| | | | | |
| | | | | |
| Nje | Jumla (B) | 603,967,817,000.00 | 609,555,384,416.21 | 100.93 |
| **JUMLA KUU (A+B)** | | **1,813,190,934,000.00** | **1,319,972,584,063.17** | **72.80** |

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilifanya uchambuzi wa kina katika mwenendo wa upatikanaji wa fedha za Maendeleo na kubaini mambo yafuatayo:-

(i) Wizara imepokea **asilimia 72.80** ya fedha za miradi ya maendeleo ikilinganishwa na **asilimia 75** ya mpango kazi wa utekelezaji wa bajeti. Hali hii inaweza kuchangia kushuka kwa ufanisi katika kutekeleza majukumu ya Wizara; na

(ii) Fedha za Mfuko wa Barabara zimepokelewa kwa **asilimia 42.66** tu ya Bajeti iliyoidhinishwa na Bunge. Hali hii inaweza kuchangia kuzorota kwa shughuli za matengenezo na ukarabati wa barabara nchini kwa kuwa Fedha za Mfuko ndio hutumika katika kufanya shughuli hizo.

### 2.4 Ukaguzi wa Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo

#### 2.4.1 Maelezo ya Awali

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilifanya ukaguzi wa miradi ya maendeleo iliyotengewa fedha katika mwaka wa fedha 2025/2026. Ukaguzi huo ulifanyika kwa mujibu wa Kanuni ya 120 (1) ya Kanuni za Bunge kwa lengo la kutathmini hali ya mapokezi

ya fedha, hatua ya utekelezaji pamoja na kubainisha changamoto za utekelezaji wa miradi hiyo. Ukaguzi wa miradi hiyo ulifanyika katika Mikoa ya Morogoro, Tanga na Dar es Salaam kati ya tarehe 12 – 19 Machi, 2026.

### 2.4.2 Miradi Iliyokaguliwa

**Mheshimiwa Spika,** naomba nitoe ufafanuzi wa miradi hiyo kwa muhtasari kama ifuatavyo: -

**(a) Mradi Na. 6304 – Ujenzi wa Jengo la Taaluma katika Taasisi ya Teknolojia ya Ujenzi (ICoT), Morogoro**

**Mheshimiwa Spika,** utekelezaji wa mradi huu unahusisha ujenzi wa jengo moja la ghorofa lenye sakafu nne (groundfloor+3). Lengo la mradi huu ni kupata jengo litakalokuwa na Ofisi za Kitaaluma pamoja na madarasa yatakayoweza kuchukua wanafunzi 1001.

**Mheshimiwa Spika,** kwa mujibu wa mkataba, gharama za mradi huu ni **Shilingi 5,978,854,556/=** (pamoja na kodi ya ongezeko la thamani VAT) na unatarajia kukamilika ndani ya miezi 36 yaani kuanzia tarehe 01 Juni, 2023 hadi tarehe 15 Juni, 2026. Hadi wakati Kamati inafanya ukaguzi wake tarehe 12 Machi, 2026, mkandarasi alikuwa amelipwa **Shilingi 2,965,420,717.89** sawa na **asilimia 49.59** ya gharama ya mradi na mkandarasi hakuwa na hati yoyote ya madai ambayo haijalipwa.

**Mheshimiwa Spika,** Serikali ihakikishe kasi ya utekelezaji wa mradi inaongezeka kwani mradi umefikia **asilimia 74** ukilinganisha na mpango kazi wa **asilimia 89** kwa mujibu wa mkataba. Kuchelewa kwa mradi huu kunaweza kuongeza gharama na kupunguza manufaa ya mradi kama ilivyokusudiwa.

**(b) Mradi Na. 6727 – Ukarabati na Ujenzi wa Uwanja wa Ndege wa Tanga**

**Mheshimiwa Spika,** mradi huu unatekelezwa chini ya usimamizi wa Wakala wa Barabara Tanzania (TANROADS). Lengo la mradi

huu ni kukifanya Kiwanja cha Tanga kuwa na kiwango cha Daraja 3C kwa viwango vya Shirika la Usalama wa Anga Duniani (ICAO).

**Mheshimiwa Spika,** kwa mujibu wa masharti ya mkataba, gharama za mradi huu ni **Shilingi 91,890,859,967.59** (pamoja na kodi ya ongezeko la thamani VAT) na utatekelezwa kwa takribani miezi 19 kuanzia tarehe 23 Novemba, 2025 hadi tarehe 22 Mei, 2027. Vilevile, gharama za mhandisi mshauri wa mradi huu ni **Dola za Kimarekani 2,250,289.50** (pamoja na kodi ya ongezeko la thamani VAT).

**Mheshimiwa Spika,** hadi wakati Kamati inafanya ukaguzi wake tarehe 13 Machi, 2026, utekelezaji wa mradi ulikuwa umefikia **asilimia 3** na mkandarasi alikuwa amepokea **Shilingi 1,803,136,436.558** kama malipo ya awali sawa na **asilimia 1.96** ya gharama ya mradi. Aidha, Mhadisi mshauri amelipwa **Dola za Kimarekani 84,276.15** na wananchi wote **274** waliotakiwa kupisha mradi wakiwa wamelipwa fidia yenye jumla ya **Shilingi 2,654,000,000/=.**

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inaitaka Serikali kuhakikisha usimamizi madhubuti wa mkataba katika utekelezaji wa mradi huo. Aidha, ni vyema mkandarasi akatoa kipaumbele kwa ajira za muda mfupi kwa wananchi wanaoishi kuzunguka eneo la mradi.

### (c) Mradi Na. 4101 – Ujenzi wa Barabara ya Tanga – Pangani – Makurunge pamoja na Ujenzi wa Daraja la Mto Pangani

**Mheshimiwa Spika,** barabara hii ni sehemu ya mtandao wa barabara ya Jumuiya ya Africa Mashariki (EAC) inayounganisha nchi ya Tanzania na Kenya kupitia ushoroba wa Pwani ya Afrika Mashariki wenye urefu wa Kilomita 454. Lengo la mradi huu ni kuchochea ukuaji wa uchumi ndani ya Jumuiya kwa kupunguza gharama na muda wa usafiri pamoja na kurahisisha muunganiko wa huduma za bandari za Dar Es Salaam, Tanga, na Mombasa.

**Mheshimiwa Spika,** kwa upande wa Tanzania, mradi huu unahusisha ujenzi wa barabara ya Tanga – Pangani – Makurunge (Bagamoyo) yenye urefu wa Kilomita 256 na daraja la mto

Pangani lenye urefu wa mita 525. Ujenzi wa barabara hii umegawanyika katika sehemu nne (Lot 1, Lot 2, Lot 3 na Lot 4).

**Mheshimiwa Spika,** hadi tarehe 13 Machi, 2026 ambapo Kamati ilifanya ukaguzi katika utekelezaji wa mradi huu, maendeleo ya ujenzi wa barabara hii yalikuwa kama ifuatavyo:-

(i) Sehemu ya kwanza **(Lot 1)** inahusisha ujenzi wa Kilomita 50 za barabara kutoka Tanga hadi Pangani. Ujenzi huu unagharamiwa na Serikali kwa jumla ya **Shilingi 103,921,131,060.63.** Utekelezaji wake umefikia **asilimia 75** ikilinganishwa na mpango kazi wa **asilimia 96.27** kwa mujibu wa mkataba na ulitakiwa kukamilika tarehe 29 Aprili, 2026;

(ii) Sehemu ya pili **(Lot 2)** inahusisha ujenzi wa daraja la mto Pangani lenye urefu wa mita 525 pamoja na barabara unganishi zenye jumla ya urefu wa Kilomita 25.6. Ujenzi huu unafadhiliwa kwa pamoja kati ya Serikali (Asilimia 13) na Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB) (Asilimia 87) kwa jumla ya **Shilingi 127,968,431,149.83.** Aidha, utekelezaji wake umefikia **asilimia 64** sawa na mpango kazi kwa mujibu wa mkataba na unatarajiwa kukamilika tarehe 5 Februari, 2027;

(iii) Sehemu ya tatu **(Lot 3)** ni ujenzi wa barabara ya kutoka Mkange – Mkwaja – Tungamaa yenye urefu wa Kilomita 95.2, ikijumuisha barabara unganishi ya Kipumbwi yenye urefu wa Kilomita 3.7. Ujenzi huu pia unafadhiliwa kwa pamoja kati ya Serikali (Asilimia 13) na Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB) (Asilimia 87) kwa jumla ya **Shilingi 100,479,649,980.11.** Utekelezaji wake umefikia **asilimia 60** ukilinganisha na mpango kazi wa **asilimia 78** kwa mujibu wa mkataba na ulitarajiwa kukamilika ifikapo tarehe 19 Machi, 2026; na

(iv) Sehemu ya nne **(Lot 4)** ni ujenzi wa barabara ya Bagamoyo (Makurunge) – Mkange Kilomita 73.25 ambao utekelezaji wake unasubiri upatikanaji wa fedha.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inaipongeza Serikali katika utekelezaji wa mradi huo. Hata hivyo, Kamati inaitaka Serikali kuhakikisha

wakandarasi wanaongeza kasi ya utekelezaji wa mradi huu ili ukamilike kwa mujibu wa mikataba ya ujenzi. Aidha, Serikali ihakikishe inatenga fedha na kutafuta mkandarasi kwa ajili ya ujenzi wa Sehemu ya nne ya barabara hiyo Kilomita 73.25 kutoka Bagamoyo hadi Mkange.

**(d) Mradi Na. 4144 – Ukarabati wa Kivuko MV Pangani II na Maegesho ya Kivuko, Pangani Mkoa wa Tanga**

**Mheshimiwa Spika,** mradi wa ukarabati wa kivuko cha MV Pangani II unatekelezwa kupitia Wakala wa Ufundi na Umeme Tanzania (TEMESA). Lengo la mradi huu ni kuongeza ufanisi wa utoaji huduma na kupunguza kero ya usafiri kwa wananchi wa eneo la Pangani na Bweni kwa Kivuko hicho chenye uwezo wa kubeba mzigo wa tani 50.

**Mheshimiwa Spika,** kwa mujibu wa masharti ya mkataba, gharama za mradi huu ni **Shilingi 2,398,282,598.40** (pamoja na kodi ya ongezeko la thamani VAT) kwa ajili ya mkandarasi na mhandisi mshauri. Aidha, utekelezaji wa mradi huu ulipangwa kukamilika ndani ya miezi minne kuanzia tarehe 12 Mei, 2025 hadi 12 Septemba, 2025.

**Mheshimiwa Spika,** hadi wakati Kamati inafika uwandani, Serikali ilikuwa imelipa **Shilingi 461,208,192/=** sawa na **asilimia 20** tu ya gharama ya mkandarasi. Vilevile, mhandisi mshauri alikuwa amepokea malipo ya **Shilingi 18,448,327.68** kwa ajili ya usimamizi wa mradi.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inasikitika kulitaarifu Bunge lako Tukufu kuwa mradi haujakamilika hadi sasa. Aidha, Kamati ilipokea taarifa kuwa Serikali imefanya marejeo ya mkataba mara mbili ambapo mara ya kwanza ilitarajiwa mradi huo kukamilika tarehe 11 Disemba, 2025 na mara pili mradi ulipangwa kukamilika tarehe 11 Machi, 2026.

**Mheshimiwa Spika,** hata hivyo, hadi tarehe 13 Machi, 2026, ambapo Kamati ilifanya ukaguzi wa mradi huo, utekelezaji wake ulikuwa umefikia **asilimia 51** tu. Kamati haikuridhishwa na

ucheleweshaji huu kwani kivuko hicho ni chombo kinachotegemewa kwa ajili ya usafirishaji wa abiria na mizigo kati ya Pangani na Bweni katika Wilaya ya Pangani kwani hadi sasa kivuko hicho hakitoi huduma kabisa.

**(e) Mradi Na. 4285 – Ujenzi wa Miundombinu ya Mabasi Yaendayo Haraka (BRT) Awamu ya Tatu (CBD – Gongolamboto)**

**Mheshimiwa Spika,** mradi huu unatekelezwa kupitia Wakala wa Barabara Tanzania (TANROADS). Lengo la mradi ni kuongeza ufanisi wa huduma za usafiri na kupunguza foleni ya magari katika jiji la Dar Es Salaam.

**Mheshimiwa Spika,** mradi huu unahusisha ujenzi wa barabara za kutoka katikati ya Jiji (CBD) hadi Gongolamboto pamoja na miundombinu ya majengo. Utekelezaji wa mradi huu umegawanyika katika sehemu mbili (Lot 1 na Lot 2).

**Mheshimiwa Spika,** tarehe 14 Machi, 2026, Kamati ilifanya ukaguzi kubaini maendeleo ya mradi huu yalikuwa kama ifuatavyo: -

(i) Sehemu ya kwanza **(Lot 1)** inahusisha ujenzi wa barabara zenye jumla ya urefu wa Kilomita 23.3. Utekelezaji wake unahusisha ujenzi wa barabara za Azikiwe, Bibi Titi, Nkrumah, Nyerere, Gongolamboto, barabara za Lindi, Shaurimoyo, Uhuru na Mandela. Ujenzi wa barabara hizi umefikia **asilimia 98** na unafadhiliwa na Benki ya Dunia kwa gharama ya **Shilingi Bilioni 231.664;**

(ii) Sehemu ya Pili **(Lot 2)** inahusisha ujenzi wa miundombinu ya majengo ambayo ni karakana ya matengenezo ya magari katika eneo la Gongolamboto, Kituo Kikuu cha mabasi (Terminal) ndani ya uwanja wa ndege wa Julius Nyerere (JNIA) na Kituo kidogo ambacho ni Kituo mlisho *(Feeder Station)* katika eneo la Banana. Ujenzi wa miundombinu hii unafadhiliwa na Serikali pamoja na Benki ya Dunia kwa gharama ya **Shilingi 56,604,653,573.03** na utekelezaji wake

upo katika hatua za maandalizi na usanifu wa majengo hayo.

**Mheshimiwa Spika,** kwa ujumla Kamati iliridhishwa na maendeleo ya utekelezaji wa mradi huu. Aidha, Kamati inaitaka Serikali kumsimamia mkandarasi anaetekeleza sehemu ya pili ya mradi kuongeza kasi na kuzingatia viwango ili mradi huo uanze kufanya kazi kama ilivyokusudiwa.

**(f) Mradi Na. 6327 – Ujenzi wa Nyumba za Serikali Zilizopo Canadian Village na Magomeni Kota awamu ya Pili**

**Mheshimiwa Spika,** miradi hii inatekelezwa na Wakala wa Majengo Tanzania (TBA). Lengo la miradi hii ni kuboresha makazi ya wananchi na kupandisha hadhi ya mji inayozingatia bei ya soko katika sekta ya milki (real estate) nchini.

**Mheshimiwa Spika,** tarehe 14 Machi, 2026, Kamati ilifanya ukaguzi wa miradi hii kama ifuatavyo:-

**(i) Mradi wa "Canadian Village" awamu ya 1**

**Mheshimiwa Spika,** mradi ulihusisha ujenzi wa majengo matatu ya ghorofa (Blocks 1, 2 and 3) katika eneo la Canadian Village yenye uwezo wa kuchukua familia 36 kwa pamoja. Ujenzi wa majengo hayo uligharamiwa na Serikali kupitia mapato ya ndani ya Wakala wa Majengo Tanzania ambapo jumla ya **Shilingi 13,755,941,803.59** zimetumika hadi kukamilika kwake. Aidha, katika Jengo moja la Block 1 tayari linakaliwa na familia 12 na majengo mawili yamekamilika tayari kwa kupangishwa. Mradi huu utazalisha mapato ya **Shilingi 1,533,600,000/=** kwa mwaka na kufanya wakala kuendelea kuongeza majengo mengi zaidi katika eneo hilo.

**(ii)Mradi wa Magomeni Kota awamu ya 2**

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilifanya ukaguzi katika ujenzi wa majengo mawili (Block C na D) ambayo yapo katika hatua mbali mbali za utekelezaji. Jengo C limefikia **asilimia 60** huku Jengo D

likiwa limefikia **asilimia 47.** Aidha, majengo yote mawilili yanatarajiwa kukamilika ifikapo tarehe 30 Juni, 2026 na yanajengwa kwa ufadhili wa Serikali kwa gharama ya **Shilingi 11,808,724,763.44.** Majengo hayo yatakapokamilika yatakuwa na uwezo wa kuchukua familia 32 kwa wakati mmoja na kuboresha taswira ya eneo hilo tofauti na ilivyokuwa hapo awali.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati iliridhishwa na utekelezaji wa miradi hiyo ambayo inaonesha nia ya Serikali kutimiza Sera ya Makazi ya kuhakikisha wananchi na watumishi wa umma wanapata makazi bora na ya kisasa kwa bei himilivu. Aidha, Kamati inaitaka Serikali kuongeza usimamizi kwa mkandarasi wa mradi wa Magomeni Kota ili mradi huo ukamilike kwa wakati.

### 2.5 Masuala Mahsusi Yaliyobainika Katika Utekelezaji wa Bajeti ya Mwaka wa Fedha 2025/2026

#### (a) Fedha za Bodi ya Mfuko wa Barabara

**Mheshimiwa Spika,** katika mwaka wa fedha 2025/2026 Bodi ya Mfuko wa Barabara iliidhinishiwa Bajeti ya **Shilingi 945,794,956,000/=** kwa ajili ya matengenezo na ukarabati wa barabara nchini. Hata hivyo, Kamati ilibaini kwamba hadi kufikia tarehe 24 Machi, 2026 kiasi cha Shilingi 418,876,857,094.82 pekee sawa na asilimia 44 tu ya bajeti ya Bodi ndio kilikuwa kimehamishiwa katika akaunti za Mfuko.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inalikumbusha Bunge lako Tukufu kuwa, Fedha za Mfuko wa Barabara ni fedha zinazolindwa kwa mujibu wa sheria. Kwa hiyo, Serikali kushindwa kuhamisha fedha hizo katika akaunti ya Mfuko wa Barabara kwa wakati inachelewesha matengenezo na ukarabati wa barabara nchini ambazo zimeathirika na hali ya mvua nyingi. Aidha, hali hii pia imekuwa ikiripotiwa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) mara kwa mara bila Serikali kuchua hatua ya kuirekebisha.

**Mheshimiwa Spika,** vilevile, Kamati imebaini kuwa Serikali inampango wa kuchukua **asilimia 5** ya Fedha za Mfuko wa

Barabara kwa ajili ya kugharamia miradi mingine ya Maendeleo. Pamoja na nia njema ya Serikali, Kamati haikubaliani na uamuzi huo na inaliomba Bunge lako Tukufu kuiunga mkono kwa ajli ya kunusuru sekta ya barabara nchini. Hii inatokana na ukweli kuwa, mahitaji ya fedha katika kufanya matengenezo na kukarabati barabara na maradaja nchini ni makubwa na kuliko kiasi cha fedha kinachopatikana. Kwa hiyo, uamuzi huo utapunguza ufanisi na tija katika kukabiliana na ubovu pamoja na uchakavu wa miundombinu ya barabara na madaraja nchini.

**(b) Hali ya Miundombinu ya Barabara na Madaraja Nchini**

**Mheshimiwa Spika,** taarifa ya TANROADS ya tarehe 30 Machi, 2026, inaonesha kuwa ni **asilimia 30** tu ya barabara za Kifaifa ndio iko katika hali nzuri wakati **asilimia 70** zikiwa katika hali ya wastani au mbaya.
Vilevile, taarifa ya Wizara ya tarehe 24 Machi, 2026 iliyowasilishwa katika Kamati inaonesha kuwa **asilimia 39.4** ya mtandao wa barabara zote za lami zinazosimamiwa TANROADS zimefikia mwisho wa uhai wake (End of Design Life) na kupelekea uchakavu. Aidha, kwa misimu ya hivi karibuni nchi yetu imepokea mvua nyingi za juu ya wastani ambazo zimechangia uharibifu wa miundombinu ya barabara na madaraja.

**Mheshimiwa Spika,** barabara nyingi zilizoathirika ni zile zinazopita katika shoroba za kiuchumi huku zikiunganisha Mikoa kwa Mikoa na nyingine zikiunganisha nchi yetu na nchi jirani. Baadhi ya barabara hizo ni pamoja na:-

(i) Dar es Salaam – Mkuranga – Kibiti- Lindi;
(ii) Igawa – Tunduma;
(iii) Ifakara – Mlimba – Njombe;
(iv) Ifakara – Malinyi – Namtumbo;
(v) Morogoro – Dodoma;
(vi) Dodoma – Iringa;
(vii) Singida – Igunga – Nzega – Mwanza ; na
(viii) Babati – Singida.

**Mheshimiwa Spika,** hali hii imesababisha baadhi ya maeneo kushindwa kufikika kwa urahisi na kuzua malalamiko miongoni mwa wananchi na wawakilishi wao katika maeneo hayo. Ili kuboresha miundombinu hiyo, Serikali inahitaji kuwekeza kiwango kikubwa cha fedha, ambapo kupitia utaratibu wa Bajeti ya Serikali pekee changamoto hii haiwezi kutatuliwa kwa wakati.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ina maoni kuwa, Serikali itekeleze mara moja Sera ya ubia baina yake na sekta binafsi (PPP) ili sekta hiyo iweze kushiriki katika kuboresha na kuendesha baadhi ya miundombinu hiyo. Vilevile, watumiaji wa Daraja la Tanzanite waanze kuchangia ili fedha hizo zitumike katika marekebisho na matengenezo ya miundombinu hiyo.

**c) Hali ya Miradi ya Zamani ya Barabara [Miradi Viporo]**

**Mheshimiwa Spika,** ibara ya 40 (i) ya Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya Mwaka 2025-2030, inaelekeza Serikali Kukamilisha kwa kiwango cha lami ujenzi na ukarabati wa barabara zinazounganisha makao makuu ya mikoa yote nchini na zile zinazounganisha Tanzania na nchi jirani. Uamuzi wa kujenga baadhi ya barabara hizo ulifanywa na Serikali kwa sababu ya umuhimu wake katika uchumi wa nchi yetu. Mathalani, baaadhi ya barabara hizo na sababu ya Serikali kuamua kuzijenga ni kama ifuatavyo:-

(i) **Magole – Mziha –Handeni:** Lengo lake ni kupitisha malori ya mizigo kutoka Bandari ya Tanga kwa ajili ya kupunguza foleni ya malori yanayotoka Bandari ya Dar Es Salaam kupitia Chalinze;

(ii) **Nzega – Itobo – Bukene:** Lengo lake ni kuunganisha Wilaya za Nzega na Igunga kuelekea katika Mradi wa Reli ya Kisasa ya SGR kuelekea Isaka;

(iii) **Simbo – Kalya pamoja na Daraja la Mto Malagarasi:** Lengo lake ni kuunganisha nchi ya Tanzania kupitia Mkoa wa Kigoma na nchi jirani ya Burundi hivyo kurahisisha biashara baina ya maeneo hayo; na

(iv) **Tarime – Serengeti (Mugumu):** Lengo lake ni kurahisisha usafiri kwa watalii wanaotoka katika Hifadhi ya Masai Mara nchini Kenya kuja katika Hifadhi ya Taifa ya Serengeti nchini Tanzania kupitia katika mpaka wa Sirari.

**Mheshimiwa Spika,** hata hivyo, tathmini ya Kamati inaonesha kuwa miradi mingi ya zamani (miradi viporo) haijatengewa fedha za kutosha kwa ajili kuendeleza ujenzi wake. Aidha, katika miradi hiyo, fedha zilizotengwa zimeelekezwa katika kulipa madeni ya nyuma ya makandarasi na sio katika kuendeleza shughuli za ujenzi ili kukamilisha miradi husika.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ina maoni kuwa, Serikali iandae mpango wa muda mfupi na muda wa kati utakaotekelezwa ili kuhakikisha miradi yote viporo ya ujenzi wa barabara na madaraja inakamilika nchini. Aidha, Serikali ipitie na kufanya upya mgawanyo wa fedha katika miradi hiyo kwa kutoa kipaumbele katika miradi viporo ili ikamilike na kuleta tija iliyokusudiwa.

**d) Madeni ya Makandarasi na Wahandisi Washauri**

**Mheshimiwa Spika,** Wizara ya Ujenzi inakabiliwa na changamoto ya madeni makubwa ya Makandarasi na Wahandisi Washauri. Madeni haya kwa kiasi kikubwa yanatokana na utekelezaji wa miradi ya barabara iliyofanyika kwa zaidi ya miaka 10.

**Mheshimiwa Spika,** hali imechangia kuathirika moja kwa moja kwa ufanisi katika utekelezaji wa bajeti ya Wizara hii. Mathalani, katika utekelezaji wa bajeti ya mwaka wa fedha 2025/2026, hadi kufikia Machi, 2026, Wizara ilikuwa imepokea jumla ya **Shilingi 1,319,972,584,063.17** sawa na **asilimia 72.80** ya fedha yote ya maendeleo. Kama fedha hizi zingeelekezwa katika vipaumbele na mpango wa bajeti kama ilivyoidhinishwa na Bunge, zingeweza kuleta tija iliyokusudiwa katika sekta ya barabara nchini.

**Mheshimiwa Spika,** hata hivyo, uchambuzi wa Kamati umebaini kuwa sehemu kubwa ya fedha hizi ziliekezwa katika malipo ya madeni hivyo kuathiri matokeo ya utekelezaji wa bajeti wa Wizara hii. Serikali ilitoa ahadi ya kulipa jumla ya **Shilingi Bilioni 800** kwa

madeni yaliyohakikiwa ya Wakandarasi na Wazabuni kupitia **Wizara ya Fedha (Fungu 21)** ili kupunguza tatizo hilo.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inaipongeza na kutambua juhudi za Serikal katika kutatua changamoto hiyo ya madeni. Hata hivyo, Kamati ina maoni kuwa juhudi hizi zinaweza zisilete matokeo yanayotarajiwa kwa sababu madeni hayo ni ya Wizara mbalimbali na sio ya Wizara ya Ujenzi pekee.

**e) Muundo wa Taasisi za TANROADS, TBA na TEMESA**

**Mheshimiwa Spika,** katika kupitia utekelezaji wa majukumu ya taasisi hizi, Kamati ilibaini kuwa Sheria zinazounda taasisi hizo zimepitwa na wakati. Aidha, taasisi hizi zimekuwa na mchango mkubwa katika sekta za ujenzi wa barabara, nyumba na ufundi nchini. Hata hivyo, taasisi hizi zinakabiliwa na changamoto ya kuingiliwa kiutendaji na kukosa uhuru wa kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi.

**Mheshimiwa Spika,** kupitia sheria ya uanzishwaji wa Wakala, taasisi hizi zimekosa Bodi madhubuti za usimamizi kwani zinasimamiwa na Bodi za Ushauri. Aidha, changamoto ya muundo wa taasisi hizi inachangia Bodi za ushauri kukosa mamlaka ya kisheria katika kuwasimamia na kuwawajibisha watendaji wake.

**Mheshimiwa Spika,** changamoto hiyo pia, imezifanya taasisi hizo kushindwa kubuni vyanzo mbadala vya mapato hivyo kudumaa na kuendelea kutegemea ruzuku ya Serikali katika utekelezaji wa miradi, mishahara na fedha za kujiendesha. Kamati imebaini kuwa taasisi hizi zina utajiri wa mali (assets) ambazo hazijatumika ipasavyo ili kuzalisha mapato ya taasisi na kupunguza utegemezi kwa Serikali. Pamoja na mali hizo, Taasisi kama TEMESA na TBA zinatoa huduma kwa taasisi za Umma na binafsi lakini zinadai malipo ya huduma hizo kwa muda mrefu na hazina mpango madhubuti katika kukusanya madeni hayo. Kamati inaona kuwa ni wakati sahihi wa kubadili muundo wa taasisi hizi kwa ajili ya kuongeza uwajibaki, ufanisi na tija katika utekelezaji wa majukumu yao.

### f) Hali ya Vivuko Nchini

**Mheshimiwa Spika,** Kamati imefanya uchambuzi wa hali ya vivuko na kubaini kuwa vivuko vingi nchini ni vya muda mrefu hivyo kukabiliwa na hali ya uchakavu na ubovu wa mitambo. Hali hii imesababisha kuwa na huduma duni ya usafiri kwa wananchi wanaotegemea kutumia vivuko hivyo.

**Mheshimiwa Spika,** ili kukabiliana na hali hiyo, Serikali imechukua hatua ya ununuzi na ukarabati wa vivuko katika maeneo mbalimbali nchini. Hata hivyo, Kamati imebaini kuwa utekelezaji wa hatua hiyo umekuwa ukichukua muda mrefu kiasi cha kuwakatisha tamaa wananchi wanaotegemea huduma kupitia vivuko hivyo.

**Mheshimiwa Spika,** katika mwaka wa fedha 2025/2026, Serikali imefanikiwa kukamlisha ujenzi wa Kivuko kimoja pekee cha Kisorya – Rugezi kati ya vivuko 5 ambavyo vilitakiwa kununuliwa. Aidha, katika vivuko 7 vilivyokuwa vinakarabatiwa hakuna hata kimoja kilichokamilika. Mathalani, kivuko cha Mafia-Nyamsati kilichofikia **asilimia 57,** ujenzi wake umechukua muda mrefu na kuwafanya wananchi wa Kisiwa cha Mafia kulalamikia kuwa Serikali imewasahau. Vilevile, Kivuko cha Mv- Kigamboni kimechukua muda mrefu kukamilika na kuanza kazi kwa ajili ya kutoa huduma katika jiji la Dar Es Salaam.

## SEHEMU YA TATU

## 3.0 UCHAMBUZI WA MPANGO NA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA 2026/2027

### 3.1 Mpango na Vipaumbele vya Wizara

**Mheshimiwa Spika,** katika mwaka wa fedha 2026/2027, Wizara ya Ujenzi **(Fungu 98)** itatekeleza vipaumbele na majukumu yake kwa kuzingatia Dira ya Maendeleo ya Taifa, 2050, Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi 2025-2030 pamoja na Mpango wa Nne wa Mendeleo wa Taifa (FYDP IV).

**Mheshimiwa Spika,** bajeti inayoombwa na Wizara ina lengo la kutekeleza vipaumbele mbalimbali vya Wizara ikiwemo vifuatavyo: -

(a) Kuendelea na ujenzi wa barabara na kupunguza msongamano hususan katika majiji ya Dar es Salaam, Arusha, Mwanza, Mbeya, Dodoma na katika miji inayokua kwa kasi;

(b) Kuendelea na ujenzi wa barabara zinazoelekea katika maeneo ya kimkakati kwa ajili ya shughuli za kiuchumi na kijamii;

(c) Kuendelea na Ujenzi wa barabara zinazounganisha makao makuu ya mikoa na zinazounganisha Tanzania na nchi jirani kwa kiwango cha lami;

(d) Kuendelea na ukarabati na matengenezo makubwa ya barabara kuu, za mikoa na za maeneo yenye changamoto ya ufikaji;

(e) Kuendelea na kuimarisha usafiri na miundombinu ya vivuko ili kuunganisha maeneo ya nchi kavu ambayo yametenganishwa na maji katika maeneo ya bahari, maziwa na mito;

(f) Kuendelea na miradi yenye lengo la kuzuia uharibifu wa barabara na kuimarisha usalama barabarani;

(g) Kuendelea kuwajengea uwezo wataalam na makandarasi wa ndani katika sekta ya ujenzi nchini;

(h) Kuendelea na ukamilishaji wa ujenzi wa viwanja vya ndege vilivyokasimiwa Wizara ya Ujenzi;

(i) Kuendelea na ujenzi wa majengo ya Serikali na nyumba za watumishi ili kuimarisha miundombinu ya majengo ya Serikali na pia kuwa na makazi ya watumishi kwa gharama nafuu; na

(j) Mapitio ya sera, miongozo na kanuni ili ziendane na mabadiliko ya teknolojia na maendeleo endelevu ili kuhakikisha mfumo wa sera na kanuni unaendana na wakati.

**3.2 Makadirio ya Mapato**

**Mheshimiwa Spika,** katika mwaka wa fedha 2026/2027, Wizara imepanga kukusanya jumla ya **Shilingi 87,001,000/=** sawa na ongezeko la **asilimia 2.35** ukilinganisha mwaka wa fedha 2025/2026. Mapato hayo yatakusanywa kupitia usajili wa magari mapya ya Serikali, uthamini wa magari ya Serikali yanayouzwa pamoja na uuzaji wa machapisho yanayohusu usalama barabarani.

**3.3 Makadirio ya Matumizi**

**Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2026/2027, Wizara ya Ujenzi **(Fungu 98)** inaomba kuidhinishiwa jumla ya **Shilingi 2,564,441,414,000/=** sawa na ongezezo la asilimia 34.71 ukilinganisha na bajeti ya mwaka wa fedha 2025/2026. **Kielelezo Na. 4** kinaonesha ulinganisho wa makadirio ya matumizi kwa bajeti ya mwaka wa fedha 2025/2026 na bajeti ya mwaka wa fedha 2026/2027.

**Kielelezo Na. 4: Ulinganisho wa Makadirio ya Matumizi kwa Bajeti ya Mwaka 2025/2026/ na 2026/2027**

| FUNGU98-WIZARA YA UJENZI | MWAKA WA FEDHA 2025/2026 (SHILINGI) | MWAKA WA FEDHA 2026/2027 (SHILINGI) | TOFAUTI ASILIMIA (%) |
|---|---|---|---|
| Matumizi ya Kawaida | 90,468,270,000.00 | 97,104,935,000.00 | +7.34 |
| Bajeti ya Maendeleo | 1,813,190,934,000.00 | 2,467,336,479,000.00 | +36.08 |
| **JUMLA KUU** | **1,903,659,204,000.00** | **2,564,441,414,000.00** | **+34.71** |

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inaipongeza Serikali kwani ongezeko hilo litaiwezesha Wizara kutekeleza vipaumbele vyake kwa ufanisi. Aidha, Wizara ihakikishe inajielekeza katika kutekeleza vipaumbele vyake katika Bajeti na kupata tija iliyokusudiwa.

### 3.3.1 Matumizi ya Kawaida

**Mheshimiwa Spika,** katika mwaka wa Fedha 2026/2027, Wizara ya Ujenzi inaomba kuidhinishwa **Shilingi 97,104,935,000/=** kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida. Kati ya fedha hizo, **Shilingi 97,104,935,000/=** ni kwa ajili ya Mishahara (P.E.) na **Shilingi 4,895,717,000/=** ni kwa ajili ya Matumizi Mengineyo (O.C.).

**Mheshimiwa Spika,** bajeti ya matumizi ya kawaida inayoombwa ni sawa na ongezekeko la **asilimia 7.34** ukilinganisha na bajeti kama hiyo kwa mwaka wa fedha 2025/2026 kama ambavyo **Kielelezo Na. 5** kinaonesha.

**Kielelezo Na. 5: Ulinganisho wa Makadirio ya Matumizi ya Kawaida kwa Bajeti ya Mwaka 2025/2026 na 2026/2027**

| FUNGU98 - WIZARA YA UJENZI | MWAKA WA FEDHA 2025/2026 (SHILINGI) | MWAKA WA FEDHA 2026/2027 (SHILINGI) | TOFAUTI ASILIMIA (%) |
|---|---|---|---|
| Mishahara (P.E) | 85,028,585,000.00 | 92,209,218,000.00 | +8.44 |
| Matumizi Mengineyo (O.C) | 5,439,685,000.00 | 4,895,717,000.00 | -10.00 |
| **JUMLA KUU** | **90,468,270,000.00** | **97,104,935,000.00** | **+7.34** |

**Mheshimiwa Spika,** Kielelezo Na. 4 hapo juu kinaonesha kuwa fedha za Mishahara ya Watumishi (P.E) katika mwaka wa fedha 2026/2027 zimeongezeka kwa **asilimia 8.44** ukilinganisha na mwaka wa fedha 2025/2026. Ongezeko hili limechangiwa na uamuzi wa Serikali kutoa ajira za kudumu kwa wafanyakazi wa mikataba wa TANROADS.

**Mheshimiwa Spika,** kwa upande wa fedha za matumizi mengineyo (O.C) kiwango hicho kimeshuka kwa **asilimia 10** katika mwaka wa fedha 2026/2027 kulinganisha na mwaka 2025/2026. Hii imetokana na uamuzi wa Serikali kupunguza matumizi yasiyo yalazima na kupeleka fedha kwenye shughuli zenye tija zaidi katika kuhudumia wananchi.

### 3.3.2 Bajeti ya Maendeleo

**Mheshimiwa Spika,** katika mwaka wa fedha 2026/2027, Wizara inaomba kuidhinishiwa **Shilingi 2,467,336,479,000/=** kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo. Fedha inayoombwa ni sawa na ongezeko la **asilimia 36.08** ukilinganisha na bajeti ya maendeleo kwa mwaka wa fedha 2025/2026 kama inavyoonekana katika **Kielelezo Na. 6.**

**Kielelezo Na. 6: Ulinganisho wa Bajeti ya Maendeleo kwa Bajeti ya Mwaka 2025/2026 na 2026/2027**

| Matumizi | Chanzo | Mwaka wa Fedha 2025/2026 (Shilingi) | Mwaka wa Fedha 2026/2027 (Shilingi) | Tofauti Asilimia (%) |
|---|---|---|---|---|
| Ndani | Mfuko Mkuu | 520,466,647,000.00 | 497,466,647,000.00 | -4.42 |
| | Mfuko wa Barabara | 688,756,470,000.00 | 1,047,405,500,000.00 | +52.14 |
| Jumla (A) | | 1,209,223,117,000.00 | 1,544,872,147,000.00 | +27.76 |
| | | | | |
| Nje | Jumla (B) | 603,967,817,000.00 | 922,464,332,000.00 | +52.73 |
| **JUMLA KUU (A+B)** | | **1,813,190,934,000.00** | **2,467,336,479,000.00** | **36.08** |

**Mheshimiwa Spika,** Kamati imefanya tathmini ya kina kwa Bajeti ya Maendeleo kwa mwaka wa fedha 2026/2027 kulinganisha na mwaka unaoisha na kupata matokeo yafuatayo:-

(i) Fedha za kugharamia Miradi ya Maendeleo zimeongezeka kwa **asilimia 36.08** hali inayoonesha dhamira ya Serikali ya kuhakikisha kuwa sekta ya Ujenzi nchini inaboreshwa ili kuchangia katika pato la Taifa na kuleta ustawi kwa wananchi; na

(ii) Fedha za kugharamia maboresho na ukarabati wa barabara nchini kupitia Mfuko wa Barabara zimeongezeka kwa **asilimia 52.14.** Hata hivyo, Kamati imebaini kuwa, mara nyingi mwenendo wa upatikanaji wa fedha hizi sio wa kuridhisha. Kwa mfano, hadi kufikia robo tatu ya utekelezaji wa bajeti katika mwaka wa fedha 2024/25 na 2025/26, fedha hizo zilipatikana kwa **asilimia 35.37** na **asilimia 42.66** mtawalia ya bajeti iliyokuwa imeidhinishwa na Bunge.

**Mheshimiwa Spika,** kufuatia mwenendo huu, Kamati inaitaka Serikali kulihakikishia Bunge lako Tukufu kuhusu upatikanaji wa

fedha za Mfuko wa Barabara kama zitakavyoidhinishwa. Kamati ina maoni kuwa, upatikanaji usioridhisha wa Fedha za Mfuko wa Barabara unachangia ufanisi mdogo katika matengenezo na ukarabati wa miundombinu ya barabara na madaraja nchini.

## SEHEMU YA NNE

## 4.0 MAONI NA USHAURI WA KAMATI

**Mheshimiwa Spika,** baada ya uchambuzi wa kina kuhusu Utekelezaji wa Bajeti pamoja na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Ujenzi **(Fungu 98)** kwa mwaka wa fedha 2026/2027, sasa naomba kuwasilisha maoni na ushauri wa Kamati kama ifuatavyo:-

### 4.1 Maoni ya Jumla

(a) Serikali isimamie kikamilifu miradi inayotekelezwa na Wizara hii ili iweze kukamilika kwa wakati na kwa kuzingatia ubora pamoja na thamani ya fedha;

(b) Wizara ya ujenzi ibuni vyanzo vya mapato na kuweka mikakati itakayoongeza ufanisi katika ukusanyaji wake ili kuifanya Wizara ya Ujenzi na taasisi zake kupunguza utegemezi wa ruzuku kutoka mfuko mkuu wa Serikali;

(c) Serikali ihakikishe kuwa taasisi zilizo chini ya Wizara ya Ujenzi zinatoa huduma bora kwa wadau wa sekta ya ujenzi nchini hivyo kuchangia katika kuleta ustawi wa maisha ya wananchi; na

(d) Serikali iongeze ubunifu na matumizi ya teknolojia kwenye sekta ya ujenzi nchini kwa ajili ya kuendelea kuchochea maendeleo ya uchumi wa kisasa, kuzalisha ajira kwa vijana nchini na kufikia malengo yaliyowekwa katika Dira ya Taifa ya Maendeleo ya 2050.

## 4.2 Maoni Mahsusi

### (a) Mapato ya Bodi ya Mfuko wa Barabara

Kamati inashauri kuwa, Serikali:-

(i) Ihakikishe inahamisha fedha zote kwenda kwenye akaunti ya Mfuko wa Barabara kama zilivyoidhinishwa na Bunge ili kutekeleza miradi ya matengenezo na ukarabati wa barabara na madaraja nchini; na

(ii) Isitishe mara moja mpango wake wa kupunguza **asilimia 5** ya fedha za mfuko wa barabara kwa ajili ya kuzihamishia katika shughuli zingine kwa sababu mpango huo utazorotesha Maendeleo ya Sekta ya barabara nchini. Aidha, Mpango huo ukitekelezwa ni wazi kuwa utakuwa unavunja Sheria kwani fedha hizi zinalindwa kwa mujibu wa Sheria (Ring-fenced); na

(iii) Bodi ya Mfuko wa Barabara ibuni vyanzo vipya vya mapato kwa ajili kuuwezesha Mfuko huo kuhudumia Matengenezo na Ukarabati wa miundombinu ya barabara na madaraja nchini. Aidha, Serikali ifanye tathmini ya kina kuhusu kuweka Tozo Maalumu ya Maendeleo ya Miundombinu ya Barabara katika Mapato ghafi ya Madini, Vibali vya Ujenzi, Muda wa Maongezi kwenye sekta ya Mawasiliano pamoja na kulipia daraja la Tanzanite kwa watumiaji wa daraja hilo.

### (b) Kukamilisha Miradi ya Zamani ya Barabara [Miradi Viporo]

Kamati inashauri kuwa, Serikali

(i) Iweke kipaumbele na kuongeza kasi katika kukamilisha miradi yote ya zamani (miradi viporo) ya ujenzi wa barabara na madaraja nchini ili kuchochea uchumi na kupata tija iliyokusudiwa;

(ii) Ipitie na kufanya upya mgawanyo wa fedha katika miradi hiyo kwa kutoa kipaumbele katika miradi viporo ili ikamilike na kuleta tija iliyokusudiwa; na

(iii) Kufanya Ukaguzi Maalumu kupitia kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) kwenye Miradi yote ya Ujenzi wa Barabara na Madaraja iliyochukua muda mrefu kwa ajili kujiridhisha na matumizi ya fedha za Umma katika miradi hiyo.

**(c) Madeni ya Makandarasi na Wahandisi Washauri**

Kamati inaishauri kuwa, Serikali:-

(i) Kuweka kipaumbele katika kulipa madai ya Makandarasi na Wahandisi Washauri ili iatakayopunguza gharama ya miradi hiyo inayotokana na riba ya ucheleweshaji wa malipo katika miradi kwenye sekta ya ujenzi; na

(ii) Ifanye uhakiki kuhusu madeni ya nyuma ya Makandarasi katika sekta ya ujenzi na kulipwa na Wizara ya Fedha (Hazina) ili bajeti ya maendeleo ya Wizara ya Ujenzi itekeleze majukumna vipaumbele vyake kama itakavyoidhinishwa na Bunge.

**(d) Hali ya Miundombinu ya Barabara na Madaraja Nchini**

Kamati inashauri kuwa, Serikali:-

(i) Ichukue hatua za haraka za kuhuisha barabara zinazopita katika shoroba za kiuchumi ambazo zimefikia mwisho wa uhai wake (end of life design) kwa sababu barabara hizi zina mchango mkubwa katika kukuza uchumi na kuongeza pato la Taifa;

(ii) Ifanye tathmini ya kina ya kubainisha barabara na madaraja ya kipaumbele yaliyo katika hali haya na kuandaa mpango wa kudumu katika kuboresha na kukarabati miundombinu hiyo; na

(iii) Ifanye upembuzi yakinifu na usanifu na kupata gharama halisi kwa ajili ya kuivutia na kuingia ubia na sekta binafsi (PPP) kwenye ujenzi na uendeshaji wa miundombinu ya barabara na madaraja nchi. Aidha, upanuzi wa barabara ya Dar Es Salaam – Chalinze – Morogoro na ile ya Tanga – Handeni – Kibrashi ziingizwe katika utekelezaji kwa njia ya PPP kwani TPA na NSSF wameonesha nia ya kuzijenga.

**(e) Malipo ya Fidia kwa Wananchi waliopisha miradi ya Maendeleo katika Sekta ya Ujenzi Nchini**

Kamati inashauri kuwa, Serikali:-

(i) Iongeze kasi katika kulipa wananchi ambao maeneo yao yametwaliwa kwa mujibu wa Sheria kwa ajili miradi ya barabara, viwanja vya ndege na vituo vya mabasi ili waweze kutafuta mahali pengine pa makazi na kuendelea na shughuli za kiuchumi;

(ii) Ifanye tathmini ya kina kuhusu maeneo ambayo yanayohitajika na inayoweza kulipa kwa sasa ikiwa ni pamoja na kuangalia uwezekano wa kurejesha baadhi ya maeneo kwa wananchi ili waweze kuyatumia katika shughuli za kiuchumi; na

(iii) Isizalishe madai mapya kwa kutwaa maeneo bila kuwa na fedha za kulipa fidia kwa wananchi ambao ardhi yao itachukuliwa kwa ajili miradi ya maendeleo ya sekta ya ujenzi nchini

**(f) Muundo wa Taasisi za TANROADS, TEMESA na TBA**

Kamati inashauri kuwa, Serikali:-

(i) Iandae na kuleta Bungeni Mabadiliko ya Sheria ya muundo wa taasisi hizi kutoka kuwa Wakala na kuwa Mamlaka ili kuongeza ufanisi na uwajibikaji katika utekelezaji wa majukumu yao;

(ii) Iongeze usimamizi kwa taasisi hizi ili ziweze kubuni vyanzo vya mapato kupitia mali zake (assets) kwani taasisi zina mali nyingi ambazo hazitumiki katika kuzalisha mapato; na

(iii) Ihakikishe taasisi hizi hasa TEMESA na TBA zinakusanya madeni kutokana na huduma ambazo wanazitoa kwa taasisi za umma na binafsi.

**(g) Hali ya Vivuko Nchini**

Kamati inashauri kuwa, Serikali:-

(i) Iongeze kasi katika kukamilisha miradi yote ya ununuzi na ukarabati wa vivuko nchini ili wananchi wapate huduma bora ya usafiri kupitia vivuko hivyo; na

(ii) Ihakikishe Ununuzi wa Vivuko vya Nyamisati– Mafia na Mv Kigamboni pamoja na Ukarabati wa Kivuko cha Mv Pangani II unakamilika kufikia tarehe 30 Juni, 2027 kwa ajili ya kutoa huduma kwa wananchi wanaotegemea vivuko hivyo. Aidha, Serikali ikamilishe vivuko vilivyopo Mwanza kwa Mkandarasi Songoro Marine.

## SEHEMU YA TANO

## 5.0 HITIMISHO

### 5.1 Shukrani

**Mheshimiwa Spika,** kwa namna ya kipekee naendelea kukushukuru wewe binafsi kwa kuendelea kuliongoza vyema Bunge letu na kwa maelekezo yako ambayo yamekuwa msaada mkubwa katika uendeshaji bora wa shughuli za kila siku za Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu. Aidha, namshukuru Naibu Spika, kwa namna anavyokusaidia kutekeleza majukumu yako, pamoja na Wenyeviti wa Bunge kwa kukusaidia kuendesha vikao vya Bunge kwa Ufanisi.

**Mheshimiwa Spika,** kwa moyo wa dhati kabisa, niwashukuru sana Wajumbe wote wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu

ambao wamekuwa mstari wa mbele katika kuendelea kuisimamia Wizara ya Ujenzi pamoja na taasisi zilizo chini yake kwa niaba ya Bunge lako tukufu. Kwa hakika, maoni, ushauri na mapendekezo yao vina mchango mkubwa katika kuboresha utendaji wa Serikali. Naomba niwatambue Wajumbe hao ili majina yao yaingie katika Kumbukumbu za Taarifa Rasmi za Bunge *(Hansard)* kama ifuatavyo: -

| | |
|---|---|
| 1. Mhe. Moshi Selemani Kakoso, Mb. | **Mwenyekiti** |
| 2. Mhe. Abubakar Damian Asenga, Mb. | **Makamu** |
| 3. Mhe. Kapt. Said Hassan Ali Mwinyi, Mb. | Mjumbe |
| 4. Mhe. Condester Michael Sichalwe, Mb. | Mjumbe |
| 5. Mhe. Anne Kilango Malecela, Mb, | Mjumbe |
| 6. Mhe. Ahmed Mabkhut Shabiby, Mb. | Mjumbe |
| 7. Mhe. Nuru Issa Kashakari, Mb. | Mjumbe |
| 8. Mhe. Prof. Joyce Lazaro Ndalichako, Mb. | Mjumbe |
| 9. Mhe. Isack Joseph Copriano, Mb. | Mjumbe |
| 10. Mhe. Eng. Johnston J. Mutasingwa, Mb. | Mjumbe |
| 11. Mhe. Sara Msafiri Ally, Mb. | Mjumbe |
| 12. Mhe. John Stephano Luhende, Mb. | Mjumbe |
| 13. Mhe. Ibrahim Mohamed Shayo, Mb. | Mjumbe |
| 14. Mhe. Kellen Rose Rwakatare, Mb. | Mjumbe |
| 15. Mhe. Fatma Ally Rembo, Mb. | Mjumbe |
| 16. Mhe. Saidi Salim Hamad, Mb. | Mjumbe |
| 17. Mhe. Mgore Miraji Kigera, Mb. | Mjumbe |
| 18. Mhe. Hija Hassan Hija, Mb. | Mjumbe |
| 19. Mhe. Nabil Ahmed Abdallah, Mb. | Mjumbe |
| 20. Mhe. Hamis Mwagao Tabasamu, Mb. | Mjumbe |
| 21. Mhe. Abdulaziz Mohamed Abdood, Mb. | Mjumbe |
| 22. Mhe. Said Ally Mbarouk, Mb. | Mjumbe |
| 23. Mhe. Mariam Said Khamis, Mb | Mjumbe |

**Mheshimiwa Spika,** naomba nitumie fursa hii kumshukuru Waziri wa Ujenzi, Mhe. Abdallah Hamis Ulega, (Mb) kwa ushirikiano ambao ameipatia Kamati katika kipindi chote cha Utekelezaji wa Majukumu ya Kamati akisaidiwa na Naibu Waziri wa Ujenzi, Mhe. Mhandisi Godfrey Msongwe Kasekenya (Mb).

Aidha, niwashukuru watendaji wote wa Wizara ya Ujenzi pamoja na taasisi zake chini ya uongozi wa Katibu Mkuu wa Wizara hiyo, Balozi Mhandisi Aisha Amour. Kamati inatambua mchango wa watendaji hao katika maendeleo ya Sekta ya Ujenzi na inaendelea kuwatia moyo kwenye utekelezaji wa majukumu yao katika ujenzi wa Taifa.

**Mheshimiwa Spika,** mwisho lakini sio kwa umuhimu, nawashukuru sana watendaji wote wa Ofisi ya Bunge chini ya uongozi wa Katibu wa Bunge, Bw. Baraka I. Leonard kwa kuisaidia Kamati kutekeleza majukumu yake hadi kukamilika kwa Taarifa hii.

**5.2 Msimamo wa Kamati Kuhusu Hoja**

**Mheshimiwa Spika,** baada ya maelezo hayo, naomba Bunge lako likubali kupokea na kupitisha makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara ya Ujenzi **(Fungu 98)** kwa mwaka wa fedha 2026/2027 kama yalivyowasilishwa na mtoa hoja.

**Mheshimiwa Spika,** naomba kuwasilisha na ninaunga mkono hoja.

Moshi Selemani Kakoso, Mb.
**MWENYEKITI**
**Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu**
20 Mei, 2026

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mwenyekiti, Mheshimiwa Selemani Kakoso.

Waheshimiwa Wabunge, tunaanza uchangiaji, na tutachangia kwa dakika nane nane kwa kuanzia. Tuna wachangiaji 40 mpaka jioni ya leo. Ninamwita Mheshimiwa George Boniface Simbachawene, atafuatiwa na Mheshimiwa Nape Moses Mnauye. Mheshimiwa Timoth Geofrey Anyosisye, ajiandae.

**MHE. GEORGE B. SIMBACHAWENE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaanza kukushukuru kwa kunipa nafasi, ili na mimi niweze kuchangia hoja iliyowekwa mbele yetu na Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, ambayo ni ya Bajeti ya Wizara ya Ujenzi ya mwaka 2026/2027. Kabla kabisa ya kwenda kusema chochote, ninaunga mkono hoja hii kwa asilimia mia kwa mia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninampongeza sana Mheshimiwa Waziri, ndugu yangu Mheshimiwa Ulega; Naibu Waziri, Mheshimiwa Kasekenya, na timu nzima ya Wizara ya Ujenzi. Kwa upande wa watendaji, ninafahamu yuko dada yangu Ndugu Aisha na Ndugu yangu wa karibu Msonde, pamoja na watumishi wote, mnafanya kazi nzuri kwa nchi yetu. Hongereni sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa namna ya pekee kabisa ninamshukuru sana Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, mbeba maono ya Watanzania, kwa utashi wake wa kisiasa, kwa utashi wake wa kuamua kuijenga Dodoma kwa dhana ile ile ya waasisi wa nchi hii iliyofanyika mwaka 1973 ilipoamriwa kwamba, Dodoma iwe Makao Makuu na baadaye tukatunga Sheria ya Bunge hapa ya *The Dodoma Capital City Declaration Act* ya Mwaka 2018, wakati wa Awamu ya Tano na kuamua kutekeleza ujenzi wa Makao Makuu ya Dodoma kwa vitendo. Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan naye amekuwa na utashi huo huo na ameamua kufanya zaidi hata ya watangulizi wake. Tumpongeze sana Mheshimiwa Rais. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi Dodoma tunasema msemo ambao ametufundisha Mkuu wetu wa Mkoa, Rosemary Senyamule kwamba, Dodoma ni fahari ya Watanzania. Nataka niseme Dodoma ni ya sote. Dodoma tumeamua kuwa ni Makao Makuu ya nchi yetu. Dodoma ni ya kila mmoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kumetokea minong'ono, kumetokea maneno hapa kwamba, Dodoma inapendelewa kwa kupewa fedha nyingi. Tulipotunga Sheria hii ya Bunge Mwaka 2018 tuliipa Dodoma hadhi maalumu, na kwa hiyo, Tanzania

kama zilivyo nchi nyingine, badala ya kusema Kenya, unaweza ukasema tu Nairobi, umemaanisha Kenya; badala ya kusema Uganda unaweza ukasema Kampala, umeitaja Uganda na hata Tanzania inatajwa kwa kuitaja Dodoma. Ni lazima iwe na vipaumbele vya kipekee ukilinganisha na maeneo mengine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kazi kubwa inayofanywa na Serikali ya Awamu ya Sita katika kuijenga Dodoma, haitasahaulika, ni ya kutukuka na historia itaandikwa. Ninawapongeza Mheshimiwa Waziri na timu yake kwa kazi wanayoifanya kutekeleza maono ya Mheshimiwa Rais. Mheshimiwa Waziri amesema hapa kwamba, uko ujenzi wa barabara ya mzunguko, kilometa 112.3, ambao unagharimu shilingi bilioni 221.7. Barabara hiyo inakamilika, inamaliziwamaliziwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika yote yaliyonifurahisha, Mheshimiwa Waziri na timu yake ya wataalamu, ni *design* ya *exchange* ya Mtumba pale, ule Mji wa Magufuli. Kama mmeiona picha yake kwa kweli, inafurahisha sana. Ni *exchange* ambayo nafikiri Afrika Mashariki na Kati hakuna kama ile. Ni zaidi ya ile ya Ubungo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ninasema, sisi Wagogo Mwenyezi Mungu ametubarikia kuwa katikati. Ukatikati aliotupatia, maana yake ni tuna raha. Raha yenyewe ndiyo hii ya ujenzi wa Makao Makuu Dodoma, ili mbaki kuwa salama kama nchi, na maamuzi yalifanyika kwa sababu ya ukatikati. Ukiwa katikati unakuwa salama kabisa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, bado Dodoma barabara zinatanuliwa. Barabara ya kutoka Dodoma kwenda Morogoro kilometa takribani 70, lakini wanaanza na njia sita. Dodoma itaonekana tofauti sana, lakini ya Iringa pia inatanuliwa njia nne, ya Arusha inatanuliwa njia nne. Kwa kweli katikati panafurahisha. Dodoma kuwa katikati, nchi yetu inabaki kuwa salama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, haya yote yakifanyika na kwa picha ya maono ya Rais wetu, Dodoma itakuwa ni ya tofauti sana

na miji mingine. Iko barabara ya mzunguko wa ndani, itajengwa, itapita katika maeneo ya Ntyuka na kuunganisha maeneo ya ndani, lakini pia, iko Barabara ya Mji wa Serikali, iko Ikulu kule, mambo yanafanyika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, angalia uwekezaji uliofanyika katika Muhimili wa Mahakama. Angalia viwanja vya ndege; kiwanja cha ndege kimekaribia 85% na kimegharimu takribani shilingi bilioni 159. Kiwanja cha ndege kile kinaileta Dodoma kuwa ya Kimataifa, kuwa *international destination in tourism* katika mambo yote ya kiuchumi. Kwa hiyo, sisi watu wa Dodoma tunasema kuwa katikati pametubeba na panatusaidia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa ujumla uwekezaji wa majengo wa Mji wa Serikali na uwekezaji wa Taasisi za Serikali kwa ujumla umewekezwa Dodoma kwa muda wa miaka nane, shilingi trilioni 1.16 ni fedha nyingi. Nchi yetu hii ni kubwa, ninajua kila mahali mngependa yafanyike mambo, lakini haya yanayofanywa kwa Dodoma ni kwa sababu ya umaalumu wake. Hata mnaostaafu, hata Wabunge mkikosa Ubunge, mimi ninaamini wengi mtabaki Dodoma. Iombeeni Dodoma iendelee kujengwa na maono ya Rais yatekelezwe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa nimezungumzia Barabara za *TANROADS* tu, sijazungumzia *TARURA* ambayo uwekezaji kwa miaka sita tu ni shilingi bilioni 139. Fedha hizi zinazotolewa kwa umaalumu kwa Dodoma ni nyingi sana. Ni lazima sasa nishauri jambo hapa, kwamba, lazima kuwe kuna *coordination* ya kisekta katika uendelezaji wa Mji wa Dodoma. Ni lazima sekta zote zizungumze. Kwa hali inavyoendelea, katika mipango miji na katika maendeleo ya makazi kidogo kuna mambo hayako sawa. Kuna tu-viwanja tunapimwa twa *square meter* 300, 400. Hivi viwanja siyo vya Mji kama wa Dodoma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna *squatter* zinaanza kuongezeka. Tusiende huko, tujitahidi sana kusimamia. Hili linawezekana kama sekta zote zitashirikiana. Uwekezaji huu ni mkubwa na ni lazima uakisi uhalisia wa *future generation*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ombi lingine, Waziri alikuja Mpwapwa na Waziri Mkuu amekuja Mpwapwa, Barabara ya kutoka *Kongwa Junction* – Mpwapwa – Kibakwe mpaka Chipogoro, tumezungumza, tumekubaliana na Wizara ya Fedha tumekubaliana, ninaomba tusimamie msimamo huo. Mimi na mwenzangu Mheshimiwa Malima tunashirikiana kwenda kwa Waziri kila siku. Tunaamini ahadi yake haitakwenda bure, na watu wa Mpwapwa watafurahi, ili na wao waweze kuona lami tangu tupate uhuru.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MHE. GEORGE B. SIMBACHAWENE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, namalizia, mwisho.

**MWENYEKITI:** Malizia, dakika moja.

**MHE. GEORGE B. SIMBACHAWENE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Bunge hili la Kumi na Tatu ni la wasomi. Bunge hili ndilo linalobeba mawazo ya sasa na ya kizazi kinachokuja. Ninapenda kuchukua nafasi hii kwa dhati ya moyo wangu, kwa uzoefu nilionao wa kukaa kwenye Mabunge matano, vijana hawa wapewe nafasi ya kutoa mawazo yao, wana michango mizuri, ni wasomi. Kila mmoja ukitafiti *CV* yake imeshiba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vijana hawa mawazo yao yasikilizwe, wana maoni mazuri, na mimi nimesimama ku-*endorse* tu kwamba, kwa kweli ninatambua michango yenu. Ni Wabunge wa kisasa, mnafaa kuwaandalia *future generation* Tanzania yao inayokuja. Hongera sana kwa Wizara ya Ujenzi, sisi tuko pamoja na ninyi. Hongera sana kwa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsanteni sana kwa kunisikiliza. Naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Nilimwita Mheshimiwa Nape Moses Nnauye, atafuatia na Mheshimiwa Timoth George Anyosisye. Mheshimiwa Timotheo Paul Mnzava ajiandae.

**MHE. NAPE M. NNAUYE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru sana kwa kunipa nafasi. Ninaanza kwa kufikisha salamu za wakulima wa korosho kwa Rais, Mheshimiwa Dkt. Samia kwa namna ambavyo ametusaidia kuliinua zao la korosho kwa mikoa yetu ambalo limesababisha msimu tuliomaliza wa mwaka 2025, tumechangia zaidi ya Dola za Kimarekani milioni 580 kwenye pato la Taifa la nchi hii. Mheshimiwa Rais wakulima wa korosho wanakushukuru sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, ninamshukuru sana kwa uwekezaji ambao umefanyika kwenye Mikoa ya Lindi na Mtwara. Sisi wananchi wa Lindi na Mtwara tunatambua kazi kubwa aliyoifanya katika kukamilisha mazungumzo na hivyo kuelekea kwenye uwekezaji wa mradi mkubwa wa gesi Kusini, ambao utagharimu zaidi ya Dola za Kimarekani bilioni 42, zaidi ya shilingi trilioni 100 na kitu. Ni mradi mkubwa sana. Mheshimiwa Rais Watu wa Kusini tunakushukuru sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukienda Kilwa, kuna mradi mkubwa pale unakamilika wa ujenzi wa bandari ya uvuvi ambao nao unachukua karibu shilingi bilioni 200 na kitu. Wananchi wa Kusini wamenituma nilete shukrani zao kwa Serikali ya Awamu ya Sita, lakini pia, kwa Mheshimiwa Rais Samia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi wa Mtama, Lindi, Mtwara na Mikoa ya Kusini tunaotumia Barabara ya Dar es Salaam – Kibiti – Lindi – Mtwara wamenituma kuja kuangalia hii bajeti. Wameniagiza, nisipoona fedha zilizotengwa kwa ajili ya ujenzi wa barabara hii nisiunge mkono bajeti hii, niipinge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba Mungu anisaidie nizungumze hili kwa uvumilivu sana. Nimeangalia randama, na bajeti ni randama. Nimeipitia mara nne, na wakati kaka yangu Mheshimiwa Simbachawene anazungumza hapa, mpaka nimesikia wivu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara hii ni katika zinazounganisha mikoa, ambayo ni mbovu kuliko barabara yoyote katika nchi hii. Mbovu kabisa, muda wake wa kutumika

umeisha, wamezibaziba mpaka haiwezekani kuzibaziba tena, lakini ni huku ambako nimeitaja miradi. Kwanza mchango wa korosho kwenye uchumi wa nchi yetu hauna mfano wake, lakini barabara hii haikutengewa fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikiunga mkono bajeti hii nitakuwa nawasaliti wananchi wa Kusini, nitakuwa nasaliti Ilani ya Uchaguzi ya Chama change, na kwa hiyo, ninatangaza wazi kabisa, siungi mkono bajeti hii mpaka fedha itengwe kwenye hii barabara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumetenga fedha kwenye barabara nyingine zote na nyingine ambazo kwa kweli, bado zinapitika, kasoro hii barabara. Hivi leo ile Bandari ya Kilwa wale samaki wanapitia wapi? Tunataka kuhujumu ule mradi? Huo mradi wa gesi, vifaa na watu, wanapitia wapi kwa ubovu wa hii barabara? Hiyo korosho inapitia wapi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, mdogo wangu Mheshimiwa Ulega, ninampenda, ninamthamini, lakini kwenye hili ninashindwa kuwasaliti wananchi wa Lindi na Mtwara. Nikipitisha bajeti hii mimi nitakuwa msaliti. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaiomba sana Serikali, wakitaka nikubali bajeti hii, ipitie iweke fedha, tuanze hata kidogo basi, hata kilomita tano basi, tuonekane tumeanza. Mheshimiwa Waziri amesema vizuri hapa, hii ndiyo bajeti ya kwanza ya utekelezaji wa Ilani ya Miaka Mitano. Hii barabara imewekwa kwenye Ilani ya Uchaguzi, Rais alipokuja ametuahidi kuijenga upya. Tusipoanza nayo mwaka wa kwanza, tunadanganyana. Hili jambo siungi mkono na nitashika shilingi mpaka tufike mahali. Tengeni fedha tuanze safari ya ujenzi wa barabara hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuunga mkono ni kuwasaliti wananchi, na mimi nina matumaini Wabunge wa Kusini watasimama na mimi kwenye hili. Fedha itengwe kwenye hii barabara ili tuelewane hapa. Vinginevyo kutupeleka kwenye hati fungani ni changa la macho. Imefanyika kwenye *EPC+F* ikashindikana. Tusibadilishe majina, tengeni fedha tutawaelewa.

Msipotenga fedha, kwa unyenyekevu sana, kwa moyo mzito sana, mnisamehe sana, siwezi kuwasaliti wananchi wangu wa Kusini nikiacha hii barabara isitengewe fedha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili na la mwisho, ninaunga mkono mapendekezo ya Kamati, na hapa ninaipongeza sana Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu, imefanya kazi nzuri ya kizalendo na wamesema ukweli hapa. Ilitungwa Sheria hapa, Namba 220, ambayo ilianzisha Mfuko wa Barabara. Mfuko ule, ile Sheria ime-*reinforce* fedha hizi. Toka mwaka 2020 hii fedha haiendi kwenye Mfuko wa Barabara, inakwenda kutunzwa kwa mujibu wa sheria. Hii fedha imepelekwa Mfuko Mkuu, na ukisoma takwimu haziendi fedha zote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa tukijenga utamaduni huu, barabara zetu zinaharibika (za *TANROADS* na za *TARURA)* kwa sababu moja tu kubwa, Serikali tumeamua kupuuza sheria iliyotungwa na Bunge ya ku-*reinforce* hizi fedha. Sasa maneno haya Mwenyekiti amesema, *CAG* anasema, hatufanyi chochote. Kamati ya Bunge inasema, hatufanyi chochote. Jamani, tunataka kwenda wapi? Barabara hizi zitakufa tu, Mheshimiwa Ulega, tutakamata kichwa chako bure! *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kazi ni moja tu. Kama Serikali inataka hii fedha isiendelee kuwa *reinforced,* ilete sheria tubadilishe. Kwa nini haibadilishi sheria, inaendelea kubaki na fedha?

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo inabidi mnisamehe. Hebu basi tuone uchungu kidogo na hizi barabara.  Hii mishipa ya damu ya uchumi wetu tunaihujumu, kwa nini hawaiheshimu sheria iliyotungwa na Bunge? Ninaiomba Serikali hebu waende wakatekeleze ushauri, nawaomba Wabunge waunge mkono Kamati yetu ya Kudumu ya Bunge, tusimame kidete, hizi hela ziletwe ziende kujenga barabara zetu.  *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuendelea kupelekwa kwenye miradi mingine siyo sawa kama tunataka ziende, tubadilishe sheria maana kazi ya Bunge ni kutunga sheria na kufuta sheria.

Walete hapa tubadilishe vinginevyo ninasema mdogo wangu Ulega na yeye mwenyewe anatoka kusini, kwa sababu yeye ni zao la sisi wakati ule tukiwa kisiwa tulikuwa tukibaki pale, yeye ni mjukuu wetu, mtoto wetu kwenye hili ninaomba nisimuunge mkono mpaka aweke fedha kwa ajili ya Barabara yetu ya Lindi na Mtwara. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana.

**MHE. NAPE M. NNAUYE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana na siungi mkono hoja hii. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Nape kwa mchango wako. Ninamwita sasa Mheshimiwa Timoth Geofrey Anyosisye, Mheshimiwa Timotheo Paul Mnzava ajiandae, Mheshimiwa Moshi Selemani Kakoso, ajiandae.

**MHE. TIMOTH G. ANYOSISYE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Awali ya yote, nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa uzima. Kipekee kabisa ninamshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunifanya kuwa sehemu ya Bunge hili Tukufu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu ni mara yangu ya kwanza kuchangia ninaomba niungane na wenzangu kumshukuru sana Mwenyekiti wa Chama chetu cha Mapinduzi pamoja na vikao vyote vilivyohusika kupitisha jina langu kupeperusha bendera ya Chama Cha Mapinduzi, Jimbo la Kawe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue fursa hii kuwashukuru Wajumbe wa Chama Cha Mapinduzi Jimbo la Kawe, kwa kunichagua kwa kura nyingi sana, lakini kwa heshima kubwa sana niwashukuru Wananchi wa Jimbo la Kawe kwa kumchagua Mama yetu, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kura nyingi sana, zaidi kwa kuwachagua Madiwani wote 10 wanaotokana na Chama Cha Mapinduzi kwa kura nyingi sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tanzania ni Dar es Salaam, sisi wote ni mashahidi na nimpongeze sana Mheshimiwa Rais amekuwa

msikivu sana, amekuwa mnyenyekevu sana na amekuwa mkweli sana.

**MHE. HAMISI S. TALETALE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa…

**MHE. TIMOTH G. ANYOSISYE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa nyakati tofauti tofauti…

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa taarifa.

**TAARIFA**

**MHE. HAMISI S. TALETALE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nimpe taarifa mzungumzaji Tanzania ni Morogoro siyo Dar es Salaam.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa unaipokea hiyo taarifa?

**MHE. TIMOTH G. ANYOSISYE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba unitunzie muda wangu, taarifa siipokei, Tanzania ni Dar es Salaam.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa endelea.

**MHE. TIMOTH G. ANYOSISYE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa nyakati tofauti tofauti sisi watu wa Dar es Salaam tumekuwa tukiomba mambo kadha wa kadha. Changamoto yetu kubwa Dar es Salaam ni miundombinu ya barabara, changamoto yetu kubwa Dar es Salaam ni foleni za barabarani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumekuwa tukiomba kujengewa barabara mpya, tumekuwa tukiomba kujengewa madaraja, lakini pia tumekuwa tukiomba kujengewa *flyovers* pamoja na barabara mpya. Kwa usikivu wa Mheshimiwa Rais, ninaomba niseme kwamba baadhi ya maombi yetu sasa yameanza kujibiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wanakawe tuliomba kujengewa *flyover* kwenye makutano ya Barabara ya Ali Hassan Mwinyi

pamoja na Barabara ya Kinondoni, lakini pia tuliomba kujengewa *flyover* kwenye makutano ya Barabara pale Morocco, tuliomba kujengewa *flyover* kwenye makutano ya barabara pale Mwenge lakini pia tuliomba kujengewa *flyover* kwenye makutano ya Barabara ya *Rainbow*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo hii nimefurahi kumsikia Mheshimiwa Waziri akisema kwamba maombi yetu ya kujengewa *flyover* Mwenge pamoja na Morocco yamekubaliwa, tunamshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa usikivu wake na tunaendelea kumwombea kwa Mungu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maombi yetu ya *flyover* hizi mbili ambazo pia tuliziomba kwa maana ya makutano ya barabara pale Kinondoni pamoja na makutano ya barabara pale *Rainbow* tunaomba pia Serikali iliangalie hili ombi letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *flyover* hizi zikijengwa zote kwa pamoja watu wanaotoka Posta wakifika kwenye makutano ya Barabara ya Kinondoni na Ali Hassan Mwinyi watapitiliza moja kwa moja, lakini wakifika Mwenge vivyo hivyo pamoja na Morocco hivyo hivyo, tunaomba sana *flyover* hizi zijengwe kama tulivyoomba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaishukuru sana Serikali, Mheshimiwa Waziri amesema hapa tuliomba kuongezewa upana Barabara ya Mwai Kibaki tunashukuru Mungu maombi yetu yamekubaliwa na Mheshimiwa Rais anastahili kupigiwa makofi mengi sana kwa usikivu wake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine ambalo tuliomba kuongezewa upana wa barabara ni kuanzia Tegeta kuelekea Mabwepande barabara ambayo inaenda hadi Bagamoyo. Nimesoma randama nimeona eneo hili limekubaliwa kuongezwa upana barabara mbili kwenda Bagamoyo, mbili kuja huku mjini. Nitaomba sana Mheshimiwa Waziri wakati wa kuhitimisha aongee chochote kuhusiana na kupanua barabara kuanzia Tegeta kuelekea Bagamoyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye eneo hili pia kuongeza upana wa barabara, tuna barabara ile Kilima cha Wazo pale zimekuwa zikitokea ajali nyingi kutokana na wembamba wa ile barabara, wananchi wa Kawe wamekuwa wakifariki, wamekuwa wakitengeneza ulemavu wa kudumu, wamekuwa wakipoteza mitaji pamoja na nyumba zao. Ningeomba sana Mheshimiwa Waziri wakati wa kuhitimisha aseme chochote kuhusiana na Barabara ile ya Kilima kwenye kile Kiwanda cha Wazo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kilichokuwa kinatokea barabara hii ya Mwai Kibaki huko mbeleni kinaenda kutokea kwenye Barabara ya Kunduchi tusipoangalia. Haya mambo makubwa anayoyafanya mama yetu ya kujenga *flyovers* magari yatakuwa hayakai tena foleni, yanakwenda moja kwa moja maeneo ya Kunduchi na zile Kata za pembezoni ya Jimbo la Kawe. Kwa hiyo, niombe sana Mheshimiwa Waziri tuanze kutazama, tuanze kuona uwezekano wa kupanua Barabara ya Kunduchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ipo barabara mpya Mheshimiwa Waziri ambayo tumekuwa tukiiomba mara nyingi, Barabara ya Bunju kuelekea Mpiji ambayo inaenda kwa dada yangu Angellah Kairuki. Barabara hii kwetu sisi wananchi wa Kawe ni barabara muhimu sana, ninaomba sana ilishawahi kutangazwa mara ya kwanza sijui iliishia wapi, lakini kwenye vikao vyangu na ufuatiliaji wangu, nimeambiwa kwamba mkandarasi amepatikana na muda siyo mrefu barabara itaanza kujengwa. Ningeomba sana Mheshimiwa Waziri aongee chochote ili wananchi wa Kawe tupone kuhusiana na hii Barabara ya Mabwepande kuelekea Mpiji kuelekea kwa dada yangu Angellah Kairuki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunamshukuru Mheshimiwa Rais tuliomba pia kujengewa madaraja sisi wananchi wa Kawe, tuliomba kujengewa Daraja la Kunduchi, tuliomba kujengwa Daraja la Ununio JKT, lakini pia tuliomba kujengwa Daraja la Ruvu Chini. Tunashukuru Mungu mama yetu alitutengea zaidi ya shilingi 27,000,000,000 na Daraja la Kunduchi limekamilika watu wetu wanapita bila kupata shida yoyote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeambiwa pia Mheshimiwa Waziri amezungumza hapa tumetengewa shilingi 5,000,000,000 kwa ajili ya Daraja la Ununio – JKT. Hivyo hivyo tumetengewa zaidi ya shilingi 17,000,000,000 kwa ajili ya Daraja la Mpiji, tunamshukuru sana mama yetu kwa kutufanyia haya mambo makubwa na mazito. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mama yetu pia ameendelea kuwa mkweli, wakati wa kampeni alituahidi kwamba mradi wa mabasi yaendayo kasi hautasimama, wananchi wa Dar es Salaam ni mashahidi, wakandarasi wako *site* kila siku na sisi mradi tunaonufaika nao sisi ni awamu ya nne.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mradi ule zimetengwa zaidi ya milioni 191.2 Dola za Kimarekani kwa ajili ya kukamilisha mradi. Kuna mpango wa kujenga kilomita zisizopungua 30, lakini vituo kwa ajili ya wasafiri visivyopungua 41, tunaambiwa mradi umefikia 47% hivi tunavyoongea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye hili ninayo machache, alitutembelea Mheshimiwa Waziri akatoa maelekezo kwamba mwenendo wa mkandarasi siyo mzuri, ninaomba nimwambie Mheshimiwa Waziri mkandarasi bado anaendelea kuzingua, mwenendo wake bado siyo mzuri, anasuasua, hivyo utekelezaji wa mradi bado hauridhishi. Kwa hiyo, tutaomba Mheshimiwa Waziri wakati wa kuhitimisha aseme chochote ikiwezekana arudi tena kutoa maelekezo ili tuone ni namna gani mradi ule unamalizika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina jambo lingine la kushauri kwenye huo mradi wa mwendo kasi, mradi wa mwendo kasi kuna mpango wa kujenga hivyo vituo, lakini wako watu ambao wangependa kutoka na magari yao majumbani kwao afike kwenye kituo, apaki gari aingie kwenye mwendo kasi aende mjini akirudi ashuke kwenye kituo aingie kwenye gari lake arudi Mabwepande ndani, huko lakini hakuna *parking* kwa ajili ya magari ya watumiaji hawa wengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo niombe sana wenzetu wa Wizara ya Ujenzi waone uwezekano pia wa kujenga *parking* kwa ajili ya watumiaji hawa wengine. Nimemsikia Mwenyekiti akisema uwezekano wa wenzetu Wizara ya Ujenzi kuangalia vyanzo vingine vya kuongeza mapato kwenye eneo hili la Wizara ya Ujenzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mabasi peke yake ya mwendokasi kwenye mradi wa mwendo kasi yanaweza yasi-*exhaust* matumizi ya ile miundombinu. Nina ushauri kwamba wapo watu mmoja mmoja ambao wangependa kupata huduma ya miundombinu hii ya mwendo kasi hata kwa kuchangia kidogo tu. Ninaomba sana wenzetu wa Wizara ya Ujenzi waone kama kuna uwezekano wa kuanzisha huduma ya kuchangia kidogo tu ili mimi ambaye mwenye haraka nipate hiyo huduma niwahi kwenda mjini nitoke jioni nirudi nyumbani. Hayo yalikuwa ni kwa ajili ya wananchi wa Kawe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine la mwisho la kumalizia, ningependa kuwatia moyo wenzangu ambao tunamtakia mema mama yetu Dkt. Samia Suluhu Hassan, kumekuwa na kasumba tunapopongeza mambo mazuri watu wanabeza, lakini unabeza vipi kwa mfano, sisi wananchi wa Kawe tumekuwa tukiomba Barabara kutoka Shoko – Londa – Mongela kwa zaidi ya miaka 10 leo hii tumepewa tukipongeza tunakuwa tumefanya kosa gani? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante.

**MHE. TIMOTH G. ANYOSISYE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Nilimwita Mheshimiwa Timotheo Paul Mnzava.

**MHE. TIMOTHEO P. MNZAVA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kutoa mchango kwenye hii hotuba ya bajeti ya Wizara ya Ujenzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kumpongeza kwa dhati kabisa Ndugu yangu Ulega, kaka yangu Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi pamoja na Naibu Waziri, Katibu Mkuu, Naibu Katibu Mkuu na Watendaji wote wa Wizara kwa kazi kubwa na kazi nzuri ambayo wanaifanya kwenye nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kweli tunayo changamoto kwenye maeneo mengi kwenye eneo la barabara, pamoja na changamoto hizo ni ukweli kwamba Mheshimiwa Ulega na timu yake wamekuwa wakijitahidi sana, wanafikika, wanapatikana na ukiwapa hoja zako na matatizo yako wanayafanyia kazi, tunawapongeza sana kwa jambo hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina mchango kwenye maeneo machache. Eneo la kwanza nitumie nafasi hii kuishukuru sana Serikali na kuishukuru Wizara, kule Korogwe tumekuwa na deni kubwa na Serikali yetu kwa muda mrefu, tumekuwa na deni kwenye ujenzi wa barabara kwa kiwango cha lami, Barabara ya kutoka Korogwe - Dindira - Bumbuli – Soni, kilomita 74 iliyoahidiwa kwenye Ilani za Uchaguzi zaidi ya nne na ilikuwa haijatekelezwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumekuwa na deni kule Korogwe ya ujenzi wa Barabara ya lami ya kutoka *Old* Korogwe kwenda Kwa Mndolwa anakoishi Mufti na Sheikh Mkuu wa Nchi hii, lakini inakwenda Magoma, Mashoe, Bombo Mtoni mpaka Mabokweni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna wakati sisi ambao tulikuwepo Bunge lililopita tukawauliza wenzetu wa Serikalini kama wananchi wamesema sisi Wabunge tumesema, Viongozi wa Dini wamesema, lakini hawasikii, wanataka aseme nani wenzetu mpaka watusikie? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, angalau tumeanza kuona hatua ambazo wenzetu wameanza kuzichukua, Mheshimiwa Waziri nimeona fedha alizotenga kwenye bajeti. Nimeona kwenye randama, lakini pia nimesoma hotuba yake kwenye ukurasa wa 82, nimshukuru kwa kuziona barabara hizi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, watu wa Korogwe wamesubiri kwa muda mrefu tunachokiomba kwao ni mambo mawili kwa ajili ya barabara hizi. Moja ni kuongeza kasi ya utekelezaji wa kazi hizi ili matunda ya barabara ya lami, wananchi wa Korogwe na Lushoto, wananchi wa Korogwe na Mkinga waweze kuyaona kwa macho yao. Tunaomba waongeze kasi kwa sababu tumesubiri kwa muda mrefu, waongeze kasi ili jambo hili liweze kutokea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili wakati tunaendelea na taratibu za ujenzi wa barabara hizi kwa kiwango cha lami, hali ya nchi yetu wanaiona, hali ya mvua wanaiona, yako baadhi ya maeneo kwenye barabara hizi kwa sasa hayapitiki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo la pale kwa Meta linasumbua, lakini kwa maeneo ya Barabara ya Old Korogwe kwenda mpaka kule kwa wenzetu wa Mabokweni upande wa Mkinga kuna maeneo korofi sana. Tunaomba tunasubiri hatua za lami, wawape fedha wenzetu wa *TANROADS,* Mkoa wa Tanga na kwa kweli wanafanya kazi nzuri sana, wawape fedha waendelee kuzikarabati ili barabara hizi ziendelee kupitika muda wote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine ambalo ninataka kulichangia leo Mheshimiwa Waziri tunamwomba sana, sisi watu wa Tanga kwa sehemu kubwa hatuna deni na Dkt. Samia Suluhu Hassan, alifanya kazi kubwa kwenye maeneo mengi na moja ya alama ya sisi watu wa Mkoa wa Tanga ni kazi kubwa ya upanuzi na maendelezo ya bandari aliyoifanya Dkt. Samia Suluhu Hassan. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kazi ya upanuzi na maboresho ya Bandari ya Tanga ambayo kwa kiasi kikubwa imeongeza shehena za mizigo zinazohudumiwa na bandari yetu. Haiwezi kuwa na maana kama hawatafanya kazi kwenye barabara ili mizigo inayokuja kupitia Bandari ya Tanga iweze kufika vizuri na kwa urahisi kwenye maeneo mengine iliyotakiwa kufika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia Barabara ya kutoka Tanga kwenda Segera, Barabara ya kutoka Segera kwenda Chalinze muda wake wa kuishi umekwisha. Pia barabara hii ni nyembamba mno muda mrefu wamekuwa na kauli kwamba wanakwenda kufanya matengenezo lakini mpaka leo hatuoni, Mheshimiwa Waziri atakapokuwa anahitimisha hotuba yake tunataka kujua ni nini mikakati ya Serikali kwenye suala la kupanua na kuboresha Barabara kutoka Tanga kwenda Segera, Segera kwenda Chalinze. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri na hili linawagusa watu wengi, watu wa Kaskazini wote kwa maana ya Kilimanjaro, Arusha na Manyara mizigo yao haiwezi kufika kutoka Bandarini Dar es Salaam kama siyo barabara hizi. Haiwezi kufika kutoka Bandari ya Tanga kama siyo barabara hii, tunaomba atuambie mipango ya Serikali kwenye upanuzi na maboresho ya barabara hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili bandari ifanye kazi vizuri na mizigo ifike vizuri, ni lazima watuambie Mheshimiwa Rais alikuja Tanga mwaka 2025 mwezi Februari, aliahidi ujenzi wa barabara ya kutoka Handeni kwenda Kiberashi kwenda kwa Mtole na kwenda mpaka Singida na Wizara wametuambia wataijenga kwa *PPP* lakini hatuoni kwamba kuna hatua ambazo wamezianza kwa ajili ya barabara hizi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri na kwenye hili kama alivyosema kaka yangu Nape wakati watu wa Lindi na Mtwara mkiungana kwa barabara ile, watu wa Tanga, watu wa Morogoro, watu wa Chemba, watu wa Singida tuungane kwa ajili ya barabara hii. Tusikubali kupitisha bajeti hii kama hatujapata mkakati madhubuti wa Serikali wa kutengeneza barabara hii kwa kiwango cha lami. Barabara ya kilomita 324 tunaomba Serikali iifanyie kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la mwisho ni ushauri, ushauri huu siyo kwa Wizara peke yake ni ushauri kwa Serikali. Tuishukuru na kuipongeza Kamati yetu ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu, Bungeni kwa tamaduni za Kibunge Kamati

inafanya kazi kwa niaba ya Bunge, tunaiunga mkono taarifa ya Kamati wamefanya kazi nzuri sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninao ushauri kwenye maeneo mawili na Kamati imeyasema. Eneo la kwanza barabara ndiyo uchumi. Barabara zetu zina hali mbaya, tunazo barabara nyingi zinahitaji kujengwa kwa lami, tuna nyingi zinahitaji ukarabati na taarifa ya Kamati inatuambia zaidi ya 30% ya barabara za lami tulizonazo muda wake wa kuishi umekwisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, maana yake pamoja na maombi ya lami tuna kazi kubwa ya ujenzi wa barabara hizi upya tena. Mheshimiwa Waziri kwenye hotuba yake ameonesha changamoto za Wizara akaonyesha mbili ambazo ni mabadiliko ya tabianchi na uvamizi wa maeneo ya barabara. Mheshimiwa Waziri ameacha changamoto nyingine kubwa ambayo ni fedha hatuna fedha za kutosha kwa ajili ya ujenzi wa barabara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Bunge hili lazima lifanye maamuzi ya kuisaidia Wizara hii ipate fedha kwa ajili ya kufanya kazi ya ujenzi wa barabara. Kaka Nape amesema ana taarifa, Kamati imesema ukisoma ukurasa wa 19 wa taarifa ya Kamati yetu ya miundombinu, wameonyesha mwaka wa fedha wa 2024/2025 Fedha za Mfuko wa Barabara iliyokwenda ni 37%, mwaka uliofuata ni 42.66%.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tulitunga sheria na tulitunga sheria ku-*reinforce* fedha hizi kwa sababu tulijua zina umuhimu na barabara ni jambo muhimu na mahsusi kwa nchi yetu, kwa nini fedha za Mfuko wa Barabara haziendi kama zinavyopatikana, zinakwenda wapi wakati maelekezo ya sheria yako wazi? Ni lazima Bunge hili lisimame. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la kwanza ni kuhakikisha kwamba Fedha za Mfuko wa Barabara zinazotengwa zinakwenda, tutamwomba Waziri Ulega Barabara, lakini kama hana fedha hawezi kujenga barabara. Waheshimiwa Wabunge lazima tufanye maamuzi, tuisimamie Serikali kwenye eneo hili,

fedha za Mfuko wa Barabara ziende zikafanye kazi ya kutengeneza barabara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na fedha za Mfuko wa Barabara zikienda zote zitatusaidia kupunguza changamoto, lakini bado hazitoshi ni wakati sahihi wa kutafakari zaidi chanzo cha ziada kwa ajili ya kuongeza mapato, kwa ajili ya kwenda kufanya kazi ya kutengeneza barabara zetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Timotheo ahsante sana kwa mchango wako. Nimwite sasa Mheshimiwa Moshi Selemani Kakoso atafuatiwa na Mheshimiwa Subira Khamis Mgalu.

**MHE. MOSHI S. KAKOSO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuwa mchangiaji. Awali ya yote ninamshukuru sana Mheshimiwa Rais ambaye ametoa fedha nyingi za maendeleo, mwaka jana tulikuwa na shida kubwa sana maeneo ya ukanda wa kusini, kulikuwa na tatizo kubwa, Serikali ilitoa zaidi ya shilingi 800,000,000,000 kukarabati miundombinu iliyokuwa imeharibika, ni kazi ambayo ilifanywa na Serikali, tunampongeza sana Mheshimiwa Rais.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini ipo miradi inayoendelea hapa nchini. Takriban kila eneo Mheshimiwa Rais amekuwa akitoa fedha ambazo zitatekeleza hiyo miradi. Juzi tumeshuhudia utiaji wa saini wa kuendeleza miradi ya maendeleo kwa Mkoa huu wa Dodoma Makao Makuu, ambapo patabadilika kwa jinsi ya michoro tulivyoiona na fedha ambazo zitatumika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninampongeza Mheshimiwa Waziri pamoja na timu yake. Wanajitahidi wanafanya kazi kwa kadri wanavyoweza. Shida kubwa tuliyonayo ni tatizo la fedha. Waziri mtamla nyama kila kona na mtashika shilingi kila eneo, lakini kama hakujawa na suluhu ya kupata fedha za ziada, hii Wizara hatuisaidii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na Waheshimiwa Wabunge kuzungumzia suala la Mfuko ninakubaliana, kwamba fedha za Mfuko haziendi kama ilivyokusudiwa. Niiombe Serikali; na kwa bahati nzuri yupo Mheshimiwa Waziri wa Fedha; kwenye bajeti hii tuliyonayo ahakikishe zile fedha za Mfuko wa Barabara zinaenda. Zikishafika huko zinaenda kutatua tatizo la barabara zilizoharibika. Hilo ni eneo ambalo tunaishauri Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lipo jambo maalum ambalo tukilichukulia maamuzi sisi Wabunge tutakuwa tumeisaidia sana hii Wizara. Wizara hii haina fedha za kutosha na inahitaji fedha nyingi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunajua, tumepitia maeneo mengi; tumepita kwenye miradi mikubwa sana ambako fedha ambazo zimetumika ni hizo hizo za Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninawakumbusha Waheshimiwa Wabunge, wale Wabunge ambao walikuwepo kwenye Bunge lililopita kwamba; wakati *TARURA* inaanzishwa ilianzishwa kwa bajeti ndogo sana, ilikuwa ya bilioni kama 400 kwa nchi nzima na Wabunge tulikuwa tukijenga hoja humu. Kila Mbunge alikuwa anaomba barabara yake ipandishwe iende ikahudumiwe na *TANROADS*. Wabunge tulichukua maamuzi tukapata chanzo kipya cha mapato ambacho kilipandisha kutoka shilingi 400,000,000,000 sasa *TARURA* wanapata zaidi ya shilingi 1,000,000,000,000, ambayo kila mtu anaisifia. Akija Mtendaji Mkuu wa *TARURA* hapa wanamsifia sana ni kwa sababu walipata fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hali ilivyo ya *TANROADS* kwa sasa, tuna miradi viporo mingi; na sisi Waheshimiwa Wabunge kila mtu atataka apelekewe miradi kwenye maeneo ya kwake. Uwezo wa Serikali kwa makusanyo yake tulishaona kwamba hapo ndipo alipoishia. Ninawaomba Waheshimiwa Wabunge; kama tunahitaji kwenda kufanya maendeleo ya barabara ni lazima tuchukue maamuzi magumu na yatokane na sisi wenyewe humu Bungeni. Tukitoka nayo hapa tutapata chanzo cha mapato ambacho kitaenda kusaidia kunusuru miundombinu iliyoharibika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, inawezekana kabisa kwamba, ambaye yuko kwenye barabara nzuri hawezi kujua adha ya barabara ilivyo. Barabara ndiyo kila kitu. Wapo Watanzania wenzetu ambao walishindwa hata kuwapeleka watoto wao shuleni kwa sababu barabara ziliharibika. Wapo Watanzania ambao wameshindwa kuwahudumia ndugu zao na wamepoteza maisha kwa sababu barabara zilipoharibika wameshindwa kufika kwenye huduma za afya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niombe yale mapendekezo tuliyoyapendekeza; la kwanza, kipaumbele cha wizara, waende wakakamilishe zile barabara walizoanzisha. Pili, wahakikishe kwamba barabara sasa zinajengwa kwa mfumo wa *PPP*. Mfano ile Barabara ya kutoka Dar es Salaam kuja Morogoro. Watafute wabia; wabia hawawezi kuacha kuja kuwekeza barabara ambayo inatumika na malori zaidi ya 10,000; ni lazima waje wawekeze. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatu, ninajua watu wataendelea kunishambulia, lakini bado nitabaki kwenye msimamo ule ule. Mapendekezo yetu ya Kamati tulipendekeza shilingi 100 itumike kwa muda wa maongezi iende ikachangie huduma. Za nini? Za barabara za vijijini. Tukipata hapa tuna uwezo wa kupata shilingi trilioni 1.1. Hizo fedha shilingi 600,000,000,000 tuwape *TANROADS*, shilingi 500,000,000,000 tuwape *TARURA*. Watashuhudia maendeleo ambayo yataenda nchi nzima, yatafanyiwa kazi sehemu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo ambalo tutatakiwa Serikali tuiambie kwa nguvu zote, ni kuhakikisha kuwa fedha za Mfuko wa Barabara *(ringfenced)* zisitumike tena kwenye njia iliyo tofauti. Hiyo ndiyo njia pekee ambako ndiko tunaweza tukapitia tukapata mahali pa kunusuru miundombinu iliyopo kwa sasa. Vinginevyo, Mheshimiwa Nape ndugu yangu atashika shilingi na wengine wote watashika shilingi. Suluhu, ni lazima tutafute chanzo kipya cha mapato.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninajua kwamba huko nje wanaharakati; ninajua akina Kazumari, akina Ananilea Nkya

wataendelea kutupiga, lakini tutoke na mawazo ambayo yanaweza yakaisaidia nchi ili tupate mahali pa kutokea. Huko ndiko kumsaidia Mheshimiwa Rais. Tutoke na azimio sisi humu ndani ya Bunge. Itatusaidia kwenda kuimarisha miradi ya maendeleo ya kwetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, ninamwomba Mheshimiwa Ulega, ile barabara yangu ya kutoka Mpanda kwenda Kigoma; alishaianzisha akaijengee, apeleke fedha huko. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana na ninaunga mkono hoja. *(Makofi/Kicheko)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mwenyekiti wa Kamati ya Miundombinu. Nimwite sasa Mheshimiwa Subira Khamis Mgalu, ninadhani muda utaturuhusu tutakwenda na Mheshimiwa John Francisco Nzilanyingi.

**MHE. SUBIRA K. MGALU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuchangia kwenye Wizara hii ya Ujenzi. Nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia uhai na afya njema.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaendelea kumpongeza Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan pamoja na Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Mheshimiwa Abdalla Ulega, watendaji wote wa sekta hii ya ujenzi pamoja na Mheshimiwa Naibu Waziri kwa kazi nzuri waliyoifanya kwenye sekta hii ya ujenzi licha ya changamoto mbalimbali. Ninapopongeza ni kwa sababu ninazo sababu kama mbili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kwa usimamizi mzuri wa miradi ya dharura ambayo ilisababishwa na mvua nyingi; na sisi Mkoa wa Pwani tulipata miradi takribani sita, kiasi cha shilingi 24,000,000,000. Mheshimiwa Ulega amefanya kazi nzuri ya kusimamia. Kama alivyosema mwenyewe kwenye hotuba yake, kwamba baadhi ya maeneo licha ya mvua nyingi kunyesha, licha ya athari mbalimbali zilizojitokeza, lakini bado wananchi wameweza kupita katika maeneo ya hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, niipongeze Serikali kwa sababu kwenye hotuba yake ameonyesha kiasi gani barabara za lami kwa kipindi cha miaka mitano, ukiangalia kwa wastani namba hazidanganyi. Awamu ya Sita kwa wastani kila mwaka imejenga kilomita 299, ukilinganisha na awamu zote zilizopita; ambazo zilijenga kilomita 156. Kwa hiyo, yote ni utayari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaposimama kuunga mkono bajeti hii ninakuwa na matumaini, kutokana na maelezo ambayo ameyaonyesha, hasa ubunifu wa Serikali; kwamba inataka kutumia *infrastructure bond*. Nina uhakika na chanzo hiki kwa sababu tuliona wakati tuna *Samia Infrastructure Bond* tuliona Serikali ilitaka shilingi 150,000,000,000, maombi yalikuwa shilingi 303,000,000,000. Kwa hiyo, nina uhakika chanzo hiki kinaweza kwenda kutusaidia. Ninakupongeza kwa Shindano la *Foleni Challenge* pamoja na kuhusisha vijana hao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninataka niongezee, mkakati wa kupunguza foleni Miji ya Dar es Salaam na Pwani, ninataka nimwombe Mheshimiwa Waziri aweze kuangalia na kukamilisha. Barabara ya *TAMCO* – Mapinga zimebaki kilomita 14 tu ambazo ni kiasi cha shilingi 16,000,000,000 na mkandarasi yupo. Pia Barabara ya Kibaha – Kisarawe nayo ni kilomita 18 tu, nayo inaweza ikasaidia kupunguza foleni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaishukuru Serikali kwa kushirikisha *PPP* katika kuongeza barabara ya njia nane kuanzia Kibaha – Mlandizi – Chalinze. Ametuthibitishia kuwa *NSSF* wako tayari kuunga mkono Serikali. Sisi Wanapwani tunafurahi kwa sababu kati ya mtandao wa kilomita 1,000 ni kilomita 50 tu ndani ya mkoa ambazo ni za kwetu zenye lami. Kilomita zaidi ya 505 ni barabara za Kitaifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimshukuru Mheshimiwa Waziri kwa fedha za dharura ambazo wamezitenga, shilingi bilioni 20. Ninakuomba ututazame Kata ya Mapinga ambayo imezingirwa na mafuriko. Pale kuna Daraja la Mpiji Chini. Nilimwona wakati anaongea na Mheshimiwa Waziri Mkuu juu ya Daraja la Jangwani. Ni miongoni mwa daraja ambalo wamelitaja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hayo, kuna baadhi ya maeneo Barabara ya Makofia – Mlandizi, barabara hii imeahidiwa awamu nne mfululizo. Nimshukuru kwamba sehemu ya hotuba hii amesema kwamba Serikali ina mpango kutafuta fedha na kuijenga kwa kiwango cha lami. Kwa kuwa Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan ametutunuku Wanabagamoyo kwa kuanzisha mji wa ekolojia ya bahari. Tunaamini, pamoja na kasi ya ujenzi wa viwanda, Mkoa wa Pwani tunaongoza kwa viwanda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara ambazo zitasaidia usafirishaji wa *material*, usafirishaji wa bidhaa zitakazozalishwa, ikiwemo barabara ambayo inaunganisha Afrika Mashariki imeanza kujengwa, Tanga – Pangani. Pia kipande cha Mkange – Makurunge. Barabara hii ipo kwenye Kiwanda cha Sukari cha Bakhresa. Nimwomba Mheshimiwa Waziri, katika moja ya vipaumbele vyake iwepo barabara hii ya kilomita 74. Ilani iliahidi na pia Mheshimiwa Rais alipokuja kwenye kampeni alituahidi, tunaomba pia kasi ya ujenzi wa barabara hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kana kwamba haitoshi, tushukuru kwa namna ambavyo mwarobaini wa foleni kuanzia Mbagala Rangi Tatu – Kongowe – Mkuranga, ambavyo kazi imeanza kwa mara ya kwanza kwa ujenzi wa *flyover* na ujenzi wa Daraja la Mzinga. Kwetu sisi Wanapwani kuelekea Kusini tunaamini, licha ya changamoto ya barabara ile lakini italeta mwarobaini na itatupatia faraja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunatambua dhamira ya Mheshimiwa Rais ya kuhakikisha kuwa nchi hii inaunganishwa kanda zote. Kuna ukarabati au ujenzi wa Barabara mpya ya kutoka Chalinze kwenda Rufiji-Utete ambapo usanifu unaendelea. Niombe usanifu ukamilike ili barabara hii ijengwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunazo Barabara kama ambavyo nimetangulia kusema; pia Daraja la Mpiji Chini ambalo tenda ilitangazwa. Hata hivyo, mkandarasi aliondolewa *site* kutokana na kushindwa kazi. Kama alivyosema jirani yangu, Mheshimiwa Mbunge wa Kawe; kazi ambayo iliahidiwa kwenye daraja hili ikamilike. Kwa ajili ya wananchi wa Mapinga kwenye Vitongoji

vya Kiharaka na Minazi Minane Barabara ya Mingoi – Kiembeni pia ifanyiwe utekelezaji wa haraka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho nimalizie kuhusu upanuzi wa Barabara ya Tegeta – Bagamoyo ambapo Mheshimiwa Mbunge wa Kawe naye ameiomba. Kwa sababu mji wetu sasa hivi una harakati nyingi na viwanda vingi vinajengwa, iendane sambamba na kumpa tabasamu mwananchi. Ipo changamoto. Ninaijua hii ningeichangia kwenye Wizara ya Uchukuzi; lakini ipo changamoto ya wananchi wa Bagamoyo kuishia kituo cha Bunju peke yake, wakati sisi tunastahili kuwa na *route* ya kwenda Bagamoyo – Mwenge, Bagamoyo – Tegeta.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, huu upanuzi wa miundombinu na mpango wa ujenzi wa barabara uendane na kuwarahisishia wananchi ili waweze kufika kwenye taasisi za umma kwa haraka badala ya kutumia muda mrefu vituo vikawa vingi. Kwa hiyo, niombe; Mheshimiwa Waziri na hili analijua na amepata kulipokea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimalizie kwa kusema ninaunga mkono hoja hii. Nina imani kwamba barabara ni maendeleo, barabara ni uchumi, barabara ni sekta ya jamii, barabara inawezesha na ndiyo maana mchango wake kwenye pato la Taifa ni zaidi ya 11%. Vilevile, ndiyo maana ukuaji wake kwenye pato la Taifa pia umeendelea kukua mara kwa mara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina imani na Serikali yetu ya Awamu ya Sita; nina imani na ubunifu wa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, maana hatujawahi kuona masuala ya *infrastructure bond* ndani ya nchi, lakini amethubutu kwenye masuala haya ya barabara *(TARURA)*. Nina imani kwenye barabara hizi chini ya Mfuko wa *TANROADS*, *bond* wakitoa *bond* fedha zitapatikana na barabara za kanda mbalimbali ili kuwezesha uchumi wa nchi yetu kukua; inawezekana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninatoa hongera kwa Wizara ya Ujenzi na ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Ninaomba tumalizie mchangiaji wetu wa mwisho kwa mchana huu. Nimwite Mheshimiwa John Francisco Nzilanyingi.

**MHE. JOHN F. NZILANYINGI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru kwa kunipa nafasi ili nipate fursa ya kusema neno kwenye hoja iliyoko mezani. Jambo la kwanza nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa kibali na hatimaye siku ya leo imefika ambayo ilikuwa inasubiriwa sana na wananchi wakaazi wa Jimbo langu la Nyamagana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hilo, ninatumia fursa hii kumpongeza sana Waziri wa Ujenzi kwa kazi nzuri anayoifanya. Kwenye Jimbo langu la Nyamagana na Jiji la Mwanza, Waswahili wanasema asiyeshukuru kwa kidogo hata akipewa kikubwa hawezi kushukuru. Chini ya uongozi wa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan upande wa Wizara ya Ujenzi kazi kubwa imefanyika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunavyozungumza tulikuwa tuna changamoto kubwa sana ya madaraja ya pale Mabatini na Mkuyuni. Kwa neema ya Mungu na mapenzi mema ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kupitia msaidizi wake ndugu yetu Mheshimiwa Ulega, ujenzi wa madaraja yale umekamilika na sasa wananchi wakazi wa Jiji la Mwanza wananufaika na matunda ya ujenzi wa madaraja yale. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kuyasema hayo, ninaomba nipate fursa ya kusema kwenye maeneo kama mawili. Jambo la kwanza; Jimbo langu la Nyamagana ndilo Jiji la Mwanza. Unapolizungumza Jiji la Mwanza unazungumzia *economic hub* ya Kanda ya Ziwa na nchi zinazopakana na nchi yetu, kwa maana ya Uganda, Kenya, *DRC* pamoja na Rwanda. Uwepo wa jiji letu hili la kimkakati ni fursa kwa ukuaji wa uchumi wa Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunavyozungumzia kwenda kuwa na uwanja wa Kimataifa wa ndege pale Mwanza, hautakuwa na maana ikiwa ujenzi wa barabara kwa kiwango cha njia nne

inayotoka Mwanza kwenda Usagara haitajengwa. Mheshimiwa Dkt. Samia anaileta reli ya *SGR* Jiji la Mwanza. Dkt. Samia amejenga Daraja la JPM Magufuli pale Busisi. Dkt. Samia amekamilisha ujenzi wa meli inayokwenda kwa wenzetu wa Bukoba maeneo ya Port Bell, Jinja pamoja na Mombasa. Miradi yote hii ni lazima iunganishwe na miundombinu ya barabara za kisasa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa muda mrefu Wanamwanza wamekuwa na kilio kikubwa sana. Barabara ya kutoka Usagara kuja Mwanza imekuwa ni kero kubwa sana. Kwa bahati mbaya kwa namna ilivyo jiografia ya Jiji la Mwanza, ni Jiji la miamba. Tunayo malango makuu mawili pekee yake. Barabara inayotoka Mwanza kwenda Usagara, barabara inayotoka Mwanza kwenda kule Kisesa. Ikitokea changamoto ya ajali ya barabara, maana yake Jiji la Mwanza linajifunga. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, namna peke yake ya kulifungua Jiji la Mwanza ni kuhakikisha kwamba sasa tunakuwa na njia nne za kutoka Mwanza Mjini kwenda Usagara na kutoka Mwanza kwenda kule Kisesa. Katika hili nimepata fursa ya kusema na Mheshimiwa Waziri mara kadhaa. Barabara hii imewekwa kwenye bajeti na kwenye mpango na kwenye ilani zaidi ya mbili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi wa Mwanza wamenielekeza, nitakapohitimisha Bunge hapa nihakikishe kwamba ninarudi na Barabara ya Mwanza – Usagara, Mwanza – Kisesa. Kwa sababu nina imani kubwa na Mheshimiwa Waziri nina uhakika hatokubali nisalie Dodoma. Njia pekee ya kunirejesha Nyamagana ni kuhakikisha kuwa ananiwekea fedha kwenye Barabara hii ya Mwanza Usagara. Mheshimiwa Waziri Ulega amekuja na mpango mzuri sana. Nimeona ameweka *Foleni Challenge* pale Dar es Salaam. Ninatamani sasa *challenge* ya kuondoa foleni kwa Jiji la Mwanza nayo iweze kufanyika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, amekuja na mpango mzuri sana kwa *economic corridor*, kwa maana ya Barabara ya kutoka Mwanza Mjini – Usagara na Usagara kwenda Kisesa. Barabara hizi

kama zitajengwa nina imani Jiji letu la Mwanza tutakwenda kulifungua. Watu wa Mwanza wameisubiria kwa muda mrefu, na namna pekee ya kuwafuta machozi ni kuhakikisha kuwa barabara hii inajengwa kwa kiwango cha njia nne.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu nina imani na Mheshimiwa Waziri sikusudii kushika shilingi yake. Waziri atakapokuja ku-*wind up*, ninatamani kuona barabara hii ya Mwanza Mjini kwenda Usagara, ameiwekea fedha kiasi gani. Kwa sababu sikusudii kushika shilingi ya Mheshimiwa Waziri ninatamani kuona mpango wa kuitengeneza hii *economic corridor* ya kutoka Mjini – Usagara, Usagara – Kisesa na Kisesa kuja kwenye Jiji letu la Mwanza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kuyasema hayo na ninapohitimisha, ninaomba nimtie moyo kaka yangu Mheshimiwa Ulega. Kazi anayoifanya ni njema, lakini ili iweze kufanikiwa anahitaji fedha. Ninaungana na michango ya Waheshimiwa Wabunge wenzangu, niungane na mapendekezo ya Kamati, ya kwamba tumsaidie fedha zile za Mfuko wa Barabara ziletwe na ziwekwe kwenye matumizi yaliyoelekezwa kwa ajili ya matumizi ya ujenzi wa barabara na siyo vinginevyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kuyasema hayo, ninaomba kuunga mkono hoja kwa 100%, lakini Mheshimiwa Ulega atakapokuja aniambie ameweka shilingi ngapi kwa ajili ya Barabara ya Mwanza – Usagara. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Waheshimiwa Wabunge, tumefika mwisho wa kipindi hiki. Ninaleta kwenu majina ya wageni walio ndani ya ukumbi wetu.

Tuna wageni wa Mheshimiwa waliokaa Jukwaa Kuu. Hawa ni wageni 13 wa Mheshimiwa Paul Christian Makonda, Waziri wa Habari, Utamaduni na Michezo. Tumebahatika leo kuwa na ugeni wa gwiji wa mpira wa miguu na mchezaji wa zamani wa Timu ya Taifa ya Uingereza na Klabu ya *Manchester United*. *I have the pleasure to introduce Ferdinand Rio Gavin*. *Welcome to Tanzania, and I hope you enjoy Dodoma*. *(Makofi/Vigelegele)*

Mgeni huyu ameongozana na Gerson Msigwa, Katibu Mkuu Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo na Msemaji Mkuu wa Serikali. Karibuni sana. *(Makofi)*

Tuna wageni wengine; *we have Esther Suleiman* Kurtz*;* huyu ni Meneja wa Ferdinand. *Hirji Ismail Anisha Karim, business partner*; *Alan Ali Ismail, business partner*; *Kimble Olivia, business partner*; pamoja na *Achieve Onyekweluje, business partner*. Hao wote wako kwenye *delegation* moja. Karibuni sana. *(Makofi)*

Pia, tunao Ndugu Boniface Tamba, Mkurugenzi wa Maendeleo ya Michezo, Wizara ya Habari na Utamaduni, Sanaa na Michezo; Ndugu Neema Msitha, Katibu Mtendaji Baraza la Michezo la Taifa (BMT); Ndugu Wallace Karia, Rais wa Shirikisho la Mpira wa Miguu Tanzania; na Pia Ndugu Athuman Nyamlani Makamu Rais Shirikisho la Mpira wa Miguu Tanzania. Karibuni sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Makonda vilevile ana wageni wengine; hawa ni wachezaji wa zamani wa Timu ya Taifa *(Taifa Stars)*. Ninadhani watakuwa wamekaa kwenye ukumbi wetu mkubwa wanatuona.

Tunayo vilevile Timu ya Taifa ya Wanawake *Under 20* na benchi la ufundi. Pia, kuna waandishi wa habari kutoka vyombo mbalimbali vya habari. Tunawakaribisha sana kwenye Bunge letu. *(Makofi)*

Tuna wageni wengine waliokaa Jukwaa la Spika. Hawa ni wageni wa Mheshimiwa Abdallah Hamis Ulega, Waziri wetu wa Ujenzi ambao ni: Ndugu Rosalynn Mndolwa, huyu ni Mkurugenzi Mtendaji *Mwananchi Communications Limited;* Ndugu Edson Sosten huyu ni Meneja Masoko *Mwananchi Communications Limited*. Karibuni sana. *(Makofi)*

Wageni wawili, hawa ni wageni wa Mheshimiwa James Kinyasi Millya, Naibu Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki. Tunaye ndugu Lilian Andrew na Gloria Novatus. Karibuni sana. *(Makofi)*

Wageni wa Waheshimiwa Wabunge:-

Wageni wengine wa Mheshimiwa Ulega, Waziri wa Ujenzi; Menejimenti na watumishi wa Wizara ya Ujenzi, Wakurugenzi na Wakuu wa Vitengo kutoka Taasisi za *TANROADS*, *TEMESA* na *TBA*. Mameneja wa Mikoa kutoka *TANROADS*, *TEMESA* na *TBA*. Wote kwa umoja wao, wengine wako pale wengine nadhani wamekaa kwenye ukumbi wetu mkubwa. Tunawakaribisha sana. *(Makofi)*

Wapo vilevile wawakilishi wa benki, tuna wawakilishi wa vyama vya wakandarasi, tuna taasisi za elimu ya juu, tuna Chama cha Wamiliki wa Malori Wadogo na Kati Tanzania. Pia, tuna wageni kutoka Jimboni Mkuranga, wametoka kwa Mheshimiwa Waziri na tuna ndugu na jamaa mbalimbali wa Mheshimiwa Waziri ambao tulikwishawatambulisha. Karibuni sana. *(Makofi)*

Wapo pia wawakilishi wa wanafunzi washindi wa Shindano la Andiko la Ubunifu na Kupunguza Msongamano wa Magari Jijini Dar es Salaam. Wawakilishi wao ninadhani wapo pale. Karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao wawakilishi na waandishi wa Shirika la Viwango *(TBS)*. Karibuni sana. *(Makofi)*

Wageni 18 wa Mheshimiwa George Boniface Simbachawene. Hawa ni Wachungaji kutoka Mtera Mkoani Dodoma. Karibuni sana. *(Makofi)*

Wageni wawili wa Mheshimiwa Mwita Waitara. Hawa ni wapigakura wake kutoka Jijini Dar es Salaam. Karibuni sana. *(Makofi)*

Hayo ni majina ya wageni wetu. Waheshimiwa Wabunge tutaendelea na uchangiaji tutakaporudi mchana. Tutaanza na Mheshimiwa Athumin Omary Mapalilo, akifuatiwa na Mheshimiwa Mary Francis Masanja, Mheshimiwa Haran Nyakisa Sanga na Mheshimiwa Phillipo Augustino Mulugo. Wengine tutawataja kadri muda utakavyozidi kwenda.

Baada ya maneno hayo, ninasitisha Kikao cha Bunge mpaka saa 11. 00 jioni.

*(Saa 7.02 Mchana Bunge Lilisitishwa hadi Saa 11.00 Jioni)*

*(Saa 11.00 Jioni Bunge Lilirudia)*

*Naibu Spika (Mhe. Daniel B. Sillo) Alikalia Kiti*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa, tukae.

Katibu.

**NDG. ASIA MINJA – KATIBU MEZANI:**

**HOJA ZA SERIKALI**

**Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Ujenzi kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027**

*(Majadiliano Yanaendelea)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na majadiliano na tutaanza na Mheshimiwa Tabasam Hamis Mwagao, atafuatiwa na Mheshimiwa Livingstone Lusinde, Mheshimiwa Abdallah Dadi Chikota, ajiandae.

**MHE. TABASAM H. MWAGAO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuwa mchangiaji wa kwanza kwa jioni hii ya leo. Ni kwamba Wizara ya Ujenzi ni Wizara muhimu sana katika uchumi wa nchi hii na hakuna Mheshimiwa Mbunge yeyote anayetoka kwenye jimbo lake ambaye hana kero ya barabara katika nchi hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kero hizi za barabara pia tunazo barabara ambazo zimegawanyika katika sehemu kuu tatu. Tuna barabara ambazo ni barabara za Taifa, lakini tuna barabara za mikoa. Hizi barabara za mikoa zinahusu mikoa kwa mikoa. Tuna barabara ambazo zinahusu wilaya na mikoa yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa hizi barabara nyingi muda wake umekwisha; hilo halipingiki kabisa hata kidogo. Tunazo barabara ndefu sana ambazo zinaunganisha nchi yetu kutoka Kusini kwenda Magharibi, kutoka Kaskazini kwenda Kusini, kutoka Mashariki kwenda Magharibi na kutoka Mashariki kwenda Kaskazini.

Mheshimiwa Naibu Spika, usafiri wa barabara ndiyo usafiri mwepesi kabisa katika nchi hii unaoweza ukafikiwa na mtu anayetembea kwa miguu, mtu anayekwenda kwa vipando na watu wanaosafirisha mizigo wanapita katika hizi barabara. Sasa tunaiomba sana Serikali, pamoja na kufanya mambo mengi sana yanayofanyika, tunataka Mungu akijaalia, basi wahakikishe miradi yote ya viporo katika barabara hizi na mipango iliyoandaliwa sahihi kwa ajili ya matumizi ya pesa katika barabara hizi tunaomba zipelekwe kwenye maeneo haya bila ajizi hata kidogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunayo mikoa ambayo bado haijaunganishwa kwa barabara za lami na ni barabara muhimu sana katika nchi hii. Kwa mfano; tunayo barabara ya muhimu sana kwa sisi watu wa kanda ya ziwa, Barabara hii inatokea Singida - Iguguno inakwenda Simiyu. Hii inaunganisha Mkoa wa Singida na Mkoa wa Shinyanga, lakini inaunganisha Mkoa wa Mara na sisi watu tunaotoka Kanda ya Ziwa kwa Mwanza, barabara hii bado ni nyepesi kwa watu wanaokwenda Kwimba na watu wanaokwenda maeneo ya Magu: hawalazimiki kuingia Mwanza Mjini.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunayo Barabara inayotokea Uvinza kwenda Katavi. Barabara hii kutoka Katavi mpaka Lugufu zaidi ya kilomita zinakaribia kilomita 200, barabara hii haijakamilika na bado ilikuwa ina mkandarasi. Tunayo barabara nyingine ya muhimu sana katika uchumi wa nchi hii, ni barabara inayotokea Ipole inakwenda Kitunda - Rungwa mpaka Makongolosi. Barabara hizi tunazipita sisi kama wafanyabiashara ni za muhimu sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara nyingine ni ya kutokea Rungwa inakwenda Itigi, imetengenezwa kilomita 20 kwenda Mkiwa. Kwa sisi tunaokatiza hiyo njia ya Singida hali ni kama ilivyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara nyingine ni Barabara ambayo inatokea Mikumi imetengenezwa kidogo mpaka Ifakara lakini barabara hii kwa watu wanaokwenda Njombe – Songea ni barabara muhimu sana katika uchumi wa nchi hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tunayo Barabara ambayo inatokea Kilosa. Hii inachukua Mikumi – Kilosa inakwenda moja kwa moja kupitia Turiani. Barabara hii inakwenda Handeni na hii barabara ikipelekwa mpaka Korogwe hatuna mizigo mingine inayotokea Tanga tukaja tukabanana katika Barabara ya Segera.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunayo Barabara ya Handeni kuja Singida inapitia Kiteto huko ndani katikati inakuja Singida. Tunataka Mheshimiwa Waziri, barabara hizi azipe kipaumbele hasa ambazo barabara bado zina vumbi. Katika hizi barabara za kwetu za mikoa, tunayo Barabara ya Mwanza – Shinyanga imekwisha na Barabara ya Mara kwenda moja kwa moja mpaka Bunda - Lamadi, nayo imekwisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tunayo Barabara ya Sengerema kutokea Usagara kwenda Geita, sasa hivi hii ina mashimo sasa hivi. Pia, tunazo barabara hizo ambazo zinaunganisha Kahama kuja Geita, hizi ni barabara ambazo hazikwepeki kutengenezwa katika nchi hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa kinachonisikitisha pamoja na kufanya kazi, kazi zimefanywa kubwa na Wizara hii kupitia Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa Mama yetu Samia Suluhu Hassan, Mwenyezi Mungu ampe maisha marefu sana katika kutufungulia hizi barabara.

Mheshimiwa Naibu Spika, pesa tunaona sisi, miradi sisi inayojengwa katika maeneo yetu inajengwa kwa pesa hizi za kuungaunga za kwetu sisi wenyewe lakini ipo mikoa ambayo inapewa pesa nyingi. Ninaangalia hapa leo asubuhi wachangiaji

wenzangu wanalalamika kuhusu jambo hili katika maeneo yao, mimi ni mjumbe wa Kamati nimeumia sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna shilingi 639,000,000,000, ni mikoa miwili tu ya Kusini kule na tunaona kazi inayofanyika, (shilingi 600,000,000,000 pesa za *ADB)*. Kama tunadanganywa sisi kwenye Kamati huku ndani waje watueleze, sisi hapa Mheshimiwa Waziri, aje atoe ufafanuzi wa hizi barabara na tunakuomba kwa sababu wewe ndiyo Mwenyekiti. Sisi Kamati ya Miundombinu, hebu watuwekee pesa nyingi tukakague hizi barabara, hakuna namna nyingine sasa, tuzikague hizi barabara. Tusipozikagua hizi barabara tukija humu ndani tutakuja tudanganyane wakati kwenye makaratasi tunaona zimepelekewa mabilioni ya shilingi, kitu ambacho kinatufanya tuumie sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tuwe tunashukuru na leo ninashukuru, kwa ujenzi wa Daraja tu la Kigongo – Busisi, shilingi 730,000,000,000, ninaishukuru Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine tulikuwa tuna kero sisi katika jimbo letu sisi, wilaya yetu tu inaunganisha majimbo matatu; inaunganisha Jimbo la kwangu la Sengerema, Jimbo la Buchosa na Jimbo la Geita Vijijini. Tumepata sisi pesa na mkandarasi anakwenda kuanza kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hizi pesa tumeshughulika kuziomba toka 2020 kwa ahadi ya Mheshimiwa Rais, marehemu hayati John Pombe Magufuli ndiyo tunazipata leo. Sasa ni lazima nishukuru lakini hii miradi iishe, tunamwomba Waziri. Pia Waziri aje hapa atuelezee hawa wenzetu kama wanawatafutia pesa mpaka pesa za Mfuko wa *ADB*, pesa za *World Bank*, sisi tunawekewa pesa za kuungaunga wakati tuna barabara za muhimu, inakuwaje? Hao wanaowapelekea hizo pesa za *ADB* na kwingine, ndiyo wanakuja kulalamika humu ndani, haikubaliki hata kidogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, yeye atakuja kusema Waziri, kwa sababu nimemwambia shilingi 600,000,000,000, ninataka niisikie hiyo shilingi 630,000,000,000 ni ya barabara zipi, kwa sababu

nisizitaje mimi, aje azitaje mwenye barabara zake. Kwa sababu si nimezisoma kwenye randama?

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MHE. TABASAM H. MWAGAO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba nimalizie.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa, malizia muda wako umekwisha.

**MHE. TABASAM H. MWAGAO:** Mheshimiwa Naibu Spika, tuna Chuo cha Ujenzi ...

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa, muda umekwisha.

**MHE. TABASAM H. MWAGAO:** Mheshimiwa Naibu Spika, dakika moja tu, kidogo tu.

**NAIBU SPIKA:** Sekunde 30 malizia.

**MHE. TABASAM H. MWAGAO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Tuna Chuo cha Ujenzi hapa Morogoro. Hiki Chuo cha Ujenzi wapelekwe sasa vijana wakasomeshwe pale *labour-based*. Hizi barabara zinazoletewa mabilioni ya shilingi wafundishwe *labour base* waje waanze kuchonga mitaro badala ya kila kitu wanapewa makandarasi wakubwa, haiwezekani hata kidogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mungu aibariki sana Tanzania na wewe Mwenyezi Mungu akupe maisha marefu, lakini bajeti ya Miundombinu isichokonolewe hata kidogo ....

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Tabasam.

**MHE. TABASAM H. MWAGAO:** Mheshimiwa Naibu Spika, pesa zake tunataka tujue nani aliyekuwa anatoboa hii *ring-fence* ili tuweze kuzuia.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba kuunga mkono hoja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Nilimtaja Mheshimiwa Livingstone Lusinde atafuatiwa na Mheshimiwa Abdallah Dadi Chikota, Mheshimiwa Athumin Mapalilo, ajiandae.

**MHE. LIVINGSTONE J. LUSINDE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru sana kwa kunipa nafasi ili nichangie katika Wizara muhimu sana kwa uchumi wa Taifa letu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukisoma Ilani ya Chama Cha Mapinduzi, ambacho ndicho Chama chenye Serikali na *slogan* zetu za muda wote, Chama hiki ndiyo chama kinachojenga nchi hii. CCM ni chama cha kujenga Taifa na ukweli ukija kwenye Wizara hii ya Ujenzi ikiongozwa na Mheshimiwa Ulega na Mheshimiwa *Engineer* Kasekenya, Katibu Mkuu na wenzake, utagundua kwamba Taifa linajengwa kila kona ya nchi yetu. Hata hizi kelele unazozisikia zinaonesha kwamba kila Mbunge ana hamu ya kuona eneo lake linafikiwa na maendeleo kwa namna yoyote.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nichukue nafasi hii kumpongeza sana Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa ajili ya kutenga fedha nyingi za kipaumbele cha kuhakikisha Taifa la Tanzania linafunguka na kufikika kila eneo.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunawapongeza watendaji wakuu wanaosimamia barabara. Kwa namna ya pekee nitakuwa mchoyo wa fadhila nisipomshukuru *Engineer* wa *TANROADS,* Mkoa wa Dodoma pamoja na mwenzake wa *TARURA*, Zuhura na mwenzake wanafanya kazi nzuri sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, kelele zinazopigwa zinaashiria nini? Kila Mbunge, angependa kuona barabara inamfikia. Ushauri wangu mimi; kwanza tumshauri Mheshimiwa Waziri, kumalizia kazi zote ambazo zimekwishasainiwa. Wamalizie kazi zote ambazo Serikali imeshasaini, tusije tukaonekana tunawapiga wananchi changa la macho. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lazima wafanye *review*. Makubaliano ya ujenzi wa barabara nyingi yalikuwa kabla ya vita kwa hiyo, gharama zilikuwa zipo chini. Sasa hivi kuna wajenzi wengi wamesimama kujenga kwa sababu ya gharama za mafuta kupanda. Ni lazima Serikali iende ikae nao, izungumze nao kuona ni namna gani hizo barabara zitaendelea kujengwa pamoja na ugumu wa hali uliopo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna barabara ambazo zimeshasainiwa, Mheshimiwa Waziri anafahamu. Mikataba imesainiwa, nazo ujenzi wake mpya uanze siyo tunapapikiza hii, hatujamaliza hii tunahamia hii, hapana. Twende kulingana na utaratibu ambao Serikali imepanga.

Mheshimiwa Naibu Spika, tukiacha hivyo tutakuwa na viporo vingi, mwisho wake kutakuwa hakuna sehemu ambayo tunaweza tukazungumza kwamba imekamilika. Tutakuwa kila sehemu ukifika unakuta kuna mashimo, kila sehemu ukifika unakuta kuna hiki, haitakuwa na maana. Twende tufunge mikanda tumalize kazi ambazo tayari Serikali imeshaingia mikataba.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninataka niwasihi Waheshimiwa Wabunge, wenzangu. Mimi nikiwa Mbunge si wa siku nyingi sana, miaka 20 siyo michache na Mjumbe wa *NEC*, tusiendekeze sana kuzungumzia ukanda, hili Taifa ni la kwetu. Tukiendekeza hiyo tutabomoa hii nchi, kila watu wana kanda yao na kila watu wana mahitaji kwenye kanda yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mipango mingi imefanyika Dar es Salaam na hapa Dodoma, lakini bado pesa zilikuwa zinakwenda kwenye mikoa mingine. Siyo kila mpango uliokuwa unapangwa ulikuwa unanufaisha Dodoma, lakini sisi tulivumilia. Kuna wenzetu wa mikoa kama Rukwa wamesubiri kwa muda mrefu kuona kipande cha lami, lakini bado walikuwa wanaunga mkono. Kwa hiyo, tukisema kila sehemu watu waji-*caucus* kwa ajili ya upande wao ninataka niwaambie tutavuruga Bunge na tutavuruga hili Taifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ni lazima tuwe na subira. Serikali kule ambapo imeshasaini mikataba, Serikali kule ambapo imeshaweka wakandarasi ipeleke nguvu za kutosha ili barabara zikamilike na wengine maendeleo yatawafikia. Hakuna Taifa linalojengwa lote kila sehemu. Tunajenga na maendeleo siyo barabara peke yake; kuna wengine wamepata zahanati na wengine wamepata meli. Sasa mimi Dodoma nitang'ang'ania tupate meli inapita wapi? *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo ni lazima tukubaliane kwamba maendeleo siyo kitu kimoja; maendeleo ni mchakato wa kila kitu. Kwa hiyo, jambo lingine ninalotaka kulizungumza hapa ni Mfuko wa Barabara. Mfuko wa Barabara uimarishwe, Mfuko wa Barabara hela zake zionekane, Mfuko wa Barabara usichanganywe mapato yake na Mifuko mingine, hii itatusumbua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tume-*ring-fence* hizi pesa zifanye kazi ya kuonekana. Wenzetu wa Serikali watuelewe, Waziri wa Fedha atuelewe kwenye jambo hili. Tunaposema Mfuko wa Barabara, tunataka tuone pesa zake zinafanyaje kazi kuanzia mwanzo wa mwaka mpaka bajeti inapokamilika. Hii itatusaidia sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la mwisho, wakandarasi wa ndani walipwe, wakilipwa hawa mzunguko wa pesa unakuwepo. Kila mtu anadai, kila mtu anadai, hii inakuwa siyo sawa. Tuheshimu watu ambao tumewapa kazi, tuheshimu wa nje, tuwaheshimu na wa ndani kwa sababu wote hawa wakifanya kazi matokeo yake uchumi wa nchi yetu, mzunguko unakuwa mzuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaunga mkono hoja, ahsante sana kwa kunisikiliza. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Lusinde. Nilimtaja Mheshimiwa Abdallah Dadi Chikota atafuatiwa na Mheshimiwa Athumin Mapalilo, Mheshimiwa Mary Francis Masanja ajiandae.

**MHE. ABDALLAH D. CHIKOTA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru kwa kunipa nafasi ili nichangie hoja iliyopo mezani. Kwanza ninapenda kuchukua nafasi hii kumshukuru Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kazi kubwa anayoifanya katika kutoa maelekezo ya Wizara hii ya Ujenzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kipekee nimpongeze Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa uteuzi wake wa wasaidizi wake katika sekta hii. Kuna Mheshimiwa Waziri, Ulega ambaye utendaji wake wa kazi hauna mashaka. Ni mbunifu, ni mvumilivu na ni mtu ambaye yupo *field*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, wote watakuwa mashahidi Mheshimiwa *Engineer* Kasekenya jinsi anavyozifahamu barabara, kuanzia Rusumo mpaka Mto Ruvuma kwenda Msumbiji. Siyo hivyo tu, tuna *Engineer,* Mwanadiplomasia Balozi ambaye ni Katibu Mkuu wa Wizara hii, *Engineer* Aisha. Ni mtendaji ambaye hana papara na ana maamuzi ambayo yanalisaidia Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niendelee kumshukuru Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa kazi anayoifanya katika Mkoa wetu wa Mtwara. Mkoa wa Mtwara, tumeshuhudia miradi mikubwa ambayo inaendelea kujengwa katika eneo letu. Nikianza na Barabara ya kilomita 160 ya Mnivata – Mitesa mpaka Masasi, barabara ambayo ina wakandarasi wawili na gharama yake ni shilingi 345,000,000,000. Tunakushukuru sana kwa kazi ambayo inaendelea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara hii ni muhimu kwetu, kwa sababu ndiyo korido ya korosho kwa nchi hii. Ilijengwa kilomita 50, lakini Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, alipoingia akasema nitamaliza zote kilomita 160 na ujenzi unaendelea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, siyo hivyo tu, kuna kilomita 210 kutoka Mtwara – Mingoyo hadi Masasi. Kuna wakandarasi wawili wapo *site* na kazi inaendelea; tunakushukuru sana Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan. Mama kule amepeleka shilingi 365,000,000,000 na wakandarasi wapo *site* na hizo ni fedha za Benki ya Dunia. Ile Barabara ya Mnivata - Newala hadi Masasi ni

fedha za *ADB*, wakandarasi waki-*raise certificate* malipo yanafanyika mara moja na kazi inaendelea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nimwombe Mheshimiwa Ulega, wakandarasi hawa wanne, kuna mkandarasi mmoja wa Mnivata kwenda Nanyamba - Tandahimba na Newala analegalega. Alikuja mara ya kwanza akampa maelekezo, bado kasi yake siyo ya kuridhisha. Hebu aingie kazini, tutapitisha fedha zake hapa aende akamsimamie zaidi barabara ikamilike. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, siyo hivyo tu, wote watakuwa mashahidi Bunge lililopita tulishuhudia ndugu yetu Mheshimiwa Bashungwa, wakati ule akiwa Waziri wa Ujenzi, alivyokuwa amelala pale Somanga na madaraja mengine ya barabara kuu wakati imetokea mafuriko. Sasa hivi madaraja yote yamekamilika. Ninampongeza sana Mheshimiwa Ulega, kwa usimamizi wako mzuri na zaidi ya shilingi 67,000,000,000 zimetumika katika kutengeneza madaraja hayo. Tunakushukuru sana Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kazi uliyobakiwa nayo Mheshimiwa Ulega; utapata fedha *ADB*, utapata fedha Benki ya Dunia, utapata fedha kwenye huo mradi wa hatifungani. Kwa kuwa madaraja umeshakamilisha tayari, anza sasa ujenzi wa barabara hiyo ya Dar es Salaam hadi Lindi, kwa sababu barabara hiyo sasa ni muhimu kiuchumi.

Mheshimiwa Naibu Spika, tuna bandari yetu ya uvuvi, lakini Bandari ya Mtwara sasa hivi kuna mzigo umeongezeka na vilevile tuna shughuli ya makaa ya mawe ambayo yanatumika kwenye barabara hii. Kwa hiyo nimwombe, sina mashaka na wewe kwa sababu barabara hii sisi tunakusemea, inatoka Dar es Salaam hadi Mkuranga jimboni kwa Waziri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ni matarajio yetu kwamba Waziri atakapokuja kufanya majumuisho, atatuambia kwamba shilingi ngapi zimetengwa kwa ajili ya ujenzi na Ilani yetu ya Chama Cha Mapinduzi imesema ndani ya miaka mitano itakamilisha. Ni

matarajio yangu kwamba kwa miaka mitano hii tutaipangilia vizuri jinsi tutakavyojenga Barabara yetu ya Dar es Salaam hadi Lindi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukijumlisha hizo takwimu zote utapata zaidi ya 765,000,000,000. Tunamshukuru sana Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa uwekezaji huo na ufunguaji huo wa mikoa yetu ya Mtwara na Lindi. Mheshimiwa Waziri kama nilivyokwambia, kazi yako sasa, sisi hatujui fedha umezitoa wapi, uanze kidogo kidogo kuijenga hiyo barabara ya Dar es Salaam hadi Lindi.

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara ya pili ambayo nitaizungumzia ni Barabara yetu ya ulinzi kutoka Mtwara - Newala hadi Songea kilomita 350. Changamoto zilizopo mpakani Waziri anazifahamu na barabara hii ni muhimu sana, sisi tuliopo kule tunajua umuhimu wa barabara hii. Wameanza ujenzi wa madaraja na baadhi ya sehemu kwa lami.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni muda mwafaka sasa hivi kutenga fedha ili barabara yetu hii nayo ijengwe ili vyombo vyetu vya ulinzi na usalama vinafanya operesheni wapite kwenye barabara ambayo inapitika katika kipindi chote cha mwaka. Ni matarajio yangu kazi ambayo Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa sababu ameanza na ujenzi wa madaraja sasa ataenda kwenye ujenzi wa kiwango cha lami ili kuhakikisha vyombo vyetu vinafanya kazi ya ulinzi kwa usalama na kwa muda wote na barabara ambayo inapitika katika kipindi chote cha mwaka.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaunga mkono hoja, kesho wakati anajumuisha Mheshimiwa Ulega atwambie tu ataanza na kilomita ngapi kutoka Dar es Salaam kwenda Lindi. Ninakushukuru sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Chikota. Nilimtaja Mheshimiwa Athumin Omary Mapalilo, atafuatiwa na Mheshimiwa Mary Francis Masanja na Mheshimiwa Haran Nyakisa Sanga ajiandae.

**MHE. ATHUMIN O. MAPALILO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuchangia katika Wizara hii ya Ujenzi. Awali ya yote, ninapenda kumpongeza Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa kazi kubwa ambayo anaifanya hasa katika uwekezaji wa ujenzi wa barabara kule katika Mkoa wetu wa Mtwara. Sisi wananchi wa Mkoa wa Mtwara, tunamshukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninamshukuru pia Mheshimiwa Waziri na kumpongeza kwa kazi kubwa ambayo anaifanya ya usimamizi wa ujenzi wa miradi ya barabara. Sisi wananchi wa Mkoa wa Mtwara hasa mikoa ya kusini ya Lindi na Mtwara, tunashukuru kwa ujenzi ambao umefanyika kwa yale maeneo korofi ya barabara hasa kutoka Barabara kuu ya Dar es Salaam kuelekea Lindi.

Mheshimiwa Naibu Spika, yale maeneo yamekuwa korofi kwa wakati fulani tulikuwa tunapata sonona tukiwa katika mabasi, tukiona wingu kubwa la dalili ya mvua tunaanza kuwaza tutapita vipi? Tulikuwa tunatembea nguo mkononi na wakati mwingine tulikuwa tunalala wiki nzima hatuvuki. Mheshimiwa Rais ametusaidia, amejenga yale maeneo korofi na hayapo tena, ile shida haipo tena. Sasa katika msimu huu wa mvua hatujapata shida tumeweza kuvuka vizuri kabisa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sisi wananchi wa Mkoa wa Mtwara tunatambua uwekezaji mkubwa wa barabara zetu ambazo ziko katika mkoa wetu. Hasa barabara ambayo inatoka Mtwara kuelekea Mnazi Mmoja imetengewa kiasi cha shilingi 150,000,000,000 na tayari mkandarasi yuko barabarani anafanya kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tunayo pia barabara yetu kutoka Mnazi Mmoja kwenda Masasi na yenyewe hali kadhalika mkandarasi ameanza kazi kwa gharama ya shilingi 200,000,000,000. Kwa kweli tunamshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa kazi kubwa ambayo anaifanya na tunamtia moyo kwa sababu kwisha kwa barabara hizi kutatufanya sisi tuweze kusafiri

vizuri, mazao yetu na biashara na uchumi wa Mikoa ya Kusini Lindi na Mtwara itafunguka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na mazuri haya ambayo yanafanywa na Serikali yetu Tukufu, nina maombi mawili kwa waziri husika; ombi la kwanza, ni barabara ya Nivata - Tandahimba. Ile barabara bado haipo vizuri na msimamizi mkandarasi ambaye alikuwa anahusika ametoka kwa muda mrefu, ujenzi umekwama.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kweli tunaomba Mheshimiwa Waziri, mtani wetu Mheshimiwa Ulega, ufanye neno, useme neno katika barabara hii. Useme ni lini tunaweza kupata barabara hii na itakamilika kwa kiwango cha lami ambacho Mheshimiwa Rais ametuahidi sisi wananchi tuweze kupata tabasamu nene?

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja yangu nyingine ni ile Barabara ya Ziwani kuelekea Msimbati. Sote tunafahamu jinsi ambavyo umuhimu wa ile barabara ulivyo. Kule kuna uwekezaji mkubwa sana, kule Msimbati ndiko ambako sehemu ambayo miradi ya gesi inafanyika kule, visima vya gesi vipo kule, lakini pale Madimba ndipo sehemu ambayo uchakataji wa gesi unafanyika kule.

Mheshimiwa Naibu Spika, wawekezaji wengi sana wako pale na wanafanya biashara kubwa sana, wanachakata gesi kwa ajili ya mustakabali wa Taifa letu. Ninaomba Mheshimiwa Waziri ashirikiane na Waziri mwenzake ambaye anahusika na nishati ya gesi waweze kukaa pamoja, watafakari na waone namna bora ya kuwaendea wale wawekezaji ili sasa wajadiliane na waone, wawashawishi tuweze kupata msaada wa kujengewa barabara ile kutoka Ziwani kuelekea Msimbati.

Mheshimiwa Naibu Spika, kukamilika kwa barabara ile kutawasaidia hata hao wawekezaji kufika kwa urahisi na kufanya shughuli zao kwa weledi kabisa. Tukumbuke kwamba barabara ile ndiyo barabara ambayo inaunganisha *border* ya Kilambo, inaenda moja kwa moja mpakani Msumbiji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tunayo rasilimali kubwa pale ya gesi. Endapo kama hakupitiki vizuri, ina maana ulinzi na usalama wa eneo letu utakuwa mdogo. Ninamwomba sana Mheshimiwa Waziri aweke kipaumbele katika hili ili tuweze kupata barabara ile kwa kiwango cha lami kwa ajili ya ulinzi wa rasilimali yetu ya gesi, lakini pia ulinzi wa jamii yetu kwa sababu tuko mpakani.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi na ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Athumin Omary Mapalilo. Nilimtaja Mheshimiwa Mary Francis Masanja, atafuatiwa na Mheshimiwa Haran Nyakisa Sanga na Mheshimiwa Deodatus Philip Mwanyika ajiandae.

**MHE. MARY F. MASANJA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii ili nichangie bajeti hii ya Wizara ya Ujenzi. Awali ya yote, nianze kwa kumshukuru sana Mwenyezi Mungu, mwingi wa rehema ambaye ametujalia afya njema na leo tuko hapa kwa ajili ya kujadili bajeti hii ya Wizara ya Ujenzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa ni mara yangu ya kwanza tangu tuingie katika Bunge lako hili la Kumi na Tatu, nianze kwa kumshukuru sana sana Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Mwenyekiti wa Chama chetu Cha Mapinduzi pamoja na Kamati Kuu kwa kuridhia na kuniteua kuwa miongoni mwa Wabunge wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Ninawashukuru sana sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nimpongeze sana sana Mheshimiwa Dkt. Emmanuel Nchimbi, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa namna ambavyo anaendelea kumsaidia Mheshimiwa Rais kuhakikisha kwamba Ilani ya Chama Cha Mapinduzi inatekelezwa ipasavyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, nimshukuru na kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri Mkuu, Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Nchemba kwa kazi kubwa anayoifanya ya kuwafikia

wananchi na kutatua changamoto mbalimbali na hii inaonyesha kwamba kaulimbiu ya kazi na utu tunasonga mbele inatekelezwa kwa vitendo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kipekee kabisa niwashukuru sana sana Wanamwanza hususani akina mama walionichagua na kunipa kura nyingi kuja kuwawakilisha nami niwaahidi tu kwamba sitawaangusha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nimpongeze sana sana Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Naibu Waziri, lakini bila kumsahau Meneja wa Mkoa wa Mwanza wa *TANROADS*. Meneja anafanya kazi kubwa sana sana, amesimamia miradi mikubwa na ya kimkakati hususan Daraja la Busisi - Kigongo. Ninampongeza sana Bwana Ambrose, ni mtu bomba sana na Mungu aendelee kumbariki na kikubwa tuendelee kuwatia nguvu na moyo watendaji wanapofanya kazi nzuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, nianze kuchangia hotuba ya ujenzi. Tukiangalia historia ya kuanzishwa kwa Wakala wa Barabara *(TANROADS)* tangu mwaka 2000 mpaka sasa si uongo wakala wa barabara wamefanya kazi kubwa sana na tuna haja ya kuwapongeza sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninasema hivyo kwa nini? Tulikuwa na changamoto kubwa za kuunganishwa barabara kimkoa. Wakala wamefanya kazi kubwa sana ya kuhakikisha sasa hivi nikitaka kwenda Katavi nitafika, nikisema leo ninakwenda Lindi - Mtwara nitafika, hii yote ni juhudi za makusanyo mazuri na usimamizi mzuri wa fedha hizi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba Serikali, kwa kuwa tangu mwaka 2000 lengo la kuanzishwa wakala huu ilikuwa ni kuzikusanya fedha hizi na ziende moja kwa moja kwenye Mfuko na kwenda kutekeleza miradi ya barabara. Tunaomba fedha hizi zianze kufikishwa moja kwa moja kwenye Mfuko wa Barabara ili kurahisisha hata hizi kelele ambazo kila mtu anataka barabara kwake itengenezwe, tupunguze hata maswali mengi Bungeni. Ninamwona kila siku Mheshimiwa Naibu Waziri namna ambavyo

anaona mikono tunavyonyanyua ni kwamba kila mtu kwake kuna changamoto.

Mheshimiwa Naibu Spika, niendelee kumshukuru sana sana na kumpongeza Dkt. Samia Suluhu Hassan. Mwanza tunajivunia yeye, kwa nini ninasema hivyo? Tangu kukamilika kwa Daraja la Kigongo - Busisi, si uongo uchumi wa kanda ya ziwa na mikoa yote ya kanda ya ziwa, lakini ukiacha hilo Nchi jirani za Rwanda, Burundi, Uganda na Kongo wanapita katika daraja hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na kwamba daraja hili sasa linatumika vizuri, haipendezi daraja likiwa limeboreshwa ilihali foleni ya kutoka Mwanza Mjini kuja pale Usagara mpaka kwenda Kigongo ni kubwa. Tunaiomba Serikali iharakishe upanuzi wa barabara hii kwa njia nne kutoka Mwanza Mjini mpaka Usagara na kwenda Kigongo - Busisi ili kurahisisha na kufungua uchumi uendelee kufika hata kwenye nchi za jirani.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukiacha hilo barabara hizi ni pacha. Ukifungua ya Mwanza Mjini kuja Usagara ukaiacha ya Mwanza Mjini kwenda Kisesa, unakuwa umetengeneza tena *congestion* kubwa ya magari ambayo pia itasababisha msongamano wa magari na kusababisha kutofikika kikamilifu kwa maana ya kupita kikamilifu.

Mheshimiwa Naibu Spika, niende moja kwa moja pia katika barabara inayotoka Magu katika Mtaa wa Isandula, Ngudu mpaka Nhungumalwa. Barabara hii tangu ilani ya uchaguzi iliyopita na nyingine huko hii ni ilani ya tatu, barabara hii ilishaingizwa kwenye ilani na ilani iliyopita ilikuwa tayari wameshaweka mkandarasi na alikuwa anafanya kazi. Tangu aanze kufanya kazi hajawahi kulipwa hata senti hivi ninavyoongea.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaiomba Serikali, ninamwomba Mheshimiwa Waziri Ulega, tafadhali mkandarasi kule anachanganyikiwa. Alipwe angalau *advance* ili barabara hii iweze kuanza na wananchi wanaopita katika Barabara ya Magu - Ngudu mpaka Nhungumalwa tuweze kuwafungua hawa wenye

Wilaya ya Kwimba na Sumve nao waweze kufurahia matunda ya dunia hii. Hawa watu tangu uhuru hawajawahi kuiona lami. Ninaomba chonde chonde tuone hilo.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa muda umekwisha, ninaomba uhitimishe.

**MHE. MARY F. MASANJA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba sasa kwa kumalizia tuna vivuko na nimeona wametenga fedha kidogo sana, lakini viko 90%, 98% lakini wananchi wanaendelea kutumia mitumbwi ya kawaida kuvuka.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba sana sana, dakika moja, kuna Vivuko vya Ijinga - Kahangala kiko 91%, kuna Kivuko cha Nyakalilo - Kome kiko 90% na kuna Kivuko cha Bwiro - Bukindo kiko 98%. Tunamwomba Mheshimiwa Waziri vivuko hivi viweze kuanza kufanya kazi ili tuweze kuokoa maisha ya wavuvi na wananchi wanaokaa kwenye visiwa.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Mary.

**MHE. MARY F. MASANJA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Nimemtaja Mheshimiwa Haran Nyakisa Sanga, atafuatiwa na Mheshimiwa Deodatus Philip Mwanyika na Mheshimiwa Phillipo Augustino Mulugo ajiandae.

**MHE. HARAN N. SANGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote, niungane na wachangiaji wenzangu waliopita kumshukuru Mwenyezi Mungu, mwingi wa rehema anayetujalia afya na nguvu na hatimaye kuendelea kufanya kazi za wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, ninataka nimpongeze sana Rais wetu Dkt. Samia Suluhu Hassan, mama jemadari ambaye ametoa fedha ambazo zimesambaza mtandao wa barabara nchi nzima, lakini pia hususani katika Jimbo langu la Kigamboni

ametupa 68,000,000,000 ambazo zimeweza kwenda kutekeleza madaraja manne, daraja la Nguva, Cheka, Tungi pamoja na Kigamboni.

Mheshimiwa Naibu Spika, leo tunachangia bajeti ya Wizara ya Ujenzi, nami nilipita nikaangalia dira ya Wizara inasema kuwa na miundombinu bora na endelevu inayowezesha maendeleo ya kiuchumi na jamii. Nikasoma majukumu yake nikachukua mawili, kusimamia utekelezaji wa sera na ujenzi na usalama barabarani, lakini pia kusimamia ujenzi na uendeshaji wa vivuko.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya wananchi wa Kigamboni, kila mtu anaelewa jiografia ya Wilaya ya Kigamboni au Jimbo la Kigamboni ilivyo kwamba imekaa kama kisiwa. Katika kupitia hii bajeti ninaomba niongelee vitu viwili tu; nitaongelea vivuko ambavyo vya boti pamoja na vivuko vya Daraja la Mwalimu Nyerere.

Mheshimiwa Naibu Spika, wananchi wa Kigamboni ni wananchi ambao wanaishi maisha ya fedha kila siku. Tunaposema maisha ya fedha, bila shilingi mia mbili au mia tano Kigamboni huwezi kufika. Waziri amewasilisha bajeti yake. Pale Kigamboni tulikuwa na vivuko vitatu, tulikuwa na Kigamboni, tulikuwa na *MV Kazi*, tulikuwa na *MV Magogoni*. Hivi sasa tunavyozungumza kivuko kimoja cha *MV Kazi* ambacho kinafanya kazi masaa 24 na zile *sea taxis* ambavyo viko vya mwekezaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo, vivuko vile bei ni shilingi 500 na bei ya zile pantoni za kawaida ni shilingi 200. Wananchi wengi hawawezi kumudu shilingi 500 kama wanavyojua kwamba haya maisha yamepanda gharama kidogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukisema wewe una gari upite uende Kigamboni, kama hutaki kulipa tozo ni dhahiri uende Mkuranga, utoke Kigamboni, uende Tuangoma, Kongowe, Mbagala ndiyo uweze kupita bila kulipa fedha. Pale kwenye Daraja la Mwalimu Nyerere hakuna mwananchi yeyote ambaye anaweza akapita pale bila kutoa tozo.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi ni muumini sana wa sekta binafsi, lakini lazima uangalie maisha ya Watanzania hususani Wanakigamboni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jana tulipata taarifa hapa kutoka kwa Naibu Waziri Kasekenya akasema Mradi wa Daraja la Mwalimu Nyerere pale Kigamboni ni mradi ambao una mchango 40% za Serikali na 60% za Mfuko wa Hifadhi.

Mheshimiwa Naibu Spika, leo niko hapa ninamwomba sana Mheshimiwa Waziri, kwa kweli siwezi kuhitimisha hii bajeti, nitashika mshahara wake mpaka tuelewane. Ile 40% ya Serikali kwa nini tusiitoe Serikali ikabeba mzigo wa wananchi wa Kigamboni ikawa ni sehemu ya fedha ambazo zinajenga barabara mahali pengine Tanzania? Ili tuweze kupata punguzo la tozo za pale kivukoni.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukibeba chakula kutoka Kariakoo kupeleka Soko la Kibada, lazima pale utalipa shilingi 7,000 kwenye gari. *Imagine* mtu ametoka amechukua maparachichi na matikiti maji, anapeleka sokoni na pale analipa. Kule sokoni atauza shilingi ngapi? Lazima maisha yatakuwa juu kwa sababu pale analipa fedha.

Mheshimiwa Naibu Spika, ombi langu kwa niaba ya wananchi, tufike mahali kama Serikali tuangalie vitu ambavyo vinatoa huduma kwa wananchi kama daladala, kama haya malori yanayopeleka chakula katika masoko yetu, yapite bure ili kuweza kuendana na maisha ya Watanzania na wananchi wa Kigamboni.

Mheshimiwa Naibu Spika, niseme tu, nimeona Mheshimiwa Waziri akiwa amezungumza kwamba kuna upanuzi mkubwa sana wa barabara za Nchi ya Tanzania. Ametaja Singida, Lindi, Songea na Dar es Salaam *(Mandela Road)*. Kitu ambacho ninataka niseme, Mkoa wa Dar es Salaam ni mkoa wa kibiashara. Ule mkoa tunavyozungumza sasa hivi kuna foleni; huwezi kupanga kwenda mahali Dar es Salaam ukasema nitaenda baada ya saa moja nimefika, huwezi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mfano, ile *Mandela Road*, sasa hivi naona Wizara imefika hatua ya kwamba wanaipanua ili waweke mpango wa *BRT*. Lakini lazima tuwe *very strategic* katika kujenga hizi barabara. Maoni yangu ni kwamba ile barabara, ingekuwa ni *exit* barabara ya malori tu yanayoenda bandarini na kutoka ili kufungua bandari yetu iweze kupunguza mizigo. Ukifanya hivyo tutakuwa tumepunguza foleni kwa kiasi kikubwa sana Dar es Salaam. *Imagine* kama meli moja inaweza ikashusha kontena pale ambalo linaweza likashusha magari 2,000. Yale makasha 2,000 yanahitaji malori 2,000 *flatbed* ili ziweze kuchukua ile mizigo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa kama yale malori yamepangwa yako 2,000 barabarani, unategemea Kigamboni utavuka vipi? Unategemea mjini utazunguka vipi? Kwa hiyo, niiombe Serikali iangalie upya mradi wa ujenzi wa barabara kutoka pale bandarini kuelekea *Mandela Road* badala ya kuweka *BRT* basi tuweke *exit* ya malori ili yaweze kutoka bandarini yatoe mizigo.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Sanga muda wako umekwisha.

**MHE. HARAN N. SANGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba nimalizie basi. *(Kicheko)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, leo wachangiaji wapo wengi sana, kengele ya pili ikilia, ninaomba uishie hapo.

Unga mkono hoja tuendelee Mheshimiwa.

**MHE. HARAN N. SANGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja, lakini nitashika shilingi ya Mheshimiwa Waziri. *(Kicheko)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Deodatus Phillipo Mwanyika atafuatiwa na Mheshimiwa Phillipo Augustino Mulugo na Mheshimiwa Joseph Enock Tama ajiandae.

**MHE. DEODATUS P. MWANYIKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru. Awali ya yote ninamshukuru sana Mheshimiwa Ulega kwa bajeti aliyoi-*present* leo.

Mheshimiwa Naibu Spika, mambo mengi sana yamefanyika katika Jimbo la Njombe Mjini, lakini ni wazi kwamba tuna changamoto kubwa sana ya barabara. Tumeshaongea barabara nyingine, lakini barabara kubwa ambayo yote mengine yaliyofanyika yanaonekana kama siyo makubwa sana na pengine hayawasaidii wananchi, jambo ambalo mimi mbunge sikubaliani nalo ni kama Barabara ya Itoni-Lusitu haitakamilishwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, tuna Barabara ya Itoni - Lusitu. Barabara hii ni kilomita 50 tu. Ni barabara kubwa, barabara ya kiuchumi, ni barabara ambayo tunafahamu kabisa umuhimu wake kiuchumi. Mimi nitasema kwa kuonesha umuhimu. Ninajua kila Mbunge anataka barabara yake ikamilishwe na kila barabara ni kipaumbele. Hata hivyo, mwaka tulioingia hapa 2021, tulijenga hoja ya kuwa na *Planning Commission*. Madhumuni ya kuwa na *Planning Commission* ni kutusaidia kuweka vipaumbele. Ili miradi ya vipaumbele iangaliwe kwanza.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata kama miradi ni mingi lakini miradi ya vipaumbele ambayo *Planning Commission* wataiona inafaa ndiyo ipewe fedha na mingine itafuata kwa sababu yote ni muhimu. Kama kuna eneo ambalo ni kipaumbele cha nchi hii ni kufufua na kuhakikisha Liganga na Mchuchuma inafanya kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ili jambo hilo litokee ni lazima miundombinu ya barabara ikamilike. Ndiyo maana sisi Wananjombe tunamshukuru Rais, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan. Barabara ya kutoka Njombe kwenda mpaka Manda kilomita 114, ina *lot* tano. *Lot* moja ya namba tatu imekamilika. Ili

barabara i-*make sense* lazima *lot* namba moja ikamilike ambayo ndiyo Itoni – Lusitu, yenye urefu wa kilometa 50. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tulimwomba sana Mheshimiwa Rais akiwa Makamu wa Rais alipita kwenye barabara hiyo, akija kwenye kampeni, akaona umuhimu na ikawa barabara moja ya mwanzo kabisa kupewa fedha. Tumesaini mkataba 2022 mwezi Agosti. Barabara hiyo ikaanza ujenzi. Tunaishukuru Serikali, iliona umuhimu, ikaanza ujenzi kwa kasi kubwa sana. Ndani ya mwaka mmoja walikuwa wamefanya kazi nzuri ya karibu 22% ilikuwa ifike 23%, lakini 2023 barabara imesimama, mpaka leo hakuna mkandarasi.

Mheshimiwa Naibu Spika, tumeiambia Serikali imrudishe, ilipe fedha mkandarasi aendelee na kazi, kwa sababu mambo ya Liganga na Mchuchuma yameshaanza kuiva. Siyo hilo tu, wawekezaji ukiacha wale wakubwa wa Hongda wa Liganga na Mchuchuma, tuna wawekezaji wengine ambao tayari wameshaanza ujenzi na wameanza kupeleka mitambo kwenye Maganga Matitu na wamejenga *yard* kubwa na *facility* ya ku-*process* Makambako. Wote hawa hawawezi kufanya kazi kama kilomita 50 za barabara zikiwa hazifanyi kazi au hazijajengwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa kwenye bajeti nimeiona imewekewa shilingi bilioni 4.1. Ninaishukuru Wizara kwa kuanza. Tunaelewa ni barabara ya zege, kilomita moja ya barabara ya zege ni karibu shilingi 3,000,000,000.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, ni wazi kwamba inahitaji fedha nyingi zaidi, lakini barabara hii ni ya kimkakati kwa sababu tukiweza ku-*explore* chuma, tukaenda ku-*process*, tukauza chuma, tuna uhakika kwamba tutapata *revenue* itajenga na barabara za mikoa mingine na Nchi ya Tanzania kwa ujumla wake. Kwa hiyo, niombe; ukiangalia madaraja yote yanahitaji chuma, *SGR* chuma, meli chuma, maghorofa chuma.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, ndiyo maana *Planning Commission* waliiweka kama barabara moja ya muhimu sana. Nimwombe Mheshimiwa Ulega, barabara hii ina kila sababu ya

kupewa kipaumbele katika barabara tatu kubwa hapa nchini, inatakiwa iwe ni mojawapo. Niombe sana, barabara hii mkandarasi atakapoanza na hatujamwona bado akiwa ameanza rasmi. Tuliambiwa mvua zikiisha atarudi *site*, hatujamwona *site* na mvua Njombe zimekwisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, tuombe kuanzia mapema inavyowezekana ndani ya mwezi huu na unaokuja, wananchi wa Njombe wanataka kuona mkandarasi akiwa *site*, kwa sababu tumeshaambiwa kwamba fedha yote ameshalipwa. Kwa hiyo, tunangoja aje *site*. Ninamshukuru Mheshimiwa Ulega, ilikuwa aje Njombe kwa ajili ya kuhakikisha jambo hili linatokea, mambo hayakuweza.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninategemea baada ya Bunge tutakuwa pamoja Njombe, tukamilishe ile safari ya kuhakikisha barabara hii inaanza. Ni barabara kubwa, lakini siyo chuma tu. Barabara hii ndiyo yenye uchumi mzima wa Njombe na Ludewa. Hatuwezi kuwa na uchumi bila barabara hii kukamilika. Niombe sana tukamilishe.

Mheshimiwa Naibu Spika, Barabara ya pili ni Makambako - Songea. Kama alivyosema Mwenyekiti wa Kamati, Barabara ya Makambako - Songea ni barabara kubwa sana. Ni barabara ambayo ilijengwa mwaka 1984, ikazinduliwa 1986. Barabara hii imekwisha haina ubora tena. Barabara hii inatakiwa ijengwe upya. Tupende tusipende, ni moja ya barabara ambazo Kamati imeiongelea. Nimwombe sana Waziri, barabara hii ya Makambako - Songea na yenyewe ianze. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tunajua fedha zimepatikana upande wa Songea, lakini kuanzia Lutukila mpaka Makambako kilomita kama 113, bado haina fedha. Tuwaombe sana na yenyewe iwe katika moja ya vipaumbele vikubwa, kwa sababu ni barabara inayofungua uchumi mkubwa. Ni barabara ambayo unapotaka kuchukua vitu kupeleka Mtwara kwenye bandari yetu kubwa, lazima vipite kwenye barabara hii. Ni barabara ambayo na yenyewe itatumika katika shughuli ya chuma, lazima ipite katika barabara hii. Kwa hiyo, tuwaombe ipewe kipaumbele

kama vile barabara hii, lakini ianze Itoni kwanza, maana yake Itoni hiyo inagusa maisha hata ya wananchi wa kawaida.

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara nyingine ataiongelea mdogo wangu Mheshimiwa Swale, Barabara ya Njombe - Lupembe. Barabara hii ni barabara muhimu sana. Inaunganisha na kufungua Mkoa wa Njombe pamoja na Mkoa wa Morogoro na kupunguza umbali wa kufika Dar es Salaam ambako sisi Wananjombe, Wanambeya na Wanarukwa ndiyo tunawalisha watu wa Dar es Salaam. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tuwaombe sana barabara hii tunajua kwamba iko katika mchakato wa kukamilishwa. Barabara hii inapita katika jimbo langu na jimbo la Mheshimiwa Swale kwa pamoja. Kwa hiyo, ninaihitaji hii barabara, Wananjombe wanaihitaji hii barabara na yenyewe ianze. Ninaambiwa hapa hata wa Mwanza wanaihitaji hii barabara, kwa sababu wanahitaji vyakula kutoka Njombe. Tumwombe sana Mheshimiwa Ulega, katika barabara za vipaumbele vya kiuchumi na siyo uchumi wa Njombe, uchumi wa nchi, barabara hizi tatu nilizozitaja ni barabara za muhimu sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tuwaombe sana barabara hizi zikamilike. Tunafahamu uhalisia wa upatikanaji wa fedha. Nimalizie kwa kutoa ombi. Wengi wamelisema hapa, mimi ni muumini sana wa sheria. *I believe in the rule of law.* Tumetunga sheria ya ku-*ringfence* mapato yanayokwenda kwa ajili ya kutengeneza barabara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kulikuwa na sababu kubwa za msingi kwa nini tulifanya hilo jambo. Tunafanya kitu kinaitwa *self-inflicted injury. We inflict injury into ourselves* kwa kujaribu kwenda kinyume na sheria tuliyoitunga. Mimi kama Mbunge, ninakubaliana na Wabunge wenzangu wote ni wakati sasa *ringfencing* tuiheshimu ili barabara hizi ziweze kujengwa. Barabara ambayo inahitaji kujengwa siyo hii peke yake, ni barabara nyingi ambazo zimekwisha muda wake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tusiporudi kwenye misingi ya kuheshimu *ringfencing,* hatutakuja kuwa na fedha za kutosha za kuhudumia hizi barabara. Uchumi wowote bila barabara ni wazi kwamba hatuwezi kufanikiwa kujenga Uchumi na dira yetu inatuambia twende mbele.

Mheshimiwa Naibu Spika, nadhani bado niko ndani ya muda. Dira yetu inatuambia tunahitaji kuhakikisha kwamba, *private sector* unachangia 70% ili tuweze kuinua uchumi na tuweze kupata zile dola 1,000,000,000,000. Bila *infrastructure* hilo jambo halitawezekana. Ndiyo maana ni muhimu tukahakikisha kwamba *ringfencing* tunaiheshimu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Nilimtaja Mheshimiwa Phillipo Augustino Mulugo, atafuatiwa na Mheshimiwa Joseph Enock Tama na Mheshimiwa *Engineer* Johnston Johansen Mutasingwa ajiandae.

Mheshimiwa Joseph Enock Tama, atafuatiwa na Mheshimiwa *Engineer* Johnston Johansen Mutasingwa na Mheshimiwa Hamisi Shabani Taletale, ajiandae.

**MHE. JOSEPH E. TAMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ili niweze kuchangia bajeti hii muhimu ya Wizara ya Ujenzi. Nianze kwa kuweka sawa jina langu lisomeke Joseph Enock Tama, Mbunge wa Jimbo la Kaliua sauti ya wanyonge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nimesimama leo kwanza nikiwa na furaha, kwa sababu ninaitazama Tanzania yangu ya miaka 60 iliyopita na leo katika sekta ya miundombinu ya barabara ni vitu viwili tofauti. Ni wazi tumetoka mbali, tuna kila sababu ya kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kazi kubwa aliyoifanya. Ni kweli huenda kukawa tuna changamoto nyingi hata jimboni kwangu zipo barabara ninazozihitaji, lakini kwa kazi kubwa ambayo imefanywa na Wizara ya Ujenzi kutoka moyoni mwangu nawashukuru sana, ninawapongeza sana na

ninawaombea kwa Mwenyezi Mungu, wachape kazi bila kuchoka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Waziri ana timu nzuri, ana Katibu Mkuu mchapakazi, mwanamama Balozi Aisha na Naibu wake Dkt. Charles Msonde, wanafanya kazi nzuri sana. Rai yangu mwendelee kujituma na kuitanguliza Tanzania kwanza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sisi watu wa Tabora, hususan kwenye Jimbo langu la Kaliua miaka ya nyuma ilikuwa watu wanaokwenda Kigoma walikuwa wanalala Kaliua. Leo ni mkeka, ukitoka asubuhi saa 12 Tabora, unakunywa chai Kigoma saa nne. Haya ni maendeleo, tunahitaji tuwatie moyo watendaji kazi wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaishukuru Wizara kwa kukamilisha kipande cha Kaliua - Kazilambwa chenye kilomita 56, eneo lililokuwa linatupa changamoto sana, imetandikwa lami shughuli zinaendelea na wananchi wanaendelea kutabasamu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaishukuru Wizara, ninaishukuru Serikali kwa kipande cha Urambo kuja Kaliua chenye urefu wa kilomita 28, maisha yetu yanakwenda vizuri na shughuli za uchumi zinasonga. Hiyo haitoshi, ninaishukuru Serikali kipande cha kutoka Ugansa kwenda Usinge kimetandikwa lami, chenye kilomita 7.4. Ndiyo maana nimesema nina furaha na Serikali yangu ya Chama Cha Mapinduzi, nina kila sababu ya kuipongeza, nina kila sababu ya kuunga bajeti hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lipo ombi langu na leo nimefurahi kuiona barabara ya kimkakati ya uchumi, barabara inayounganisha mikoa takriban minne: Mkoa wa Katavi, Mkoa wa Tabora, Mkoa wa Shinyanga na Mkoa wa Geita. Barabara hii ni Barabara ya Mpanda – Ugalla – Kaliua – Ulyankulu - Kahama. Ninampongeza sana Mheshimiwa Waziri kwa kuitengea fedha. Ombi langu, ombi langu, ombi langu kwa mara ya tatu, ujenzi uanze, kazi ianze kufanyika.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli ili tuweze kuifikia Dira ya miaka 50 ni lazima tuboreshe miundombinu ya barabara. Hata hivyo, barabara hii ninayoizungumza kwenye Ilani ya Chama 2015 - 2020 ilikuwepo ikafanyiwa kazi kidogo kwa maana ya usanifu wa awali. 2020 - 2025 ilikuwemo, 2025 - 2030 imo. Leo nitamwambia Waziri kwa nini nilikuwa nampigia kelele. Barabara hii ndiyo iliyokuwa inabadilisha Wabunge, kila baada ya miaka mitano hujatekeleza umekaa pembeni. Mimi nitawasumbua sana kuhakikisha kwamba barabara hii inakamilika.

Mheshimiwa Naibu Spika, faida na umuhimu wa kuanza kujenga barabara hii, kwanza inahudumia majimbo zaidi ya saba. Tafsiri yake ni kwamba inahudumia Watanzania zaidi ya 4,000,000. *Corridor* ya Katavi kwa maana ya Mpanda, Kaliua (Tabora), na Kahama, sisi ni wafugaji, sisi ni wakulima, uchumi wetu sisi ni wa kilimo. Kama tunalima tutashindwa kusafirisha mazao maana yake hatujamsaidia Mtanzania wa leo. Ndiyo maana ninaomba sana tuweze kuiangalia hiyo barabara.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninafahamu kwenye jimbo langu kuna maeneo korofi na leo nimeyaona yameingizwa kwenye bajeti hii. Eneo la Ushokola - Kaliua Mjini, Mwangaza kwenda Kasungu kwenye kilomita 1.1 imetengewa shilingi 315,000,000. Ninaungana na mawazo ya wengi, ule Mfuko wa Barabara ni kweli fedha hizi bwana ziheshimiwe. Fedha hizi zikafanye kazi iliyokusudiwa. Nitakuwa wa kwanza, nitakuwa wa kwanza kutekeleza jukumu langu la Kibunge la kuisimamia Serikali kuhakikisha, fedha hizi zinafanya kazi yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kupanga ni kuchagua. Ni kweli kazi ya kupanga ni nyingine na kazi ya kutoa fedha ni nyingine. Tuiombe Serikali tuuheshimu Mfuko huu itoe hizi fedha zikafanye kazi iliyokusudiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kuyasema hayo machache kwa umuhimu wake, ninaunga mkono hoja kwa asilimia mia moja ili Wizara hii iende ikatufanyie kazi Watanzania na Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan dhamira yake ya

kuhakikisha anawaacha Watanzania wakiwa na tabasamu iende ikatimizwe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba kuunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Nilimtaja Mheshimiwa Mhandisi Johnston Johansen Mutasingwa, atafuatiwa na Mheshimiwa Hamisi Shabani Taletale, Mheshimiwa Joshua Samwel Nassari ajiandae.

**MHE. ENG. JOHNSTON J. MUTASINGWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi hii na mimi niweze kuchangia kwenye Wizara ya Ujenzi. Kwanza, nimshukuru Mungu aliyetujalia afya njema na tunaendelea na mjadala huu. Pili, niishukuru sana Wizara ya Ujenzi kwa kazi kubwa sana wanayoifanya. Nimshukuru sana Waziri unafanya kazi nzuri sana; na Naibu wake Engineer Kasekenya kwa kweli wanafanya kazi nzuri sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninawashukuru sana Makatibu Wakuu wote, wanafanya kazi vizuri sana. Kipekee niwashukuru na watendaji wote wa Wizara kwa kazi nzuri wanazozifanya na Mungu awabariki sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninawashukuru sana Mameneja wa *TANROADS* mikoa yote, wanafanya kazi nzuri sana. Kipekee ninamshukuru sana Meneja wangu wa Mkoa wa Kagera, *Engineer* Joel Mwambungu na Meneja aliyehama mkoa wetu, *Engineer* Ntuli Mwaikokesya, wanafanya kazi nzuri sana na Mungu awabariki sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, historia ya barabara kuanzia mwanzo mpaka sasa kuna mafanikio na maendeleo makubwa sana. Ninaweza nikasema tulipo ni pakubwa, lakini tunapoelekea ni pakubwa zaidi. Serikali imefanya kazi kubwa sana katika sehemu ya miundombinu. Watu wote wakiongea humu Bungeni, hakuna anayelalamika kwamba, hakuna barabara, hapana! Barabara zipo, ila wengi wanataka *either* ipandishwe daraja iwe

ya lami au itengenezwe kwa hiyo, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan amefanya kazi kubwa sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninamwomba Mheshimiwa Waziri afikishe salamu za shukrani kwa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kazi kubwa sana aliyoifanya katika Mkoa wetu wa Kagera. Sisi tulikuwa tuna madaraja, ambayo kihistoria tangu tunazaliwa yalikuwa hayajawahi kujengwa na wala hatukuwa na ndoto kwamba, yatakuja kujengwa. Hayo ni madaraja ambayo yamejengwa kupitia *SEKI*; tuna madaraja matano, Daraja la Kalebe, Kietema, Kianyabasa, Kamishango na Daraja la Kanoni. Mungu awabariki sana kwa maana wametua changamoto iliyokuwepo katika Mkoa wetu wa Kagera.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninavyosema hayo, haya mambo yote yamefanyika katika nchi nzima, lakini kupitia *SEKI*, Mheshimiwa Waziri amepata picha kwamba, hata wakandarasi wazawa wakiwezeshwa, wanaweza, kwa hiyo, sasa hivi hatuna haja tena ya kuwa na kilometa 100, tunampa Mchina, hapana! Tunaweza kuwa na kilometa 100, tukazigawa kwa makundi tukapata wakandarasi wanne wazawa na wakafanya kazi nzuri sana, pesa ikabaki nchini, kama pesa ya *SEKI* ilivyobaki katika Nchi yetu ya Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, ninashukuru sana, katika Jimbo langu la Bukoba Mjini Mheshimiwa Waziri umetuletea pesa sasa tunamalizia barabara ya njia nne pale Nyangoye na mkandarasi anaendelea vizuri. Kwa taarifa aliyoitoa, iko 75%, lakini nina uhakika kwa leo na jana itakuwa imefikia 80%, maana mkandarasi yuko *site* na anaendelea na kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba anavyoendelea yale madeni yake madogo madogo, Abemura, anayodai aweze kuya-*clear,* ili ile barabara iweze kumalizika maana ni kipindi hiki ambacho ameleta pesa nyingi, ile barabara imeanza tangu mwaka 2023 na ilikuwa ni barabara ya mwaka mmoja kwa hiyo, ninashukuru kwa kazi nzuri inayofanyika.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa katika bajeti hii, ninaomba katika Barabara yetu ile ya Bukoba *Port*, tuna Daraja la Kasarani, lile daraja ninaomba Waziri aliangalie wakati tunaenda kujenga zile njia nne kufika *customs;* lile daraja mvua ikinyesha huwa linajaa maji, watu hawawezi kupita. Tunaomba atusaidie, ili liweze kutengenezwa katika kipindi hiki.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Barabara yetu ile ya Nyangoye, kuanzia pale *Roundabout* ya Rwamishenye, kuna *feasibility study* imefanyika ya kilomita 6.6, ambayo inatoka pale kwenda Kyakairabwa, inatoka pale *Roundabout* ya Rwamishenye kwenda Magoti. Ninaomba sasa, ili Bukoba iwe Rio de Janeiro kweli, kama walivyosema watu, tujengee hizi njia nne ziweze kuongeza hizi kilomita sita.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na yote waliyoyafanya ninaishukuru sana Kamati ya Miundombinu na mimi ni Mjumbe. Ninashukuru sana taarifa yake aliyoisoma, zote zinashabihiana na zinafanana. Maoni yote yanayotolewa na Wajumbe ni kuboresha. Hakuna mtu anayepaswa kulalamika, Serikali imefanya kazi kubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa nina ushauri katika maeneo matatu; upande wa *TANROADS*. Ninashauri *TANROADS* iwe *Authority*. Hii itasaidia sana kupunguza mambo mengi na maeneo ya mapato yapo. Tuna *road reserve,* kwa mfano kama pale Kibaha, Waziri aniambie ile *road reserve* tukiweka maduka, tukawapangisha watu, tutapata shilingi ngapi?

Mheshimiwa Naibu Spika, tuna *borrow pits* ambazo tunakuwa tunazifanyia *compensation*. Tuna *TEKU,* ikifanya kazi kama *consultancy unit* ambayo inajitegemea tunaweza tukapata pesa kubwa sana kwa hiyo, ninashukuru wamesema na ninaomba ifanyiwe kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, upande wa madeni nina ushauri. Serikali ina madeni na madeni ya ujenzi kila siku yanaongezeka, deni la jana siyo la leo, madeni ni *accumulative*. Kwa hiyo, nina ushauri mara mbili; moja ni, deni la sasa lililopo na barabara

zilivyoharibika, ninaomba kama Kamati ilivyoshauri, libebwe na Wizara ya Fedha, ili pesa iliyopangwa ya maendeleo ya Wizara ya Ujenzi yote iende kutengeneza maendeleo. Hii itaondoa changamoto kabisa, hilo la kwanza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, tunaweza tukafanya tathmini kwa Wanasheria wetu, wakaona tuna deni la shilingi ngapi? Je, hii riba inayoongezeka ni asilimia ngapi? Wakaenda benki, wakakopa pesa, ili walipe deni la wakandarasi na tubaki na riba ndogo ya benki kuliko riba iliyoko sasa hivi. Hapo tutakuwa tunadaiwa na taasisi moja tu ya kibenki, lakini siyo wakandarasi wote kama wanavyotudai. Hii itasaidia sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, upande wa kazi viporo, mimi nina ushauri Mheshimiwa Waziri; unaposema kazi viporo, zimegawanyika katika sehemu tatu; moja, kuna kazi zinazoendelea, kuna kazi ambazo zinasubiri kusainiwa na kuna miradi ambayo tumefanya *feasibility studies*, haijaanza. Ninashauri tusiongeze miradi mingine, tukamilishe kwanza hii miradi iliyopo. Ninamwambia Mheshimiwa Waziri akikamilisha hii miradi ya viporo, hakuna Mbunge yeyote atakayesimama kuongelea barabara kwa sababu, kazi imefanyika sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mfano, Mkoa wa Kagera tuna Mradi wa Kakunyu, Kagera *Sugar,* unajengwa, ni kiporo, unaendelea. Tuna Burigi, Chato, unajengwa. Tuna Omurushaka, Murongo, unajengwa, kilometa 50. Hii yote Waziri akiitengeneza na akaweka pesa mle tutakuwa hatuwezi kusema barabara.

Mheshimiwa Naibu Spika, tuna miradi ya *feasibility studies*, hiyo ni *sample* ndogo tu; Lutengeru – Bale – Kishoju, Katoma – Bukwali, Kukunyakaura – Ruhengele – Muragarama, Kyakatuka – Kanazi – Ketema, hizi zote ziko kwenye *feasibility studies*. Waziri aniambie akizitengeneza nani atasimama kulalamika? Kwa hiyo, tunashauri kwamba, tutengeneze miradi ambayo ni ya viporo. Tusiwe na miradi mingine mipya, ili kwanza tumalize miradi hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, upande wa vyanzo vya mapato. Bila kuwa na vyanzo vya mapato hatuwezi kufanya jambo lolote.

Kamati imeshauri, ninaomba tufuate hivi vyanzo vya mapato vilivyoshauriwa na Kamati yetu ya Miundombinu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba kuunga mkono hoja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Nilimtaja Mheshimiwa Hamisi Shabani Taletale, atafuatiwa na Mheshimiwa Joshua Samwel Nassari na Mheshimiwa Paschal Inyasi Chinyele ajiandae.

**MHE. HAMISI S. TALETALE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Kwanza ninamshukuru Mwenyezi Mungu kwa kupata bahati ya kuchangia siku ya leo kwenye ukumbi huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaipongeza Wizara ya Ujenzi. Ninampongeza Ndugu yangu Mheshimiwa Ulega maana hata kama nilikuwa na hamu ya kumshikia shilingi, sitoishika kwa heshima ya baba na mama yake tu, siyo yeye. Ametuletea wazazi wake hapa, kwa heshima yao, basi mimi sitoshika shilingi yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, sisi siku zote tumekuwa tukilia na barabara. Wabunge wote humu wamekuwa mashahidi kwamba, tukija maswali ya barabara, Mheshimiwa Naibu Waziri anajibu vizuri sana, mpaka unadhani hata yeye mwenyewe kafanikiwa. Naibu Waziri huyu naye tumwombee, juzi kaenda jimboni kanasa kwenye tope. Mimi nikianza kuiomba Bigwa – Kisaki hapa, kama Naibu Waziri hajapata barabara, sipati ng'o.

Mheshimiwa Naibu Spika, amekuja hapa Mwenyekiti wa Kamati yao, Mheshimiwa Kakoso, alichosema kuhusu ile shilingi 100 kinaleta maana kubwa sana maana kama tunataka kujenga nchi, lazima tukubali kuumia sehemu moja. Leo hii mimi nimeletewa shilingi 6,000,000,000, ipo jimboni pale, lakini haifanyi kazi kwa sababu, kuna hela inayohitajika.

Mheshimiwa Naibu Spika, tumekuwa tunalia kuhusu Bigwa – Kisaki, miaka sita. Kwa huruma ya Mheshimiwa Rais, Dkt. Mama Samia Suluhu Hassan alipopita jimboni kwangu akamwelekeza

Waziri wa Fedha, tukapata shilingi 6,000,000,000. Ninavyozungumza na Mheshimiwa Waziri shilingi 6,000,000,000, twende tukaangalie imekata miti na kujenga kibanda kimoja! Jamani humu kuna wajenzi na kuna ma-*engineer,* shilingi 6,000,000,000 ya kulipia miti kweli? Hawa wakandarasi ni wa kutazamwa!

Mheshimiwa Naibu Spika, ukiwa huna, halafu mtu akakutia hasara, unakuwa huna zaidi. Wabunge wengi humu wanalalamika kwamba, barabara zao zile zilizolipwa, wakandarasi wengine hawaendi *site,* wengine hela wamepewa na *site* hawaendi. Sasa leo hii kuna Mbunge mwenzetu, yeye ni Naibu Waziri, sheria na taratibu za Serikali zimemfunga mdomo, lakini sisi wote tumemwona amenasa kwenye matope.

Mheshimiwa Naibu Spika, hiyo siyo siri. Kama yeye amenasa kwenye tope, maana yake ni Serikali, maana yake ni hii Wizara haina hela. Amekuja Mheshimiwa Kakoso ameelezea mpango mzuri, ametoka Mwenyekiti pale, naye ameelezea mpango mzuri. Leo hii tutaacha kushika shilingi ya Mheshimiwa Ulega kama mshahara, ili baba na mama wapate posho ya mtoto wao, lakini tunakwenda kuzuia hii bajeti mpaka Serikali, leo tuna bahati Waziri Mkuu yupo, wafanye maamuzi yaliyonyooka hapa. Kwamba, je, hii shilingi 100 ambayo tunasema kama ni kodi ya hiari, siyo! Iende kwenye hii Wizara, tutapata shilingi *1.1 trillion,* itagawiwa kwenye miundombinu vizuri. Tukishindwa kujipanga, tutapangiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, leo hii nina Barabara yangu ya Ubena – Zomozi. Tukirudi kwa wakandarasi wazawa, wako *very active,* Barabara ya Ubena – Zomozi, Mheshimiwa Ulega ni shahidi. Siyo kama wamewapa pesa yote, lakini mkandarasi yuko *site*. Kwa nini yuko *site*?

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kwa sababu, ana hofu ya kupoteza kazi na ana zile chembe za uzalendo. Tunapowapa wageni, hawana uzalendo, basi kama alivyosema *engineer* aliyepita hapa, tutengeneze utaratibu wa kuwapa wazawa hizi barabara. Watengeneze nusu nusu mpaka zimalizike.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna jambo lingine ninataka niongee kidogo na ndugu yangu Mheshimiwa Ulega. Tunajua Wizara yako haina hela na tunakuonea huruma, leo ametujia na jiwe la kuja na wazazi wake, ili tumwonee huruma zaidi, tumemwonea huruma. Sasa mimi ni mpangaji wako kwenye nyumba za *TBA;* hizi nyumba zetu za *TBA* hapa Dodoma, ni nyumba nzuri sana. Wanauza nyumba zingine zote, zile hawatuuzii, watuuzie basi na sisi. Hakuna mtu asiyetaka kuzinunua, kwanza zimechakaa. Sisi tukizinunua tutazi-*edit*, zitakuwa nzuri, ndiyo watajiongezea pesa kwenye Wizara yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, jana amesema Mheshimiwa Waziri wa Utalii hapa, kama Mheshimiwa Ulega naye anahusika na *AFCON; AFCON* nilipata bahati ya kutembea Dar es Salaam juzi, mjini hakuna taa kuna giza! Posta ile, ukipita *IFM*, giza! Sisi kwetu Morogoro Mjini Waluguru wanasema "yan'gaa duu" kweupe, hakuna *AFCON* huku! Arusha panawaka kidogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama tunashindwa kujiandaa, kwa ajili ya wageni, wageni hawapokelewi na Wizara ya Michezo tu. Wageni, pia, Mheshimiwa Ulega ni zoezi lake, kama Dar es Salaam haiwaki taa huyo mgeni usiku si atakabwa! Unataka kumpa kazi ngumu ndugu yangu Mheshimiwa Katambi kwenye kuwalinda? Haiwezekani! Ndugu yangu Mheshimiwa Ulega ninamwomba, siyo kama hana, ndiyo huna kabisa! Huna za kujenga barabara, ila kuweka taa unazo kaka! Weka taa kwenye miji, fanya miji ionekane, hawa wageni wanaokuja tuwe sehemu ya sisi kutamba.

Mheshimiwa Naibu Spika, la mwisho, lakini si kwa umuhimu sana. Mimi nakuomba Mheshimiwa Ulega, Bunge litakapomalizika twende Bigwa – Kisaki ukamkague yule mkandarasi. Ile shilingi 6,000,000,000 ndiyo inakata miembe tu pale na kujenga vibanda viwili.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema maneno hayo, ninaunga mkono hoja. Ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Nilimtaja Mheshimiwa Joshua Samwel Nassari, atafuatiwa na Mheshimiwa Paschal Inyasi Chinyele. Mheshimiwa Nuru Issa Kashakari ajiandae.

**MHE. JOSHUA S. NASSARI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninashukuru kwa kuniona na kunipa nafasi ya kutoa maoni yangu kwa niaba ya wananchi wa Meru kuhusu Wizara hii ya Ujenzi. Kwa kuanza, mimi naanza kwa kumshukuru rafiki yangu Mheshimiwa Ulega na kumpongeza yeye, pamoja na Mheshimiwa Kasekenya.

Mheshimiwa Naibu Spika, unajua hapa Bungeni tuna Mawaziri wengi, Manaibu Waziri wengi, wamekuwa wakiingia na kutoka, tumezoea, lakini kwa kweli, ni kwamba, ukipata Mawaziri wa Wizara nyeti kama hii ambayo inamgusa kila Mtanzania, inamgusa kila Mbunge na kila Jimbo ndiyo maana hata leo tumetangaziwa hapo kwamba, wachangiaji wa Wizara hii ni wengi kuliko Wizara nyingine yoyote.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukiwa na jambo, ukiwa na tatizo ukampigia simu Waziri, ukamtafuta, kwa maana ya ku-*engage* naye, aka-*engage,* viongozi wa namna hiyo ndiyo wa kupongezwa. Kwa hiyo, Mheshimiwa Ulega mimi ninampongeza kabisa. Nimeambiwa wazazi wake wako hapa, nilikuwa sijui! Ninawapongeza, ninawaambia walikuzaa na kukulea vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hali kadhalika, ninawapongeza Watumishi wa Wizara hii, Katibu Mkuu, Aloyce, Naibu Katibu Mkuu, Dkt. Msonde, na Watumishi wote pale Wizarani. Kwa kweli, *I've been to the Ministry a couple of times,* mimi ni yule mtu ambaye sijui kukaa na jambo moyoni, huwa ninazungumza. Hawa Waheshimiwa hata ukienda ofisini, ukienda wapi, ukipiga simu, uki-*engage*, ukitaka kuzungumza, ukipeleka ushauri, nao wanakupa ya kwao kwa hiyo, kwa hilo pekee kwa kweli, ninawapongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, sisi hatuipangii mamlaka, yenyewe ndiyo inayoamua, kwa maana ya Mkuu wa Nchi kwamba, nani akae wapi, nani acheze namba gani, lakini kwa sababu, kazi ya

Bunge ni kuelekeza na kushauri, leo ninashauri kwamba, siku nyingine Mheshimiwa Mkuu wa Nchi akitaka kuangalia Wizara zimekaa namna gani, amwache hapo alipo, amwache Katibu Mkuu hapo alipo, ili tumalize haya mambo ambayo tumeyazungumza hapa. Ukikuta ninampongeza Waziri au watendaji, mara nyingi ujue wanafanya kazi vizuri kwa sababu, mara nyingi huwa sipongezi bila kuona kazi ikifanyika.

Mheshimiwa Naibu Spika, leo ninafanya kazi ya kushauri zaidi. Ninasema tu kwamba, sitashika shilingi kwa sababu ya mambo ninayoenda kuyasema.

Mheshimiwa Naibu Spika, la kwanza ni, Mheshimiwa Waziri ninataka niwapongeze kwa ile kazi ambayo wameifanya pale Malula, wao wanaita King'ori, lakini kwa sisi watu wa Meru panaitwa Malula. Kutoka *KIA*, pale *Airport Junction*, kwenda moja kwa moja mpaka eneo la Panoni, kuvuka kwenda mpaka kwa Mama Kuku, sisi watu wa Meru tume-*celebrate* zile siku 100 za Mheshimiwa Dkt. Rais Samia madarakani kwa Wizara ya Ujenzi, *celebration* zimefanyika kwenye wilaya yangu Kitaifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, zimefanyika pale kwa sababu ya kazi ambayo imefanywa ya kuondoa tabaka la juu la barabara, ambayo ilikuwa mbovu, kufunga taa za barabarani na upande wa pili hata kuelekea Mkoa wa Kilimanjaro kutoka pale *KIA*. Ninamwona na ndugu yangu, Mheshimiwa Mafue, anapiga makofi, anajua kazi iliyofanyika ni nzuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa kwa hayo tunawashukuru na kuwapongeza, wametuwekea vituo pale, *service bay, bus bays,* zinakaa, zina nini, *highly appreciated,* lakini sasa kuna kitu kinakuja nchini na mimi leo ninataka kushauri.

Mheshimiwa Naibu Spika, hii nchi imepata neema ya ku-*host* kitu kinachoitwa *AFCON,* Mashindano ya Afrika. Neema hii inakuja mara moja ndani ya miaka mingi sana na upatikanaji wake haujawa rahisi, *the Government have spent a lot of money* kwa sababu hata kulipia ile *bid* tu peke yake ni *billions of cash,* ambayo hairudi moja kwa moja Serikalini, lakini inarudi *indirect*

kwa maana ya kwenda kwenye mifuko ya watu wakati wa mashindano yale, kusisimua uchumi na mambo mengine kama hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa kwa bahati mbaya sana au kwa bahati nzuri, Tanzania tuna-*host AFCON* kwenye maeneo matatu tofauti ukilinganisha na wenzetu ambao tunashirikiana nao kwenye *Pamoja Bid,* Waganda na Wakenya; sisi tunafanya Arusha, tunafanya Dar es Salaam na Zanzibar. Wenzetu, nchi jirani, ukiangalia wanakofanyia, kwa mfano Nchi jirani ya Kenya hapo, wao wanafanyia pale Nairobi tu. Kwa hiyo, sisi kwetu ni fursa, ingawa inakuja na majukumu kwamba, nchi yetu itakuwa *well explored,* lakini na maeneo yote ambayo yanakwenda ku-*host* haya mashindano ni maeneo nyeti kibiashara, kiutalii na masuala mengine kama hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninazungumzia Mkoa wangu wa Arusha. Barabara pekee ambayo inaingia na kutoka Mkoa wa Arusha ipo moja, wageni hao watatumia Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Kilimanjaro *(KIA),* lakini Barabara inayotoka *KIA* kwenda Arusha ni moja pekee yake. Ninataka niwape siri, nimesema leo ninazungumza kama kushauri tu; *one of the things* ambavyo ni lazima tuwe tunazungumza na tuambiane ukweli, Waheshimiwa Wabunge, ni viongozi wetu wanapokuja, Mheshimiwa Waziri Mkuu yuko hapa, kwenye maeneo yetu barabara zinafungwa, saa nyingine zinafungwa kwa nusu saa, lisaa limoja, dakika 45, dakika ngapi.

Mheshimiwa Naibu Spika, *I am being honest* kusaidia Bunge letu, kusaidia viongozi na kusaidia nchi hii, watu huwa hawafurahi sana, watu wanalalamika, wananchi huwa wanatukana barabarani, ninawaambia ukweli, wapite waone. Watu wanapozuiwa, shughuli zinakwamishwa na wa kwenda *Airport* wanakosa ndege, watalii wanashindwa kufika kwenye *destination* zao *on time*, wengine wanashindwa kufika hotelini, wengine wanashindwa kuingia kwenye mageti ya porini *on time* na wakivuka muda hawawezi kuingia kwa sababu, saa 12.00 ni mwisho. Wanakwenda kuwahi ndege, barabara zikifungwa huwa ni tabu Arusha.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye Mashindano haya ya *AFCON* barabara yetu ni moja. Tukiacha hiyo barabara pekee yake, *I have been speaking about this and am telling you*, mimi ninalisema wazi kwa sababu, nimezungumza na rafiki yetu Mheshimiwa Waziri Mkuu na akalitolea maelekezo. Nimekwenda Wizara ya Ujenzi mara kibao, hata leo nilikuwa kwa Mheshimiwa Profesa Kitila Mkumbo, ninamshukuru naye amenipokea, tunayazungumza vizuri, tunayajenga, *I really appreciate*.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini ukweli ni kwamba, tusipofanya mambo ambayo tumeyashauri hapa ndani tutapata aibu. Hii *AFCON* sisi tumekuwa tukisemwa na majirani zetu, sitaki kuwasema kwa jina kwa sababu ya diplomasia na nchi jirani; Tanzania haiko tayari! Wametusagia kunguni vya kutosha! Wanafanya namna gani?

Mheshimiwa Naibu Spika, wanasema hivi, wanasema vile, *it's our duty to prove them wrong*. Sasa kwa bahati mbaya barabara ni moja tu. *AFCON* inachezwa mwezi Juni na Julai, miezi ambayo ni *high season*. Wageni ni wengi wa utalii wa kawaida *at the same time, delegations* zitakuwa ni nyingi kwa sababu ya mpira; *teams,* nini, wageni wanaokuja, tunategemea barabara moja peke yake! Haiwezekani.

Mheshimiwa Naibu Spika, tumejenga Barabara kutoka *KIA Airport* kwenda Mererani, *over 20 kilometers*, tumejenga barabara ya *bypass* ya Arusha, zaidi ya kilomita 40 imekamilika, tumeacha kipande kidogo pale ambacho kitafanya Arusha iwe na *entrance* mbili na *exit* mbili za kutoka Mererani mpaka pale *bypass*, inaitwa Tengeru - Mererani, lakini siyo Tengeru Mjini ni Mererani *bypass*, tutakuja kuaibika.

Mheshimiwa Naibu Spika, tuna maadui wa ndani na maadui wa nje, ninaliongea hili wazi kabisa siku moja nitawaambia hapa ndani. Ninashukuru Mungu nilipitia siasa za *opposition*, nimekuja kufanya kazi Serikalini na leo niko kwenye Chama Tawala. Ninawaambia ukweli mpaka leo bado wana *linkage* za upande wa pili na upande huu, haki ya Mungu ninawaambia, tusipotengeneza kipande cha kilomita 28 kutoka pale Mererani

kwenda mpaka kwenye *bypass*, tutakuja kuaibika kwenye mashindano ya *AFCON*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninarudia tena, tuna maadui wa ndani na maadui wa nje, tusipofanya kazi hiyo na wengine wanaona kama vile ninatetea kwa sababu inapita kwenye Jimbo langu, lakini *listen, AFCON* siyo ya Jimbo la Arumeru Mashariki, *AFCON* hii ni ya Tanzania! Kwa hiyo najenga hoja yangu, malori ya Tanga yameongezeka, leo hii malori ambayo yanatoka Tanga na Mombasa *Port* ni karibu 400 kwa siku! *As we speak today* haikuwepo hiyo na tunapongeza, lakini imetuletea tatizo lingine kwenye barabara kuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, leo unapokea watalii unapitishaje watalii kwenye barabara moja na malori, mabasi, wasafiri na watu wa kawaida, halafu barabara yenyewe ni ya njia moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimalize, kutokana na hilo ninaomba kushauri vizuri kabisa. Tumejenga Bondeni *City*, inaunganishwa na hii barabara ninayoizungumza. Tumejenga *bypass* inaunganishwa na hii barabara tunayozungumza. Tumejenga uwanja wa mpira wa kisasa, unaunganishwa na hii barabara tunayozungumza. Tumeboresha *Airport* pale *VIP* imejengwa na hiyo Barabara ya Mererani imejengwa, inaunganishwa na Barabara ya kutoka Mererani kuipita Mbuguni kwenda Tengeru.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Nassari muda wako umekwisha.

**MHE. JOSHUA S. NASSARI:** Mheshimiwa Naibu Spika, tusisahau, kwa hiyo ninaomba kusisitiza hilo. Ninaomba nisiongee mambo mawili au matatu, ni hilo tu.

**NAIBU SPIKA:** Malizia, Mheshimiwa muda wako umekwisha.

**MHE. JOSHUA S. NASSARI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba kuunga mkono hoja, nikitegemea majibu mazuri kutoka Serikalini kuhusu barabara hii. Ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana.

**MHE. JOSHUA S. NASSARI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kumalizia wale watumishi wetu wa *TANROADS* pale Arusha wawaache kama walivyo wasiwaguse, tunakwenda nao sawasawa. Ahsante sana. *(Makofi/Kicheko)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Nassari muda umekwisha. Nilimtaja Mheshimiwa Paschal Inyasi Chinyele, atafuatiwa na Mheshimiwa Nuru Issa Kashakari na Mheshimiwa Josephine Joseph Kapoma ajiandae.

Waheshimiwa Wabunge, ninaomba tujadili kidogo kwa sauti ya chini ili wabunge wanapochangia Waziri aweze kuwasikia kwa umakini.

**MHE. PASCHAL I. CHINYELE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Kwanza kabisa ninamshukuru Mwenyezi Mungu kwa zawadi ya uhai, ninamshukuru sana na kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kutujengea barabara ya mzunguko, *ring road* yenye urefu wa kilomita 112 kuzunguka Jiji la Dodoma.

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara hii imetupa heshima na kwa kweli, imetoa msaada mkubwa sana kwa wakazi wa Jiji la Dodoma wanaokaa pembezoni kwa ajili ya kuja Mjini kirahisi. Ninamshukuru pia, Ndugu yangu Ulega kwa hotuba nzuri yenye matumaini makubwa kwa barabara za Nchi yetu ya Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, niende moja kwa moja kwenye mchango wangu. Kwanza kabisa ninaomba niongelee kuhusiana na Miradi ya *DIST* ya *TANROADS* ama Wizara ya Ujenzi ambayo kwa hapa Dodoma tunaita *Dodoma Integrated and Sustainable Transport Project (DIST)*. Mradi huu uko maalum kwa ajili ya

kuhakikisha kwamba barabara za ndani ya Jiji la Dodoma zinakuwa nzuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba tu kushauri hapa, Ndugu yangu Ulega, tafadhali huu Mradi wa *DIST* ufike pia katika kata ambazo hazina watu wengi, kata za pembezoni mwa Jiji. Ninaongelea hasa hapa barabara yetu ya kwenda Iringa kwenda eneo la Michese. Barabara hii ni mbaya sana, ndiyo imepangiwa fedha, lakini ninaomba usimamizi uwe ni mkubwa ili barabara hii iweze kukamilika mwaka huu ili ndugu zangu wa Michese waweze na wenyewe kuona kwamba, wanaishi katika Jiji la Dodoma.

Mheshimiwa Naibu Spika, niende sasa kwenye jambo kubwa ninataka kuongea siku ya leo, jambo linalohusu barabara ambayo ninaipendekeza kila wakati, barabara mpya ambayo inapendekezwa itoke hapa Dodoma Mjini katikati kupita Mkoa wa Singida sehemu inaitwa Nondwa kuelekea Sanza. Baada ya kutoka Sanza ikatize Hifadhi ya Muhesi, Kizigo, pamoja na Rungwa ili ikakutane na barabara inayotoka Itigi kwenda Makongolosi. Barabara hii ni fupi ukitoka hapa Dodoma Jiji kuelekea Mbeya hususani katika mpaka wa Tunduma ni mwendo usiozidi kilomita 380 kutoka hapa Dodoma.

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara hii ni muhimu na ina faida zifuatazo, niseme tu kabla sijataja faida, mimi ni Mbunge wa Dodoma Mjini nitanufaika na barabara hii kwa kilomita 20 tu basi, zilizobaki zote zinaihusu Mkoa wa Singida, Mkoa wa Rukwa, Katavi, Mbeya, Songwe na Tabora pia. Hawawezi kusema sana ndugu zangu hao, kwa sababu hawana manufaa moja kwa moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niseme faida zake: Faida ya kwanza, barabara hii itasaidia sana Bandari ya Dar es Salaam, Tanga pamoja na Bagamoyo ambayo itajengwa. Mizigo inayotoka nje ya nchi kwenda katika hizi bandari *destination* yake kubwa ukiacha zingine ni mpaka wa Tunduma - Nakonde. Tusiendelee kutegemea Barabara ya TANZAM pekee yake,

tunaiongezea mzigo na kuiharibu kila mara. Tufungue barabara nyingine itasaidia sana mizigo hii kufika kwa haraka.

Mheshimiwa Naibu Spika, faida ya pili, usafiri wa kati ya Dodoma kwenda mikoa hii niliyoitaja utakuwa rahisi sana ni kilomita chache. Kwa hiyo, hata Wabunge walioko humu ndani, ikifunguliwa barabara hii hawatahangaika tena kupita Iringa. Watapita moja kwa moja Nondwa, Sanza kupita mapori ya Muhesi na Kizigo kuingia Rungwa na kuingia Makongolosi, kuingia Mbeya na mpaka wa Tunduma - Nakonde.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna faida nyingine kubwa sana kitaifa faida ya utalii. Mapori ama hifadhi za Muhesi na Kizigo zina wanyama wale wakubwa wanaopatikana Ngorongoro na Serengeti. Tukifungua barabara hii, nchi itapata faida zinazotokana na utalii kwa kiasi kikubwa na sisi kama Dodoma tutafaidika, tutajenga hoteli nyingi na watalii wanapofika Uwanja wa Ndege wa Msalato watakwenda moja kwa moja kuangalia wanyama. Ni kama vile tu ambavyo tumefungua njia Mikumi na hivyo kuna mageti kule Mikumi kwa ajili ya utalii.

Mheshimiwa Naibu Spika, faida nyingine, nilishaitaja kidogo lakini barabara ya TANZAM inabeba magari mazito peke yake, barabara hii itasaidia kupunguza uzito. Pia barabara hii itapunguza ajali za barabarani, Barabara ya kutoka Dar es Salaam - Morogoro, Iringa kwenda Mbeya ina ajali ambazo hata huwa hazitangazwi, ajali ni nyingi sana, hii barabara itapunguza ajali hizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho ni usalama wa wanyama. Wanyama wanahujumiwa sana na majangili, barabara hii itaokoa wanyama wetu wasishambuliwe na hawa majangili. Pia, uchumi wa maeneo ya katikati ambapo barabara hii itapita kwa maana ya Mkoa wa Dodoma na katika Wilaya ya Bahi pamoja na Wilaya ya Manyoni uchumi utakuwa mkubwa kwa sababu usafirishaji wa bidhaa utakuwa rahisi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba nipendekeze. Ninafahamu barabara nyingi *TANROADS* wanabeba mzigo

mkubwa sana wa barabara nyingi katika Nchi hii ya Tanzania. Ninaomba nishauri mambo mawili tu. Jambo la kwanza Serikali iingie *PPP* kujenga hii barabara. Ninashauri kama ikiwezekana Wizara ya Uchukuzi kwa maana ya bandari waangalie namna ya kuijenga hii barabara, kwa sababu barabara hii ni ya Kitaifa na itaimarisha uchumi wa nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ushauri mwingine kama itaonekana fedha hamna kabisa, basi nimshauri tu Mheshimiwa Ndugu yangu Ulega, ninaomba uagize *Engineer* Zuhura wa *TANROADS* hapa Dodoma na *Engineer* Singano wa *TANROADS* Singida, waifungue njia hii ambayo kutoka Sanza kwenda mpaka Rungwa, hazifiki kilomita 60. Waifungue, ipitike kwa vumbi yale makorongo yaliyopo katika maeneo yale, yajengewe makalavati iweze kupitika kwa vumbi, kama fedha hawana, waifungue hiyo njia ipitike kwa vumbi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Ulega ninatarajia katika majumuisho yake ataniambia kitu kuhusiana na hii barabara kwa sababu tumeshaongea mara nyingi, ifunguliwe tu basi. Kwa sababu ikifunguliwa na kwa sababu kuna mradi mkubwa wa lami, kutoka Itigi kwenda Makongolosi mpaka Chunya na Mbeya, basi hii barabara ikishapita kwa vumbi itakuta barabara ya lami inayotoka Itigi kwenda Makongolosi, basi watu wanaotoka Mbeya na wanaokwenda Mbeya wanaweza kutumia njia hii kirahisi kuliko njia ambayo tumeizoea ya kwenda Iringa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaipendekeza kwa nguvu zote hii barabara na nitakapopata nafasi wakati wote nitaisemea hii barabara kwa sababu ina umuhimu mkubwa sana katika uchumi wa nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana na ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Paschal Chinyele. Waheshimiwa Wabunge tunao wageni waliokaa jukwaa la Spika.

Tunao wageni 51 wa Mheshimiwa Onesmo Merdson Mnkondya, ambao wanaunda Kamati ya Maombi Maalum ya Ujenzi wa Barabara ya Mlowo – Kamsamba - Mbozi, Mkoani Songwe, wakiongozwa na viongozi wafuatao Ndugu Radwell Mwampashe, Mwenyekiti wa CCM Mkoa wa Songwe; Ndugu Marco Mbanga, Katibu wa CCM, Mkoa wa Songwe; Ndugu Mlawizi Majaliwa, Mwenyekiti wa CCM, Wilaya ya Mbozi; Ndugu Joseph Ludovic, Katibu wa CCM, Wilaya ya Mbozi; Ndugu Godfrey Zambi ambaye ni Mbunge Mstaafu na Naibu Waziri Mstaafu na Ndugu Roid Mkisi, Mwenyekiti wa Wadau wa Kahawa Tanzania. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tutaendelea na Mheshimiwa Nuru Issa Kashakari, atafuatiwa na Mheshimiwa Josephine Joseph Kapoma na Mheshimiwa Abubakari Damian Asenga, ajiandae.

**MHE. NURU I. KASHAKARI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Awali ya yote ninamshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema ambaye amenijalia kuwepo hapa katika Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Vilevile ninamshukuru Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kuwezesha kuniteua mimi kuwa Mbunge wa Jimbo la Kigoma Kusini.

Mheshimiwa Naibu Spika, nikishukuru sana pia chama changu, Chama Cha Mapinduzi kwa kuniteua kuwawakilisha wananchi wa Jimbo la Uvinza. Pia ninawashukuru sana wananchi wa Jimbo la Kigoma Kusini - Uvinza, kwa kunichagua niwe mwakilishi wao kuhakikisha kwamba wanapata maendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika, pongezi hizo zote nazipeleka kwa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, hususani kwa kutuwezesha kupata barabara nzuri katika Mkoa wetu wa Kigoma. Mheshimiwa Dkt. Mama Samia Suluhu Hassan amevunja ule ukimya wa kusema kwamba, Mkoa wa Kigoma mwisho wa reli, sasa hivi Mkoa wa Kigoma tena si mwisho wa reli, kwa sababu ukienda Kigoma pale una uwezo wa kutoka Kigoma saa 12.00 jioni, lakini asubuhi saa 12.00, ulishafika Dar es Salaam.

Mheshimiwa Naibu Spika, unaweza vilevile kutoka pale Kigoma mjini saa mbili usiku na saa nane usiku ulishafika Mwanza. Kwa hiyo, ni jinsi gani Mheshimiwa Dkt. wetu Samia Suluhu Hassan amejitahidi sana kadri ya hali, ukiangalia kulikuwa na kipande kidogo pale Nguruka, kuanzia Nguruka mpaka Uvinza kulikuwa na kilomita 54. Baada ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kuapishwa alielekeza zile fedha ziende kule, kwa kweli ninampongeza sana na namwombea dua kwa Mwenyezi Mungu. Mungu amjalie ampe maisha marefu na amwondolee chuki na fitna. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli Kigoma tulikuwa mwisho wa reli, lakini kwa kipindi hiki ukienda utakuta barabara zote kuanzia Kigoma kwenda Burundi ni lami, lakini kuanzia Kigoma Mjini mpaka Mwanza ni lami tupu. Kuanzia Kigoma Mjini mpaka Dar es Salaam ni lami tupu. Kwa kweli, Waheshimiwa Wabunge tumpigie makofi Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, amefanya kazi kubwa sana, amejitahidi kadri ya hali, Watanzania tusije tukawa kama Wanamisri ambao Nabii Musa alikwenda akawa anawapa chakula kila mara, lakini mwisho wa siku Nabii Musa wakamtupia mawe.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kweli ni pongezi kubwa sana, ukienda Kigoma sasa hivi tuna meli mbili ziko zinakarabatiwa na mwezi Julai zitakuwa tayari. Kuna Mwongozo, kuna Liemba, hizo meli zote Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan ameelekeza fedha, mabilioni ya fedha amekwenda kuwapa wananchi wa Kigoma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, si hivyo tu, tunao uwanja wetu, Uwanja wa Ndege Kigoma leo hii ni hadithi, ni uwanja mpana, mkubwa wa kimataifa. Kwa hiyo, ninaposimama mbele yako hapa, ninajivunia sana uwepo wa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan.

Mheshimiwa Naibu Spika, yote hayo yamefanyika kwa juhudi na maarifa aliyomruzuku Mheshimiwa Rais wetu, Dkt. Samia Suluhu Hassan, *Allah Subhanahu wata'ala,* kumruzuku. Sisi wananchi wa Uvinza Jimbo la Kigoma Kusini, Jimbo la Kigoma Kusini pale tuna

matatizo, bado tuna matatizo wanasema, penye kheri hapakosi shari na penye riziki pana mtihani, sisi Wanakigoma Kusini, Wilaya ya Uvinza tuna changamoto ya barabara kutoka Simbo kwenda Karia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Waziri kwa unyenyekevu mkubwa sana, tuwaangalie hawa wananchi wa Uvinza, hakika katika Majimbo makubwa zaidi ni Jimbo hasa la Kigoma Kusini. Saa hizi kuna vijiji 36 havina barabara kabisa. Kuwathibitishia hivi vijiji, tangu Uhuru hawajawahi kuona mwenge wa uhuru. Hawajawahi kuuona hata kwa macho. Kwa hiyo, niombe Barabara kutoka Simbo mpaka Karia na Daraja la Mto Malagarasi pale Ilagala, iweze kujengwa angalau hata wananchi wafurahie matunda ya nchi yao. Si hivyo, angalau na sisi tuweze kupata angalau kuuona hata huo Mwenge wa Uhuru, angalau ufike maeneo hayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna Kijiji cha Mwakizega, kuna Vijiji vya Kabeba, Sambala, Ilagala, Kajeje, Mahanga, Kanywangili…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Mbunge, malizia muda wako umekwisha.

**MHE. NURU I. KASHAKARI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninashukuru sana. Kwa hiyo kuna vijiji 36.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa. Unga mkono hoja.

**MHE. NURU I. KASHAKARI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninaunga mkono hoja kwa asilimia mia moja ama asilimia elfu moja. Ninawaomba Wabunge wote tuunge mkono hoja ili twende mbele. Ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Nimemtaja Mheshimiwa Josephine Joseph Kapoma, atafuatiwa na Mheshimiwa

Abubakari Damian Asenga na Mheshimiwa Zainab Rashid Kawawa, ajiandae.

**MHE. JOSEPHINE J. KAPOMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kupata nafasi hii na mimi leo nichangie katika Wizara nyeti hii ya Ujenzi. Pia ninawashukuru wananchi wa Morogoro na wananchi wa Morogoro wanaishukuru sana Serikali ya Awamu ya Sita.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Rais wakati wa kampeni zake tulimwomba Barabara ya kaka yangu Babu Tale, Bigwa - Kisaki ambayo anaiongea kila siku na sasa mkandarasi ameshapewa *advance* ya bilioni 6.8, anaendelea japokuwa kasi yake ni ndogo sana. Pia, tuna barabara ya Ubena Zomozi inaendelea vizuri, mkandarasi ameshapewa *advance* na barabara inaenda kwa *speed* sana na mkandarasi huyu ni mzawa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia tuliomba barabara ya Ifakara - Mbingu, mkandarasi ameshapewa zaidi ya shilingi 10,000,000,000, lakini yuko *slow* sana. Shilingi 10,000,000,000 kwa pesa hiyo, tulikuwa tunategemea mpaka sasa hivi *at least* tuone hata ile kwenye *mobilization,* tuone hata madaraja mawili tu yameanza, lakini mpaka sasa hivi ninavyokwambia, mkandarasi huyu anajenga tu ofisi, ndiyo kitu ambacho kimefanyika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hili ninamwomba kaka yangu Mheshimiwa Waziri Ulega, kama ikiwezekana, baada ya kuhitimisha bajeti hii, tunaomba afanye jambo kwenye suala hili, kwa sababu wananchi wa Mlimba hawatuelewi na wananchi wa Bigwa – Kisaki hawatuelewi, kwa sababu wanaona ofisi tu, lakini hakuna kinachoendelea.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa *advance* ya shilingi 6,000,000,000 ya Bigwa – Kisaki na *advance* ya shilingi 10,000,000,000 ya Ifakara – Mbingu tulikuwa tunategemea kuona makubwa sana yanayoendelea.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaendelea pia kuipongeza Serikali kwa madaraja, kule kwa kaka yangu Shabiby, Gairo. Tumepata madaraja makubwa sana; Daraja la Chakwale na Nguyani ambayo yatatusaidia kuelekea Kilindi - Tanga. Pia tunashukuru, pale Morogoro Mjini tumepata Daraja la Mkundi, ambalo lilikuwa linasababisha tupate athari kubwa sana kipindi cha mvua; mradi unaendelea vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa nina ombi moja, lakini pia nitatoa na ushauri. Morogoro kama mnavyojua ni mkoa wa kimkakati. Unapoongelea chakula na ghala la chakula Tanzania huwezi kuiacha Morogoro. Vilevile, si tu kwa chakula, Morogoro pia tuna madini mengi. Sasa hivi tuna wawekezaji wa madini kule Ulanga, lakini Barabara ya Ulanga ni kati ya barabara ambazo ni mbovu sana kiasi kwamba hata wawekezaji ninajua wanajishauri ni vipi wanakuja kuwekeza kule.

Mheshimiwa Naibu Spika, niliongea na kaka yangu Mheshimiwa Ulega na ametupa matumaini kwamba Barabara ya Lupiro – Ulanga – Mahenge pamoja na barabara ya Mikumi, Kidatu itapata ufumbuzi muda si mrefu. Tunategemea kumwona mwekezaji yule wa *Graphite* ataanza kazi mapema sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa ninaomba niishauri Serikali. Serikali inatoa fedha nyingi sana katika miradi hii ya barabara. Mheshimiwa Waziri na timu yake, Katibu Mkuu na viongozi wa huku juu wanafanya kazi nzuri sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, hawa wakandarasi wamekuwa wana *delay* na ninadhani ni kama na wao wanashika shilingi, mimi sielewi. Tatizo kubwa linatokea kwa ajili ya ucheleweshaji wa fedha; hasa fedha za *advance*. Ninaishauri Serikali, kwamba, ni wakati wa kuangalia sasa; na ninadhani sasa hivi ni muhimu tukaja na *strategy* ya *phase out, roll out (FIFO); first in, first out;* na nitaipanga hii katika utaratibu huu;

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa hivi tuna miradi ambayo inaendelea tayari ambayo iko katika 20%, 30%, 40% na 80%; tuna miradi ambayo wakandarasi wamekwishapewa *advance;* tuna

miradi ambayo iko katika mchakato. Sasa ninadhani, kama walivyoongea Waheshimiwa Wabunge wengine, ni wakati wa Serikali kujikita katika hii miradi ambayo tayari ipo kwenye utekelezaji, ambayo wakandarasi wamekwishapewa *advance*, na ambayo tumekwishafanya *tendering* ya kupata wakandarasi wanasubiri mikataba na hii itatupunguzia kulipa gharama ambazo siyo, gharama ambazo tunazilipa sana sana za kuchelewesha kuwalipa *advance*.

Mheshimiwa Naibu Spika, mfano, huyu mkandarasi wa Ifakara – Mbingu, ninajua kabisa ana *delay* kuendelea na mradi kwa sababu alitakiwa kulipwa zaidi ya shilingi 15,000,000,000, lakini kalipwa shilingi 10,000,000,000. Kwa hiyo ninajua kwamba anabonyeza *button* ili aone tunafanyaje aweze kumaliziwa ile shilingi 5,000,000,000. Mkataba amesaini zaidi ya mwaka mmoja lakini fedha amelipwa hivi karibuni ilihali mkataba utakwisha mwezi huu, Juni.

Mheshimiwa Naibu Spika, kingine ambacho ninapenda kuishauri Serikali; tunajua kabisa mikataba inavyoelekea kwisha, tufanye *extension* ya mikataba kabla watu hawa hawajatupa *penalty* za kubwa zaidi. Kwa sababu ukiangalia hata ripoti ya *CAG*, *penalty* ambazo tunazilipa tungeweza kujenga barabara zingine.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo kuna haja sasa ya kuangalia fedha tunazozipoteza kulipa *fine* ni kubwa mno. Sasa, *monitoring and evaluation* ya kaka yangu Mheshimiwa Ulega iko wapi? Inafanya kitu gani? Kuna watu huko chini *accountability* ni ndogo mno, hawezi kusubiri Mheshimiwa Waziri Ulega aende Mlimba. Tanzania tuna halmashauri zaidi ya 184, aende akaangalie utekelezaji unaendaje.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo nilichokuwa ninakiona, kwanza tu-*stick* kwa hizi sehemu tatu; miradi ambayo inaendelea, wakandarasi ambao wamepewa *advance* na hawa ambao tumesha-*tender* wanasubiri wapate mikataba. Tukipata mikataba, tuwalipe hawa watu fedha zao za *advance* kusudi wasi-*raise* hizo *interest* kwa sababu zinatuumiza sana na hii pesa ni

pesa ya umma na Mheshimiwa Samia anahangaika sana, Mama wa watu, kuzitafuta hizi fedha.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi kama Mhasibu, hakuna kitu ambacho kinaniuma na ninaumia kama kulipa *interest* kwa kitu ambacho kimewezekana. Kama hii miradi tunayoianzisha, kama hatuna uhakika wa fedha tuache tusianzishe, tutawaelewa wakituambia.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimeongea na kaka yangu Mheshimiwa Ulega, amesema Malinyi tusubiri kidogo kwa sababu sasa hivi fedha hatuna na tumemwelewa! Sasa…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Josephine, ahsante sana.

**MHE. JOSEPHINE J. KAPOMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba kuunga mkono hoja na ninashukuru sana. *(Kicheko/Makofi)*.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Waheshimiwa Wabunge, bado orodha ni ndefu sana, ninaomba tufanye dakika sita, sita ili angalau Waheshimiwa Wabunge wengi mpate kusema, kwa sababu kila mmoja angetamani aseme. Tukienda kwa hivi wengine hawatapata nafasi. Kwa hiyo turidhie dakika sita.

Mheshimiwa Abubakari Damian Asenga, atafuatiwa na Mheshimiwa Zainab Rashid Kawawa na Mheshimiwa Onesmo Merdson Mnkondya ajiandae.

**MHE. ABUBAKARI D. ASENGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru sana, japokuwa dakika sita zimeanzia kwangu. Mtihani mkubwa huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabla sijasahau ninataka kushukuru, kama ninavyoshukuru mara zote, kuhusu barabara yangu ya Ifakara kwenda Kidatu na nakumbuka namna ambavyo barabara hii ilinitesa. Leo Waheshimiwa Wabunge

wanavyozungumza hapa kwa uchungu mkubwa tunajua, lakini leo tunavyozungumzia Kilombero, tuna barabara ya lami ya kutoka Ifakara kwenda Kidatu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu dakika ni sita, ninaanza kwa kuunga mkono hoja na mapendekezo yote ya Kamati. Katika mambo yote kuifanya *TANROADS* kuwa mamlaka iweze kutumia *assets* zake kujipatia mapato zaidi pamoja na *TEMESA*, kulinda fedha za Mfuko wa Barabara, suala la hati fungani na *PPP*, ujenzi wa Barabara ya Dar es Salaam kuja Morogoro kwa wawekezaji binafsi kama wanaweza, kumaliza miradi viporo, Serikali kubeba deni la Wizara ya Ujenzi ili iweze kupata salio la fedha za kusaidia miradi mingine endelevu. Pia, tozo na Waheshimiwa Wabunge tuendelee kutoa maoni hapa. Kama tulivyosema, tulivyojadili kwenye kamati, kama kweli hatuongezi fedha katika barabara, katika Wizara ya Ujenzi, tutakuwa tunadanganyana hapa, tutashika shilingi ya Mheshimiwa Waziri bure, lakini vinginevyo hatuwezi kutoka.

Mheshimiwa Naibu Spika, mapendekezo yalikuwa kwenye magari ya madini. Kwa mfano, kuna malori ambayo yanabeba makaa ya mawe, tunayaona kila siku, yanaharibu barabara. Kwa hiyo kwenye asilimia pale inaweza ikatoka, ama kwenye tozo ya madini, ama tozo ya simu kama kadri itakavyoonekana inafaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ibara ya 40(1) ya Ilani ya Uchaguzi ya CCM imeelekeza Wizara ya Ujenzi kujenga barabara kwanza za mikoa zinazounganisha mkoa na mkoa, baadaye iende kwenye wilaya kwa wilaya na barabara zinazounganisha nchi yetu na nchi nyingine. Haya ni maelekezo ya Chama Cha Mapinduzi. Sasa ninawashangaa sana watu wanaokaa Masaki na wao wanadai barabara. Ilani ya uchaguzi wewe unakaaje Masaki unadai lami, kama unataka kujenga lami hama njoo Manzese. Sisi tunazungumza hapa barabara za mkoa kwa mkoa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Chama Cha Mapinduzi, Ibara ya 40(1) imeielekeza ikijua kwamba mahitaji ya barabara ni makubwa, *resources* vyanzo vya pesa ni vichache. Sasa leo tuna mikoa haijaunganishwa na mikoa mitatu. Sisi tunasema Mkoa wa

Morogoro ni ghala la Taifa, lakini bado tunazungumza barabara. Bora kaka yangu Mheshimiwa Nape kidogo wamepata pata, nimemsikia Mheshimiwa Mzee Chikota anasema, sisi tuna barabara tumesaini miaka mitatu iliyopita.

Mheshimiwa Naibu Spika, Barabara ya Ifakara kwenda Malinyi. Malinyi kutokea Songea (Ruvuma) hakuendeki kabisa. Kuna Barabara ya Ifakara kwenda Njombe, kwa Mheshimiwa jirani yangu, Mheshimiwa Kellen Rose Rwakatare hapa; kwenda Mgeta huko, kutokea Mkoa wa Njombe. Kuna Barabara, nimeisema, ya Malinyi – Ruvuma kwenda kwa Mheshimiwa Makamu wa Rais, kuna Ifakara kwenda Ulanga, ambayo inatokea Lindi.

Mheshimiwa Naibu Spika, hizi barabara zote zinataka fedha, pamoja na hizi nyingine tumezisaini. Sasa ninawaomba Waheshimiwa, kama Mwenyekiti wangu alivyochangia hapa, sote tunahitaji barabara na ilani imeelekeza tujenge barabara zinazounganisha mkoa kwa mkoa na nchi yetu na nchi jirani kwa sababu ya kiuchumi. Tuendelee kutoa mapendekezo ya mapato, jambo hili tusilisahau. Kwa sababu tutamaliza kesho kutunga bajeti hapa, tutapitisha bajeti, tutabaki hivi tulivyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninalijua jambo hili kupitia Kamati ndiyo maana Mwenyekiti wangu wa Kamati amelizungumza kwa sauti kubwa na ninataka kulirudia; sisi sote tunahitaji barabara. Tutoe mapendekezo zaidi, tumependekeza kwenye Kamati, Wabunge waunge mkono ile shilingi 100, ama kama Mbunge hataki kuunga mkono, aiboreshe, apendekeze pendekezo lingine hata kwenye maji ya kunywa basi tuweke, kama hatutaki kuweka huko ili tupate.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukweli ni kwamba, Serikali isipochukua deni la shilingi 1,000,000,000,000, kwa sababu bajeti ikiwa *2.6 trillion*, shilingi 1,000,000,000,000 inaenda kulipa wakandarasi; ambapo wakandarasi wengine wameshafura. Tumekuta Mkandarasi *Estim* kule kafura, Wachiko kafura, *Kings* kafura; hawezi kuchukua miradi mipya.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo tunaomba Wizara ya Fedha ichukue lile deni la angalau shilingi 1,000,000,000,000, ilibebe yenyewe, ili bajeti ya Wizara ipumue. Bajeti ile ikipumua itaweza kuwezesha barabara nyingine mpya tunazozisema hapa zikajengwa. Ninaomba Waheshimiwa Wabunge tupendekeze vyanzo vya mapato, tutakuja kupitisha bajeti kesho pale, tutamkaba Mheshimiwa Waziri koo bure. Bila kufanya hivyo hatuwezi kutoboa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Asenga, ahsante sana kwa kutunza muda vizuri. Mheshimiwa Zainab Rashid Kawawa, atafuatiwa na Mheshimiwa Onesmo Merdson Mnkondya na Mheshimiwa Dkt. George Venance Lugomela ajiandae.

**MHE. ZAINAB R. KAWAWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru kwa kunipa hii nafasi ili niweze kutoa mchango wangu.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi ni Mbunge wa Viti Maalum wa Mkoa wa Lindi. Mwaka huu mwezi uliopita Mkoa wetu wa Lindi tulikimbiza Mwenge wa Uhuru na nilibahatika kushiriki Mbio za Mwenge wa Uhuru na nikakimbia nao Mkoa mzima wa Lindi. Nimesema haya kwa sababu ninataka kusema yale niliyoyaona kuhusiana na barabara zetu za Mkoa wa Lindi, kwa maana niliyoyaona hivi karibuni na kilikuwa kipindi cha mvua pia.

Mheshimiwa Naibu Spika, cha kwanza ninataka nitoe pongezi kwa Mheshimiwa Rais. Tulikuwa tuna madaraja mabovu mengi sana kwenye ile Barabara kuu inayotokea Kibiti kuja mpaka Lindi - Mingoyo kuanzia pale Somanga - Mikereng'ende – Matandu - Mbwemkuru kote huku kulikuwa kuna shida sana ya madaraja na mvua zilikuwa zikinyesha barabara zinakatika. Upande mwingine wa Kilwa huku maeneo ya kwa M-south, tumezoea kupaita kwa M-south; Zinga, Miguruwe, kote huko kumejengwa madaraja. Kwa upande wa Liwale pia Mlowoka na Mbwemkuru iliyoko Kijiji cha Nangano.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimeona kuna maendeleo ya barabara. Barabara inayotokea Mingoyo kuelekea Masasi, kwa maana sasa inaunganisha Mkoa wa Lindi na Mkoa wa Mtwara. Pia kutokea Mingoyo kuelekea Mtwara kupitia njia ya Madangwa. Haya ni maendeleo makubwa sana. Tunamshukuru sana Mheshimiwa Rais, ametutendea haki sisi wananchi wa Mkoa wa Lindi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba nielezee hali halisi ya barabara za Mkoa wa Lindi. Barabara za Mkoa wa Lindi zina kilomita 1,326, barabara za mkoa zenyewe ni kilomita 978, ambapo barabara kuu kilomita 347. Tuna barabara zilizojengwa kwa kiwango cha lami kilomita 450; yaani hii inajumlisha hizi barabara ambazo ni *trunk roads* kilomita 347. Sasa uki-*minus* hapo unapata zile barabara zinazounganisha wilaya kama kilomita 100 tu.

Mheshimiwa Naibu Spika na ukienda kwenye uhalisia wilaya zetu bado hazijaunganishwa na wilaya zingine kwa kiwango cha lami. Mimi sisemei tu kiwango cha lami, kiwango cha barabara zinazotakiwa kupita katika misimu yote.

Mheshimiwa Naibu Spika, *Vision 2050* imeeleza wazi mchango wa sekta hii ya ujenzi katika kukuza na kuchochea ukuaji wa sekta zingine. Sisi Mkoa wetu wa Lindi tunategemea barabara kwenye ukuaji wa kilimo, kwenye ukuaji wa sekta ya madini, kwenye ukuaji wa sekta ya uvuvi, hata kwenye ukuaji wa sekta ya ajira kwa vijana ambao wanaendesha bodaboda, kwenye ukuaji wa sekta ya bandari, sekta ya uchukuzi ambako kwa sasa tuna bandari ya uvuvi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni dhahiri kwamba muda hautoshi siwezi kueleza mengi lakini ninaomba sasa, hebu tuitoe Liwale kutoka kuwa kisiwa. Liwale imekuwa kisiwa, siyo kisiwa kilichozungukwa na Bahari bali kisiwa ambacho hakina barabara inayopitika muda wote. Ninamwomba Mheshimiwa Ulega aifungue hii barabara...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa, ahsante sana.

**MHE. ZAINAB R. KAWAWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba nimalizie.

**NAIBU SPIKA:** Malizia, kwa sekunde tatu.

**MHE. ZAINAB R. KAWAWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, tumekubaliana tutashika shilingi kwa ajili ya ile Barabara yetu ya kutoka ya Dar es Salaam mpaka Mingoyo bado hatujasikia neno lake...

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana.

**MHE. ZAINAB R. KAWAWA:** ...tunahitaji kulisikia neno kutoka kwa...

**NAIBU SPIKA:** Ahsante Mheshimiwa...

**MHE. ZAINAB R. KAWAWA:** ...kwa sababu ile ndiyo barabara ambayo ndiyo roho ya Mikoa ya Lindi na Mtwara kiuchumi...

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa kengele ya pili imeshagonga.

**MHE. ZAINAB R. KAWAWA:** ...tunaomba na tunasubiri majibu mazuri kutoka kwake...

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa kengele ya pili tayari.

**MHE. ZAINAB R. KAWAWA:** ...tunaamini wali wa kushiba unaonekana kwenye sahani. Wameshaanza kutuonjesha wali wa kushiba sasa...

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Zainab kengele ya pili tayari.

**MHE. ZAINAB R. KAWAWA:** ...tunaomba mwongeze ili tuweze kushiba. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Onesmo Merdson Mnkondya atafuatiwa na Mheshimiwa Dkt. George Venance Lugomela na Mheshimiwa Silvery Luboja Salvatory ajiandae.

**MHE. ONESMO M. MNKONDYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninapenda kutoa shukrani nyingi sana kwako kwa kunipa nafasi ya kutoa mchango wangu kwenye wizara hii pendwa kabisa Wizara ya Ujenzi. Nilivyosimama tu viongozi wangu Waheshimiwa Mawaziri wangu kwenye wizara hii wanajua ninataka kusema nini, na walishanipa jina wao wenyewe. Mheshimiwa Ulega alishanipa jina kwamba mimi ni Mlowo – Kamsamba, ninataka kuomba Barabara ya Mlowo – Kamsamba.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilishamwambia Mheshimiwa Waziri na Mheshimiwa Naibu wake na niongeze kwa Katibu wake na Serikali kwa ujumla kwamba, sisi watu wa Mbozi kipaumbele chetu miaka hii mitano 2025 - 2030 ni Barabara Mlowo – Kamsamba; ndicho kipaumbele chetu namba moja, namba mbili na namba tatu. Tupo tayari kwa sasa kukosa vitu vyote, lakini tupate barabara hii kwa sababu ndiyo ambayo imeshika uchumi wa Wanambozi, Wanasongwe na wa Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, niseme tu, kwamba unaweza ukaona hata ujio wangu usiku wa leo sitafoka sana kwa hao wenzangu, hawa Waheshimiwa Mawaziri, lakini ninalo ombi moja kwao; nimekuja na jopo, nawe umelitambulisha hapo; umesema Kamati ya maombi maalum ya ujenzi wa Barabara ya Mlowo – Kamsamba, wako hapa Bungeni. Wamesafiri takribani kilomita 850 hadi 900 kuja hapa Dodoma kuifuata barabara. Maana wameona sisi Waheshimiwa Wabunge tukisimama ni kama tunampigia mbuzi gitaa, tukizungumza ni kama hatusikilizwi. Sasa wanatutuma halafu tunaokuja kuomba waliyotutuma hatupati.

Mheshimiwa Naibu Spika, wakasema hapana, mwanetu tumekuchagua mtoto wa mkulima, mtoto wa Merdson nikatoka kwenye walimu nije nipambane nipate Barabara hapa ya Mlowo – Kamsamba. Barabara hii wamepita Waheshimiwa Wabunge 11 na mmojawapo amesikika hapa, Mheshimiwa Godfrey Weston Zambi, ametumika kama Mheshimiwa Mbunge na Mheshimiwa

Naibu Waziri, lakini hajapata hii barabara. Wametoka Waheshimiwa Wabunge Gilbart Nzowa tangu mwaka 1965 hadi 1970...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MHE. ONESMO M. MNKONDYA:** ...kengele imelia? Akafuata Feston Mnkondya babu yangu mimi, amekuja Twins Harrison hajapata, Japhet Sishone hajapata...

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mbunge, kutokana na muda uliopo kuwa mdogo ninakushauri nenda kwenye hoja yako ya barabara moja kwa moja, kutaja hao Waheshimiwa Wabunge 11 pengine hawatasaidia sana...

**MHE. ONESMO M. MNKONDYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, hoja yangu mimi leo siombi barabara na sitawashikia shilingi, nitawaunga mkono kwa sababu kwanza wamekubali kukaa na hiyo kamati iliyopo juu. Yupo Mwenyekiti wa CCM Mkoa na Katibu wake, Mwenyekiti wa CCM Wilaya na Katibu wake, umemwona Mheshimiwa Zambi, umemwona Mwenyekiti wa Wadau wa Kahawa Tanzania, wapo Wachungaji, wapo Masheikh, wapo Machifu wapo kule, wapo viongozi wa chama wengine wapo kule, wapo walimu, wapo wafanyabiashara, wapo vijana na akina mama wamekuja hapa Bungeni kutaka mwafaka kwa barabara yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimeangalia kwenye randama hakuna kitu nimeangalia...

**MBUNGE FULANI:** Na waganga.

**MHE. ONESMO M. MNKONDYA:** na waganga eh! Ahsante sana na wewe. Nimekuja na Msukuma naye yuko hapa. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, bahati nzuri nimemwona Mheshimiwa Waziri Mkuu; kwamba sitasema ninaomba tukae kikao. Mheshimiwa Waziri Mkuu ni msikivu amekubali kukaa na hili

jopo kutoka Mbozi na hii kamati. Nimeongea na Mheshimiwa Ulega na ninamwomba yeye kesho aje na kauli kwa ajili ya Wanambozi.

Mheshimiwa Naibu Spika, sisi barabara hii ina shida gani? Wana-Mbozi wana shida gani? Mbona wanatupenda, wanaipenda Serikali na wanampenda Rais Samia ambaye amewaahidi kujenga barabara hii kilomita 130 zote? Yeye mwenyewe Mheshimiwa amekuja akasema hakuna shida Mheshimiwa Mnkondya wewe, Mlowo - Kamsamba ninajua Mbozi mnaitaka sana barabara, ninakwenda kujenga.

Mheshimiwa Naibu Spika, hapa bajeti tunakwenda kupitisha lakini hakuna hela. Tutazungumza, amekwishakubali kukaa naye tutazungumza.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa ahsante sana muda wako umekwisha.

**MHE. ONESMO M. MNKONDYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninaunga mkono hoja, tuna vikao vya kimkakati hapa tupate barabara yetu. Hawarudi hawa wazee bila kupata barabara, hawarudi. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Nimemtaja Mheshimiwa Dkt. George Venance Lugomela, atafuatiwa na Mheshimiwa Silvery Luboja Salvatory na Mheshimiwa Abdallah Jafari Chaurembo ajiandae.

**MHE. DKT. GEORGE V. LUGOMELA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nishukuru kwa kunipa nafasi hii ili niweze kuchangia hoja hii ya Wizara ya Ujenzi. Nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuniwezesha kusimama hapa kwa ajili ya kuchangia bajeti hii. Nimpongeze Waziri wa Ujenzi, Mheshimiwa Ulega kwa kazi kubwa anayoifanya ya kusimamia Wizara hii ya ujenzi, lakini pia kwa uwasilishaji wa bajeti yake leo asubuhi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimpongeze pia Mheshimiwa Naibu Waziri *Engineer* Kasekenya kwa kazi kubwa na nzuri anayoifanya ya kumsaidia Mheshimiwa Waziri kufuatilia usimamizi

wa miradi ya Wizara ya Ujenzi. Niwapongeze pia watendaji wote katika sekta hii; Katibu Mkuu, Naibu Katibu Mkuu na Wakuu wa Taasisi chini ya Wizara ya Ujenzi kwa kazi wanayoifanya.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimpongeze zaidi Rais wetu Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kutoa fedha za ujenzi wa barabara na ni kweli tumeona maendeleo makubwa katika ujenzi wa barabara katika miaka ya hivi karibuni.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na pongezi hizo, ninazo changamoto kadhaa ambazo ninahitaji kuziwasilisha ili Wizara ya Ujenzi iweze kuzifanyia kazi. Katika Mkoa wa Simiyu tunayo barabara moja kubwa ya kutoka Mwigumbi kwenda Lamadi takribani kilomita 170. Mheshimiwa Waziri barabara hii ilikamilika kipande cha Mwigumbi - Maswa kilikamilika mwaka 2017/2018.

Mheshimiwa Naibu Spika, toka wakati huo barabara hii imekuwa ikifumuliwa mwaka hadi mwaka, kipindi hadi kipindi, kwa sababu ilijengwa chini ya kiwango. Kwa hiyo, ombi letu ni kwamba sasa sintofahamu katika barabara hii ikamilike. Tunaomba barabara hii ikamilishwe vizuri ili iweze kuleta matumaini kwa Wanasimiyu.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunao utaratibu wa kuunganisha mikoa kwa barabara za lami. Nimeona kwenye bajeti na Randama ya Wizara kuna usanifu wa barabara kutoka Bariadi kwenda Itilima - Mwandoya mpaka Ng'hoboko ambayo ni sehemu ya kipande cha barabara kitakachounganisha kwenda Mkoa wa Singida. Ombi langu ni kwamba barabara hii ikamilishwe, usanifu ukamilishwe mwaka huu wa fedha ili ujenzi uweze kuanza.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kuunganisha mikoa ninaomba pia tuunganishe Mkoa wa Arusha na Mkoa wa Simiyu. Tunayo Barabara ya kutoka njia panda ya Karatu pale kuja Mang'ola kuja Matala mpaka Sibiti. Barabara hii ikifika pale Sibiti itaungana na ile inayotoka Simiyu na inayotoka Singida na kuunganisha Mkoa wa Arusha, lakini pia Mkoa wa Singida. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara hii itafupisha safari ya kutoka Arusha kwenda Mwanza kwa sababu itapunguza takriban kilomita 200. Pia, itaongeza fursa ya utalii na shughuli zingine za utalii katika Mkoa wa Simiyu kwa vile itaweza kuleta watalii kutoka Arusha.

Mheshimiwa Naibu Spika, kulikuwa na ule mradi mkubwa wa Barabara ya kutoka Mbulu – Haydom – Sibiti – Mwanuzi - Lalago mpaka Maswa kupitia Mradi wa *EPC+F*. Mradi ule ulishindikana kwa sababu moja au nyingine. Kilichobaki sasa hivi ni kilomita 65 kutoka Nkoma mpaka Lalago na nimekiona kwenye Randama ya Mheshimiwa Waziri.

Mheshimiwa Naibu Spika, rai yangu ni kwamba kipande hiki cha barabara sasa kijengwe kutoka Nkoma mpaka Lalago. Hii ni sehemu pia ya barabara inayoenda Singida na inayoenda Lalago na kuunganisha Mkoa wa Simiyu pamoja na mikoa hiyo miwili. Kwenye Randama imeandikwa mkandarasi anajiandaa na ujenzi wa barabara hii. Kwenye kuhitimisha Mheshimiwa Waziri ningeomba atuthibitishie kiwango cha fedha kilichotengwa kwa ajili ya kuanza ujenzi wa barabara hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunazo barabara zingine ambazo ziko kwenye Ilani ya Uchaguzi ya CCM. Tunayo Barabara ya kutoka Sakasaka kuja Mwandoya kuja Senani kuja Mwabayanda mpaka Maswa pale tunaita *Sola Junction*. Barabara hii ni muhimu sana kwa uchumi wa Mkoa wa Simiyu na Wilaya ya Maswa na Meatu na inaunganisha majimbo mawili ya Kisesa pamoja na Maswa Mashariki. Tunaomba pia barabara hii iangaliwe iweze kuanza kujengwa kwa kiwango cha lami. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini tunayo barabara ya kutoka Maswa mpaka Lalago...

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa ahsante sana.

**MHE. DKT. GEORGE V. LUGOMELA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ilikuwa sehemu ya ile barabara kubwa ya *EPC+F*. Tunaomba kipande hiki pia kianze kujengwa kwa kiwango cha lami. *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mbunge ahsante sana, muda wako umekwisha.

**MHE. DKT. GEORGE V. LUGOMELA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana na ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Nimemtaja Mheshimiwa Silvery Luboja Salvatory atafuatiwa na Mheshimiwa Abdallah Jafari Chaurembo, Mheshimiwa Salehe Mbwana Mhando ajiandae.

**MHE. SILVERY L. SALVATORY:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru kwa nafasi hii. Pia, ninamshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijalia afya njema na kuniwezesha kusimama mbele ya Bunge lako Tukufu jioni hii ya leo.

Mheshimiwa Naibu Spika, sisi Wana-Misungwi tutakuwa wachoyo wa fadhila tutakapochangia bajeti ya ujenzi bila kumshukuru Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba nianze kusoma maandiko matakatifu kutoka Kitabu cha Kutoka sura ya 14 mstari wa 21. *"Musa akanyoosha mkono wake juu ya bahari, Bwana akaifanya bahari irudi nyuma kwa upepo wa nguvu utokao Mashariki. Usiku kucha akaifanya bahari kuwa nchi kavu, maji yakagawanyika".*

Mheshimiwa Naibu Spika, miujiza hii ya Nabii Musa tumeiona kwenye Jimbo letu la Misungwi ambapo Serikali ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan imeweza kutujengea Daraja la Kigongo - Busisi kama ambavyo wengi wametangulia kusema. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nilijaribu kukaa kwa utulivu mahali baada ya kuwa nimevuka kwenye *beach* kule kwa Mheshimiwa Tabasam kuna hoteli moja imeandikwa *Rocky Bay*, inaitwa *Rocky*

*Bay*. Nikakaa pale kwenye ufukwe ule nikawa ninapata upepo mzuri kutoka kwenye Ziwa Victoria.

Mheshimiwa Naibu Spika, nikawa ninatafakari, nikatafakari hotuba ya Mheshimiwa Rais wakati anazindua lile daraja ilisema kwamba daraja lile limejengwa kwa shilingi 718,000,000,000 na kati ya hizo 566,000,000,000 alizitoa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan na shilingi 152,000,000,000 alizitoa Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli, Hayati Rais wetu kipenzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na Waheshimiwa Wabunge nilipiga hesabu tangu mkataba usainiwe mpaka kwisha zilikuwa ni siku 1,970 wastani wa shilingi 300,000,000 na kitu kwa siku, hela zilizokuwa zinakuja hapo. Kwa kipindi cha Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan pekee yake kila siku tangu akabidhiwe nchi zilikuwa zinatoka shilingi 357,000,000 za Kitanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo niseme tu kwamba hatuna cha kumlipa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan sisi Wanamisungwi na Watanzania pamoja na nchi jirani za nchi za maziwa makuu kwa kutunusuru na shida iliyokuwepo hapo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mengi yameelezwa na ndugu yangu Mheshimiwa Mary Masanja na Mheshimiwa Nzilanyingi kutokana na *impact* ya daraja hilo, (*impact* chanya, matokeo chanya ya daraja hilo). Kwa hiyo tunaomba huo ushoroba na hizo njia zipanuliwe kwa haraka kuja Usagara kwenda kwenye *SGR*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nimuombe ndugu yangu Mheshimiwa Ulega kabla sijasahau kutoka kwenye hii hoja, wakati anahitimisha atuambie wananchi wa Usagara fidia zao pale kwenye mzani ambako kutakuwa na upanuzi mkubwa wa mzani.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba nihitimishe. Tunayo Barabara ya kutoka Mwanangwa – Misasi - Salawi. Barabara ile niungane na kaka yangu Mheshimiwa Deo Mwanyika ina umuhimu wake. Tunao mradi wa maji chanzo kikuu cha maji

yanayoenda Shinyanga na yatakayokuja hapa Dodoma chanzo chake kiko Ihelele. Ukifika Buhingo kuna kilomita 39 kwenda Ihelele na kwenda Mbarika ambako tunategemea kutoa Gridi ya Taifa ya Maji kuja hapa Dodoma.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba Mheshimiwa Waziri Ulega atakapokuwa anahitimisha atoe ufafanuzi wa hii Barabara ya Mwanangwa - Salawi pamoja na hiyo Barabara ya kutoka Buhingo kwenda Ihelele kilipo chanzo cha maji pamoja na hiyo Gridi ya Maji ya Taifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, ninaunga mkono hoja. Ninawashukuru sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Salvatory. Nimemtaja Mheshimiwa Abdallah Jafari Chaurembo atafuatiwa na Mheshimiwa Salehe Mbwana Mhando na Mheshimiwa *Engineer* Saidi Salim Hamad ajiandae.

**MHE. ABDALLAH J. CHAUREMBO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nikushukuru wewe binafsi, nimshukuru Rais wangu, nikishukuru Chama changu Cha Mapinduzi na niwashukuru watendaji wote wa Wizara ya Ujenzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, leo hii tumeona hapa Wabunge wote wanalilia barabara na wananchi wetu katika majimbo yetu wote wanasikiliza kwa makini mjadala unaoendelea.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kuwa sote tumegundua matatizo yetu ni Barabara, lakini dira ya kutatua matatizo yetu Mwenyekiti wa Kamati na Kamati yake ametuonesha. Niombe sana tutafute namna ambayo dira aliyotuonesha Mwenyekiti wa Kamati ya kutafuta fedha kwa ajili ya kujenga barabara hizi tuweze kupata ufumbuzi wake na hatimaye migongano, migogoro na ushikaji wa shilingi utakuwa ni historia.

Mheshimiwa Naibu Spika, niombe sana Wizara hii, nimeona katika bajeti ambayo tunaijadili hii leo barabara yangu ya kilomita

15 inayotoka Rangi Tatu kuja Maji Matitu kuja Chamazi – Mbande - Kisewe mpaka Msongola imewekwa katika kitabu cha bajeti.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nimwambie Mheshimiwa Waziri wananchi wa Jimbo la Mbagala na Chamazi ambao ndiyo watumiaji wakubwa wa barabara hii hasa wale wa Jimbo la Chamazi wanakushukuru sana sana sana kwa kuona barabara yao imeingia katika kitabu cha bajeti. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara kuingia kwenye kitabu cha bajeti ni jambo moja na utekelezaji na ujenzi wa barabara hiyo ni jambo la pili. Nimwombe sana Mheshimiwa Waziri, juzi alijibu swali hapa ambalo nilitaka kujua ujenzi wa Barabara hii ya kutoka Rangi Tatu mpaka Msongola, akatujibu kwamba barabara hii ni muhimu na hasa ujio wa *AFCON* ni lazima barabara hii ijengwe. Ninashukuru nimeona imetengewa fedha.

Mheshimiwa Naibu Spika, niombe sana tuanze sasa michakato ya kuijenga barabara hii. Wananchi wa Jimbo la Chamazi sasa hivi wanachokifanya ni kukuombea dua, kuiombea Serikali yetu dua ili mradi tu barabara hii itekelezwe kwa wakati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tumeona mwaka juzi tulitengewa fedha kwa ajili ya kujenga Barabara ya kutoka Mbande kwenda Msongola. Waziri ameona mkandarasi tuliyempa kazi anavyosuasua, barabara inatupa tabu sana. Tumwombe sana kama kweli tumeamua kwa dhati kuijenga barabara hii basi na suala la kuwapa wakandarasi wenye uwezo, wenye uzalendo nalo tulizingatie kwa kina sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tumezungumza sana mambo ya ujenzi wa Barabara, lakini kuna jambo moja muhimu ambalo tunatakiwa tulizingatie. Tunapojenga barabara lazima tuangalie namna ambavyo barabara hizi zinaenda kuondoa msongamano.

Mheshimiwa Naibu Spika, yapo maeneo ya vipande vifupi na madaraja mafupi ambayo yanaunganisha barabara mbili za

*TANROADS* wilaya na wilaya. Madaraja haya yakijengwa yanaenda kuondoa misongamano katika barabara kuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna Barabara ya Mbango - Kwaru – Bamia – Churwi – Videte – Mapunda - Magohe - Kwa Mzala Magohe - Rufu kwenda Mkuranga. Vipande hivi vya barabara vikijengwa vinaenda kuondoa msongamano wa barabara kuu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu ya muda, nichukue nafasi hii kumshukuru sana Rais wangu Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan ametuwezesha wananchi wa Jimbo la Chamazi, wananchi wa Jimbo la Mbagala na wananchi wa Mikoa ya Kusini, Lindi na Mtwara. Nilikuwa ninapigia kelele sana kwenye Bunge hili namna ambavyo mlango wa kuingia Dar es Salaam kwa wananchi wa Lindi na Mtwara ulivyokuwa umefungwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Rais wetu ametupa fedha. Tunajenga barabara pale ya njia sita kutoka Kokoto mpaka Kongowe. Vilevile, ndugu zangu wa Kusini sasa watapita kwenye *flyover* ambayo inaingia Dar es Salaam.

Mheshimiwa Naibu Spika, hili ni jambo kubwa sana la kuwashukuru na kumshukuru Rais wetu. Pia, kwa niaba ya wenzangu wote ambao tunatumia barabara hii ya kwenda Kusini na mimi nikiwa mdau, Wabunge wote wa Kusini tunaishukuru Serikali kwa kutufungulia mlango wa kutoka Dar es Salaam kwenda Kusini.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Abdallah Chaurembo. Nimemtaja Mheshimiwa Salehe Mbwana Mhando atafuatiwa na Mheshimiwa *Engineer* Saidi Salim Hamad, Mheshimiwa Henry Charles Kabeho ajiandae.

**MHE. SALEHE M. MHANDO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba nichukue nafasi hii kumshukuru sana Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema aliyenijalia na mimi siku ya leo kuchangia hotuba ya bajeti ya Wizara ya Ujenzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba nichukue nafasi hii kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri, ndugu yangu Mheshimiwa Abdallah Ulega, Naibu Waziri na timu nzima ya watendaji wa Wizara ya Ujenzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kipekee kwa dhati ya moyo wangu ninaomba nichukue nafasi hii kumshukuru sana Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa namna anavyoendelea kuchapa kazi, kulitumikia Taifa letu hususan katika Wizara hii na sekta hii ya ujenzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tunamshukuru sana kwa niaba ya Wanakilindi ametupatia shilingi bilioni 5.1 tumejenga Daraja la Sagasa pale Kata ya Lwande. Pia, ametujengea Daraja la Kibirashi limekamilika na wananchi wanafurahia na kupata tabasamu la Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nimesimama kutoa na kuwasilisha sauti ya Wanakilindi. Nimesikiliza na kupitia hotuba ya Waziri wa Ujenzi na hoja ya Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Miundombinu ndugu yangu kaka yangu Mheshimiwa Selemani Moshi Kakoso.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa Mkoa wa Tanga, kwa Wilaya ya Kilindi bila kuitaja Barabara ya Handeni – Kibirashi – Kiteto - Chemba - Kwa Mtoro - Singida pamoja na Kibirashi - Songe bado hujagusa maendeleo ya Mkoa wa Tanga kwa ujumla. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nimshukuru sana Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Miundombinu wakati akiwasilisha maoni ya Kamati kwa kuigusia barabara hii. Tayari kulikuwa kumezuka taharuki kwa wananchi wa Jimbo la Kilindi kwa kutokuona uzito wa suala la Barabara ya Handeni - Kibirashi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nimekuwa nikizungumza mara kadhaa na nitarudia mpaka pale tutakapopata muafaka wa jambo hili wa barabara ile kujengwa kwa kiwango cha lami. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara hii kwenye mioyo ya Wanakilindi, Wanatanga, Wanakiteto na Wanachemba iko kwenye moyo wa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan. Miaka 25, mimi nikiwa kidato cha sita barabara hii kwenye Serikali ya Awamu ya Tatu iliingizwa kwenye mpango wa ujenzi kwa kiwango cha lami, lakini haikufanikiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tukaenda Awamu ya Nne, Ilani na dhamira ya Serikali Awamu ya Nne, lakini bahati mbaya haikufanikiwa. Tukaenda Awamu ya Tano Ilani ya Chama Cha Mapinduzi na dhamira ya Serikali ya Awamu ya Tano, lakini haikufanikiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan pekee kwa moyo wa huruma, mama mfariji ndiye aliyekuja kuagiza na kuanza ujenzi rasmi wa Barabara hii ya kilomita 460 kutoka Handeni - Kibirashi - Songe - Kiteto - Chemba, kwenda Kwa Mtoro - Singida. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tunapozungumza suala la utaifa, uzalendo, hii barabara ndiyo inayogusa mikoa minne kwa wakati mmoja na hii ni kiunganishi cha Bandari ya Tanga ambayo imefanyiwa mageuzi makubwa sana. Leo Mheshimiwa Nassari anaelezea suala la Usa River, tayari malori 400 yanaleta shida pale. Suluhu yake ilikuwa ni hii barabara. Kwa nini ninalizungumza hivi?

Mheshimiwa Naibu Spika, nimesikiliza hotuba ya Waziri, nimwombe sana rafiki yangu Mheshimiwa Ulega. Kabla ya kuhitimisha, ninafahamu barabara hii ina maelekezo ya viongozi akiwemo Mheshimiwa Rais, Waziri Mkuu na kuna tofauti ya ahadi na maelekezo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninapenda kujua wakati anahitimisha, maelekezo ya Ujenzi wa kilomita 20 kutoka Handeni Mafureta na kilomita 30 kutoka Mafureta kwenda Kireguru, mkandarasi aliagizwa aanze kazi, hawajafika *site*, hawako *site* mpaka sasa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa ninaomba wakati wa kuhitimisha kabla sijashika, mshahara wa Waziri, ninajua dada yangu atatusamehe, shemeji yangu atusamehe, kwa ajili ya ndugu zake wa Kilindi dada yangu itabidi avumilie shida ili kusudi tupate mwafaka lini Ujenzi wa mkandarasi atakuwa *site*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kama haitoshi, yalitolewa maelekezo barabara hii kwenda Wizara ya Ujenzi na Wizara ya Uchukuzi, kwenda kufanya makubaliano ya namna gani itajengwa kwa mfumo wa *PPP* tangu mwaka 2023, leo ni miaka miwili bado hatujajua hatima yake ni ipi. Ninamwomba Mheshimiwa Waziri, atakapokuja kuhitimisha ninataka atwambie nini hatima ya Ujenzi wa Barabara ile kutoka Kireguru kwenda Kibirashi, kwenda Songe na hatimaye kwenda Kiteto, Chemba, hatimaye kwenda kwa Mtoro Singida. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninataka nikwambie Mheshimiwa Waziri, kwa mapenzi makubwa ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, ninajua awamu zote kuanzia ya tatu wamempa alama. Ukienda Kusini kuna Daraja la Mkapa, ukienda kule Malagarasi kuna Daraja la Kikwete, ukienda pale Kigongo Busisi, kuna Daraja la Magufuli. Sisi wananchi wa Kilindi, wa Kiteto, wa Chemba na Singida tunakwenda kumpa barabara hii itaitwa Samia *Road*! Hii itaitwa Samia *Road* iwe kumbukumbu yake. Tutakuwa tunampongeza kwa kusema, itafutika lakini kwa kumpongeza kwa kutenda kupitia barabara hii, Samia ataishi kwenye mioyo ya Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba kuunga mkono hoja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Mbunge wa Kilindi. Nimemtaja Mheshimiwa *Engineer* Saidi Salim Hamad, atafuatiwa

na Mheshimiwa Henry Charles Kabeho na Mheshimiwa Ramadhani Hamza Singano, ajiandae.

**MHE. SAIDI SALIM HAMAD:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru, awali ya yote ninapenda nimshukuru Mwenyezi Mungu, nikishukuru chama changu Chama Cha Mapinduzi. Aidha, ninawashukuru kwa dhati ya nafsi yangu wananchi wa Jimbo la Ole kwa imani kubwa ambayo wamenipatia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara yetu hii ya Ujenzi inayoongozwa na Mheshimiwa Ulega pamoja na Naibu Mheshimiwa *Engineer* pale, ni Wizara ngumu sana, lakini mahusiano ambayo wanaishi na Wabunge wenzao, pamoja na mahusiano wanayoishi na Katibu Mkuu na watendaji wao wa Wizara hii ya Ujenzi, imeifanya Wizara hii kuwa Wizara muhimu ya kimkakati na kutembea katika mwendo wa *smoothness* kabisa. Hongera sana kwa Mheshimiwa Waziri kwa kazi nzuri ambayo wanaifanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, utamaduni wa nchi yoyote duniani unalindwa na kujengwa na wananchi. Demokrasia ya nchi yoyote duniani inajengwa na kulindwa na wananchi, lakini vilevile ulinzi na usalama wa nchi yoyote duniani utajengwa na kulindwa na wananchi. Vivyo hivyo, miundombinu ya nchi yoyote duniani itajengwa na kulindwa na wananchi wa nchi husika.

Mheshimiwa Naibu Spika, Nchi yetu hii ya Tanzania tumeshaona jitihada za Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwenye kuleta bajeti kubwa kwenye Wizara hii na mwaka huu bajeti hii imeongezeka kwa takriban 30%, lakini bado kuna vilio vya barabara kwenye Taifa letu. Ndiyo hapo sisi kama Wabunge ambao tumekaa hapa tukiwawakilisha wananchi wetu, tunapaswa sasa kwa umoja wetu, tuchekeche vichwa vyetu na kufikiria namna gani tutaweza kutafuta *new sources of income* ili tuweze ku-*top up* kwenye bajeti aliyoileta Mama Samia tuweze kulisukuma hili gurudumu mbele.

Mheshimiwa Naibu Spika, lengo la Wabunge wote hapa ni kurudi baada ya miaka hii mitano na moja ya siasa kubwa

ambayo itatupelekea kurudi hapa ni siasa hii ya barabara katika maeneo yetu. Sasa, kama bajeti imekuwa kwenye *ceiling amount* hapo, sisi kama Wabunge tunakuja na mawazo gani ili kuweza kuiwezesha hii Wizara kuweza ku-*generate new source of income*?

Mheshimiwa Naibu Spika, mawazo ya Kamati ya Miundombinu ni kuwa na *sources* mpya za kipato ambazo zitaiwezesha Wizara hii. Mojawapo ni daraja letu la Tanzanite. Kama daraja la Kigamboni wananchi wanaokaa kule, licha ya *life standard* yao kuwa duni kidogo, wanachangia, kwa nini daraja letu la *Tanzanite* ambalo watu wetu wa Masaki wanaokaa huku *life standard* zao ziko juu wanashindwa, tukaweka katozo hata kama kidogo, kuweza kukuza katika Wizara yetu hii bajeti yake? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tumefurahia vilevile Wabunge wenzetu wa Kanda ya Ziwa, wanafurahia vivuko ambavyo vimepelekwa pale, lakini vilevile wanafurahia daraja jipya alililoliacha Dkt. Magufuli na Mama Samia akalikamilisha. Kwa nini tusiwe tuna *source of income* hata katozo kadogo katika daraja lile pale, ili kuweza ku-*generate income* kuiwezesha Wizara hii kuweza kukua katika bajeti yake?

Mheshimiwa Naibu Spika, wazo la Kamati ya Miundombinu ni kuanzisha tozo ya shilingi 100 katika muda wa maongezi ili tuweze kwa kila mwaka kupata trilioni 1,080,000,000,000, *with a minimum*! *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hii inakuja, Watanzania ambao *line* zao ziko *active* ni takriban 58,000,000. Watanzania 28,000,000 tunawaweka wale ambao hawatatoa *plus-minus*, 30,000,000 wakitoa kila siku shilingi 100, *it means* kwa mwezi ni shilingi 3,000 na kwa mwaka itakuwa ni shilingi 36,000. Kwa kila Mtanzania mmoja mwaka mzima shilingi 36,000. Kwa Watanzania 30,000,000, itakuwa ni shilingi 1,080,000,000,000. Tutakwenda ku-*top up* bajeti hii na Wabunge wote tutaweza kutengeneza siasa katika majimbo yetu kupitia barabara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niombe Wabunge wetu na Watanzania kwa ujumla, tukubali kiroho safi, *Billahi Taala*, hii bajeti, wazo hili la tozo hii ndogo, tuweze kwenda kufanikisha hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, wazo langu la pili katika Wizara hii, Wizara hii tuko nyuma kidogo kwenye *local content*, kuziwezesha taasisi zetu za ndani. *TBA* ni taasisi moja inayofanya uzuri sana. Ina Kampuni ya Ujenzi ya *Class One*, ina Kampuni ya *Consultancy Class One*. Kwa nini tunaiweka kwenye *Agency* tusiipandishe kwenye *Authority*? *TANROADS* iko *Agency* mpaka leo kwa nini isiwe *Authority*?

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante Mheshimiwa muda wako umekwisha.

**MHE. SAIDI SALIM HAMAD:** Mheshimiwa Naibu Spika, hizi wakala zote mbili zinajengwa na Bodi ya Ushauri, sasa ni muda wa kuwa na Bodi ya Utendaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Engineer Hamad. Nimemtaja Mheshimiwa Henry Charles Kabeho, atafuatiwa na Mheshimiwa Ramadhani Hamza Singano na Mheshimiwa Dkt. Ritta Enespher Kabati, ajiandae.

**MHE. HENRY C. KABEHO:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa sisi Wabunge wote kuwa salama na kuendelea na shughuli zetu za kuwakilisha wananchi wetu. Ninamshukuru sana Mheshimiwa Daktari Bingwa wa matatizo na changamoto za Watanzania, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa kuendelea kuwatumikia wananchi wa Tanzania bila kuchoka na kuleta maendeleo muda wote anaofanya kazi zake, Mwenyezi Mungu ambariki sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru wewe kwa kunipatia nafasi hii ya kuchangia Wizara muhimu sana hii ya Ujenzi. Ninashukuru sana na ninampongeza Waziri Ulega kwa kazi

nzuri anazofanya na timu yake, kazi tunaiona lakini hatuwezi kuacha kuomba. Niliomba barabara kwenye bajeti ya Waziri Mkuu TAMISEMI, barabara za *TARURA*, nilishaomba; sasa ninaomba kwenye barabara za *TANROADS* ambazo ziko chini ya Wizara yake Mheshimiwa Ulega.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba Barabara ya Igunga - Igurubi, Ukenyenge - Kolandoto ya kilomita 90. Ikiweza kuwekwa lami, wananchi wa Igunga ambao wanafanya biashara, wanachukua mazao kutoka Ukenyenge na Kolandoto na pia watu wa Korandoto na Ukenyenge wanaleta mazao Igurubi na Igunga, wakiweka lami itatusaidia sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna Barabara ya Igunga - Ziba, kwenda Puge na kwenda Tabora. Tukitumia barabara hii ikiweza kuwekwa lami, tutakuwa hatupiti Nzega tena, tutapunguza kilomita 100 na pia wananchi wetu wanaokwenda kutibiwa Hospitali ya Ndala, watapata unafuu mkubwa ingawa Barabara hii kuanzia Ziba kwenda Puge imeanza kufanyiwa kazi tunashukuru sana Mheshimiwa Abubakari, Mbunge wa Manonga aliipambania sana kuanzia Ziba kwenda mbele. Kwa hiyo, nina-*cement* kidogo kwa sababu wananchi wetu wote wanapita huko.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna Barabara ya kutoka Igunga - Loya kwenda Mabeshi. Barabara hii ni mbovu sana haifai kabisa magari yanaharibika kila siku wenye magari wafanyabiashara wanayatoa kila siku zinabaki gari chache. Kwa hiyo, wananchi wanapata shida sana kwenye barabara hiyo, tunaomba sana Wizara hii kwa Mheshimiwa Ulega, aitengeneze barabara hii kwa kiwango cha lami ili wananchi wetu wengi ni wafanyabiashara, wanaenda Loya mpaka Mabeshi na Mabeshi wanakuja kwetu kuleta bidhaa na vitu vingine muhimu kwa ajili ya uchumi wa Igunga.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, ninakushukuru tena wewe na uongozi wote wa Bunge pamoja na Mheshimiwa Spika, ninawashukuru sana na ninaomba niunge mkono hoja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Kabeho. Nilimtaja Mheshimiwa Ramadhani Hamza Singano, atafuatiwa na Mheshimiwa Dkt. Ritta Enespher Kabati na Mheshimiwa Ibrahim Mohamed Shayo, ajiandae.

**MHE. RAMADHANI H. SINGANO:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nikushukuru kwa fursa hii ya kuchangia. Kwa dhati ya moyo wangu niitumie fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu, mwingi wa rehema. Nimshukuru Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na kumpongeza, Mama yetu kipenzi, Mama Dkt. Samia Suluhu Hassan. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niupongeze Wizara ya Ujenzi, Wizara yenye watendaji makini sana, sijawahi kuwa na wasiwasi nao. Nimpongeze Mheshimiwa Waziri, ndugu yangu Ulega na Mheshimiwa Naibu Waziri, lakini na Katibu Mkuu na timu yake yote.

Mheshimiwa Naibu Spika, kawaida hata kama ukipewa kidogo lazima ushukuru. Anatwambia Mwenyezi Mungu, *La'in shakartum laazidannakum* (Hakika mkishukuru hata kidogo nitawazidishieni). Sasa kwa niaba ya Wanabumbuli nianze kushukuru kwa sababu kwa mara ya kwanza rekodi imevunjwa, maana nilitaka niondoke na shilingi ya Waziri. Tena kwa kilomita chache, kilomita 22 za lami kutoka Soni - Bumbuli, ingekuwa ni kioja kikubwa sana, lakini kwa bahati nzuri, kwa maana ya uchungu wa Mama Samia, ametoa maelekezo barabara hii sasa iingie ikiwa ni historia kubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wanabumbuli wakiwa wanasikiliza saa hizi, wana tabasamu kubwa, lakini atakapohitimisha, Mheshimiwa Waziri, ninaomba nimuulize maswali mawili. Lini barabara hii itatangazwa tena baada ya marudio ya gharama? Lini Ujenzi utaanza? Mheshimiwa Waziri atambue kwamba Mheshimiwa Mbunge wa Jimbo la Bumbuli ni *Professional Engineer* na ni *Civil Engineer*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna barabara ya kimkoa, ambayo inaunganika na ile ya Kibirashi kule Handeni. Barabara

ya Mabokweni - Maramba - Mashewa - Magoma - Korogwe – Handeni, kilomita 127. Hii nayo atupe maelezo kidogo kwa sababu kilomita anazoziweka kwa mapinduzi haya ya uchumi, tunaona kama bado haijaigusa vizuri. Atupe ufafanuzi tupate chanzo kingine cha kui-*support* barabara hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa nami ni mtaalam pia kwenye eneo hili, kuna maeneo machache ninaomba kuwashauri ndugu zangu na sitamaliza maana nina pointi 12 za muhimu, lakini mengine nitayafikisha kwenye meza ya Waziri kwa maandishi na lengo langu kubwa ninataka kushauri namna ya kutunisha ule Mfuko. Ukiacha kutumia tozo na *PPP* na maeneo mengine nieleze kwamba kuna maeneo mengi ya kuweza kutengeneza tozo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo mojawapo, wanaweza wakaliona la ajabu sana, lakini kwa sababu tuna *interchange* kama ile ya pale Mtumba, kuna uwezekano tukaongea na makampuni kama *Vodacom*, wakaitumia *interchange* ile kwa jina lao huku wakitupa tozo. Tunaweza tukawapa miaka 10 mpaka miaka 50 na maeneo mengine katika majiji makubwa na tozo hiyo ikitoka iende mara moja kwenye Mfuko wa Barabara. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, maeneo mengine ni ada za matumizi ya barabara. Kuna baadhi ya maeneo tunaweza tukatengeneza *bypass* muhimu kwa ajili ya kuokoa foleni, lakini zilipiwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna maeneo yataongezeka gharama kwa sababu ya miradi ya barabara. Maeneo haya kuwe na tozo maalum zilizosababisha maeneo haya kuongezeka gharama. Kuna maeneo kiwanja kikiuzwa 20,000,000, baada ya kuweka *flyover* tu, kiwanja kinauzwa shilingi 80,000,000. Sasa ongezeko hili lazima lichangie kwenye barabara pia.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna maeneo tunaweza tukachukua kitu kinaitwa *Betterment Levy*. Tozo kwa maeneo yaliyoongezeka thamani, lakini inawezekana ikawa ni kwenye

viwanja na kwenye biashara. Kuna maeneo tunaweza tukapata *levy* inaitwa *Utility Corridor*. Kawaida katika barabara kuna maeneo tunaruhusu *utilities* za umeme na mabomba ya maji na gesi yapite. Yakipita haya yatozwe tozo ichangie katika Mfuko wa Barabara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna mambo mengi manono hapa kwa sababu ya muda siwezi kuyaeleza, lakini ninaomba Mheshimiwa Waziri atakapoyaona kwenye meza yake, hebu wayatumie ni sawa na mtori, ukienda haraka nyama utaziacha chini. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo lingine ambalo ningeshauri, kuwe na maeneo ambayo kuna *Flight and Logistic Levy*, tozo kwenye usafirishaji wa mizigo, lakini ifike mahali pia hizi barabara tuzipunguzie mzigo. Kama tunayo *SGR*, kwa nini malori mengine yasipungue tukapitishia mizigo huko?

**MBUNGE FULANI:** Kweli.

**MHE. RAMADHANI H. SINGANO:** Mheshimiwa Naibu Spika, utakapoiangalia Sheria ya Madini, Sura 123, Sehemu ya 131, inaturuhusu kutumia *Ploughing Back*.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana kwa kuwa umeahidi kupeleka kwa maandishi kwa Mheshimiwa Waziri, basi tunakushukuru na muda wako umekwisha.

**MHE. RAMADHANI H. SINGANO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba kuunga hoja mkono, lakini baada ya ufafanuzi mzuri. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Nilimtaja Mheshimiwa Dkt. Ritta Enespher Kabati na atamalizia Mheshimiwa Ibrahim Mohamed Shayo.

**MHE. DKT. RITTA E. KABATI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ili niweze kuchangia jioni hii ya leo. Ninaomba kwanza nimshukuru Mwenyezi Mungu, lakini ninaomba nimtangulizie Mwenyezi Mungu katika mchango wangu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kumpongeza Mheshimiwa Ulega, Waziri ambaye kwa kweli ni mtu na nusu, anafanya kazi nzuri anatusikiliza sisi Wabunge wenziwe wote. Nimpongeze sana pia Naibu Waziri ambaye kwa kweli anajibu maswali vizuri na kwa uhakika. Nimwombe Mwenyezi Mungu azidi kuwabariki na kuwajalia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nami niendelee kumpongeza pia *TANROADS* Iringa wanafanya kazi nzuri, lakini *Engineer* Msangi amestaafu tunaye *Engineer* Machaka ambaye anafanya kazi nzuri sana. Ninamwomba Mheshimiwa Waziri, huyu Machaka, hebu tumpandishe kwa sababu tayari anazijua barabara zote za Mkoa wa Iringa na anafanya kazi nzuri, kila siku yuko *site*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Wilaya yetu ya Kilolo ina barabara nne tu za *TANROADS*, zenye kilomita 260. Tunampongeza sana Rais wetu Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, ambaye kwa kweli Watanzania ni lazima tumshukuru, lazima tumwombee na sisi Wanakilolo tunamwombea sana kwa kazi nzuri ambayo ameendelea kuifanya pale Kilolo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tumejengewa barabara ya lami, kilomita 33.2, inatoka Ipogolo kwenda Idete. Hii barabara tayari imekamilika, tunapatiwa taa 350 na zitaanza kuwaka Kilolo. Karibuni Kilolo mwone kulivyokuwa kuzuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, stendi ya kisasa pia inajengwa. Kwa hiyo, tunaomba wawekezaji wote wa mabasi, akina Shabiby, waje pale Kilolo ili sasa mabasi yaanze kutokea Kilolo kwenda mikoa mingine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo, ombi letu Mheshimiwa Waziri, kuna ile barabara imeishia pale Kilolo Kibaoni, nilimpigia magoti Waziri siku ile. Ninamwomba zile kilomita 16 kwenda

Dabaga, sasa zijengwe kwa sababu lile ndiyo eneo korofi. Ametujengea barabara ile nzuri, asipopitisha zile kilomita 16, yaani hakuna alichofanya kwa sababu magari ndiyo yanakwama pale. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara hii ikikamilika inakwenda kufungua uchumi wa Morogoro na Iringa. Kuna kipande cha kutoka Idete, Itonya, Muhanga kinakwenda mpaka Mgeta, kilomita 30.5. Hili eneo sasa hivi wanatunza *TARURA*, tunaomba sasa barabara hii ipandishwe ili *TANROADS* waweze kutunza hili eneo, maana yake kule wananchi wanapata mateso. Sasa hivi hakuna gari linalofika kule Itonya.

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara yetu ya pili ni Kitonga. Tunamshukuru sana Mheshimiwa Waziri alikuja Kitonga na akaona changamoto kubwa. Hii ni barabara ya kimataifa, magari makubwa yanapita, lakini yanakwama sana na uchumi wote unaotoka bandarini unapita pale kwenye nchi ambazo zinakwenda kusini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, ninamwomba hii barabara ni muhimu sana kwa uchumi wa nchi yetu, ifunguke na Waziri alituahidi kwamba itajengwa njia nne na tunaomba sasa atakapokuwa anahitimisha atuambie ujenzi utaanza lini ili kuondoa changamoto kubwa iliyopo pale Kitonga.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunayo barabara ya tatu ambayo hii barabara inatoka Kilolo kwenda Ilula. Hii barabara inatoka Kilolo, inakwenda Lulanzi, inakwenda Kising'a, inapita Udekwa na pia inapita Mlafu, inakwenda mpaka Ilula. Hata hivyo, liko daraja la Mto Lukosi la muda mrefu toka 2022, hili ni changamoto. Wakati wa mvua hii barabara haipitiki kabisa na kuna uchumi mkubwa sana Kilolo ambao unaweza ukalisha hata nchi nzima kwa sababu mvua zinanyesha mwaka mzima. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, tukuombe utoe umuhimu wa kujenga hili Daraja la Lukosi ili barabara hii ipitike na ndiyo inaunga wananchi wa Kilolo ya juu na chini. Kuna kata 12

juu na chini, barabara hii ndiyo inawaunga kwenda kwenye makao makuu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tunayo Barabara nyingine ya nne, inatoka Ihemi – Kibaoni - Ihimbo, ina kilomita 24.52. Tunaomba barabara hii ifanyiwe matengenezo ili iweze kupitika, kuna eneo ambalo ushuru magari yanakuwepo yanapeleka kwenye wilaya nyingine. Tunashukuru sana.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Dkt. Kabati.

**MHE. DKT. RITTA E. KABATI:** Mheshimiwa Naibu Spika, Mungu akubariki, lakini ninaomba Wabunge wote tuunge mkono mapendekezo ya Kamati hii ya Miundombinu ili tuweze kupata fedha za barabara na Mungu awabariki sana. *(Makofi)*

**WABUNGE FULANI:** Amina.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mchangiaji wa mwisho ni Mheshimiwa Ibrahim Mohamed Shayo.

**MHE. IBRAHIM M. SHAYO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuwa mchangiaji wa mwisho na kwa kuwa ni mchangiaji wa mwisho, ninaamini muda utakuwa wa kutosha kwa sababu hakuna mwingine wa kuchangia. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba kwanza nimshukuru na nimpongeze sana Mheshimiwa Rais kwa kazi nzuri na kubwa anazozifanya. Hata hivyo, nimpongeze sana kaka yangu Mheshimiwa Waziri pamoja na dada yangu *Eng*. Balozi Aisha na watendaji wote kwa kazi nzuri wanazozifanya za kuiongoza Wizara hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, nami niseme tu kwamba nichukue nafasi hii kwa niaba ya wasafirishaji wote wa Tanzania, naomba ku-*declare interest* nami ni msafirishaji, nina mabasi, lakini tatizo

kubwa la wasafirishaji lililokuwa linawasumbua ni kuhusu mabasi kuingia mizani.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimshukuru sana Waziri Mkuu na ninampongeze sana Waziri Mkuu kwa kuyaondoa yale mabasi kupita mizani. Sasa hivi mabasi yote nchini hayaingii mizani, lakini haya yote ni kwa sababu ya maono na ushauri na maelekezo ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, nimpongeze sana kwa hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nimpongeze sana Waziri Mkuu kwa tamko la mabasi kutokuingia wilayani kwenye stendi ambazo hazina umuhimu. Kama wenye mabasi hawashushi wala hawapakii, hakuna umuhimu wa kuingia stendi, ninampongeza sana Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, niwashukuru sana na niwapongeze *sana TBA*. *TBA* sasa hivi inajiendesha kibiashara na ukiangalia *TBA* kweli sasa hivi ni *TBA*. Tumetembelea majengo wanayojenga kule Masaki, Magomeni, majengo yenye viwango, *finishing* yenye viwango, niwapongeze sana, sana, sana. Hata hivyo, pamoja na pongezi hizo, vipo viwanja ambavyo ni viwanja vizuri viko sehemu nzuri kama kule Masaki, waende wakatafute wawekezaji waweze kuingia kwenye *PPP* ili viwanja vile visikae bure, vijengwe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niwaombe *TBA*, Moshi Mjini kuna uwanja uko katikati ya mji majengo zaidi ya heka 15. Niwaombe sana waende wakawekeze pale ili hata wale wakazi wanaoishi kwenye zile nyumba wapate faida sasa ya kumiliki na wao nyumba moja bure kutokana na Ujenzi ule. Kwa hiyo, niwaombe katika uwekezaji wasitusahau sisi watu wa Moshi Mjini.

Mheshimiwa Naibu Spika, Waziri ameongelea sana mikoa karibu yote, lakini nimepata wasiwasi mkubwa sana. Kwenye Ilani barabara hii ipo na tumeambiwa kwenye majibu ya maswali yangu kwamba tarehe Mosi, Juni mkandarasi anaingia *site*, lakini kwenye maelezo yake hapa sikumsikia.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, ninamwomba anapokuja kuhitimisha, aitaje Barabara ya Maili Sita - Shatwazi ambayo iko Moshi Mjini ambayo inaenda kujengwa kwa njia nne. Ninaomba barabara hii wana Moshi wanataka kusikia kauli ya Serikali. Kwa hiyo, ukifika wakati wa hitimisho, ninaomba aiitaje barabara hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, shida yetu kubwa ni barabara za lami. Leo ninaomba nitoe mawazo jinsi ya kutengeneza barabara za lami Tanzania nzima kwa gharama nyepesi. Sisi wauzaji wa mafuta, mafuta yote yanachukuliwa kwa *bulk*. Mafuta yanachukuliwa kwa *bulk*, bei inapangwa na Serikali na sisi wauza mafuta tunapewa bei.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa ninamwomba Mheshimiwa Waziri, sasa hivi lami inakuwa ghali, kilomita moja ya lami ni zaidi ya bilioni 1.8. Sasa ninamwomba Mheshimiwa Waziri, lami sasa iagizwe kwa *bulk*, kama yanavyoagizwa mafuta. Tutakapoagiza lami kwa *bulk*, tukachukua *forced labour* yetu ya wafungwa tukaenda kujenga lami, tutajenga lami kwa shilingi 900,000,000 badala ya bilioni 1.8. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, ninaomba sana waende wakatengeneze mpango wa kuagiza lami kwa jumla kwenye meli, tuagize meli nzima tuje tuingize kila jimbo lipate lami na tutumie *labour charge* ya wafungwa, wafungwa wako pale tunawagharamia, tunawalisha ndugu zetu na wengine hawana kazi pale. Ma-*engineer* watatusaidia kuendeleza Taifa letu. Kwa hiyo ninamwomba sana Waziri alifikirie hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho niseme kwamba fedha ambazo zinahitaji kwenda kwenye Mfuko wa Barabara, ninaomba sana, tena ninaomba kwa msisitizo sana. Hakuna mwingine wa kuchangia, kengele usilie! *(Kicheko)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Malizia Mheshimiwa.

**MHE. IBRAHIM M. SHAYO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nikuombe sana fedha zinazopaswa kwenda kwenye Mfuko wa Barabara, ninaomba ziende kwenye Mfuko wa Barabara, zile fedha ziende kwenye Mfuko wa Barabara na zisichukuliwe na Wizara ya aina yoyote. Kwa kufanya hivyo itatufanya hata sisi barabara zetu ziweze kutengenezwa.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa.

**MHE. IBRAHIM M. SHAYO:** Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maneno hayo, ninaomba kuunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Waheshimiwa Wabunge, huyu alikuwa mchangiaji wetu wa mwisho kwa jioni hii ya leo. Ninalo tangazo moja hapa; Katibu wa Wabunge wa Chama Cha Mapinduzi anawatangazia Wabunge wote wa Chama Cha Mapinduzi kwamba kesho saa saba na nusu mchana, baada ya kikao cha asubuhi, kutakuwa na kikao cha Wabunge wa CCM katika ukumbi huu wa Msekwa.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema hayo, ninaahirisha Shughuli za Bunge hadi kesho 3.00 kamili asubuhi.

*(Saa 1.48 Usiku Bunge Liliahirishwa hadi Siku ya Alhamisi, Tarehe 21 Mei, 2026, Saa Tatu Asubuhi)*